28 APRILI, 2026

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Kumi na Nane - Tarehe 28 Aprili, 2026

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Mwenyekiti (Mhe. Cecilia D. Paresso) Alisoma Dua

MWENYEKITI: Waheshimiwa, tukae.

Katibu.

NDG. MONICA MWAGA – KATIBU MEZANI:

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

NAIBU WAZIRI WA KILIMO:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

MHE. DKT. RITTA E. KABATI K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

MWENYEKITI: Katibu.

NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na maswali na sasa swali la kwanza linaelekezwa Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI. Ninamwita Mheshimiwa John Francisco Nzilanyingi, Mbunge wa Nyamagana, aweze kuuliza swali lake.

Na. 203

Ujenzi wa Barabara za Pembezoni Jimbo la Nyamagana

MHE. JOHN F. NZILANYINGI aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga barabara za pembezoni na mtaani maeneo ya Kushiri, Mahina, Luchelele na Lwanchima?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa John Francisco Nzilanyingi, Mbunge wa Jimbo la Nyamagana, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea na utekelezaji wa miradi ya ujenzi na matengenezo ya mara kwa mara ya barabara za vijijini na mjini ili kuwezesha shughuli za usafirishaji kufanyika kwa urahisi kote nchini ikiwemo katika Jimbo la Nyamagana Mkoani Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya fedha za barabara katika Jimbo la Nyamagana imeongezeka kutoka shilingi bilioni 3.47 mwaka 2020/2021 hadi shilingi bilioni 6.49 mwaka 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya barabara zinazoendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sasa katika Jimbo la Nyamagana ni pamoja na ujenzi wa barabara ya Mwananchi - Mahinakati kilometa 0.3, Mwananchi - Bugurika kilometa 0.16, Igelegele - Mahinakati, Buhongwa - Lwanchima (kilometa 3.8) ambazo kwa pamoja zinagharamia jumla ya takribani shilingi milioni 853.28. Aidha, ujenzi wa barabara ya Buhongwa - Lwanchima (kilometa 3.8) umetekelezwa kwa shilingi bilioni 5.9 kupitia mradi wa *TACTIC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia bajeti ya mwaka 2024/2025 Serikali imeendelea na ujenzi wa barabara ya Kishiri - Fumagila (kilometa 1.5) kwa shilingi milioni 304.99 na katika mwaka wa fedha 2026/2027 zimetengwa fedha kiasi cha shilingi milioni 83.93 ujenzi wa barabara ya Bugayamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutenga bajeti ya kujenga barabara za pembezoni kwa awamu katika Jimbo la Nyamagana zikiwemo barabara za Kushiri, Mahina, Luchelele na Lwanchima. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa John Nzilanyingi, maswali ya nyongeza.

MHE. JOHN F. NZILANYINGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali miwili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru kwa majibu ya Serikali swali langu la kwanza hali ya barabara kwenye Jimbo la Nyamagana kutokana na uharibifu ulioletwa na madhara ya mvua ni mkubwa sana, maeneo ya Mahina, maeneo ya Luchelele, maeneo ya Lwanchima maeneo ya Igogo, hali ni mbaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni nini mpango wa Serikali wa kwenda kufanya kazi kwa haraka ili tuweze kuwanusuru wananchi kwenye maeneo yao ili barabara ziweze kupitika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, barabara ya Mkuyuni Mahina - Mandu kwenda mpaka Nailipichi yenye urefu wa kilometa 10.5, imeshafanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. Tarehe 19 Disemba ya mwaka 2024 Waziri wa TAMISEMI alikuja kuitembelea barabara ile na akaahidi kutoa fedha ili ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami uweze kuanza mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ...

MWENYEKITI: Uliza swali Mheshimiwa.

MHE. JOHN F. NZILANYINGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, toka Waziri wa TAMISEMI amekuja sasa yapata zaidi ya miaka mitatu. Ni nini kauli ya Serikali juu ya uanzaji wa ujenzi wa barabara hiyo yenye urefu wa kilometa 10.5 ili iweze kuwasaidia wananchi wa Jimbo la Nyamagana? Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza, nimshukuru sana Mheshimiwa Mbunge, nimhakikishie tu kwamba Serikali inatambua kwamba tuna changamoto ya uharibifu mkubwa wa baadhi ya barabara katika Jimbo la Nyamagana zikiwemo barabara za Mahina, Luchelele na nyingine ambazo Mheshimiwa Mbunge amezitaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie tu kwamba tayari tumeshapokea taarifa rasmi ya tathmini ya gharama zinazohitajika kwa ajili ya mategenezo ya barabara hizo na hivi sasa Serikali inaendelea na hatua za mwisho za kuandaa utaratibu wa fedha ili kupelekwa fedha katika maeneo yote yenye uharibifu wa barabara, zikiwemo barabara za Jimbo la

Nyamagana kwa ajili ya matengenezo ya dharura na ya kawaida ili ziweze kupitika vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Nzilanyingi, kwamba tunafahamu na tuko katika hatua za kupeleka fedha ili barabara hizi ziweze kujengwa na kuweza kupitika vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye swali lake la pili kuhusiana na barabara hiyo ya Mbuyuni yenye urefu wa kilometa 10.5 kufanyiwa usanifu, maana yake ni hatua ya mwanzo kuelekea kumpata mkandarasi na baadaye kuendelea na ujenzi wa barabara hiyo. Kwa hiyo, kauli ya Serikali ni kwamba kama ambavyo tumedhamiria na kufanya usanifu tutaendelea kujiandaa kwa maana ya kutafufa fedha na kuhakikisha kwamba barabara hiyo inajengwa kwa kiwango cha lami kama ambavyo ipo kwenye mpango. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nilikuona Mheshimiwa Kafiti Kafiti, swali dogo la nyongeza.

MHE. KAFITI W. KAFITI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Ilemela, ninaomba kujua, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa barabara ya Pasiansi Lumala – Kiseke, kwa sababu barabara hii ni muhimu kwa wakazi wa Jimbo la Ilemela na imechukua zaidi ya Kata tatu? Ni nini kauli ya Serikali katika hilo? Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Pasiansi katika Jimbo la Ilemela ambayo Mheshimiwa Kafiti ameifuatilia mara kwa mara na tunafahamu kwamba Serikali imeendelea kuweka kipaumbele kuhakikisha kwamba barabara hiyo inajengwa, kwa sababu ni barabara muhimu sana kwa wananchi wa eneo la Ilemela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ipo kwenye mpango wa Serikali na hatua za utekelezaji wa barabara hizo zitafanyika ili kuhakikisha kwamba inakamilika kwa wakati na inakuwa na ubora unaotakiwa kwa manufaa ya wananchi wa Ilemela. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nilikuona Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, kwa ufupi swali la nyongeza.

MHE. DKT. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Boma ya Ng'ombe, Masisiwe ni barabara ya kiuchumi, toka mvua zimeanza kunyesha barabara hii haipitiki magari yamekwama.

Nini mpango wa Serikali tunusuru barabara zote za Kilolo ikiwepo hii barabara ya Masisiwe Boma La Ng'ombe? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Boma Ng'ombe - Masisiwe katika Jimbo la Kilolo ni barabara muhimu sana, na kwa hakika Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati amefuatilia mara kadhaa. Nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tayari iko kwenye orodha ya barabara zetu za kipaumbele, mara baada ya mvua kukatika na tutaenda na mpango ule wa dharura kwa ajili ya matengenezo kuhakikisha kwamba barabara ile inapitika vizuri na kusaidia shughuli za usafiri katika Jimbo la Kilolo. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nilikuona Mheshimiwa Mwita Waitara, swali dogo la nyongeza.

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru. Ninapozungumza sasa hivi hapa Kata ya Bumera, Susuni, Nyarero, Ganyange, Pemba, Mbugi hakuna mawasiliano,

njia zimekatika. Nini kauli ya Serikali kwa watu wa Tarime Vijijini maeneo ambayo nimeyataja? Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na changamoto ya barabara kote nchini ikiwemo katika Jimbo la Tarime Vijijini kwa Mheshimiwa Waitara, na changamoto hii imetokana na mvua nyingi ambazo zimenyesha na kupelekea uharibifu wa barabara nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba yapo baadhi ya maeneo ambayo mvua bado zinaendelea kunyesha, kinachofanyika sasa ni tathmini ya gharama zinazohitajika kwa ajili ya marekebisho ya barabara hizo, lakini tunasubiri angalau hali ya mvua ipungue kwa sababu kwenda kufanya matengenezo katika kipindi hiki cha mvua nyingi hakutakuwa na faida kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge, Serikali inafahamu inawapa pole wananchi wa Jimbo la Tarime lakini imeshaandaa utaratibu wa fedha za dharura kwa ajili ya kwenda kutengeneza mara mvua zikipungua ili barabara hizo zipitike vizuri. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nilikuona Mheshimiwa *Engineer* Ezra Chiwelesa, swali kwa kifupi.

MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Barabara za Mtaa wa Ng'ambo Wilaya ya Biharamulo Mjini pale zimeharibika vibaya sana. Tunajua ni msimu wa mvua, lakini *technically* ziko *means* za ku-*repair* barabara ili ziendelee kupitika hata wakati wa mvua. Ni nini kauli ya Serikali kuwasaidia wananchi wa Ng'ambo ili sasa waweze kutoka majumbani na kurejea huku wakilitumikia Taifa lao?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ziko barabara ambazo zimeharibiwa, lakini zinaweza zikafanyiwa matengenezo ya muda ili kuwezesha shughuli za usafirishaji kuendelea wakati tunajiandaa na matengenezo ya kudumu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, nimwelekeze Meneja wa *TARURA* Mkoa wa Kagera na Wilaya ya Biharamulo kwenda kufanya tathmini ya haraka kwenye barabara hiyo na kufanya matengenezo ili barabara angalau iendelee kupitika wakati tunasubiri muda wa kufanya matengenezo ya kudumu. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Edwin Swalle, kwa kifupi.

MHE. EDWIN E. SWALLE: Mheshimiwa Mwenyekiti, iko barabara ya Lupembe kwenda Ikondo, na hii barabara inapita nyumbani kwangu pale Kanikelele, yako maeneo matatu yameharibika vibaya sana hata mimi leo siwezi kufika pale kwangu nyumbani Kanikelele. Ni nini maagizo ya Meneja wa Njombe kufanya marekebisho sehemu hizo tatu watu waweze kusafiri kwenye hii barabara?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kuwakumbusha Mameneja wa *TARURA* katika Wilaya zetu zote na katika Mikoa yetu yote kwamba tunafahamu kuna hali ya mvua inaendelea, lakini tuna barabara muhimu sana katika maeneo yetu ambazo ni lazima ziendelee angalau kupitika wakati tunasubiri matengenezo ya kudumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, katika Jimbo la Lupembe ninamwelekeza Meneja wa *TARURA,* Mkoa wa Njombe na Wilaya ya Njombe kwenda kufanya tathmini kwenye barabara hiyo na

kuona linaloweza kufanyika angalau matengenezo ya muda yafanyike, barabara iendelee kupitika, wakati tunasubiri hali ya hewa kukaa vizuri kwa ajili ya matengenezo ya kudumu. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa, tunaendelea. Sasa ninamwita Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Mbunge wa Nsimbo, aweze kuuliza swali lake.

Na. 204

Ukarabati Shule ya Msingi Mtapenda – Nsimbo

MHE. ANNA R. LUPEMBE aliuliza:-

Je, lini Serikali itakarabati Shule ya Msingi Mtapenda Kata ya Mtapenda – Nsimbo?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Mbunge wa Jimbo la Nsimbo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shule ya Msingi Mtapenda ilijengwa mwaka 1970, na hivyo ni chakavu na inahitaji ukarabati. Katika mipango ya ukarabati wa shule chakavu, Serikali katika mwaka 2021/2022 ilifanya tathmini na kubaini jumla ya shule 10,595 chakavu kote nchini ambapo jumla ya shilingi trilioni 2.8 zinahitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kuptia Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI, imeandaa andiko la mradi unaoitwa *SIFA* yaani *(School Infrastructure Facelifting Programme)* na kuwasilisha Wizara ya Mipango na Uwekezaji ili kuwezesha upatikanaji wa fedha za kufanyia ukarabati wa shule zote kongwe za awali, msingi na Sekondari nchini ikiwemo Shule ya Msingi Mtapenda, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Anna Lupembe, maswali ya nyongeza. Mheshimiwa washa *microphone*.

Waheshimiwa Wabunge, tuliowasha *microphone,* wote tunaomba tuzime. Waheshimiwa tuliowasha *microphone,* ninawaona hapa, ninaomba tuzime.

MHE. ANNA R. LUPEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na pole kwa usumbufu. Kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri, hii shule imejengwa toka mwaka 1970 mpaka leo haijafanyiwa marekebisho ya aina yoyote. Katika kipindi cha mvua, hasa hii ya mwaka huu, kwa kuwa mabati yote yameoza, watoto wananyeshewa, hawawezi kupata usikivu katika masomo yao. Lini Serikali itachukua dharura ya kurekebisha Shule hii ya Msingi ya Mtapenda ili watoto waweze kukaa kwa amani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, kwa kuwa katika Shule ya Msingi ya Mtapenda, hakuna nyumba za Walimu, wananchi wa Kata ya Mtapenda, Kijiji cha Mtapenda, wakaamua kujichangisha ili waweze kujenga hata nyumba mbili za walimu na mimi Mbunge wao nikawachangia kutoka Mfuko wa Jimbo, lakini Serikali mpaka leo haijafanya kitu chochote. Ni lini Serikali itajenga nyumba za walimu katika Kata ya Mtapenda? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba ziko shule kongwe na chakavu kama Shule ya Msingi Mtapenda na Serikali inaandaa mpango mahususi kwa ajili ya ukarabati wa shule zote kongwe kama ambavyo nimejibu kwenye jibu langu la msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa shule hii ni chakavu sana na kwa mujibu wa Mheshimiwa Mbunge kwamba inavuja na wanafunzi hawawezi kusoma vizuri, ni wajibu wa Halmashauri ya Nsimbo na Mkurugenzi kupitia mapato ya ndani angalau kufanya marekebisho ya haraka kwenye shule hii ili wanafunzi waendelee

kusoma wakati Serikali Kuu ikiendelea na utaratibu wa kutafuta fedha kwa ajili ya kufanya ukarabati mkubwa wa shule hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI nimwelekeze Mkurugenzi wa Halmashauri ya Nsimbo, kufanya tathmini ya haraka na kufanya matengenezo ya madarasa yanayovuja ili wanafunzi waendelee kusoma wakati Serikali inaandaa bajeti kubwa kwa ajili ya kwenda kufanya ukarabati mkubwa wa shule hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu swali lake la pili, tunafahamu kwamba yapo maeneo mbalimbali ya shule zetu ambako kuna upungufu wa nyumba za walimu na Serikali hii ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, imeendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za walimu katika shule zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa kuna zaidi ya nyumba 650 zinaendelea kujengwa kote nchini. Niwapongeze wananchi wa Nsimbo kwa kuanza ujenzi wa nyumba, nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kuchangia nguvu za wananchi. Nimhakikishie kwamba na sisi Serikali Kuu tutafanya utaratibu wa kupata fedha kwenda kuhakikisha nyumba hiyo ya walimu inakamilishwa.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Naibu. Tunaendelea, sasa ninamwita Mheshimiwa Devotha Daniel, Mbunge wa Viti Maalum, aweze kuuliza swali lake. *(Makofi)*

Na. 205

Dirisha Maalum kwa Sekta za Kipaumbele Kagera

MHE. DEVOTHA D. MBURARUGABA aliuliza:-

Je, Serikali ipo tayari kutenga dirisha maalumu la mikopo kwa sekta za kipaumbele za kilimo cha kahawa, ufugaji na biashara ndogo ndogo – Kagera?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Devotha Daniel Mburarugaba, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchumi wa Mkoa wa Kagera unategemea sana sekta za kilimo, mifugo, uvuvi na biashara ndogo ndogo. Serikali imekuwa ikitoa mikopo mbalimbali ili kuwawezesha wananchi wake. Mikopo hiyo ni pamoja na mikopo ya 10% inayotokana na mapato ya ndani ya halmashauri; mikopo ya kuwezesha shughuli za ufugaji wa mifugo na samaki kwa kutumia vizimba inayotolewa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi; mikopo kupitia Programu ya Jenga Kesho Iliyo Bora *(Building a Better Tomorow – BBT)* na Mfuko wa Pembejeo inayoratibiwa na Wizara ya Kilimo. Aidha, ipo mikopo inayotolewa na Serikali kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii kwa wajasiliamali wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Serikali imeanzisha Benki ya Maendelo ya Kilimo na Ushirika ambayo imepewa jukumu mahsusi la kutoa mikopo kwa ajili ya kuwezesha sekta za kipaumbele za kilimo ikiwemo kilimo cha kahawa, ufugaji na biashara ndogo ndogo. Mwaka 2024/2025 Serikali imetoa mikopo ya shilingi milioni 742.67 kwa makundi mbalimbali ya Mkoa wa Kagera kupitia mikopo ya 10%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kwa sasa Wizara ya Mifugo na Uvuvi imetoa matangazo ya kutoa mikopo ya shilingi bilioni 200 ambazo ni ahadi ya Mheshimiwa Dkt Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kuwezesha wananchi kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kiuchumi zikiwemo kilimo, ufugaji wa mifugo na samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutoa elimu na hamasa kwa jamii na makundi husika ili kunufaika na fursa za mikopo mbalimbali.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Devotha Daniel, swali la nyongeza.

MHE. DEVOTHA D. MBURARUGABA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa majibu mazuri ambayo nimeyapata kwa Naibu Waziri, lakini ningependa kuishauri Serikali. Mkoa wa Kagera ni mkoa ambao una wakulima wengi wa kahawa, na wakulima hawa wamekuwa wakivuna kahawa kabla hazijakomaa na wengine kushawishika kuuza nchi jirani. Je, ni lini Serikali itaamua kutoa mikopo ya dharura kwa wananchi hawa ambao wanahusiana na kilimo cha kahawa ili tuweze kutatua changamoto hizi na kuongeza mapato ya Mkoa wa Kagera kupitia *AMCOS* zao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini wananchi hawa wanaweza wakapata hiyo mikopo ya dharura ili tuwapunguzie adha wakati wa msimu wa kahawa.

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kumekuwa na changamoto ya baadhi ya wakulima wa kahawa katika Mkoa wa Kagera kuvuna kahawa kabla haijakomaa vizuri na kuuza ndani pia na nchi jirani. Suala hili linaleta hasara, lakini pia linaathiri ubora wa kahawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hii imeshaweka utaratibu mzuri. Kwanza kuna fursa ya mikopo ya 10% ambayo wakulima wanaweza wakakopa, wakafanya shughuli zao za kilimo na baada ya mavuno wakarejesha zile fedha kwa utaratibu uliowekwa. Pili, kwa fursa ya mikopo ya kilimo yenye riba nafuu chini ya asilimia tisa inayopatikana katika Mkoa wa Kagera pamoja na nchini kote. Tuna fursa ya mikopo ya Benki ya

Maendeleo ya Kilimo na Ushirika na pia tuna Mfuko wa Mikopo ya Pembejeo za Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nitumie nafasi hii kuwashauri na kuwahamasisha wananchi, wakulima wa kahawa katika Mkoa wa Kagera na mikoa mingine kote nchini kuhakikisha wanatumia fursa za madirisha haya ya mikopo ya dharura ambayo yapo, hayana ukiritimba mkubwa, wapate fedha hizo ili waendeshe shughuli zao za kilimo, na baada ya mavuno, waendelee kurejesha kwa mujibu wa utaratibu.

MWENYEKITI: Ahsante. Nilikuona Mheshimiwa Agnes Hokororo.

MHE. AGNES E. HOKORORO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kama ilivyo katika swali la msingi, je, Serikali haioni haja ya kuwakopesha wakulima wa korosho kupitia wale wenye stakabadhi ghalani?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inatoa mikopo kwa wakulima wa mazao mbalimbali. Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, tutashirikiana kwa karibu na Wizara ya Kilimo kuona uwezekano wa shughuli hiyo ya mikopo kwa wakulima wa korosho na stakabadhi ghalani kuweza kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tumeichukua hoja hiyo, tutaifanyia kazi na wenzetu wa Wizara ya Kilimo ili kurahisisha upatikanaji wa mikopo kwa wakulima wa korosho.

MWENYEKITI: Nilikuwa namwona Mheshimiwa Morris Makoi.

MHE. MORRIS J. MAKOI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona. Kama ambavyo swali la msingi limesimama, mikopo ya 10% ambayo inatolewa na Halmashauri, inalenga zaidi

vijana na wanawake, lakini wakulima wa kahawa ni makundi mbalimbali. Je, Serikali ina kauli gani kwamba mikopo hiyo sasa ijumuishe wazee pamoja na makundi mengine ambayo hayajatajwa kwenye hiyo sheria ya mikopo?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba mikopo ya 10% ni ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, lakini hao pia ni moja ya makundi ambayo yanafanya shughuli za kilimo. Kwa hiyo, wanaweza wakanufaika kupitia dirisha hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ipo mikopo mingine ambayo haiendi *specifically* kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Kama ambavyo nimesema, mikopo ya kilimo yenye riba nafuu inakopeshwa kwa wakulima wote; mikopo ya Benki ya Maendeleo ya Kilimo, Ushirika, na pia mikopo ya Mfuko wa Mikopo ya Pembejeo za Kilimo. Hizi ni fursa ambazo mkulima yeyote anaweza akapata mkopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nitumie nafasi hii kuwashauri na kuwahamasisha wakulima ambao hawapo kwenye kundi la wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kutumia fursa za madirisha mengine haya ya mikopo.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa. Sasa ninamwita Mheshimiwa Patali Shida Patali, Mbunge wa Mbeya Vijijini, aweze kuuliza swali lake.

Na. 206

Kujenga Soko la Mazao la Uhakika – Mbeya Vijijini

MHE. PATALI S. PATALI aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga soko la uhakika la mazao Mbeya Vijijini?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Patali Shida Patali, Mbunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali katika kuhakikisha kwamba kunakuwa na soko la uhakika la mazao ili kuboresha sekta ya nyama na lishe katika Jimbo la Mbeya Vijijini, imetenga eneo lenye ukubwa wa ekari 14.3 kiwanja namba 26 kitalu 13A katika Kata ya Utengule Usongwe kwa ajili ya kuchakata mazao ya nyama kwa kujenga kiwanda kikubwa cha kisasa. Eneo hilo limekabidhiwa kwa taasisi ya Serikali inayosimamia masuala ya uwekezaji *(TISEZA)* tarehe 26/02/2026 ili kupata mwekezaji wa kujenga kiwanda hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, eneo kwa ajili ya kujenga soko kubwa la mazao la kisasa limetengwa katika Kata ya Nsalala Kiwanja Na. 831 Kitalu 13F chenye ukubwa wa ekari 6.1. Taratibu za kuandaa maandiko ya miradi na kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa soko hilo zinaendelea, ambapo shilingi milioni 20 zimetengwa kupitia mapato ya ndani ya halmashauri katika mwaka wa fedha 2026/2027 kwa ajili ya kukamilisha maandalizi hayo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Patali Shida Patali, maswali ya nyongeza.

MHE. PATALI S. PATALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali. Ninaiomba sana Serikali kuharakisha mchakato huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, 85% ya wananchi wa Jimbo la Mbeya Vijijini ni wakulima na wafugaji. Mathalani kwa mwaka huu

unaoisha, umezalisha zaidi ya tani 700,000 za mazao ya chakula. Wakati huo mahitaji yetu ni tani laki 200,000...

MWENYEKITI: Mheshimiwa, ninaomba uulize swali.

MHE. PATALI S. PATALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la msingi ni kuiomba Serikali kuharakisha ujenzi wa hilo soko, lakini pamoja na kiwanda kilichoahidiwa kwa ajili ya uchakataji wa nyama ili wananchi wa Jimbo la Mbeya Vijijini wapate soko, sehemu ya kwenda kuuzia mifugo yao kama mbuzi na ng'ombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili. Ninatambua hivi karibuni Mheshimiwa Waziri Mkuu kupitia hotuba yake alikemea vikali uuzaji wa mazao uliozidi kiwango, almaarufu kwa jina la lumbesa. Je, Serikali haioni haja sasa ya kuleta Muswada hapa Bungeni ili tupitishe sheria ya udhibiti wa kudumu suala hili la lumbesa ambalo limekuwa likisababisha maumivu makali sana kwa wakulima?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini pamoja na wananchi wa Mbeya Vijijini kwamba Serikali inatambua kwamba zaidi ya 85% ya wananchi wa Mbeya Vijijini ni wakulima na wafugaji, na ndiyo maana tayari tumeshaandaa eneo kwa ajili ya kujenga kiwanda cha kisasa cha nyama. Eneo hili limeshakabidhiwa kwa *TISEZA* kwa ajili ya kufanya utaratibu wa kupata mwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba suala hili lipo, linaendelea na utaratibu wa kufanyiwa kazi na Serikali. Mara utaratibu utakapokamilika, tutapata mwekezaji ambaye atajenga kiwanda hicho ili kuboresha huduma za nyama katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, eneo la mazao ya nafaka pia limetengwa kwa ajili ya utekelezaji huo na tutakwenda

kutekeleza. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba dhamira ya Serikali ni kuhakikisha tunakuwa na masoko mazuri kwa ajili ya bidhaa za mifugo na mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili kuhusiana na lumbesa, ni kweli kumekuwa na changamoto kubwa ya lumbesa na inaleta hasara kwa wakulima. Wizara ya Viwanda na Biashara na Serikali kwa ujumla imeendelea mara kwa mara kutoa miongozo, maelekezo na kusimamia ili kudhibiti lumbesa kwa wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepokea wazo lake la kuwa na Mswada wa Sheria na sisi kama Serikali tutalifanyia kazi kuona uwezekano wake. Lengo ni kuhakikisha kwamba tunadhibiti lumbesa na kuleta faida kwa wakulima.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru kwa majibu yako. Sasa tunahamia Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora. Ninamwita Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, Mbunge wa Hai aweze kuuliza swali lake.

Na. 207

Kuongeza Kada Zisizo kwenye Orodha ya Sekretarieti ya Ajira

MHE. SAASHISHA E. MAFUWE aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza kada ambazo hazipo kwenye orodha ya kada za Sekretarieti ya Ajira kwa kuwa zinafundishwa vyuoni?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na

Utawala Bora, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, Mbunge wa Hai kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua kuwa vyuo Vikuu na vyuo vya elimu ya juu hutoa mafunzo ya programu za fani mbalimbali kwa vijana ambao wanaweza kuajiriwa katika utumishi wa umma au katika sekta binafsi nchini. Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma husimamia taratibu za ajira kwa kuzingatia sifa zilizoainishwa katika miundo ya maendeleo ya utumishi ya kada zilizo chini ya Wizara mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua kuwa baadhi ya fani zinazofundishwa katika vyuo vikuu na vyuo vya elimu ya juu hazijawekewa utaratibu wa ajira kama fani nyingine ambazo wahitimu wake wanaajiriwa katika utumishi wa umma au sekta binafsi. Hivyo, tunaelekeza vyuo kuwasiliana na Serikali mapema kabla ya kuanzisha programu za fani ili kuwezesha utengenezaji wa mifumo ya ajira hizo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, swali la nyongeza.

MHE. SAASHISHA E. MAFUWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, niwashukuru sana wananchi wa Hai, ndugu, rafiki na jamaa na ninyi Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa namna ambavyo mlinisindikiza wakati wa msiba wa mama yetu mpendwa. Sifa na utukufu tunamrudishia Mungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali imekubali kwamba wanachelewesha kuweka kozi hizi kwenye Sekretarieti ya Ajira, je, Serikali iko tayari sasa kuunda chombo maalum kitakachohusisha vyuo vikuu ambavyo vinatengeneza hii mitaala na hizi kozi pamoja na Sekretarieti ya Ajira ili waweze kuthamini mahitaji ya hizi kozi na zile ambazo zinahitajika mtaani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali iko tayari sasa kurekebisha sifa za wahadhiri wa vyuo vikuu ambazo zinawataka ili mhadhiri kufundisha kozi fulani lazima awe amebobea kwa umaalum kwenye kozi hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, mhadhiri anayefundisha *International Relation,* anatakiwa awe amesoma *degree* ya kwanza *International Relation, degree* ya pili na ya tatu, ilhali aliyesoma *Political Science* anaweza kufundisha *International Relation,* jambo linalopelekea vyuo sasa kuanza kufuta kozi. Kwa mfano Chuo cha *UDOM* kimefuta kozi ya *International Relation* kwa sababu wahadhiri wenye sifa hiyo Tanzania hawapatikani. Je, Serikali iko tayari kufanya marejeo ili kozi hizi ziendane na sifa halisi zilizopo kwenye vyuo vyetu?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza mitaala inayoandaliwa na vyuo vikuu siyo kwa ajili ya ajira za Serikali pekee yake. Mitaala hii inaandaliwa kwa ajili ya ajira za Serikali pamoja na *private sector,* pamoja na *international organizations.* Ndiyo maana inaundwa mitaala ambayo inaweza ikakidhi mahitaji ya soko la ajira kwenye Serikali, pia na hizo *private sectors.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ombi la Mheshimiwa Mbunge, kwamba kuwe na chombo maalum kwa ajili ya kushiriki katika kuandaa mitaala; ombi lake tunalichukua. Hata hivyo, kutokana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia pamoja na mahitaji ya kisera, Serikali imeendelea kupitia sifa na miongozo ya miundo ya maendeleo ya utumishi katika kada mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuangalia, kwamba kada zile ambazo zinaandaliwa au zinatolewa katika vyuo vikuu zinaendana na soko la ajira. Sekretarieti ya Ajira inatangaza ajira kulingana na uhitaji wenyewe wa soko, kwamba soko la ajira linahitaji nini? Ndiyo maana Sekretarieti inapotangaza ajira inaangalia miundo ya maendeleo ya kiutumishi katika kada mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye kipengele au swali lake la pili kuhusu kurekebisha sifa za lazima kwa wahadhiri wa vyuo vikuu, vyuo vikuu vimekuwa na miongozo na mifumo

inayojitegemea ambayo inawalazimu kuandaa sifa ambazo zinatakiwa ili kupata mhadhiri, kwamba lazima awe na sifa hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, swali alilouliza Mheshimiwa Mbunge kuhusu *International Relation,* kwamba mhadhiri ili aweze kufundisha *International Relation* awe amesoma *undergraduate,* amesoma *masters* na pia amesoma mpaka *Ph.D;* vyuo vikuu vinafanya hivyo kwa sababu ya kupata wabobezi wanaoweza kufundisha fani hizo katika vyuo vikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo nimwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba suala lake tutalichukua kama Serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu ili tuweze kuliangalia kwa upana wake na kuona umuhimu wake.

MWENYEKITI: Nilikuwa nimemwona Mheshimiwa Asha Feruz, swali dogo la nyongeza.

MHE. ASHA J. FERUZ: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Kwanza ninampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri anayoifanya. Kutokana na majibu ya swali la msingi, kwamba ni kweli vipo vyuo ambavyo vinatoa kozi ambazo hazipo kwenye kada za Sekretarieti, je, ni upi mkakati wa Serikali sasa kuweza kuwa-*accommodate* kwa haraka wale wanafunzi ambao tayari wameshamaliza masomo kwenye hizo kozi ambazo hazipo kwenye kada za Sekretarieti, kwa sababu tayari zilisharuhusiwa kufundishwa kutokea Serikalini, zilipewa kibali?

MWENYEKITI: Nilikuona Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza na mimi nimpongeze Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Pia, niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pole kwa familia ya Mheshimiwa Saashisha Mafuwe kwa msiba mkubwa wa mama yake, Mwenyezi Mungu amhifadhi na aendelee kuwapa faraja familia nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali la nyongeza lililoulizwa na Mheshimiwa Mbunge, ukweli ni kwamba Serikali imekuwa na mawasiliano ya moja kwa moja na vyuo vikuu pale wanapounda kozi au eneo lolote la masomo. Ninataka nitoe mfano ili jibu liwe jepesi. Chuo Kikuu Mzumbe wana kozi inaitwa Maendeleo ya Vijana. Kozi ile inatengeneza maafisa vijana. Kama unavyojua, kwenye Serikali mfumo wetu sisi unazo nafasi kwenye TAMISEMI za maafisa wa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ile kozi walikuwa hawajaingizwa katika muundo. Tunapozungumza sasa hivi, Serikali imeshakamilisha mawasiliano kwanza ndani ya Serikali, na pia kutengeneza muundo ambao vijana wale ambao wamemaliza kozi ile wote wanakwenda kuwa *adopted* katika mfumo wa ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunachokifanya ambacho ameeleza Mheshimiwa Naibu Waziri, ninataka nieleze, ni yaleyale, kwamba msingi mkubwa, vyuo vikuu viwasiliane na Wizara husika kwa maana ya Wizara mama kama Wizara ya Elimu ili sisi ambao tunahusika na kutengeneza miundo ya kazi, tuweze kufanya kazi nzuri ya kuhakikisha kwamba watu wote wanaomaliza vyuo vikuu tunawa-*adopt* katika mfumo wa kazi, waingie katika mfumo wa ajira ili waweze kupata kazi ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninashukuru.

MWENYEKITI: Tunakushukuru Mheshimiwa Waziri na tunakushukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

Sasa tunaendelea na Wizara ya Nishati. Ninamwita Mheshimiwa Nape Moses Nnauye, Mbunge wa Mtama, aweze kuuliza swali lake.

Na. 208

Mpangokazi wa Mwelekeo wa Mradi wa *LNG* - Lindi

MHE. NAPE M. NNAUYE aliuliza: -

Je, Serikali ipo tayari kuweka wazi mpangokazi wa mwelekeo wa mazungumzo juu ya Mradi wa *LNG* - Lindi kwa kuwa umechukua muda mrefu?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa David Silinde.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO K.n.y. WAZIRI WA NISHATI alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Nape Moses Nnauye, Mbunge wa Jimbo la Mtama, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Serikali na wawekezaji wa mradi wa *LNG* wapo katika hatua ya mwisho ya majadiliano hususani kwenye masuala ya kisheria ili kuwezesha usainishaji wa mikataba na makubaliano na hatimaye utekelezaji wa mradi kuanza. Aidha, majadiliano yatakapokamilika, rasimu za mikataba hiyo zitawasilishwa Serikalini kwa ajili ya mapitio na kupata ridhaa kabla ya kusainiwa rasmi ili kuwezesha utekelezaji wa Mradi kuanza mara moja.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Moses Nape Nnauye, maswali ya nyongeza.

MHE. NAPE M. NNAUYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Pamoja na maelezo ya Serikali ya mara kwa mara juu ya mradi huu mkubwa nchini na tukizingatia kuwa wakati Mheshimiwa Waziri wa Nishati anahitimisha bajeti yake hapa wiki iliyopita, aliahidi Bungeni hapa kwamba wiki hii wakuu wa hizi kampuni kubwa ambazo zinawekeza kwenye huu mradi watakuwepo hapa nchini kwa ajili ya kukamilisha mazungumzo ya jambo hili. Ahadi hii imefikia wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kwenye miradi mikubwa kama hii maandalizi ya wananchi na hasa wa *level* ya chini katika kushiriki kwenye hii miradi mara nyingi inakuwa ni jambo ambalo lina changamoto kubwa kama Serikali haitaingiza mkono wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inampango gani wa kufanya maandalizi ya kutosha kwa wananchi hasa wa kawaida na hasa wa maeneo ya Lindi na Mtwara ambako mradi huu unatekelezeka ili kuwaandaa kuzijua na kushiriki fursa zinazotokana na uwekezaji huu mkubwa katika nchi yetu? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO K.n.y. WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Nape Moses Nnauye, Mbunge wa Mtama kwa maswali ya msingi na kulifuatilia jambo hili. Ukweli ni kwamba amekuwa akilipigania hili kutaka lifike mwisho kwa sababu lina manufaa makubwa kwa Taifa, hususan katika Mikoa ya Lindi na Mtwara, nimpongeze sana kwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimthibitishie tu Mheshimiwa Nape kwamba leo tunavyozungumza, Waziri wa Nishati pamoja na timu ya Wizara wanakutana na wawekezaji wa Kimataifa kwa maana ya *IOC's,* wameshawasili hapa nchini. Ninavyozungumza hivi, ni kwamba jioni ya leo utaona picha zitakavyopigwa kwa sababu ni sehemu ya huo mjadala kuhakikisha kwamba wanafanya majadiliano na jambo hili linakwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili kuhusu mpango wa Serikali ni kwamba moja ya mpango wa Serikali kwa sasa ni kuhakikisha; moja, zitatolewa kozi maalum kwenye vyuo vyetu vya *VETA* kwa ajili ya kuwanufaisha wale wananchi ambao kupitia ujuzi watakaoupata watautumia ule ujuzi ili wanufaike na fursa zote zinazotokana na mradi wa *LNG*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kuna *component* ya *local content* ambayo wananchi wa kawaida katika maeneo hayo watanufaika. Kwa hiyo, niseme mradi huu kwa sababu *phase* ya kwanza, ni karibu miaka mitano, lakini wananchi watanufaika zaidi kwa sababu Serikali imejipanga kuhakikisha kila kilichopo hapa nchini wananufaika moja kwa moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa ahsante. Tunaendelea, sasa ninamwita Mheshimiwa Innocent Bashungwa, Mbunge wa Karagwe, aulize swali lake.

Na. 209

Kupeleka Umeme Kwenye Taasisi – Karagwe

MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka Umeme katika Shule za Sekondari, Msingi na Taasisi zote za Wilaya ya Karagwe?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO K.n.y. WAZIRI WA NISHATI alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Innocent Lugha Bashungwa, Mbunge wa Jimbo la Karagwe kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Karagwe jumla ya vitongoji 334 kati ya vitongoji 612 vimepatiwa umeme hadi sasa na Shule za Msingi 109, Shule za Sekondari 37 za vitongoji hivyo zimeunganishiwa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakandarasi wanaendelea na utekelezaji wa mradi wa kupeleka umeme katika vitongoji 61 ambapo kipaumbele ni kufikisha umeme katika taasisi zinazohudumia jamii zikiwemo shule, vituo vya afya, pampu za maji na nyumba za ibada. Aidha, Serikali itaendelea kuziunganishia umeme taasisi katika vitongoji 217 vya Wilaya ya Karagwe vilivyosalia kupitia miradi mbalimbali ya umeme inayotarajia kuanza kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2026/2027.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Innocent Bashungwa maswali ya nyongeza.

MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina swali moja la nyongeza. Mamlaka ya Kayanga na Omurushaka yapo maeneo ambayo pamoja na kuwa kwenye Mamlaka ya Mji, kiuhalisia ni vijijini na maeneo haya gharama za kufunga umeme ni shilingi 320,000 kama mwananchi anafunga umeme kutoka kwa jirani, yaani bila nguzo. Kwa hiyo, shilingi 320,000 waya pamoja na mita, lakini akilazimika kulipia gharama ya nguzo pamoja na mita ni shilingi 515,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe tu mfano, kwa Kata ya Ihanda maeneo kwa mfano Kantikimo, Chamezi, Katunguru, Ruswa, Nyakakiri, Omukagera, na hata Kata ya Bugene maeneo ya Bujuruga *Centre* ya Ibombo, Ruzinga eneo la Mkiziku hata Kayanga maeneo ya Miti wananchi wanalipa gharama kubwa. Swali langu, je, Serikali ipo tayari kufunga umeme kwa gharama ya shilingi 27,000 kama maeneo mengine ya vijijini? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO K.n.y. WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nami pia nimpongeze vile vile Mheshimiwa Innocent Lugha Bashungwa, Mbunge wa Karagwe kwa swali zuri la msingi ambalo lina maslahi makubwa kwa wananchi wake lakini ni kwa Taifa zima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimthibitishie tu jambo moja, wiki iliyopita Waziri wa Nishati, Komredi Deo Ndejembi akiwa kwenye *podium* hii alishatolea maelekezo kwamba moja ya mpango wa Serikali ni mpango ule ambao unahusisha maeneo ya miji, lakini yana vijiji *(Peri-urban plans)* na katika ule mradi Mheshimiwa Waziri hapa alishasema wameuchukua na aliwataka *REA* pamoja na *TANESCO* kukaa pamoja na kuainisha yale maeneo ambayo yako ndani ya miji lakini yana vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, yeye mwenyewe Mheshimiwa Waziri amenithibitisha niwaambie Waheshimiwa Wabunge, hivi karibuni watu wa *REA* wataanza kuwapigia wananchi pamoja na Waheshimiwa Wabunge na watu wa

TANESCO kwa jambo moja tu la kuainisha yale maeneo ili yaweze kufanyiwa tathmini na yaweze kuingizwa katika mpango wa utekelezaji kuanzia mwaka huu fedha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa ahsante, tunakushukuru kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, sasa ninamwita Mheshimiwa Kassimu Amari Mbaraka, Mbunge wa Tanga Mjini aweze kuuliza swali lake.

Na. 210

Ujenzi wa Barabara ya Kiomoni - Pande - Mjesani Hadi Muheza – Tanga

MHE. KASSIMU A. MBARAKA aliuliza: -

Je, lini ujenzi wa Barabara ya Kiomoni, Pande, Mjesani hadi Muheza inayounganisha Wilaya ya Tanga na Muheza utaanza?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Kassimu Amari Mbaraka, Mbunge wa Tanga Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Kiomoni, Pande, Mjesani ni sehemu ya barabara ya Mkoa ya Mlingano – Mjesani - Pande hadi Kiomoni yenye urefu wa kilometa 39.5 na inahudumiwa na Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)*. Kazi ya upembuzi yakinifu na Usanifu wa Kina wa barabara hii kwa ajili ya ujenzi wa kiwango cha lami inaendelea na inatarajiwa kukamilika mwezi Machi, 2027. Baada ya usanifu kukamilika na gharama za ujenzi kujulikana, Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kassimu Amari Mbaraka swali la nyongeza.

MHE. KASSIMU A. MBARAKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani. Nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, kwa kuwa kuna miradi mikubwa miwili ya shughuli za kiuchumi eneo la Chongoleani pamoja na eneo la Gombero pale ule mradi wa Chuo Kikuu *Campus* ya Mzumbe, je, ni lini sasa nayo Barabara ya Mabokweni kuelekea mpaka *Old* Korogwe Kwamndolwa nayo itakamilika kwa kiwango cha lami?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Je, Serikali ina mpango gani wa kibajeti wa kuhakikisha kwamba kilometa 15 za kutoka Tanga mpaka Kirare kwenye Barabara ya Pangani zinaenda kukamilika ndani ya mwaka huu wa 2026?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Mabokweni kwenda Kwamndolwa inajengwa kwa vipande viwili kuanzia Mabokweni kwenda Bombo Mtoni; tuna kilometa 10 ambayo tutaishia pale Maramba, na pia huku Kwamndolwa tutaanza kilometa 10 na tuko kwenye hatua za mwisho za manunuzi ili wakandarasi waweze kuanza pande zote mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo ni kuijenga barabara yote kwa kiwango cha lami kadiri fedha inavyoendelea, na hata katika bajeti inayokuja tutaendelea kutengea fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya pili kama nimemsikia vizuri, nadhani ni ya Tanga - Pangani sijui kama nimemsikia vizuri ili niweze kumjibu vizuri.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbaraka.

MHE. KASSIMU A. MBARAKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani. Ninauliza kuhusiana na barabara ya Tanga - Pangani kuna kilometa 15 za kutoka Tanga Mjini mpaka Kirare pale

ambayo inaungana na eneo la Tundaua ambayo tayari kuna lami...

MWENYEKITI: Sasa Mheshimiwa hayo ni maswali karibia matatu.

MHE. KASSIMU A. MBARAKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, swali ni moja tu!

MWENYEKITI: Hebu uliza swali moja Mheshimiwa Naibu Waziri akusikie vizuri.

MHE. KASSIMU A. MBARAKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mpango gani wa kibajeti wa kukamilisha kipande cha barabara kilometa 15 kutoka Tanga mpaka Kirare? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Barabara ya Tanga - Pangani yenye urefu wa kilometa 50 ipo kwenye utekelezaji na tuko takribani 50%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipande hiki cha Tanga hadi Kirare kwanza kilichelewa kwa sababu hilo eneo lilikuwa lina miundombinu ambayo ilikuwa hatuwezi kuanza, kwa hiyo, tulilazimika kwenda kuanzia Kirare kwenda Pangani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishe Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa kuwa karibu miundombinu yote imeondolewa, na sasa mkandarasi yupo, tunategemea tutakapokuwa tumemlipa fedha, ataendelea na hiyo kazi ili aweze kuikamilisha ambayo pia Meneja wa Mkoa tumeshamwelekeza, kwa sababu pia barabara hiyo tulipata taarifa kwamba kutokana na hali ya mvua imeharibika sana, kwanza aweze kuhakikisha mkandarasi anaitengeneza, na baada ya hapo, basi aweze kurudi ili kuijenga hiyo barabara yote kwa kiwango cha lami, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa ahsante. Tunaendelea, na sasa ninamwita Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma, Mbunge wa Viti

Maalum aweze kuuliza swali lake. Mheshimiwa Husna Sekiboko kwa niaba ya Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma.

Na. 211

Ujenzi wa Barabara ya Mlandizi – *Ruvu Station (SGR)*

MHE. HUSNA J. SEKIBOKO K.n.y. MHE. HAWA M. CHAKOMA aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya kilometa 23 kutoka Mlandizi hadi *Ruvu Station (SGR)* kwa kiwango cha lami?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Mlandizi hadi Stesheni ya *SGR* kilometa 23 inaunganisha barabara ya Morogoro *(TANZAM)* katika eneo la Mlandizi na Reli ya *SGR* katika Stesheni ya Ruvu. Kwa kutambua umuhimu wa barabara hii, tayari Serikali imesaini mkataba na Mkandarasi wa ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara hiyo, na kwa sasa, Serikali inaendelea na taratibu za malipo ya awali ili kumwezesha Mkandarasi kuanza kazi za ujenzi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Husna Sekiboko maswali ya nyongeza.

MHE. HUSNA J. SEKIBOKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii inaungana na Barabara ya Tanga – Segera - Dar es Salaam na Barabara ya Dar es Salaam – Segera – Moshi - Arusha ambayo kwa sasa imezidiwa na magari mengi hasa malori kutoka Bandari ya Tanga. Je, ni upi mkakati wa upanuzi wa barabara hii pamoja na barabara ambayo Mheshimiwa Hawa ameuliza?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba hizi barabara nyingi zimechoka, lakini pia zimekuwa finyu. Mkakati ambao tunao, kwanza kuanzia Mlandizi hadi Chalinze ni kuweka *expressway* ambazo zitakuwa ni njia nne, lakini kuanzia Mlandizi kwenda Segera tulishafanya usanifu ili kuweza kuongeza upana wa hiyo barabara na kuweza kwenda na upana wa barabara ambazo sasa hivi zinajengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua ni barabara ambayo imejengwa muda mrefu, na kwa kweli ni finyu hasa kulingana na kazi kubwa ambayo imefanyika kuipanua Bandari ya Tanga na kuongeza mizigo na kufanya magari yawe mengi. Kwa hiyo, tuko na mpango wa kuweza kuipanua hiyo barabara.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Sasa ninamwita Mheshimiwa Edibily Kazala Kinyoma, Mbunge wa Kasulu Vijijini, aweze kuuliza swali lake.

Na. 212

Changamoto ya Mawasiliano – Kasulu Vijijini

MHE. EDIBILY K. KINYOMA aliuliza: -

Je, lini Serikali itamaliza changamoto ya Mawasiliano kwa kujenga Minara Kata za Heru Ushingo, Kagerankanda na Asante Nyerere - Kasulu Vijijini?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Edibily Kazala Kinyoma, Mbunge wa Jimbo la Kasulu Vijijini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote – *UCSAF* ilikamilisha ujenzi wa Mnara Mwaka 2014 kupitia Kampuni ya Honora au *(Yas Tanzania)* kwa ajili ya kuhudumia Vijiji vya Seruhemebe na Heru vilivyopo katika Kata ya Heru Ushingo. Aidha, katika Kata za Kagerankanda, *UCSAF* ilijenga Mnara mwaka 2021 katika Kijiji cha Mvinza kupitia Shirika la Mawasiliano Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, katika Kata ya Asante Nyerere, *UCSAF* ilikamilisha ujenzi wa mnara mwaka 2025 kupitia Kampuni ya *Vodacom Tanzania* katika Kijiji cha Sogeeni Kwiliba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada nilizozitaja awali, Serikali kupitia *UCSAF* itatuma wataalamu kwenda Kasulu Vijijini katika Kata husika kufanya tathmini ili kujua mahitaji halisi na hatimaye kuviingiza vijiji vyote vyenye changamoto ya mawasiliano katika miradi itakayotekelezwa na *UCSAF* hususan katika Mpango Mkakati wa Ujenzi wa Minara wa Mwaka 2025 – 2030.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Edibily Kazala Kinyoma maswali ya nyongeza.

MHE. EDIBILY K. KINYOMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nishukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, na pia nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa timu ambayo ameshatuma tayari iko *field* inafanya kazi yake na wameungana na Makatibu wa Mbunge wanafanya kazi nzuri sana. Ninawashukuru sana. Sina swali la nyongeza. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Tunakushukuru. Mheshimiwa Naibu Waziri pia tunakushukuru kwa majibu.

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ya muda tunaendelea, na sasa yatakuwa ni maswali ya msingi tu, hatutakuwa na maswali ya nyongeza.

Tunakwenda Wizara ya Fedha, ninamwita Mheshimiwa Dickson Lutevele, Mbunge wa Mafinga aweze kuuliza swali lake. Kwa niaba Mheshimiwa Timida Mpoki Fyandomo.

Na. 213

Kuondoa Kodi ya 30% Kwenye *Export* ya Mazao ya Misitu

MHE. TIMIDA M. FYANDOMO K.n.y. MHE. DICKSON N. LUTEVELE aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuondoa Kodi ya 30% katika *export* ya Mazao ya Misitu ambayo imeua kabisa Viwanda?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Fedha, majibu.

WAZIRI WA FEDHA alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya marekebisho ya Sheria, kulikuwa na usafirishaji mkubwa wa mazao ya misitu nje ya nchi yasiyochakatwa au yaliyochakatwa kidogo na ni mfano wa magogo na *Veneer sheets*. Hivyo, mwaka 2025 Serikali ilifanya marekebisho kwenye Sheria ya Usafirishaji wa Bidhaa Nje ya Nchi, Sura 196 ili kutoza ushuru kwa kiwango cha 30% au shilingi 150 kutegemeana na kiwango kitakachokuwa kikubwa kwa kila kilo moja ya vinia inayotambulika kwa *Tariff Heading* 44.08 inayosafirishwa kwenda nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilifanya marekebisho hayo ili kulinda viwanda vya ndani katika kuhakikisha upatikanaji wa malighafi za viwanda vyetu vya ndani vinavyotengeneza bidhaa za mbao ikiwemo *plywood* na *marine board*. Pamoja na marekebisho hayo, Serikali pia ilifanya marekebisho kwa kuongeza ushuru wa forodha kwa *marine board* zinazoingizwa

nchini kutoka 25% hadi 35% ili kuviongezea viwanda vyetu vya ndani ushindani dhidi ya bidhaa zinazoagizwa kutoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Serikali imepokea changamoto aliyoieleza Mheshimiwa Mbunge kuwa hatua hii imeathiri baadhi ya Viwanda. Viwanda vinavyoweza kuathirika ni vile vinavyochakata mazao ya misitu bila kufikia hatua za mwisho za uzalishaji wa bidhaa za misitu kwa matumizi yaliyokusudiwa. Hivyo, Serikali inaendelea kujielekeza kwenye kutafuta suluhu ambayo haitaleta athari hasi kwenye sekta hii ndogo kutokana na hatua zinazochukuliwa ili kuilinda sekta hii muhimu katika uchumi wetu, na pia kwa kuhakikisha kuwa kuna uongezaji thamani wa mazao ya misitu kabla ya kuuzwa nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kufanya tathmini ya kina kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii na Wizara ya Fedha ili kuona namna ya kurekebisha kodi hii pale itakapothibitika kuwa inazuia ukuaji wa viwanda badala ya kuvilinda, ili kuhakikisha mnyororo wa thamani wa misitu unamnufaisha mwekezaji na Taifa kwa ujumla.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Timida Mpoki, swali la nyongeza.

MHE. TIMIDA M. FYANDOMO: Mheshimiwa Mwenyekiti nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Tangu kuanzishwa kwa kodi hii, idadi ya kontena za vinea ambazo zimekuwa zikisafirishwa zimepungua kutoka kontena 3,765 mpaka kontena 2,110 mwaka 2026 hadi mwezi huu Machi. Je, Serikali imefanya tathmini ya kulinganisha mapato inayopata kupitia kodi hii dhidi ya ajira zilizopotea kwenye viwanda vya misitu?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba kunakuwa kuna haja ya kufanya tathmini kwenye athari ambazo zimetokeza kutokana na hatua hizi. Hata hivyo, kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi, dhamira moja ya hatua hii ilikuwa ni kupunguza usafirishaji

nje ya nchi. Kwa hiyo, kutokana na alichokisema Mheshimiwa Mbunge, inaonekana kweli upande mmoja tumefanikiwa, lakini upande wa pili tunahitaji kufanya tathmini kuona sasa zile faida ambazo zilitarajiwa kama zimepatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kama ambavyo imesemwa hatua hii ilianza kutekelezwa mwezi Julai, 2025, vipindi ni vifupi kufanya tathmini. Tunalipokea na kwamba tutafanya tathmini kama nilivyosema awali, sisi kwa ushirikiano na Wizara ya Utalii na Maliasili.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Waziri kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea, sasa ni Wizara ya Kilimo. Ninamwita Mheshimiwa Esther Edwin Malleko, Mbunge wa Viti Maalum, aweze kuuliza swali lake."

Na. 214

Kuongeza Skimu za Umwagiliaji – Kilimanjaro

MHE. ESTHER E. MALLEKO aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza skimu za umwagiliaji katika Mkoa wa Kilimanjaro?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Esther Edwin Maleko, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuchukua jitihada mbalimbali za kuendeleza sekta ya umwagiliaji nchini ikiwemo katika Mkoa wa Kilimanjaro. Katika kutekeleza hilo, mwaka 2025/2026, miradi 42 ya umwagiliaji inatekelezwa katika

Mkoa wa Kilimanjaro ikijumuisha ujenzi na ukarabati wa skimu 15 zenye jumla ya hekta 18,154.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya skimu hizo, skimu nane ni za ujenzi zenye jumla ya hekta 9,514 ambapo utekelazaji wake umefikia wastani wa 28%. Aidha, miradi ya ukarabati ni saba ambapo utekelezaji wake umefikia wastani wa 45%. Kukamilika kwa ujenzi na ukarabati wa miradi hiyo kutawezesha kumwagilia eneo lenye ukubwa wa hekta 18,154 na kunufaisha wakulima 283,877.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Serikali imekamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa miradi ikiwemo Bonde la Mtambo lenye miradi ya Kikavu chini, Mapacha, Mtambo, Ismail na Ngosero (Mpenda Roho na Longoi) yenye jumla ya hekta 8,500. Aidha, miradi 18 ya skimu zenye zaidi ya hekta 29,000 usanifu wake unaendelea.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Esther Malleko, maswali ya nyongeza.

MHE. ESTHER E. MALLEKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa baadhi ya miradi iko kwenye wastani wa 28% na 45%, je, ni upi mkakati wa Serikali sasa kuhakikisha miradi hii inatekelezwa kwa kasi ili wananchi waweze kufaidika mapema?

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Esther Maleko kwa swali zuri la msingi na kufuatilia wananchi wake wa mkoa mzima wa Kilimanjaro. Jambo moja ambalo ninaweza nikamthibitishia kwa 100% ni kwamba miradi hii itakamilika kama ambavyo imepangwa. Kwa kuwa Wizara ya Fedha, sasa hivi ilishaweka *commitment* ya kuipatia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kila mwezi shilingi bilioni 25 zitakazokwenda kwenye miradi ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, fedha hizo zitasaidia kusukuma hii miradi iweze kukamilika kwa wakati kwa sababu tutawalipa kwa wakati, na sisi tutawasimamia kuhakikisha miradi hii inaenda kwa kasi. Kwa hiyo, nimwondoe shaka Mheshimiwa Mbunge kwamba na sisi tuko katika *area of comfort* kwamba miradi hii inakwenda kukamilika, ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa. Tunaendelea, na sasa ninamwita Mheshimiwa Zuberi Yahya Mfaume, Mbunge wa Morogoro Kusini, aweze kuuliza swali lake.

Na. 215

Malipo ya Wakulima wa Zao la Ufuta Morogoro Kusini

MHE. ZUBERI Y. MFAUME aliuliza:-

Je, lini wakulima wa ufuta wa Kisaki, Mvuha, Mngazi, Bwakila chini na Selembala waliouza kwa Mfumo wa Stakabadhi Ghalani watalipwa?

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zuberi Yahya Mfaume, Mbunge wa Jimbo la Morogoro Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika msimu wa mwaka 2024/2025, wakulima wa ufuta katika Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro waliuza jumla ya tani 3,984 zenye thamani ya shilingi bilioni 9.841 kupitia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala na minada ya kidijiti. Kati ya kiasi hicho, madai ya shilingi bilioni 8.469 yalilipwa kwa wakulima kupitia mfumo huo na shilingi bilioni 1.372 hazikulipwa kwa wakati kutokana na dosari mbalimbali katika mifumo ya malipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufikia mwezi Oktoba, 2025, madai yote ya wakulima waliouza ufuta kupitia mfumo huo yalilipwa kikamilifu katika maeneo ya Mngazi, Selembala, Bwakila Chini, Kisaki na Mvuha. Mfumo huo umeendelea kuongeza uwazi, kuondoa ucheleweshaji wa malipo na kuhakikisha wakulima wanapata stahiki zao kwa wakati. Aidha, Serikali inatoa wito endapo kuna Mkulima ana changamoto katika malipo yake, awasilishe madai yake ili yaweze kupatiwa ufumbuzi kwa mujibu wa taratibu zilizopo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Zuberi Mfaume, maswali ya nyongeza.

MHE. ZUBERI Y. MFAUME: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri, lakini ninakushukuru kwa kukiri kwamba kulikuwa na malipo ambayo yalichelewa. Kwa kweli tuna changamoto kubwa kwa vyama vya ushirika vya msingi katika kushughulikia uuzaji wa nafaka hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini Serikali itarasimisha mfumo mbadala na mfumo shindanishi ambao utaleta tija kwa wakulima? La pili, Morogoro Kusini tumekuwa wazalishaji wa ufuta ambao una daraja la juu. Kuna changamoto kubwa ya vifaa vya kilimo pamoja na pembejeo. Ni lini sasa Wizara itapeleka vituo vya ukodishaji matrekta pamoja na kusambaza pembejeo ili kuwawezesha wakulima kuzalisha kwa wingi zaidi? Ahsante.

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza tena Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Morogoro Kusini, Mheshimiwa Mfaume kwa kufuatilia sana wananchi wake mara kwa mara. Nimwondoe shaka tu kwamba, moja, Serikali ipo karibu sana na kuwasikiliza wananchi kero zao zinapokuwa zinatatuliwa, ndiyo maana katika wiki mbili zilizopita, nilijibu swali la namna hii hapa Bungeni, watu wakiomba tupitie mfumo ili kurekebisha ule upungufu. Kwa hiyo, Serikali tuko tayari kupitia, sisi pamoja na wadau na kuainisha yale maeneo yenye upungufu ili tuweze kuongeza ufanisi katika mifumo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sisi kama Serikali tuko tayari muda wowote kufanya kazi pamoja ili tuweze kutengeneza mfumo mbadala na shindanishi ambao unaweza kuwasaidia wananchi hao. Kuhusu ni lini tutapeleka matrekta huko na pembejeo, mpango wa Serikali ni kuanzisha vituo vya zana za kilimo katika halmashauri zote nchini. Lengo la Serikali ni kuanzisha vituo 1000, na mpaka sasa hivi tumeshafungua vituo 79 katika halmashauri kama 25 hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mpango huu ni endelevu, na katika mipango inayokuja, Jimbo la Morogoro Kusini lipo katika mpango huo, ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante. Nilimwona Mheshimiwa Eric Shigongo.

MHE. ERIC J. SHIGONGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kuniona. Katika historia ya nchi yetu, awamu pekee iliyojenga skimu nyingi za umwagiliaji, ni Awamu ya Sita. Kule kwetu Buchosa zimejengwa skimu za Mwigulukenda, Sukuma. Je, Serikali ina mpango gani kujenga skimu nyingine za umwagiliaji katika mabonde ya Bupandwa, Buchiri na Iseni?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimthibitishie tu Mheshimiwa Shigongo kwamba, maelekezo ya Serikali ambayo Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu alishayatoa, ni kwamba Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ifanye upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwenye mabonde yote nchini. Kazi hiyo inaendelea, ikiwemo maeneo haya ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyaainisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la Serikali ni kupata gharama halisi, na baada ya hapo tuweze kutangaza na kupata wakandarasi ambao watatekeleza kazi hiyo. Kwa hiyo, kwa sasa tuko katika hatua ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina, na baada ya hapo sasa tutakwenda katika hatua inayofuatia, ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

Sasa tunaendelea, Wizara ya Uchukuzi. Namwita Mheshimiwa Kiza Hussein Mayeye, Mbunge wa Kigoma Kaskazini aweze kuuliza swali lake.

Na. 216

Manufaa ya Mkataba wa Uendeshaji wa Bandari ya Kigoma

MHE. KIZA H. MAYEYE aliuliza:-

Je, wananchi wa Kigoma watanufaikaje na Mkataba baina ya Mamlaka ya Bandari Tanzania na Kampuni ya Zijin ya China kuendesha Bandari ya Kigoma?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uchukuzi.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi, Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa Mnyaa, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Kiza Hussein Mayeye, Mbunge wa Kigoma Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia *TPA* inaendelea na mpango wa maboresho ya Bandari ya Kigoma ili kunufaika na fursa za Tanzania kuwa lango la biashara katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati hususan Mashariki mwa nchi ya *DRC* kwani, Bandari ya Kigoma ni kiungo muhimu katika Ushoroba wa Kati kuelekea Bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutimiza azma hiyo, Serikali kupitia *TPA* waliingia makubaliano na Kampuni ya *Zijin International Mining PTE Limited* ambaye kwa Tanzania anatambulika kama *Gold Marine Tanzania Limited* ili kuboresha Bandari ya Kigoma na gati la "*Malindi Wharf*" katika Bandari ya Dar es Salaam. Mawanda ya makubaliano baina ya *TPA* na Mwekezaji

yanajumuisha usanifu na kugharamia maboresho ya miundombinu, usimikaji wa mifumo ya kisasa, ununuzi wa vitendea kazi na uendeshaji. Aidha, *TPA* ataendelea kutoa huduma kwa meli na huduma nyingine zilizoainishwa kwenye makubaliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla, wananchi wa Kigoma na nchi watanufaika kwa namna mbalimbali ikiwemo kuongeza mtaji wa uwekezaji nchini; kupitia uwekezaji huo, kutaongeza ufanisi wa utoaji wa huduma katika bandari hiyo, na hivyo kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi katika Mkoa huo na Ziwa Tanganyika kwa ujumla; kupatikana kwa mapato yatokanayo na ada ya uendeshaji na upangishaji; kujenga uwezo wa Watanzania kuwa na ujuzi stahiki; kuongeza ajira kwa Watanzania; kuongeza upatikanaji wa shehena mpya hususan kutoka Mashariki mwa *DRC;* ushiriki wa kampuni za ndani; na kuchochea ukuaji wa sekta nyingine za uchumi, kama vile kilimo, uvuvi na viwanda.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kiza Mayeye, maswali ya nyongeza.

MHE. KIZA H. MAYEYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, uendeshaji wa Bandari ya Kigoma unakwenda sambamba na uwekezaji wa meli, hasa meli za mizigo ambazo zingeweza kwenda *Congo DRC* katika mgodi mkubwa sana wa madini ya lithiamu, pale Manono katika Jimbo la Tanganyika. Sasa ni miaka mitatu Serikali imesaini mkataba wa ujenzi wa meli ya mizigo, hakuna ambacho kinaendelea. Serikali haioni inawakosea watu wa Kigoma kwa kuwakosesha fursa na mapato? Ni lini mradi huu utakamilika ili tuweze kupata meli hizo za mizigo?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninampongeza Mheshimiwa Mbunge wa Kigoma Kaskazini, Mheshimiwa Kiza Mayeye kwa namna anavyoungana na Wabunge wote wa Chama cha Mapinduzi katika mkoa huo, na Tanzania kwa ujumla, katika kufuatilia kwa karibu miradi ya kimkakati katika Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Sita, chini ya Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan inatambua umuhimu na umadhubuti wa Ziwa Tanganyika kwa uchumi wa nchi yetu na kwa uchumi wa wananchi wa Kigoma. Ndiyo maana kwa mara ya kwanza tunaona uwekezaji mkubwa unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niseme kwa ufupi kidogo. sote tunakubaliana katika maji yote ambayo yapo duniani, Ziwa Tanganyika linakuwa namba mbili likiwa na ukubwa wa kilomita za mraba 32,900 na takribani upana wa karibu kilomita 50. Hata hivyo, ziwa hili ndiyo la pili duniani kwa kuwa na kina kirefu zaidi kwa maziwa yenye maji masafi; pia, kama nchi tuna karibu 41% ya ziwa lote, na wengine wanabaki na sehemu inayobaki. Hivyo, inaturahisishia kupeleka bidhaa au vitu mbalimbali kwenye nchi ya Congo, Burundi pamoja na Zambia na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hivi ninavyozungumza mpaka kufika mwaka 2020 Ziwa Tanganyika, meli karibu zote zitakuwa zimelala. Nini Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanya? La kwanza kabisa, amesaini mikataba ya uboreshaji wa bandari, uboreshaji wa meli. Meli ya kwanza ni MV Liemba ambayo Mheshimiwa Mbunge mwenyewe mara kadhaa alizungumza hapa na tumekwenda wote kuitembelea, ipo karibu 64%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, MV Sangara, hii ni meli kwa ajili ya kubeba mafuta, tayari imeshaanza kufanya kazi. Tatu ni MV Mwongozo, hii tumeshasaini mkataba, tunachosubiri kwa sasa hivi ni kulipwa fedha ili kazi ianze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyozungumza kuhusu meli ya mizigo, inayobeba tani 3,500, Serikali imeshasaini mkataba, na nimhakikishie, inakamilisha taratibu za ndani za kulipa fedha. Fedha zikipatikana, atalipwa mkandarasi ili kuanza ujenzi kama ambavyo miradi mingine imeshaanza.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Maji. Sasa ninamwita Mheshimiwa *Engineer* Fadhili Sandali Chilombe, Mbunge wa Tunduru Kusini, aweze kuuliza swali lake.

Na. 217

Ujenzi wa Miundombinu ya Maji Safi na Salama - Tunduru Kusini

MHE. ENG. FADHILI S. CHILOMBE aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Miradi ya Maji katika Jimbo la Tunduru Kusini?

MWENYEKITI: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mhandisi Fadhili Sandali Chilombe, Mbunge wa Jimbo la Tunduru Kusini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na utekelezaji wa jumla ya miradi ya maji sita yenye thamani ya jumla ya shilingi bilioni 7.8 katika Wilaya ya Tunduru ikiwemo Jimbo la Tunduru Kusini mkoani Ruvuma. Baadhi ya miradi hiyo ni pamoja na mradi wa Tuwemacho, Masuguru - Mchoteka Awamu I, Misechela - Liwanga, Msinjili na Azimio.

Zijin ya China Miradi hiyo inajumuisha ujenzi wa vyanzo vya maji, ujenzi wa matanki manne yenye ujazo wa lita 750,000, ulazaji wa mabomba umbali wa kilometa 74.1 sanjari na ujenzi wa vituo 25 vya kuchotea maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeshalipa jumla ya shilingi bilioni 2.9 kwa miradi hiyo ambapo ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji na inatarajiwa kukamilika ndani ya mwaka wa fedha 2026/2027 kulingana na upatikanaji wa fedha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mhandisi Fadhili Chilombe, maswali ya nyongeza.

MHE. ENG. FADHILI S. CHILOMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Msingi wa swali hili umetokana na hayo majibu yaliyotolewa kwamba kuna miradi inaendelea, na vijiji vilivyotajwa ni Mchoteka, Masuguru, Azimio, Misechela pamoja na Tuwemacho imekuwa ni miradi ya muda mrefu ambayo ilikuwa haikamiliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, ninayo furaha kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba tumekaa na viongozi hawa, kwa maana ya Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri tulijadili juu ya jambo hili, tumefikia mwafaka, tumepata matumaini. Kwa maana hiyo sina swali la nyongeza, Mheshimiwa Waziri.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge tunaomba mpunguze kidogo sauti ili Mheshimiwa aweze kusikika vizuri. Mheshimiwa *Engineer* tunaomba urudie maswali yako.

MHE. ENG. FADHILI S. CHILOMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Msingi wa swali nililouliza ulitokana na majibu mazuri yaliyotolewa na Naibu Waziri kwamba kuna Vijiji vya Tuwemacho, Misechela, Masuguru na Azimio vyenye miradi ambayo ilianzishwa muda mrefu na haijakamilika kwa muda huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, ninaishukuru Serikali, jana nilikaa na Mheshimiwa Naibu Waziri tukajadiliana vizuri sana na imetolewa *statement of hope* inayoonesha kwamba ndani ya kipindi kifupi miradi hiyo inakwenda kukamilika, hasa kuanzia ule Mradi wa Tuwemacho pamoja na Mradi wa Masuguru - Nchoteka. Kwa maana hiyo, ninaishukuru Serikali na ninamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuchagua viongozi hawa…

MWENYEKITI: Swali Mheshimiwa.

MHE. ENG. FADHILI S. CHILOMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sina swali la nyongeza. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa, maoni yako yamepokelewa na Naibu Waziri. Ninampa nafasi Mheshimiwa Azza Hilal aweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

MHE. AZZA H. HAMAD: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Je, ni lini Serikali itakwenda kukamilisha awamu ya pili ya ujenzi wa Mradi wa Maji wa Masengwa katika vijiji vya Ibingo, Isela, Bubale, Ng'wang'halanga na Ishinabulandi?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana dada yangu, Mheshimiwa Azza, kwa kuendelea kuwasemea vyema kabisa wananchi na kwa kuendelea kufuatilia utekelezaji wa miradi ndani ya jimbo lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali tumejipanga na tutakwenda kuhakikisha miradi yote inakamilishwa, lakini jambo la kukubaliana ni kwamba tunayo miradi mingi, ni lazima tuwalipe wakandarasi awamu kwa awamu na utekelezaji wa miradi uende awamu kwa awamu kulingana na vipaumbele. Ninamhakikishia Mheshimiwa Azza, mradi wake awamu ya pili tunakwenda kuupatia kipaumbele kwa ajili ya kuutekeleza mara moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nilikuona Mheshimiwa Josephine Chagula, Mbunge wa Viti Maalum.

MHE. JOSEPHINE T. CHAGULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona ili niulize swali langu la nyongeza. Je, ni lini Serikali itamaliza tatizo la maji katika Wilaya ya Nyang'hwale? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Josephine, ninaomba uulize tena swali lako.

MHE. JOSEPHINE T. CHAGULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona ili niulize swali la nyongeza. Je, ni lini Serikali itamaliza tatizo la maji katika Wilaya ya Nyang'hwale? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Umemsikia Mheshimiwa Naibu Waziri? Wilaya ya Nyang'hwale.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kutoka Mkoa wa Geita. Ninapenda kumpongeza kwa kazi nzuri sana ambayo anaendelea kuifanya na kuwasemea wananchi wa mkoa mzima wakiwemo wananchi wa Wilaya ya Nyang'hwale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo miradi mingi inayoendelea ndani ya Jimbo la Nyang'hwale na ipo katika hatua nzuri. Pia, mpaka sasa upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama ni wa kuridhisha sana ndani ya jimbo hilo. Bahati nzuri mimi nimeshafanya ziara pale nikajionea na tukasimamia utekelezaji wa miradi iliyokuwa inaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna miradi ambayo tayari imeshakamilika na kuna miradi ambayo inahitaji kumaliziwa kwa kupelekewa fedha tu. Ikishakamilika, basi upatikanaji wa huduma ya maji utakuwa zaidi ya 85%. Ninakushukuru sana.

MWENYEKITI: Nilikuona Mheshimiwa Amina Mkumba.

MHE. AMINA M. MKUMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuuliza swali la nyongeza. Je, ni lini Serikali itatenga bajeti ili kuanzisha miradi katika Jimbo la Kibiti katika maeneo ya Visiwani ambapo kuna kata nne: Kata ya Kiongoroni, Mbuchi, Maparoni na Msala? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nijue ni jimbo au wilaya gani, kwani ni kata tu amezitaja.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Amina, ninaomba uulize swali lako tena, lakini tunaomba Waheshimiwa Wabunge tupunguze sauti ili tuweze kusikilizana.

MHE. AMINA M. MKUMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Swali langu linauliza, ni lini Serikali itaanzisha miradi katika Jimbo la Kibiti, maeneo ya Visiwani ambapo kuna Kata nne za Msala, Maparoni, Kiongoroni na Mbuchi?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa Serikali ni kuhakikisha kwamba tunaendelea kutekeleza miradi yote na kuikamilisha ili iweze kutoa matokeo kwa wananchi. Pia, ni dhamira ya Serikali ya CCM ambapo falsafa ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ni kumtua mama ndoo kichwani. Hapo ni Sera yetu ya Maji ya Mwaka 2002 ambapo toleo la mwaka 2025 linatutaka kuhakikisha kwamba maji yawe siyo zaidi ya meta 400.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, dhamira hiyo hiyo inatusukuma kuhakikisha kwamba tunaweka msukumo kwenye kupeleka fedha ili miradi mbalimbali iendelee kutekelezwa ikiwemo na miradi ambayo Mheshimiwa Mbunge ameiongelea, Tutakwenda kuipatia msukumo mkubwa ili iweze kutekelezwa na kukamilika na kutoa matokeo na wananchi ambao wamemtuma kuwasemea ili sauti yako iweze kutambulika kwa matokeo zaidi ambayo yatakuwa yametokea katika jimbo lake. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Tunakushukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali na majibu. Sasa, ninaomba niwaletee matangazo ya wageni tulionao siku hii ya leo.

Kwanza, tunaanza na wageni waliokaa Jukwaa Kuu la Spika ambao ni wageni wawili kutoka Bunge la Ghana nao ni Ndugu Camillo Pwamang, Naibu Katibu wa Bunge anayesimamia

Huduma za Usimamizi wa Bunge. Pia, tuna Ndugu Peter Binipom, Mwandishi wa Taarifa Rasmi za Bunge. *(Makofi)*

Tunao wageni wa Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Daniel Godfrey Chongolo ambao ni Ndugu Gerald Mweli, Katibu Mkuu; Ndugu Athuman Kilundumya, Naibu Katibu Mkuu; Prof. Peter Msoffe, Naibu Katibu Mkuu; Mheshimiwa Nurdin Babu, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro; Ndugu Mwajuma Nasombe, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Moshi; na *Capt*. Mstaafu John Chiligati, Mwenyekiti wa Bodi ya Kampuni ya Mbolea *(ITRACOM)*. *(Makofi)*

Vilevile, tunaye Ndugu Filbert Mponzi, Mwenyekiti wa Bodi ya Sukari Tanzania na Afisa Mkuu wa Biashara Benki ya *NMB;* Prof. Sifuni Mchome, Mwenyekiti wa Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko; Prof. Aurelia Kamuzora, Mwenyekiti wa Bodi ya Kahawa; Brigadia Mstaafu Aloyce Mwanjile, Mwenyekiti Bodi ya Korosho; Ndugu Victor Mwambalaswa, Mwenyekiti wa Bodi ya Tumbaku; na Dkt. Richard Masika, Mwenyekiti wa Bodi ya Tume ya Umwagiliaji. *(Makofi)*

Tunaye Ndugu Hawa Mniga, Mwenyekiti wa Bodi ya Kampuni ya Mbolea *(TFC)*; Ndugu Godfrey Nurra, Mkurugenzi Mtendaji, Benki ya Ushirika; na Ndugu Frank Nyabundege, Mkurugenzi Mtendaji, Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania. *(Makofi)*

Tunaye Ndugu Essau Mbegete, Mjumbe, Baraza la Kumshauri Rais kuhusu utekelezaji wa masuala ya kilimo na chakula nchini; Ndugu Andrew Massawe, Mjumbe wa Baraza la Kumshauri Rais kuhusu utekelezaji wa masuala ya kilimo na chakula nchini; Ndugu Godffrey Kirenga, Mjumbe wa Baraza la Kumshauri Rais kuhusu utekelezaji wa masuala ya kilimo na chakula nchini; na Dkt. Jaqualine Mkindi, Mjumbe, Baraza la Kumshauri Rais kuhusu utekelezaji wa masuala ya chakula na kilimo nchini. *(Makofi)*

Tunaye Ndugu Reuben Ndege, Mkuu wa Ubunifu na Mikakati, *Clouds TV*; na Ndugu Faudhia Kulani, Meneja wa Masoko, *Clouds TV*. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Mheshimiwa Godfrey Chongolo ni wenyeviti wa Chama Cha Mapinduzi Mkoa wa Njombe. Wapo pia Makatibu na Makatibu wenezi wa Chama Cha Mapinduzi Mkoa wa Njombe. Wapo pia Wajumbe wa Kamati ya Siasa, Makambako. Karibuni sana Waheshimiwa wageni wetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na wageni wa Waheshimiwa Wabunge.

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Wanu Hafidh Ameir, Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, ambaye ni Ndugu Nassoro Rajab Mwalim, Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi kutoka Makunduchi, Zanzibar. *(Makofi)*

Wapo pia wageni 27 wa Mheshimiwa David Ernest Silinde, Naibu Waziri wa Kilimo, ambao ni marafiki zake kutoka Tunduma mkoani Songwe. *(Makofi)*

Yupo pia mgeni wa Mheshimiwa Festo Richard Sanga ambaye ni Ndugu Gerald Sanga, Mkurugenzi wa *Agribusiness Solution Co. Ltd* kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Pia, wapo wageni watano wa Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo, ambao ni makatibu wa UWT kutoka wilaya za Mkoa wa Mtwara. *(Makofi)*

Wapo pia wageni wa Mheshimiwa Ghati Zephania Chomete ambao ni ndugu zake kutoka Tarime Mkoani Mara. *(Makofi)*

Pia, wapo wageni watano wa Mheshimiwa Yannick Ikayo Ndoinyo, wanafunzi kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa cha Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Pia, wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Anna Richard Lupembe ambao ni wanamaombi kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wapo pia wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo ambao ni Dkt. Godwin Kalolola, Mkurugenzi wa Kampuni ya Bima ya *THORNSTORN*. *(Makofi)*

Wapo pia wanafunzi 35 kutoka Chuo cha Elimu ya Biashara Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wapo pia wanafunzi 60 na walimu wawili wa Taasisi ya Uhasibu Tanzania kutoka Jijini Dar es Salaam. Wageni wetu wote karibuni sana hapa Bungeni. *(Makofi)*

Pia, ipo orodha ya wageni waliotutembelea, kwanza ni Mheshimiwa Balozi Simon Sirro, Mkuu wa Mkoa wa Kigoma. *(Makofi)*

Wapo pia wageni sita wa Mheshimiwa Mgore Miraji Kigera, Makatibu wa Chama Cha Mapinduzi kutoka Mkoani Dodoma. Karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Katibu.

NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

MWENYEKITI: Sasa ninamwita Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Daniel Godfrey Chongolo. *(Makofi)*

WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, ninaomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa lipokee, kujadili na kupitisha Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka 2025/2026 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka 2026/2027. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba hotuba yangu iliyowasilishwa Mezani iingie kwenye Kumbukumbu za Bunge lako

Tukufu. Aidha, hotuba yote inapatikana kwenye tovuti ya Wizara ya Kilimo, *www.kilimo.go.tz*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukutana hapa siku ya leo tukiwa na afya njema kwa ajili ya kujadili taarifa ya utekelezaji wa Wizara ya Kilimo ya mwaka 2025/2026 na bajeti ya mwaka 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuaminiwa na kuchaguliwa na Watanzania katika Uchaguzi Mkuu uliofanyika Oktoba, 2025. Kuchaguliwa kwake ni ishara tosha kuwa wananchi wana imani kubwa, naye katika kuwaletea maendeleo wanayoyahitaji. Ninamwombea afya njema na ninampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninampongeza Balozi Mheshimiwa Dkt. Emmanuel John Nchimbi, Makamu wa Rais, kwa kuendelea kutekeleza vyema wajibu wake wa kumsaidia Mheshimiwa Rais katika kuliongoza Taifa letu. Ninamtakia utekelezaji mwema wa majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa kuchaguliwa kwa mara nyingine kuiongoza Serikali ya Zanzibar. Ninamwombea afya njema na mafanikio katika kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachukua nafasi hii pia kumpongeza Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Mheshimiwa Rais na kuridhiwa na Bunge kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninaamini kupitia yeye, uratibu wa shughuli za Serikali utaendelea kuimarika na kuwezesha kufikiwa kwa malengo ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2025/2030.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu kwa kuchaguliwa kwa kishindo na Waheshimiwa

Wabunge kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge. Ninaamini weledi, maarifa na busara zenu zitaendelea kutuongoza katika majadiliano ndani ya Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, ninawapongeza Wabunge wenzangu wote kwa kuaminiwa na kuchaguliwa na wananchi wa majimbo yenu kuwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ninatumia fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Kilimo. Ninamwahidi Mheshimiwa Rais na Watanzania wote kuwa nitatumikia nafasi ya Uwaziri kwa bidii, maarifa, weledi na uadilifu mkubwa ili kuhakikisha malengo na matarajio ya Taifa na wananchi yanafikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, ninampongeza Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mbunge wa Jimbo la Tunduma, kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Kilimo, ninaahidi kuwa nitaendelea kushirikiana naye katika kuendeleza jitihada za kuimarisha kilimo nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, Mbunge wa Jimbo la Njombe Mjini, na Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge wa Viti Maalum, kwa kuchaguliwa kuwa Wenyeviti wa Bunge hili. Aidha, ninawapongeza kwa jinsi mnavyoliongoza Bunge letu Tukufu kwa weledi na maarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, Mbunge wa Jimbo la Njombe Mjini, na Mheshimiwa Mariamu Ditopile Mzuzuri, Mbunge kutoka Jimbo la Kondoa Mjini, kwa kuchaguliwa kuiongoza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, ninawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote walioteuliwa kuwa Wajumbe wa Kamati hiyo. Ninawaahidi, nitaendelea kutoa ushirikiano wa dhati katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishukuru kwa dhati Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kwa ushirikiano, maoni, usimamizi, ufuatiliaji na miongozo mbalimbali waliyoitoa kwa ajili ya kuendeleza sekta ya kilimo. Maoni na ushauri wao umezingatiwa katika kipindi chote cha utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2025/2026 na maandalizi ya Mpango na Bajeti ya mwaka 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Ndugu Gerald Geofrey Mweli, Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuratibu wataalamu ndani ya Wizara, Mhandisi Athumani Juma Kilundumya, Naibu Katibu Mkuu anayesimamia Umwagiliaji na Zana za Kilimo, na Prof. Peter Lawrence Makenga Msoffe, Naibu Katibu Mkuu anayesimamia Maendeleo ya Mazao na Usalama wa Chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, ninawashukuru Wakuu wa Idara na Vitengo, Wakuu wa Taasisi, Bodi, Wakala zilizo chini ya Wizara na Watumishi wote kwa ushirikiano wanaonipatia katika kutekeleza majukumu yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee na kwa unyenyekevu mkubwa, ninawashukuru wananchi wa Jimbo la Makambako kwa kuniamini na kunichagua kwa kura nyingi. Imani hiyo kwangu ni deni la kuwatumikia usiku na mchana katika kuwaletea maendeleo kwa vitendo. Mipango yetu tuliyoiweka ni msingi bora wa maendeleo na tumaini jipya la kuimarisha uchumi wa mtu mmoja mmoja na Makambako kwa ujumla, ikizingatiwa kuwa Makambako ni lango la uchumi kwa Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee, ninamshukuru sana mke wangu Bi. Getrude na familia yangu kwa

ujumla kwa kuniunga mkono katika utekelezaji wa majukumu yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutumia nafasi hii pia, kutoa pole kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwako wewe binafsi, Waheshimiwa Wabunge, familia na Watanzania wote kwa msiba wa aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu, kaka yangu, Hayati William Vangimembe Lukuvi, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Isimani. Hakika Taifa limepoteza kiongozi shupavu aliyekuwa mwalimu kwa wengi katika uwanja wa siasa na uongozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, ninatoa pole kwako wewe, Bunge lako Tukufu, familia na Watanzania wote kwa ujumla kwa kuondokewa na wapendwa wetu, Hayati Jenista Joakim Mhagama aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Peramiho na Hayati Halima Iddi Nassor aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalumu (Wafanyakazi). Wakati wote tutaendelea kukumbuka mchango wao katika maendeleo ya Taifa letu. Bwana alitoa, Bwana ametwaa, Jina lake lihimidiwe. Amen.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Kilimo imeendelea kuwa mhimili muhimu katika kuhakikisha usalama wa chakula, upatikanaji wa ajira, malighafi za viwandani na kuchangia katika pato la Taifa. Katika mwaka wa 2025, Sekta ya Kilimo imekua kwa asilimia nne nukta sifuri. Aidha, imechangia kwa 24.6% katika pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Utekelezaji wa Mpango na Bajeti Kwa Mwaka 2025/2026 kwa upande wa makusanyo ya maduhuli, Wizara ilipanga kukusanya shilingi bilioni 12.2 kupitia Fungu 43, Fungu 24 na Fungu 05. Hadi Machi, 2026, Wizara imekusanya shilingi bilioni 15.83 sawa na 129.75% zimekusanywa. Katika mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara ya Kilimo ilitengewa jumla ya shilingi trilioni 1.19 kupitia Fungu 43, Fungu 24 na Fungu 05. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 961.69 ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na shilingi bilioni 231.28 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zilizotolewa Machi, 2026, ni shilingi bilioni 532.51 sawa na 42.84% ya fedha zilizoidhinishwa kwa Fungu 43, Fungu 24 na Fungu 05. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 436.54 ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na Shilingi 9.97 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2025/2026. Uzalishaji wa mazao asilia ya biashara unaohusisha mkonge, miwa inayozalisha sukari, pamba, kahawa, korosho, tumbaku, pareto, chai na kakao umefikia tani milioni 1.59 sawa na 71.9% ya lengo la kuzalisha tani milioni 2.22.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa mazao ya chakula; uzalishaji wa mazao hayo katika Msimu wa 2024/2025 ulifikia tani milioni 23.78 ikilinganishwa na tani milioni 22.8 katika Msimu wa Kilimo wa 2023/2024. Sawa na ongezeko la asilimia nne nukta tatu na kufanya utoshelevu wa chakula nchini kufikia 130%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzalishaji wa mazao ya bustani umefikia tani milioni 9.78 Mwaka 2024/2025 sawa na 108.68% ya lengo la kuzalisha tani milioni tisa. Aidha, uzalishaji wa mazao ya mafuta umefikia tani milioni 2.24 mwaka 2024/2025 sawa na 102.18% ya lengo la kuzalisha tani milioni 2.2 ikilinganishwa na tani milioni 2.181 mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio haya ya kuongezeka kwa uzalishaji siyo ya bahati mbaya, bali ni matokeo ya uwekezaji wa makusudi katika maeneo ya kimkakati uliofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita. Maeneo ya kimkakati ni pamoja na kuwezesha wakulima kupata pembejeo za kilimo, ikiwemo mbolea, mbegu bora, viuatilifu na zana za kilimo kupitia mpango wa ruzuku, ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji, kuimarika kwa huduma za ugani, kilimo na masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa utafiti wa mbegu, Wizara, kupitia *TARI,* imefanya utafiti wa aina 30 za mbegu ya mazao ya kimkakati. Pia, *TARI* imesafisha na kutunza aina 54 za mbegu za asilia. Mbegu zetu za asili ni nguzo muhimu ya usalama

wa chakula na uhifadhi wa mazingira. Mbegu hizo siyo tu kielelezo cha urithi wetu, bali ni nyenzo madhubuti ya kukabiliana na mabadiliko ya tabiachi kutokana na ustahimilivu wake wa asili dhidi ya ukame na magonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukusanyaji na uhifadhi wa mbegu hizo ni chanzo cha utafiti na uzalishaji wa mbegu bora. Pia, ni uwezeshaji wa wananchi kuwa na uwezo wa kulima, kutunza na kutokuwa na gharama za kununua mbegu kila msimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu miundombinu ya utafiti, tayari inaendelea na ujenzi wa maabara ya kudhibiti visumbufu vya mimea ambao umefikia 60% na ujenzi wa maabara ya kuzalisha miche kwa njia ya chupa *(tissue culture)* ambao umefikia wastani wa 30%. Katika Mwaka 2025/2026, upatikanaji wa mbegu bora ndani ya nchi umefikia tani 79,214.48.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu *ASA* imekuwa ikizalisha mbegu katika mashamba yake yaliyopo mikoa mbalimbali nchini. Kuanzia Msimu wa Kilimo 2024/2025, *ASA* ilianza kuzalisha mbegu bora kupitia Mfumo wa Kilimo cha Mkataba *(Contract Growing Scheme)* ambapo kumekuwa na utaratibu wa sekta binafsi kutumia Mashamba ya *ASA,* kwa ajili ya uzalishaji wa mbegu bora. Mfumo huo umewezesha kuongeza uzalishaji wa mbegu bora kutoka tani 4,510 mwaka 2023/2024 hadi kufikia tani 9,303 mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa udhibiti wa ubora wa mbegu na kukabiliana na changamoto ya mbegu zisizo na ubora. Wizara, kupitia *TOSCI,* imekagua mashamba ya mbegu 1,269 yenye ukubwa wa hekta 19,004. Pia, ujenzi wa Maabara ya Taifa ya Mbegu iliyopo Makao Makuu ya *TOSCI,* Morogoro, umefikia 95%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa mbolea, ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, upatikanaji wa mbolea nchini umefikia tani milioni 1.21. Kwa namna ya pekee, ninaishukuru Manispaa ya Kinondoni na Manispaa ya Moshi kwa kuanzisha viwanda vinavyotengeneza mbolea hai kwa kutumia

taka ozo. Mchango wao siyo tu unalenga kuimarisha uzalishaji na tija ya mazao ya kilimo, bali unalenga pia kutunza na kuhifadhi mazingira kwa kazi hiyo, nawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoa rai kwa halmashauri nyingine nchini kuiga mfano huo kwa kuwekeza kwenye viwanda vya kutengeneza mbolea hai kwa kutumia fursa ya taka ozo ambazo zinapatikana kwa wingi katika maeneo yao zikiwa na lengo pia la kusafisha na kutunza mazingira. Kwa mfano, Jiji la Dar Es Salaam kwenye dampo la Pugu, kwanza itasaidia kupunguza taka na kuzalisha mbolea hai ambayo ni muhimu kwa kilimo chetu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo la viuatilifu na udhibiti wa visumbufu vya mazao na mimea, Wizara imekamilisha usajili na kibali cha kuruka kwa ndege iliyonunuliwa ili kutoa huduma za kudhibiti visumbufu vya mimea na mazao, mfano kweleakwelea na nzige, badala ya kutegemea ndege kutoka nje ya nchi. Ndege hiyo aina ya *Thrush 510P2+* ina uwezo wa kubeba lita 1,930 za viuatilifu pamoja na mbolea au mbegu, mita za ujazo 1.9. Pia, ndege hiyo ina uwezo wa kunyunyuzia viuatilifu kwenye eneo lenye ukubwa wa takribani hekta 3,000 kwa siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha urasimishaji wa shughuli za kilimo unatekelezwa kikamilifu, Wizara imesajili wakulima milioni 5.38 na Maafisa Ugani 8,472. Kati ya hao, Maafisa Ugani wa Serikali ni 6,618, wa Sekta Binafsi ni 1,854 na usajili unaendelea. Natoa rai kwa Maafisa Ugani wa Sekta Binafsi kuendelea kujisajili katika mfumo, ili kutambulika na kuendelea kutoa huduma kwa wakulima wakiwa rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha utoaji wa huduma za ugani, Wizara inaendelea kukamilisha taratibu za kuanzisha Wakala wa Taifa wa Huduma za Ugani Kilimo *(National Agricultural Extension Services Agency – NAESA)* ambao unatarajiwa kuanzishwa rasmi mwaka mpya ujao wa fedha, yaani tarehe 01 Julai, 2026. Wakala huo, utawezesha kuongeza ufanisi wa huduma za ugani, kuratibu na kusimamia shughuli za ugani na

kuhaulisha teknolojia kutoka kwa watafiti na wadau wengine kwenda kwa Maafisa Ugani na wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuwawezesha wakulima kujua aina sahihi ya mbolea ya kutumia na mazao yanayotakiwa kupandwa kwenye maeneo yao, Wizara imekusanya sampuli za udongo katika eneo la kilimo lenye ukubwa wa hekta milioni 40.13 nchi nzima ambazo zitafanyiwa uchambuzi kwenye maabara za udongo na matokeo yake kuwezesha kuandaa ramani ya afya ya udongo nchini, sambamba na upimaji wa afya ya udongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imebaini uwepo wa tindikali katika udongo kwenye baadhi ya maeneo inayoathiri, tija na uzalishaji wa mazao ya kilimo. Hivyo, Wizara inaendelea kutoa huduma ya kurejesha afya ya udongo katika Mikoa ya Njombe, Iringa na Katavi ikiwa ni maeneo ya majaribio kupitia Mradi wa Ruzuku Makini kwa kutumia chokaa mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uendelezaji wa kilimo cha umwagiliaji, Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji, imekamilisha ujenzi na ukarabati wa miradi 28 ya umwagiliaji na kuendelea na ujenzi wa miradi 118 yenye ukubwa wa hekta 232,658. Kati ya miradi hiyo, miradi 18 utekelezaji wake umefikia 50%, miradi 52 utekelezaji wake upo chini ya 50% na miradi 48 ipo katika hatua za awali za utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara, kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji, imekamilisha uchimbaji wa visima 345 vyenye uwezo wa kumwagilia eneo lenye ukubwa wa hekta 6,743 katika mikoa 15. Hivi sasa zinasubiriwa pampu na *solar panels* kwa ajili kufunga na kuanza kuzalisha maji ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa miradi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa skimu na mabwawa Wizara, kupitia Tume, imekamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa Skimu mbili za Mbakiamtuli na Ngorongo. Aidha, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa skimu zilizobaki katika Bonde la Rufiji pamoja na mabonde mengine sita yaliyobaki umefikia wastani wa 54.3%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha matumizi ya zana za kilimo na kuwawezesha wakulima kupata huduma za zana za kilimo karibu na maeneo ya uzalishaji, Wizara imeanzisha vituo 79 vya kutoa huduma ya zana za kilimo kwa wakulima nchini. Aidha, Wizara imenunua na kusambaza matrekta 360 katika vituo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo sasa ni fursa ya ajira kwa vijana na wanawake inayolenga kuchochea ubunifu, kuleta utajiri na kulisha Taifa kwa ujumla. Hii inasadifu shairi maarufu tulilokuwa tukilisoma shule la baba aliyekuwa akitoa wosia kwa watoto wake katika dakika za mwisho za uhaki wake, ”*kama mnataka mali, mtaipata shambani*.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha vijana na wanawake wanapata ajira zenye staha na kuongeza kipato, Wizara inaendelea kutekeleza *Program* ya *BBT*. Yaani, ‘Jenga Kesho Iliyo Bora’ katika maeneo ya huduma za ugani, mashamba makubwa katika ngazi ya halmashauri, visima vya umwagiliaji na uongezaji thamani na mitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji wa Mradi wa Jenga Kesho Iliyo Bora, mashamba makubwa ya Halmashauri 18 za Chemba, Bahi, Kisarawe, Kibaha, Kilolo, Njombe, Chunya, Manyoni, Musoma, Ikungi, Kaliua, Kakonko, Nkasi, Muleba, Misenyi, Njombe Mji na Manispaa za Geita na Mpanda zimetenga maeneo ya kilimo ili kuanzisha mashamba ya pamoja ya vijana na wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Wizara imenunua seti 1,250 za pampu, jenereta na mipira ambapo seti 250 zimesambazwa kwa wakulima na seti 1,000 zitaendelea kusambazwa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji kwa wakulima katika mikoa yenye vyanzo vya uhakika vya maji, ikiwemo pembezoni mwa Ziwa Victoria, Tanganyika na mito mikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa kuimarisha usalama wa chakula na lishe, Wizara imenunua tani 135,290.39 za nafaka na kufanya hifadhi ya akiba ya chakula ya Taifa kufikia tani 553,077.37. Wizara imeendelea kuimarisha upatikanaji wa

masoko nje ya nchi kusimamia mauzo ya mazao ya kilimo nje ya nchi, ambapo hadi Machi, 2026 thamani ya mauzo ya mazao ya kilimo nje ya nchi imeongezeka kutoka Dola za Marekani bilioni 3.54 mwaka 2023/2024 hadi Dola za Marekani bilioni 3.73 mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Wizara imeendelea kuimarisha mifumo ya masoko ya kilimo kwa kuongeza uwazi na ushindani, ili wakulima waweze kupata soko la uhakika na bei nzuri ya bidhaa zao. Katika kuhakikisha mauzo ya mazao nje ya nchi yanaendelea kuongezeka na kwa kuzingatia mahitaji makubwa ya zao la parachichi katika masoko ya Uingereza na Marekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia *TPHPA* imeanza kutekeleza operesheni maalum inayolenga kudhibiti visumbufu vya kikarantini aina ya Nondo wa Matunda katika zao la parachichi. Lengo la operesheni hiyo inayotekelezwa katika mikoa ya Njombe, Iringa na Mbeya ni itaiwezesha Tanzania kukidhi kigezo muhimu na pekee kilichobaki, ili kufungua masoko ya parachichi katika nchi za Uingereza na Marekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha ushirika, Wizara kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania, imesajili vyama 6,545 vyenye jumla ya wanachama 3,357,366 katika Mfumo wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika, *MUVU,* kwa ajili ya kurahisisha utoaji wa huduma na usimamizi. Pia, Tume imeendelea kuhamasisha Vyama vya Ushirika kujiendesha kibiashara kwa kuratibu uanzishwaji na ufufuaji wa viwanda vya Vyama vya Ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua hiyo imewezesha Chama Kikuu cha *KACU* kuanzisha ujenzi wa kiwanda cha kuchakata mafuta ya kula chenye uwezo wa kuchakata tani 10,800 kwa mwaka. Chama Kikuu cha Nyanza kuanzisha ujenzi wa kiwanda cha kuchakata pamba na Chama Kikuu cha *TANECU* kujenga kiwanda cha kubangua korosho chenye uwezo wa kubangua tani 3,500 kilichopo ndani ya Halmashauri ya Newala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Bajeti ya Mwaka 2026/2027 ya Wizara ya Kilimo imebeba maono mapana ya Serikali kupitia kilimo ambacho ni msingi na dira itakayoiwezesha Tanzania kufikia hadhi ya nchi ya Kipato cha Kati cha Juu ifikapo 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango na Bajeti ya Wizara ya Kilimo ya Mwaka 2026/2027 imezingatia Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2050, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano Awamu ya Nne, kwa maana ya 2026/2027 - 2030/2031, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2026/2027, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi wa Mwaka 2025/2030, Hotuba ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoitoa wakati wa ufunguzi wa Bunge la Kumi na Tatu, Tarehe 14 Novemba, 2025 Jijini Dodoma, Sera ya Taifa ya Kilimo ya Mwaka 2013, Sera ya Taifa ya Umwagiliaji ya Mwaka 2010, Sera ya Maendeleo ya Ushirika ya Mwaka 2002 na Mpango Kabambe wa Mageuzi ya Kilimo 2050.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia imezingatia agenda ya Kikanda na Kimataifa, ikiwemo Malengo ya Maendeleo ya Endelevu *(SDGs)* na Azimio la Kampala kuhusu Programu ya Kuendeleza Kilimo Barani Afrika 2026/2035, Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2026/2027 na Maoni na Ushauri wa Kamati za kudumu za Bunge, Maoni ya Baraza la Rais la Ushauri wa Kilimo na wadau wa maendeleo na masuala mtambuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa 2026/2027 Wizara itaendelea kutekeleza vipaumbele sita ambavyo ni kuongeza tija na uzalishaji; kuchangia kuongeza ajira zenye staha na ushiriki wa vijana na wanawake kwenye kilimo; kuimarisha usalama wa chakula na lishe; kuimarisha upatikanaji wa mitaji, masoko na mauzo ya mazao nje ya nchi; kuimarisha maendeleo ya ushirika; kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika uendeshaji wa sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa utafiti wa kilimo Wizara kupitia *TARI,* katika mwaka 2026/2027 itazalisha mbegu za

awali tani 1,227 za mazao ya kimkakati, itasafisha na kutunza aina ya 2,325 za mbegu za asili, itaendelea na ujenzi wa kituo cha kibiolojia katika Mkoa wa Morogoro na ujenzi wa benki ya mbegu katika kituo cha *TARI Selian* Mkoani Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa 2026/2027 wa fedha, Wizara imepanga kuongeza upatikanaji wa mbegu kufikia tani 105,000. Upatikanaji huo utachangiwa na kilimo cha mkakati cha mkataba kati ya *ASA* na wazalishaji binafsi wa mbegu. Aidha, itaendelea kutoa ruzuku ya mbegu bora za mazao ya kimkakati tani 600,000. Lengo ni kuwawezesha wakulima kupata mbegu kwa gharama nafuu ili kuongeza tija na uzalishaji wa mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuongeza upatikanaji wa miche, Wizara kupitia taasisi zake itazalisha na kusambaza miche milioni 46.6 ya mazao ya mkonge, kahawa, tufaa au *apple* kwa Kiingereza, chikichi, korosho, chai, kakao na parachichi kwa mpango wa ruzuku na kuweka mfumo wa kusimamia uandaaji, usambazaji na utunzaji wa miche inayozalishwa. Lengo ni kuwawezesha wakulima kupata miche bora kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wa mapinduzi ya kilimo unaanza na mbegu bora ambapo hubeba hatma ya mavuno yetu na kiini cha tija na usalama wa chakula nchini kwa ujumla. Katika kukabiliana na changamoto iliyopo ya uuzaji wa mbegu zisizo na ubora, jambo ambalo ni hujuma ya wazi dhidi ya wakulima, Wizara katika mwaka 2026/2027, itatoa mafunzo kwa vitendo *(demonstration)* kwa wakulima na wauzaji wa mbegu yatakayolenga kuwawezesha kutofautisha mbegu zisizo na ubora na mbegu bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoa wito kwa wafanyabiashara wasio waaminifu wanaofikiri kuuza mbegu feki kufahamu kuwa mkono wa sheria hautawaacha salama. Ninawasihi wakulima kuwa macho na kuhakikisha wananunua mbegu bora kutoka kwa mawakala waliosajiliwa na kukagua kwa makini nembo za udhibiti ubora kwenye vifungashio na siyo vinginevyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2026/2027, Wizara kupitia *TFRA* imepanga kuratibu upatikanaji wa tani 1.5 za mbolea na kuzisambaza kwa wakulima kwa mpango wa ruzuku. Aidha, *TFC* itanunua na kusambaza mbolea tani 270,500, kati ya hizo tani 50,000 za mbolea zitanunuliwa kutoka kwenye viwanda vya ndani wazalishaji wa ndani ili kuviwezesha viwanda vya ndani kwa lengo la kuchochea uzalishaji wa mbolea ndani ya nchi. Hatua hiyo itawezesha wakulima kuendelea kupata mbolea kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuendeleza kilimo cha umwagiliaji nchini, Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji itaendelea na ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji katika miradi 118. Vilevile, Tume itaendelea na miradi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa skimu za umwagiliaji 389, mabwawa 49 na mabonde ya kimkakati saba yenye ukubwa takribani hekta 168,796.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jitihada za kuwafikia na kuwasaidia wakulima wadogo ambao ndio mgongo wa uzalishaji wa chakula na malighafi za viwandani, Wizara kupitia Tume imepanga kutekeleza miradi midogo midogo 30 ya umwagiliaji katika mikoa 25 itakayowezesha kumwagilia eneo lenye ukubwa wa hekta 11,810. Miradi hiyo itatekelezwa kwa gharama nafuu na kwa muda mfupi ili ianze kutoa huduma kwa wananchi na kuleta matokeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa vituo vya kutoa huduma za zana za kilimo, Wizara itaanzisha vituo 100 vya kutoa huduma hizo na kununua trekta 500, *power tiller* 200 na mashine 50 za kuvuna na kukausha nafaka kwa ajili ya shughuli za kilimo katika mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuendeleza uzalishaji wa mazao ya kilimo Wizara imepanga kuongeza uzalishaji wa mazao asilia ya biashara mazao hayo ni ya pamba, kahawa, mkonge, korosho, tumbaku, pareto, kakao na chai kutoka tani 1,599,945.66 kwa mwaka 2025/2026 hadi tani 2,118,000 kwa mwaka 2026/2027.

Vilevile uzalishaji wa mazao ya bustani utaongezeka kutoka tani 9,781,236.74 mwaka 2024/2025 hadi tani 10,000,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu nchi yetu imekuwa ikiingiza tunda la tufaa *(apples)* kutoka nje ya nchi licha ya uwepo wa fursa ya kutosha ya uzalishaji wa zao hilo hapa nchini, hadi Machi, 2026 takribani tani 1,481.98 za tufaa ziliingizwa kutoka nje ya nchi. Hali hiyo inaonesha mahitaji ya zao hilo ni makubwa ndani ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika safari hii ya kipekee, Wizara kupitia *TARI* na *COPRA* itazalisha na kusambaza miche 600,000 ya tufaa kwa wakulima katika maeneo ya uzalishaji. Nitoe wito kwa vijana na wanawake na wawekezaji kuchangamkia kilimo cha tufaa na fursa zilizopo katika mnyororo wake mzima, tufaa siyo tunda tu linalotumika kuonyesha upendo pekee bali ni biashara yenye tija na faida ya muda mrefu na ni urithi tunaoweza kuwaacha kwa vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa mazao yenye mahitaji makubwa, Wizara imepanga kuongeza uzalishaji wa zao la ngano kutoka tani 115,826 mwaka 2024/2025 hadi tani 200,000. Pia Wizara itahamasisha wakulima kuongeza uzalishaji wa mazao ya mafuta kutoka tani 2,248,046 hadi tani 2,300,000. Lengo ni kupunguza matumizi ya fedha nyingi za kigeni zinazotumika kuagiza bidhaa za mazao hayo nje ya nchi na badala yake kuzalisha ajira kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchangia uzalishaji wa ajira zenye staha na ushiriki wa vijana na wanawake kwenye kilimo. Wizara inaendelea kutekeleza programu ya Jenga Kesho Iliyo Bora katika miradi ya mashamba makubwa katika maeneo walipo vijana na wanawake ngazi ya Halmashauri, uwezeshaji mitaji, uchimbaji wa visima, uongezaji thamani na huduma za ugani kwani lengo ni kuwawezesha vijana na wanawake kupata ajira zenye staha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usalama wa chakula na lishe ni nguzo muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu, kiuchumi na kijamii.

Katika mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara kupitia *NFRA* itaendelea kununua nafaka kutoka kwa wakulima kwa lengo kuhakikisha usalama wa chakula na upatikanaji wa bei ya uhakika kwa wakulima inaendelea kuimarishwa. Vilevile itaendelea na ujenzi wa miundombinu yenye uwezo wa kuhifadhi tani 250,000 za nafaka ili kuongeza uhifadhi wa nafaka nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamira ya Serikali siyo tu kuona wakulima wanazalisha mazao ya kutosha, bali ni kuhakikisha kuwa jasho lao linalindwa kupitia mfumo thabiti ya masoko na mitaji kwa kuimarisha mazingira wezeshi na kuweka mifumo itakayowezesha mauzo ya mazao ya kilimo kwa bei ya soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2026/2027 Wizara imepanga kukamilisha ujenzi wa masoko matano ya kimkakati na kuanzisha ujenzi wa masoko mengine matano kwenye maeneo ya mipakani na maeneo ya kimkakati katika Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Kanda ya Ziwa na Kanda ya Mashariki ambayo ni malango muhimu ya biashara kati ya Tanzania na nchi jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Sita inatambua kuwa nguvu ya wakulima ipo katika uzalishaji, usindikaji, mitaji na masoko kupitia *AMCOS* na *SACCOS*. Katika mwaka 2026/2027, Wizara kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania itafanya ukaguzi wa mara kwa mara wa utendaji na ukaguzi wa hesabu katika vyama vya ushirika 6,545 sawa na 100% ya vyama vyote kwa lengo la kuimarisha usimamizi na kuongeza uwajibikaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Tume itaratibu ujenzi wa kiwanda cha kubangua korosho chenye uwezo wa kubangua tani 3,500 kwa mwaka katika Wilaya ya Tandahimba kitakachojengwa na *TANECU* na kuendesha Kampeni ya Linda Ushirika Chagua Uadilifu kwa ajili ya kuelimisha wadau wakiwemo vyama vya ushirika, Mahakama, Polisi, TAKUKURU na Wanasheria kuhusu ushirika, uadilifu na utatuzi wa migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha mahusiano na jamii *(Corporate Social Responsibility)* Wizara kupitia taasisi zake

itatekeleza miradi itakayolenga kuimarisha uzalishaji wa mazao kwenye maeneo mbalimbali nchini, kwa lengo la kuhamasisha na kutoa motisha kwa jamii husika kushiriki katika shughuli za kilimo hususan vijana na wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhitimisha hotuba yangu mbele ya Bunge lako Tukufu, ninapenda kuwakumbusha Watanzania wote kuwa kilimo ni biashara na mkulima ni mwekezaji. Serikali ya Awamu ya Sita kupitia uongozi mahiri wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, umetafsiri dhana hiyo kwa vitendo na kuendesha kampeni ya 'Mali Shambani' yenye lengo la kuhakikisha kuwa mkulima wa Kitanzania anahama kutoka kilimo cha mazoea na cha kujikimu na kuingia katika kilimo biashara chenye tija, endelevu, uhakika wa soko na manufaa kwa mkulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo siyo tu kujitosheleza kwa chakula kwa 100% bali tunalenga kuwa ghala la chakula kwa ukanda wa Afrika Mashariki, *SADC* na Afrika kwa ujumla ili kuongeza fedha za kigeni na kuimarisha thamani ya shilingi yetu. Malengo hayo hayawezi kufikiwa bila ushirikiano wa karibu na sekta binafsi, hivyo Wizara inaendelea kuwakaribisha wawekezaji wa ndani na nje kwenye mnyororo wa kilimo ili kuzalisha ajira na kuwa na bidhaa zenye chapa ya *Made in Tanzania*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa unyenyekevu mkubwa nitumie nafasi hii ya kipekee kumshukuru sana kwa mara nyingine Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye ameendelea kuweka nguvu kubwa katika kusaidia sekta ya kilimo na wakulima nchini. Aidha, nitumie nafasi hii kuwashukuru Wabunge wote kwa kuwa pamoja na wakulima na kuendelea kuhamasisha shughuli za kilimo katika Majimbo yetu sote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitumie fursa hii kuzishukuru nchi ambazo zimeendelea kuunga mkono juhudi za Serikali katika kutekeleza shughuli za kilimo nchini, nchi hizo ni pamoja na Serikali ya Japan, Marekani, Uingereza, China, Urusi, Indonesia, Korea Kusini, India, Italia, Misri, Kuwait, Israel, Saudi Arabia, Thailand, Iran, Ukraine, Ubelgiji, Ujerumani, Ufini, Norway,

Brazil, Uholanzi, Ireland, Malaysia, Denmark, Austria, Ufaransa, Romania, Belarus, Vietnam, Sweden, Canada, Poland, Qatar, Oman, Uturuki pamoja na Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika, Umoja wa nchi za Afrika, Umoja wa Ulaya, Jumuiya ya Madola na Umoja wa Falme za Kiarabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninayashukuru mashirika mbalimbali ya Kitaifa na Kimataifa, ikiwemo Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, *JICA, IMF, IFAD, FAO, WFP, AGRA, KOICA, Care International, World Vision, UNIDO, UNDP, TAHA, World Vegetable Centre. Pia SAT, SUGECO, AGCOT, Aspires Tanzania, CIAT, RIKOLTO, HELVATAS, ENABEL, CAMFED, BIVAC, IRRI, Agriedo, Mazao Hub, Global Community, TASTA, GAIN, NORAD, IITA, AATI, AMDT, SNV, FSDT, ANSAF,* MVIWATA, *SWISS AID, TOAM, GIZ, UN Women, ESAFF, IFC, ESRF, PASS Trust, Action Aid* Tanzania, *EAGC, Global Crop Diversity Trust na EFTA. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninazishukuru Taasisi za Elimu, utafiti, wasanii na vyombo vya habari kwa mchango wao mkubwa nchini katika maendeleo ya sekta ya kilimo. Aidha, ninawashukuru sana viongozi wa dini kwa kuendelea kutuombea na kutushauri katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaomba uniruhusu niwasilishe maombi ya fedha kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Wizara katika mwaka wa fedha 2026/2027, imepanga kukusanya Shilingi 28,600,000,000 kupitia Fungu 43, Fungu 24 na Fungu 05. Kati ya fedha hizo, Shilingi 25,000,000,000 zitakusanywa kutokana na ukaguzi wa mazao, kodi za majengo na uuzaji wa nyaraka za zabuni kupitia Fungu 43 na Shilingi 3,600,000,000 zitakusanywa kutokana na ada za huduma ya umwagiliaji na ukodishaji wa mitambo kupitia Fungu 05.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa fedha za matumizi ya Fungu 43, Fungu 24 na Fungu 05, Wizara ya Kilimo inaliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 1,105,950,115,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Fungu 43 katika mwaka 2026/2027, shilingi 698,985,584,000 zinaombwa. Kati ya fedha hizo, shilingi 567,345,730,000 ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ambapo shilingi 360,678,811,000 ni fedha za ndani na kiasi cha shilingi 206,666,919,000 ni fedha za nje. Aidha, shilingi 131,639,854,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambapo shilingi 84,956,697,000 ni mishahara na shilingi 46,683,157,000 ni matumizi mengineyo ya Wizara, Bodi na Taasisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Fungu 24 katika mwaka 2026/2027, Tume ya Maendeleo ya Ushirika inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 22,673,770,000. Kati ya fedha hizo, shilingi 21,976,594,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 697,176,000 ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya Fedha za matumizi ya kawaida zinazoombwa, shilingi 8,130,236,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi 13,846,358,000 ni kwa ajili ya mishahara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Fungu Na. 05 kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inaomba kuidhinishiwa shilingi 384,290,761,000. Kati ya fedha hizo, shilingi 308,721,961,000 ni fedha za maendeleo na shilingi 75,568,800,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha za maendeleo zinazoombwa, shilingi 259,617,801,000 ni fedha za ndani, na shilingi 49,104,160,000 ni fedha za nje. Aidha, kati ya fedha za matumizi ya kawaida zinazoombwa shilingi 65,148,830,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi 10,419,970,000 ni kwa ajili ya mishahara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

28 APRILI, 2026

HOTUBA YA WAZIRI WA KILIMO, MHESHIMIWA DANIEL GODFREY CHONGOLO (MB), KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA KILIMO KWA MWAKA 2026/2027 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

1 UTANGULIZI

1. ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, ninaomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa lipokee, kujadili na kupitisha taarifa ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka 2025/2026 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka 2026/2027.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba Hotuba yangu iliyowasilishwa mezani iingie kwenye kumbukumbu za Bunge lako Tukufu. Aidha, Hotuba yote itapatikana kwenye tovuti ya Wizara ya Kilimo, www.kilimo.go.tz

Shukrani na Pongezi

3. ***Mheshimiwa Spika,*** ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukutana hapa siku ya leo tukiwa na afya njema kwa ajili ya kujadili Taarifa ya Utekelezaji ya Wizara ya Kilimo ya mwaka 2025/2026 na Mpango na Bajeti kwa mwaka 2026/2027.

4. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba nitumie nafasi hii kumpongeza Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuaminiwa na kuchaguliwa na wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Uchaguzi Mkuu uliofanyika Oktoba 2025. Kuchaguliwa kwake ni ishara tosha kuwa wananchi wana imani kubwa katika kuwaletea maendeleo wanayohitaji. Ninamuombea afya njema na ninampongeza sana!

5. ***Mheshimiwa Spika,*** pia ninampongeza Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kutekeleza vyema wajibu wake wa

kumsaidia Mheshimiwa Rais katika kuliongoza Taifa letu. Ninamtakia utekelezaji mwema wa majukumu yake.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** nitoe pongezi za dhati kwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa kuchaguliwa kwa mara nyingine kuiongoza Serikali ya Zanzibar. Ninamuombea afya njema na mafanikio katika kutekeleza majukumu yake.

7. ***Mheshimiwa Spika,*** nichukue nafasi hii pia kumpongeza Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb) kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninaamini kupitia yeye uratibu wa shughuli za Serikali utaendelea kuimarika na kuwezesha kufikiwa kwa malengo ya Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2025 – 2030 na Dira ya Taifa ya mwaka 2050.

8. ***Mheshimiwa Spika,*** ninakupongeza wewe binafsi kwa kuchaguliwa kwa kishindo na Waheshimiwa Wabunge kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Daniel Baran Sillo (Mb), kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninaamini weledi, maarifa na busara zenu zitaendelea kutuongoza katika majadiliano ndani ya Bunge hili. Pia, ninawapongeza wabunge wenzangu wote kwa kuaminiwa na kuchaguliwa na wananchi wa Majimbo yenu kuwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

9. ***Mheshimiwa Spika***, nitumie fursa hii kumshukuru sana Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Kilimo. Ninamuahidi Mheshimiwa Rais na Watanzania wote kuwa nitatumikia nafasi ya uwaziri kwa bidii, maarifa, weledi na uadilifu mkubwa ili kuhakikisha malengo na matarajio ya Taifa na Wananchi yanafikiwa. Pia, ninampongeza Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mbunge wa Jimbo la Tunduma kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Kilimo. Ninaahidi kuwa nitaendelea kushirikiana naye katika kuendeleza jitihada za kuimarisha kilimo nchini.

10. ***Mheshimiwa Spika,*** ninawapongeza Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, Mbunge wa Jimbo la Njombe Mjini; Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge wa Viti Maalum; na Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, Mbunge wa Viti Maalum kwa kuchaguliwa kuwa Wenyeviti wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, ninawapongeza kwa jinsi mnavyoliongoza Bunge letu Tukufu kwa weledi na maarifa.

11. ***Mheshimiwa Spika,*** ninawapongeza Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, Mbunge wa Jimbo la Njombe Mjini na Mheshimiwa Mariamu Ditopile Mzuzuri, Mbunge wa Jimbo la Kondoa Mjini kwa kuchaguliwa kuiongoza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo. Pia, ninawapongeza wabunge wote walioteuliwa kuwa Wajumbe wa Kamati hiyo. Ninawaahidi nitaendelea kutoa ushirikiano wa dhati katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Kamati.

12. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaishukuru kwa dhati Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kwa ushirikiano, maoni, usimamizi, ufuatiliaji na miongozo mbalimbali waliyotoa kwa ajili ya kuendeleza sekta ya kilimo. Maoni na ushauri wao umezingatiwa katika kipindi chote cha utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2025/2026 na maandalizi ya mpango na bajeti ya mwaka 2026/2027.

13. ***Mheshimiwa Spika,*** ninamshukuru Ndugu Gerald Geofrey Mweli, Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Mhandisi Athumani Juma Kilundumya Naibu Katibu Mkuu anayesimamia Umwagiliaji na Zana za Kilimo na Prof. Peter Lawrence Makenga Msoffe Naibu Katibu Mkuu anayesimamia Maendeleo ya Mazao na Usalama wa Chakula. Vilevile, ninawashukuru Wakuu wa Idara na Vitengo, Wakuu wa Taasisi, Bodi, Wakala zilizo chini ya Wizara na Watumishi wote kwa ushirikiano wanaonipatia katika kutekeleza majukumu yangu.

14. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya kipekee na kwa unyenyekevu mkubwa, ninawashukuru wananchi wa Jimbo la Makambako kwa kuniamini na kunichagua kwa kura nyingi. Imani hiyo kwangu ni deni la kuwatumikia usiku na mchana katika

kuwaletea maendeleo kwa vitendo. Mipango yetu tuliyoiweka ni msingi bora wa maendeleo na tumaini jipya la kuimarisha uchumi wa mtu mmoja mmoja na Makambako kwa ujumla, ikizingatiwa kuwa Makambako ni lango la uchumi kwa mikoa ya Nyanda za juu kusini.

15. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya pekee ninamshukuru sana mke wangu Bi. Getrude na familia yangu kwa ujumla kwa kuniunga mkono katika utekelezaji wa majukumu yangu.

Salamu za Pole

16. ***Mheshimiwa Spika,*** ninatoa pole kwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwako wewe binafsi, wabunge, familia na watanzania wote kwa msiba wa aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu) Hayati William Vangimembe Lukuvi aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Ismani. Hakika Taifa limepoteza kiongozi shupavu aliyekuwa mwalimu kwa wengi katika uwanja wa siasa na uongozi.

17. ***Mheshimiwa Spika,*** pia, ninatoa pole kwako wewe, Bunge lako Tukufu, familia na watanzania wote kwa ujumla kwa kuondokewa na wapendwa wetu, Hayati Jenista Joakim Mhagama aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Peramiho; na Hayati Halima Iddi Nassor aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalumu (Wafanyakazi). Wakati wote tutaendelea kukumbuka mchango wao katika maendeleo ya Taifa letu. **Bwana alitoa, Bwana ametwaa, Jina lake lihimidiwe** Amina.

MAFANIKIO YA WIZARA YA KILIMO KWA KIPINDI CHA MWAKA 2021/2022 – 2025/2026

18. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Kilimo imeendelea kutekeleza Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/2022 – 2025/2026) chini ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na kiongozi shupavu na mwenye maono ya kuleta mapinduzi katika sekta ya kilimo, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

19. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita, sekta ya kilimo imeimarika kwa kuendelea kuwekeza katika maeneo muhimu yanayodhihirisha dhamira ya dhati ya kumuinua mkulima na kuifanya Tanzania kuwa ghala la chakula barani Afrika.

20. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Awamu ya Sita tumeshuhudia ongezeko kubwa la bajeti ya Wizara ya Kilimo kutoka Shilingi Bilioni 294 mwaka 2021/2022 hadi Shilingi Trilioni 1.19 mwaka 2025/2026 ikiwa ni ishara tosha kuwa kilimo si ajenda ya pembeni bali ni kipaumbele namba moja cha Taifa katika kukuza uchumi na kuzalisha ajira.

21. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hiki tumeshuhudia dhamira ya dhati ya Mheshimiwa Rais ya kumpunguzia mkulima gharama za uzalishaji kwa kuwezesha ruzuku ya pembejeo za kilimo kupitia mfumo wa kidijiti hadi vijijini. Huu ni ushahidi kuwa, Serikali hii inajali utu na ni hatua inayolenga kuhakikisha kuwa jasho la mkulima linazaa matunda kwa kuimarisha kipato cha mkulima.

22. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ya Awamu ya Sita imedhamiria kuandaa kizazi kipya cha wakulima matajiri kupitia Programu ya Jenga Kesho Iliyobora (BBT). Programu hii inawatambua vijana kama injini ya mabadiliko kwa kuwapatia teknolojia, ardhi kwa ajili ya kilimo, mitaji, kuwajengea miundombinu ya umwagiliaji na kuwaunganisha na masoko ya mazao ya kilimo.

23. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Awamu ya Sita tumeshuhudia jitihada kubwa za Mheshimiwa Rais katika kuimarisha masuala ya kidiplomasia na kuwezesha mazao yetu kuuzwa kwa wingi katika masoko makubwa yaliyopo nchi za Asia, Ulaya, Amerika na Afrika.

24. ***Mheshimiwa Spika,*** jitihada hizo zimechangia kupatikana kwa mafanikio yafuatayo:-

i. Sekta ya Kilimo katika mwaka 2024, ilikua kwa asilimia 4.1 ikiliganishwa na ukuaji wa asilimia 3.9 mwaka 2021. Aidha, mchango wa Sekta ya kilimo katika ukuaji wa Pato la Taifa

ulikuwa asilimia 26.3 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 26.8 mwaka 2021;

ii. Uzalishaji wa mazao ya chakula umeongezeka kutoka tani 17,148,290 mwaka 2021/ 2022 hadi tani 23,783,128 mwaka 2024/2025 sawa na ongezeko la asilimia 38.69 na kufanya utoshelevu wa chakula nchini kufikia asilimia 130 ikilinganishwa na asilimia 126 mwaka 2021/2022;

iii. Uzalishaji wa mazao asilia ya biashara umeongezeka kutoka tani 973,436 mwaka 2021/2022 hadi tani 1,596,311.18 mwaka 2024/2025 sawa na ongezeko la asilimia 63.99;

iv. Uzalishaji wa mbegu bora ndani ya nchi umeongezeka kutoka tani 30,167.11 mwaka 2020/2021 hadi tani 54,750.47 mwaka 2025/2026 sawa na ongezeko la asilimia 81.49. Uzalishaji huo umechangia kuongezeka kwa upatikanaji wa mbegu bora kutoka tani 44,581.08 mwaka 2020/2021 hadi tani 79,214.48 mwaka 2025/2026 sawa na ongezeko la asilimia 77.68;

v. Uzalishaji wa mazao ya bustani umeongezeka kutoka tani 7,304,723 mwaka 2020/ 2021 hadi tani 9,781,236.74 mwaka 2024/2025 sawa na ongezeko la asilimia 33.9;

vi. Uzalishaji wa mazao ya mbegu za mafuta umeongezeka kutoka tani 1,713,178 mwaka 2020/2021 hadi tani 2,248,046.24 mwaka 2024/2025 sawa na ongezeko la asilimia 31.22;

vii. Uzalishaji wa ndani wa mbolea umeongezeka kutoka tani 32,239 mwaka 2020/2021 hadi tani 123,203 mwaka 2025/2026 sawa na ongezeko la asilimia 282.16. Uzalishaji huo umechangia upatikanaji wa mbolea kuongezeka kutoka tani 678,017 mwaka 2020/2021 hadi tani 1,098,990 mwaka 2025/2026 sawa na ongezeko la asilimia 62.09;

viii. Uwezo wa Hifadhi ya Taifa ya Chakula (NFRA) umeongezeka kutoka tani 251,000 mwaka 2020/2021 hadi tani

776,000 mwaka 2025/2026 sawa na ongezeko la asilimia 209.16; na

ix. Thamani ya mauzo ya mazao ya kilimo nje ya nchi imeongezeka kutoka Dola za Marekani Bilioni 2.1 mwaka 2021/2022 hadi kufikia Dola za Marekani Bilioni 3.73 mwaka 2024/2025.

25. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza dhamira ya Mheshimiwa Rais ya kuleta mageuzi makubwa ya sekta ya kilimo, Serikali ipo katika hatua za mwisho za kuanzisha Wakala ya Taifa wa Huduma za Ugani Kilimo (National Agriculture Extension Service Agency - NAESA). Uanzishaji wa NAESA si tu uamuzi wa kiutawala bali ni mkakati unaolenga kufikisha huduma za ugani karibu zaidi na mkulima.

26. ***Mheshimiwa Spika,*** katika eneo la miundombinu ya umwagiliaji, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imeendelea kutekeleza miradi 780. Kati ya hiyo, ujenzi na ukarabati wa miradi 28 yenye uwezo wa kumwagilia hekta 23,528 umekamilika na miradi 118 yenye uwezo wa kumwagilia hekta 232,658 ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Aidha, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa miradi 189 umekamilika na miradi 445 ipo katika hatua mbalimbali ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina.

27. ***Mheshimiwa Spika,*** katika eneo la Ushirika, usajili wa vyama vya ushirika kwenye Mfumo wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika - MUVU umeongezeka kutoka vyama 4,661 mwaka 2022/2023 hadi vyama 6,545 mwaka 2025/2026. Kati ya hivyo, Vyama vya Ushirika wa Kilimo na Masoko (AMCOS) ni 4,685 na Vyama vya Akiba na Mikopo (SACCOS) ni 1,182. Aidha, mauzo ya mazao ya kilimo kupitia AMCOS yameongezeka kutoka Shilingi Trilioni 1.696 mwaka 2021/2022 hadi Shilingi Trilioni 3.74 mwaka 2025/2026. Vilevile, mali zinazomilikiwa na SACCOS zimeongezeka kutoka Shilingi Bilioni 836.74 mwaka 2021/2022 hadi Shilingi Trilioni 1.46 mwaka 2024/2025.

2 HALI YA KILIMO KATIKA MWAKA 2025

2.1 Ukuaji na Mchango katika Pato la Taifa

28. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Januari hadi Septemba 2025, Pato halisi la Taifa lilikua kwa wastani wa asilimia 6.0 ikilinganishwa na asilimia 5.5 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Aidha, Sekta ya kilimo imeendelea kuwa mhimili muhimu katika kuhakikisha usalama wa chakula, upatikanaji wa ajira, malighafi za viwandani na kuchangia katika Pato la Taifa (GDP). Katika kipindi cha Januari hadi Septemba 2025, Sekta ya Kilimo ilikua kwa asilimia 4.0. Vilevile, katika kipindi hicho, Sekta ya Kilimo iliongoza kwa kuchangia Pato la Taifa kwa asilimia 24.6.

2.2 Hali ya Chakula

29. ***Mheshimiwa Spika,*** tathmini ya hali ya chakula nchini ilibaini kuwa, uzalishaji wa mazao ya chakula katika msimu wa kilimo wa 2024/2025 ulifikia tani 23,783,128 ikilinganishwa na tani 22,803,316 katika msimu wa kilimo wa 2023/2024 sawa na ongezeko la asilimia 4.3. Kwa mazao ya nafaka uzalishaji ulikuwa tani 14,924,582 msimu wa 2024/2025, ikilinganishwa na tani 14,587,177 msimu wa 2023/2024 sawa na ongezeko la asilimia 2.3. Aidha, uzalishaji wa mazao yasiyo ya nafaka ulifikia tani 8,858,546 msimu wa 2024/2025 ikilinganishwa na tani 8,216,139 msimu wa 2023/2024 sawa na ongezeko la asilimia 7.8. Uzalishaji wa mazao ya chakula umeoneshwa kwenye **Jedwali Na. 1.**

30. ***Mheshimiwa Spika,*** uzalishaji wa mazao ya chakula kwa msimu wa kilimo wa 2024/2025 ulitosheleza mahitaji ya chakula ya tani 18,279,054 kwa mwaka 2025/2026 na kuwepo kwa ziada ya tani 5,504,074. Kutokana na hali hiyo, Taifa limejitosheleza kwa chakula kwa asilimia 130.

Jedwali Na. 1: **Uzalishaji wa Mazao ya Chakula kwa Msimu 2024/2025 (Tani) na Upatikanaji wa Chakula kwa Mwaka**

Nafaka	Mahindi	Mtama	Uwele na Ulezi	Mchele	Ngano	Nafaka
Uzalishaji	10,925,025	1,029,306	214,456	2,639,969	115,826	14,924,582
Mahitaji	7,386,333	582,045	2,521,245	1,238,367	328,703	12,056,694
Uhaba (-)/ Ziada (+)	3,538,692	447,261	2,306,790	1,401,602	-212,876	2,867,889
SSR (%)	148	177	9	213	35	124
Yasiyonafa	**Maharage**	**Mikunde mingine**	**Ndizi**	**Muhogo**	**Viazi**	**Yasiyona**
Uzalishaji	1,245,906	1,277,302	1,413,582	2,649,254	2,272,502	8,858,546
Mahitaji	483,645	497,036	1,148,964	2,868,655	1,224,060	6,222,361
Uhaba (-)/ Ziada (+)	762,261	780,266	264,618	-219,402	1,048,443	2,639,286
SSR (%)	258	257	123	92	186	142
Jumla	**Nafaka**	**Yasiyonafaka**	**Jumla**			
Uzalishaji	14,924,582	8,858,546	23,783,128			
Mahitaji	12,056,694	6,222,361	18,279,054			
Uhaba(-)/ Ziada (+)	2,867,889	2,639,286	5,504,074			
SSR (%)	**124**	**142**	**130**			

2025/2026 – kwa Mlinganisho wa Nafaka

Chanzo: *Wizara ya Kilimo, 2026*

3 UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2025/2026

3.1 Makusanyo ya Maduhuli Fungu 43

31. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/ 2026, Wizara ilipanga kukusanya Shilingi **8,665,370,000.00** kupitia Fungu 43 kutokana na ukaguzi wa mazao, kodi za mazao na uuzaji wa nyaraka za zabuni. Hadi Machi 2026, kiasi cha Shilingi **13,780,925,984.21** sawa na asilimia 159.03 zimekusanywa. **Fungu 05**

32. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/ 2026, Wizara ilipanga kukusanya mapato ya Shilingi **3,600,000,000.00** kupitia Fungu 05, kutokana na vyanzo mbalimbali. Hadi Machi 2026,

Wizara imekusanya Shilingi **2,059,882,529.88** sawa na asilimia 57.22 ya lengo.

3.2 Fedha Zilizoidhinishwa kwa Fungu 43, 24 na 05

33. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/ 2026, Wizara ya Kilimo ilitengewa jumla ya Shilingi **1,192,975,075,000.00** kupitia Fungu 43, Fungu 24 na Fungu 05. Kati ya fedha hizo, Shilingi **961,695,070,000.00** ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na Shilingi **231,280,005,000.00** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

34. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026, Fungu 43 lilitengewa jumla ya Shilingi **788,259,822,000** ikijumuisha Shilingi **652,275,933,000** kwa ajili ya miradi ya maendeleo na Shilingi **135,983,889,000** kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Aidha, Fungu 24, lilitengewa jumla ya Shilingi **22,576,845,000** ambapo kati ya hizo Shilingi **697,176,000** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo na Shilingi **21,879,669,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Pia, jumla ya Shilingi **382,138,408,000** zilitengwa kwa ajili ya Fungu 05, ambapo Shilingi **308,721,961,000** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo na Shilingi **73,416,447,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida. **Fedha zilizotolewa**

35. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Machi 2026, jumla ya Shilingi **532,512,056,288.15** sawa na asilimia 42.84 ya fedha zilizoidhinishwa kwa Fungu 43, Fungu 24 na Fungu 05 zimetolewa. Kati ya fedha hizo, Shilingi **436,540,226,893.57** ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na Shilingi **95,971,829,394.58** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

36. ***Mheshimiwa Spika,*** fedha zilizotolewa zinajumuisha Shilingi **369,926,241,178.68** kwa ajili ya Fungu 43 (maendeleo Shilingi **294,210,308,543.25** na matumizi ya kawaida Shilingi **75,715,932,635.43**); Shilingi **14,387,652,536.16** kwa ajili ya Fungu 24 (maendeleo Shilingi **278,880,000** na matumizi ya kawaida Shilingi **14,108,772,536.16**); na Shilingi **152,709,956,737.82** kwa ajili ya Fungu 05 (maendeleo Shilingi **142,051,038,350.32** na matumizi ya kawaida shilingi **10,658,918,387.50**).

4 UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2025/2026

37. ***Mheshimiwa Spika***, utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2025/2026, umezingatia Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025; Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano Awamu ya Tatu (2021/2022 - 2025/2026); Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020; Sera ya Taifa ya Kilimo ya Mwaka 2013; Sera ya Taifa ya Umwagiliaji ya Mwaka 2010; na Sera ya Maendeleo ya Ushirika ya Mwaka 2002. Aidha, utekelezaji umezingatia Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030; Mpango Kabambe wa Mageuzi ya Kilimo wa Mwaka 2050; Mkakati wa Ukuzaji wa Sekta ya Kilimo 2030; Mkakati wa Kuongeza Fedha za Kigeni (2023/2024 – 2027/2028); Azimio la Kampala kuhusu Program ya Kuendeleza Kilimo Barani Afrika (CAADP 2035); Mwongozo na Mpango wa Bajeti wa Mwaka 2025/2026; Maoni na Ushauri wa Kamati za Kudumu za Bunge; Maoni ya Baraza la Rais la Ushauri wa Usalama wa Chakula na Kilimo, wadau wa maendeleo na masuala mtambuka ya jinsia, mazingira, lishe, mabadiliko ya tabianchi, vijana, kutokomeza ajira kwa watoto katika Sekta ya kilimo, VVU na UKIMWI.

38. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2025/ 2026, Wizara ya Kilimo imetekeleza vipaumbele sita (6) ambavyo ni kuongeza uzalishaji na tija; kuchangia kuongeza ajira zenye staha na ushiriki wa vijana na wanawake katika kilimo; kuimarisha usalama wa chakula na lishe; kuimarisha upatikanaji wa masoko, mitaji na mauzo ya mazao nje ya nchi; kuimarisha maendeleo ya ushirika; na kuimarisha matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika uendelezaji wa sekta ya kilimo. Vipaumbele hivyo, vimetekelezwa kupitia mikakati 30. Mafanikio ya utekelezaji wa bajeti ni kama ifuatavyo:-

4.1 Kuongeza Uzalishaji na Tija

39. ***Mheshimiwa Spika,*** uzalishaji wa mazao ya chakula katika msimu wa kilimo wa 2024/2025 ulifikia tani 23,783,128 ikilinganishwa na tani 22,803,316 katika msimu wa kilimo wa 2023/2024 sawa na ongezeko la asilimia 4.3. Mathalani:- uzalishaji wa mazao ya nafaka ulifikia tani 14,924,582 ikilinganishwa na tani 14,587,177

mwaka 2023/2024 na mazao yasiyo ya nafaka tani 8,858,546 ikilinganishwa na tani 8,216,139 mwaka 2023/2024.

40. ***Mheshimiwa Spika,*** uzalishaji wa mazao asilia ya biashara unaohusisha mkonge, miwa/sukari, pamba, kahawa, korosho, tumbaku, pareto, chai na kakao umefikia tani 1,599,945.66 sawa na asilimia 71.9 ya lengo la kuzalisha tani 2,225,000. Mwenendo wa uzalishaji wa mazao hayo umeoneshwa kwenye **Jedwali Na. 2.**

Jedwali Na. 2: Uzalishaji wa Mazao Asilia ya Biashara Mwaka 2025/2026

Na.	Mazao	Uzalishaji (Tani)
1	Korosho	617,683.77
2	Pamba	222,014
3	Pareto	2,780*
4	Kahawa	74,663.60
5	Tumbaku	185,776
6	Chai	11,631.48*
7	Mkonge	64,321.77
8	Sukari	410,979.04*
9	Kakao	10,096*
Jumla		**1,599,945.66**

Chanzo: *Wizara ya Kilimo, 2026 *Uzalishaji unaendelea*

41. ***Mheshimiwa Spika,*** uzalishaji wa mazao ya bustani umefikia tani 9,781,936.74 mwaka 2024/2025 sawa na asilimia 108.68 ya lengo la kuzalisha tani 9,000,000. Aidha, uzalishaji wa mazao ya bustani umeoneshwa katika **Jedwali Na. 3**.

Jedwali Na 3: Uzalishaji wa Mazao ya Bustani Mwaka 2024/2025

Na.	Mazao	Uzalishaji (Tani)
1.	Matunda	8,051,887.41
2.	Mboga	1,634,590.96
3.	Viungo	95,458.37
	Jumla	**9,781,936.74**

Chanzo: *Wizara ya Kilimo, 2026*

42. ***Mheshimiwa Spika,*** uzalishaji wa mazao ya mafuta ulifikia tani 2,248,046.23 mwaka 2024/2025 sawa na asilimia 102.18 ya

lengo la kuzalisha tani 2,200,000 ikilinganishwa na tani 2,181,603.65 mwaka 2023/2024. Uzalishaji wa mazao ya mafuta umeoneshwa kwenye **Jedwali. Na. 4.**

Jedwali Na. 4: Uzalishaji wa Mazao ya Mafuta Mwaka 2024/2025

Na	Mazao	Uzalishaji (Tani)
1.	Alizeti	1,222,209.64
2.	Ufuta	257,040.84
3.	Nazi	85,152.70
4.	Chikichi	74,302.65
5.	Karanga	609,340.40
	Jumla	**2,248,046.23**

Chanzo: *Wizara ya Kilimo, 2026*

43. ***Mheshimiwa Spika,*** mafanikio haya ya kuongezeka kwa uzalishaji si ya bahati mbaya bali ni matokeo ya uwekezaji wa makusudi katika maeneo ya kimkakati uliyofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita. Maeneo ya kimkakati ni pamoja na kuwawezesha wakulima kupata pembejeo za kilimo ikiwemo mbolea, mbegu bora, viuatilifu na zana za kilimo kupitia mpango wa ruzuku, ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji, kuimarika kwa huduma za ugani kilimo na masoko.

44. ***Mheshimiwa Spika,*** mikakati iliyotekelezwa na Wizara kufikia mafanikio hayo ni ifuatayo:-

4.1.1 Utafiti wa Mbegu

45. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuendeleza teknolojia za kilimo, Wizara kupitia TARI katika mwaka 2025/2026 ilipanga kuendelea na utafiti wa mbegu aina 56 za mazao ya kimkakati; kutafiti teknolojia za afya ya udongo na mbolea; kutafiti na kutambua gharama za uzalishaji wa tumbaku zinazokaushwa kwa mvuke, moshi, hewa na jua; kutoa mafunzo kuhusu kurejesha afya ya udongo kwa wakulima 600; kutafiti magonjwa ya fungashada – BBTV katika zao la migomba, *cashew leaf and nut blight*, ubwiri unga na mnyauko fusari katika zao la korosho; kutafiti funza wa vitumba na chawa jani katika zao la pamba; *thrips* kwenye zao la

miwa; na tafiti za viuatilifu vya visumbufu vya mimea katika zao la mtama.

46. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, ilipanga kutafiti aina ya miti ya kivuli inayofaa katika zao la chai; kutafiti teknolojia saba (7) za kuongeza thamani ya mazao ya kilimo; kusafisha na kutunza aina 360 za mbegu za asili za mazao ya kilimo; kukusanya na kutunza vinasaba 12,968 vya mazao ya kilimo; kuzalisha mbegu za mazao ya kimkakati tani 1,500; kuendelea na ujenzi wa ghala 11; kuendelea na ujenzi wa maabara za kuzalisha miche kwa njia ya chupa; na kuendelea na ujenzi wa maabara ya kudhibiti visumbufu vya mimea na mazao.

47. ***Mheshimiwa Spika***, katika kulinda mashamba ya utafiti wa mbegu dhidi ya uvamizi, Wizara ilipanga kuendelea na ujenzi wa uzio katika mashamba ya utafiti wa mbegu; kulipa fidia kwa wananchi watakaohamishwa katika Kituo cha TARI Uyole; kuhakikisha upatikanaji wa hatimiliki katika vituo 17 na mashamba ya majaribio 18; kuendelea na ujenzi wa Kituo cha *Bioscience;* kuendelea na ujenzi wa Benki ya Mbegu (Genebank) katika Kituo cha TARI Selian; kuendelea na ujenzi wa Ofisi ya TARI Makao Makuu (Njedengwa, Dodoma); kukamilisha ukarabati wa nyumba 49 za watumishi; kujenga ofisi moja (1) katika kituo cha TARI Hombolo na kununua vifaa vya Ofisi ya TARI Kihinga.

48. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara ilipanga kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji yenye jumla ya hekta 2,120.9 katika vituo 16 vya TARI; kutoa mafunzo kuhusu kanuni za kilimo bora na uongezaji thamani wa mazao ya zabibu na korosho kwa wakulima 800 na Maafisa Ugani 180. Vilevile, kuendelea na ujenzi wa nyumba tatu (3) za watumishi, jiko na hosteli katika Kituo cha Utafiti wa Kahawa cha Mwayaya (Buhigwe) na kununua mashine ya kukaanga kahawa.

49. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, hadi Machi 2026, Wizara kupitia TARI imetekeleza yafuatayo:-

Utafiti

50. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha utafiti wa mbegu, aina 30 za mbegu za mazao ya kimkakati ya nafaka, jamii ya mikunde, mizizi na mafuta zimefanyiwa utafiti, sawa na asilimia 54 ya lengo la aina 56 za mbegu. Kati ya hizo, aina mbili (2) ni mbegu za muhogo zenye uwezo wa kuzalisha kati ya tani 20 hadi 28.8 kwa hekta ambazo zipo katika hatua za kuidhinishwa kwa ajili ya matumizi; na aina 28 ni mbegu za mazao ya mahindi (6), maharage (3), ufuta (3), mpunga (9), ngano (3) na mtama (4) zimewasilishwa Taasisi ya Uthibiti Ubora wa Mbegu (TOSCI) kwa ajili ya majaribio ya utambuzi na umahiri. Pia, aina 14 za mbegu za migomba zenye uwezo wa kuzalisha kati ya tani 50 hadi 60 kwa hekta zimeidhinishwa na Kamati ya Taifa ya Mbegu kwa ajili ya matumizi.

51. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, imegundua *genotype* tatu (3) za karanga zenye sifa ya mavuno mengi na ustahimilivu wa magonjwa ambazo ni NALX-22-18 (tija kilo 1,356.77 kwa hekta), ICGIL 17113 (tija kilo 1,371.91 kwa hekta) na ICGIL14466 (tija kilo 1,313.65 kwa hekta). Mbegu hizo zitawasilishwa TOSCI kwa majaribio ya utambuzi na umahiri wa mbegu.

52. ***Mheshimiwa Spika,*** pia, imefanya tathmini ya mbegu mpya aina tatu (3) za tumbaku ya mvuke (PVH2343 na TRF23) na hewa (TRB24) na kubaini kuwa zinafaa kwa uzalishaji nchini. Mbegu hizo zimewasilishwa TOSCI kwa ajili ya Majaribio ya Kitaifa ya Umahiri wa Mbegu kwa hatua za kuidhinishwa. Vilevile, sampuli 34 za udongo zimechukuliwa katika mashamba ya wakulima wa tumbaku katika wilaya za Uyui, Kaliua, Uvinza, Kasulu, Tanganyika, Chunya, Namtumbo, Kahama, Mbogwe na Serengeti kwa ajili ya utafiti wa afya ya udongo ili kubaini kiwango sahihi cha uwekaji wa mbolea ya kupandia na kukuzia kwa tumbaku ya mvuke.

53. ***Mheshimiwa Spika***, ili kuimarisha udhibiti wa visumbufu vya mimea na mazao, utafiti wa aina 10 za viuatilifu umekamilika na aina tano (5) zipo katika hatua ya uthibitisho kwa ajili ya udhibiti wa ugonjwa wa ubwiri unga katika zao la korosho. Pia, inaendelea na utafiti wa vitumba na chawa jani katika zao la

pamba, BBTV katika zao la migomba, *thrips* katika zao la miwa na tafiti za visumbufu vya mimea katika zao la mtama.

54. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara inaendelea kutambua thamani ya kipekee ya mbegu zetu za asili kama nguzo muhimu ya usalama wa chakula na uhifadhi wa mazingira. Mbegu hizo si tu kielelezo cha urithi wetu bali ni nyenzo madhubuti ya kukabiliana na mabadiliko ya tabiachi kutokana na ustahimilivu wake wa asili dhidi ya ukame na magonjwa. Ukusanyaji na uhifadhi wa mbegu hizo ni chanzo cha utafiti na uzalishaji wa mbegu bora. Pia, ni uwezeshaji wa wananchi kuwa na uwezo wa kulima, kutunza na kuhifadhi mbegu hizo kwa matumizi ya sasa na ya siku zijazo kwa gharama nafuu. Katika kutekeleza hilo, Wizara imesafisha na kutunza aina 54 za mbegu za asili. Kati ya hizo, aina 49 ni za mpunga na aina tano (5) ni za migomba.

55. ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, nasaba 33,164 mazao ya korosho (20,573), chikichi (5,885), mpunga (1,519), parachichi (999), matunda (839), mahindi (574), muhogo (521), ufuta (350), pamba (342), viazi vitamu (311), migomba (294), kakao (293), dengu (183), miwa (126), alizeti (91), maharage (85), mkonge (75), zabibu (36), viungo (18), choroko (16), mazao ya misitu (14), nyanya (8), uwele (7) na mtama (5) vimekusanywa na kutunzwa kwa lengo la kuendeleza shughuli za utafiti.

Miundombinu ya Utafiti

56. ***Mheshimiwa Spika***, ili kukamilisha mnyororo wa utafiti na uzalishaji, ujenzi wa ghala za kisasa katika vituo vya utafiti ni hitaji la lazima na la kimkakati. Ghala hizo ni muhimu kwa ajili ya uhifadhi wa mbegu za utafiti ambazo ndiyo msingi wa mbegu bora zinazowafikia wakulima. Bila ghala za kisasa, kazi kubwa ya watafiti wetu inaingia hatarini kwa mbegu za utafiti kuharibika kutokana na unyevu na wadudu.

57. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha uhifadhi wa mbegu za utafiti zinazozalishwa na TARI ujenzi wa ghala 11 zenye uwezo wa kuhifadhi tani 415 kila moja katika vituo vya utafiti vya TARI Maruku, TARI Ukiriguru, TARI Kifyulilo, TARI Uyole (Igeri na Nkundi),

TARI Tumbi, TARI Selian, TARI Hombolo, TARI Dakawa na TARI Naliendele umefikia wastani wa asilimia 35.2 na ujenzi unaendelea.

58. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuongeza uzalishaji wa miche kwa ajili ya wakulima, Wizara imezingatia kwa umuhimu wa kipekee matumizi ya teknolojia ya kuzalisha miche kwa njia ya chupa (tissue culture) ikiwa ni hatua muhimu ya kisayansi kuelekea kilimo cha kibiashara. Hivyo, ujenzi wa maabara ya *tissue culture* katika kituo cha TARI Tengeru mkoani Arusha na kituo cha TARI Maruku mkoani Kagera umefikia wastani wa asilimia 30 na ujenzi unaendelea.

59. ***Mheshimiwa Spika***, kukamilika kwa maabara hizo kutachangia kuzalisha kwa wingi miche ya mazao yasiyozalishwa kwa mbegu za kawaida kwa asili yenye uwezo wa kuzalisha kwa mwaka migomba miche 1,500,000, muhogo pingili 10,000,000 na viazi vipando 1,000,000.

60. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha udhibiti wa visumbufu vya mimea na mazao, ujenzi wa maabara ya kudhibiti visumbufu vya mimea katika Kituo cha utafiti cha TARI Naliendele umefikia asilimia 60 na ujenzi unaendelea. Aidha, ujenzi wa Benki ya Taifa ya Mbegu kwa ajili ya kuhifadhi mbegu za utafiti katika Kituo cha TARI Selian umefikia asilimia 5 na mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha *Bioscience* katika Mkoa wa Morogoro amepatikana.

61. ***Mheshimiwa Spika***, ili kulinda mashamba ya utafiti wa mbegu dhidi ya uvamizi wa wanyama na shughuli za kibinadamu, ikiwa ni hatua muhimu ya kulinda uwekezaji mkubwa wa Serikali na kazi za kitaalamu zinazofanyika, ujenzi wa uzio katika mashamba ya utafiti wa mbegu ya TARI Kifyulilo, TARI Dakawa, TARI Hombolo, TARI Maruku, TARI Ifakara na TARI Kihinga umefikia wastani wa asilimia 30 na ujenzi unaendelea.

62. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha mazingira ya utendaji kazi na kuongeza ufanisi kwa watumishi, TARI inaendelea na ujenzi wa Ofisi ya Makao Makuu (Njedengwa, Dodoma) ambapo ujenzi huo umefikia asilimia 75 na ujenzi wa Ofisi katika kituo cha utafiti

cha TARI Hombolo umefikia asilimia 15. Vilevile, ukarabati wa majengo sita (6) ya ofisi na nyumba za watumishi katika vituo vya utafiti vya TARI Mlingano umefikia asilimia 35, TARI Ilonga asilimia 20 na TARI Tumbi asilimia 20.

63. ***Mheshimiwa Spika***, pia mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa nyumba tatu (3) za watumishi, jiko na hosteli katika Kituo cha Utafiti wa Kahawa cha Mwayaya (Buhigwe) amepatikana. Pia, ununuzi wa vifaa vya ofisi za TARI Kihinga umekamilika.

64. ***Mheshimiwa Spika***, ili kuendana na mabadiliko ya teknolojia na kuongeza ufanisi, Wizara kupitia TARI imetoa mafunzo kuhusu kanuni za kilimo bora na uongezaji thamani wa mazao ya zabibu, alizeti na korosho kwa wakulima 549 na Maafisa Ugani 990 katika mikoa ya Dodoma, Singida, Mtwara, Lindi, Ruvuma, Pwani na Singida. Aidha, mzabuni kwa ajili ya ununuzi wa mashine yenye uwezo wa kukaanga kahawa kilo 60 kwa siku amepatikana.

65. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha uzalishaji wa mbegu za utafiti unafanyika kipindi chote cha mwaka, ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji yenye jumla ya hekta 1,120.9 katika vituo 16 vya TARI unaendelea. Pia, mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji yenye jumla ya hekta 1,000 katika vituo vya utafiti vya TARI Uyole (hekta 800) na TARI Ukiriguru (hekta 200) amekabidhiwa maeneo kwa ajili ya kuanza ujenzi.

Uzalishaji wa mbegu za utafiti na kulinda maeneo ya utafiti

66. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia TARI imezalisha mbegu tani 1,037.59 sawa na asilimia 69.17 ya lengo la tani 1,500. Kati ya hizo, tani 77.33 ni mbegu mama, tani 355.28 ni mbegu za awali, tani 435.58 ni mbegu za msingi na tani 169.40 ni mbegu zilizothibitishwa.

67. ***Mheshimiwa Spika***, tathmini kwa ajili ya malipo ya fidia kwa wananchi watakaopisha ujenzi wa uzio katika shamba la TARI - Uyole imefanyika na kubaini wananchi wanaotakiwa kulipwa fidia ni 186 ambapo takriban Shilingi Bilioni 6 zitatumika kulipa fidia na taratibu za malipo ya fidia zinaendelea. Pia, upimaji wa maeneo

katika vituo 17 vya utafiti wa kilimo vya TARI na mashamba ya majaribio 18 umefanyika na taratibu za upatikanaji wa hatimiliki zinaendelea.

4.1.2 Uzalishaji na Usambazaji wa Mbegu na Miche Bora kwa Mpango wa Ruzuku kwa baadhi ya Mazao

68. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2025/2026, ilipanga kuongeza uzalishaji wa mbegu bora kufikia tani 90,000; kuongeza upatikanaji wa mbegu bora kufikia tani 105,000; kutoa ruzuku ya mbegu bora za alizeti tani 5,000 na mahindi tani 52,000; kujenga miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba ya mbegu yenye ukubwa wa hekta 3,000; na kujenga miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba ya mbegu yenye ukubwa wa hekta 495.

69. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ilipanga kujenga uzio katika mashamba ya kuzalisha mbegu; kujenga ofisi moja (1), karakana katika shamba la mbegu la Kilimi na kukarabati ofisi mbili (2) katika mashamba ya mbegu ya Mwele na Mbozi; kujenga ghala mbili (2); kununua na kusimika mitambo minne (4) ya kuchakata mbegu na mashine moja (1) ya kukausha mbegu; kununua magari matano (5) na lori moja (1); kukarabati nyumba za watumishi, karakana na jengo la kuanikia mbegu katika shamba la mbegu Msimba; na kununua chokaa mazao tani 1,000.

70. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ilipanga kuzalisha na kusambaza miche 64,183,900 ya mazao ya kilimo na pingili za muhogo 4,361,600; kuandaa mfumo wa kidijiti kwa ajili ya ufuatiliaji wa maendeleo ya miche; kukagua mashamba ya mbegu yenye ukubwa wa hekta 100; kununua mtambo wa kuchapisha lebo na kutoa lebo 32,000,000 za mbegu bora; kutoa mafunzo kwa wakaguzi wa mbegu 50 na wakaguzi wa mbegu walioidhinishwa (ASI's) 40; na kuendelea na ukarabati wa ofisi za TOSCI Makao Makuu na ofisi za kanda.

71. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, hadi Machi 2026, Wizara imetekeleza yafuatayo:-

72. ***Mheshimiwa Spika,*** upatikanaji wa mbegu bora ndani ya nchi umefikia tani 79,214.48 sawa na asilimia 75.44 ya lengo la kuzalisha tani 105,000. Kati ya kiasi hicho, tani 54,750.47 sawa na asilimia 69.12 zimezalishwa ndani ya nchi na tani 24,464.01 sawa na asilimia 30.88 zimeagizwa kutoka nje ya nchi. Aidha, kati ya tani 54,750.47 zilizozalishwa ndani ya nchi, tani 47,178.47 zimezalishwa na sekta binafsi na tani 7,572 zimezalishwa na ASA.

73. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa muda mrefu, ASA imekuwa ikizalisha mbegu katika mashamba yake yaliyopo mikoa mbalimbali nchini. Kuanzia msimu wa kilimo 2024/2025, ASA ilianza kuzalisha mbegu bora kupitia mfumo wa kilimo cha mkataba (Contract Growing Scheme) ambapo kumekuwa na utaratibu wa sekta binafsi kutumia mashamba ya ASA kwa ajili ya uzalishaji wa mbegu bora. Mfumo huo umewezesha kuongeza uzalishaji wa mbegu bora kutoka tani 4,510 mwaka 2023/2024 hadi kufikia tani 9,303 mwaka 2024/2025.

Ruzuku ya Mbegu Bora

74. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali ilianza rasmi kutekeleza mpango wa ruzuku ya mbegu za mahindi katika msimu wa kilimo wa 2024/2025. Katika mwaka 2025/2026, jumla ya tani 55,041.124 zenye thamani ya jumla ya Shilingi Bilioni 374.2 zimeuzwa kwa mfumo wa ruzuku ikilinganishwa na tani 9,639.63 za mbegu bora za mahindi zenye thamani ya Shilingi Bilioni 12.3 zilizouzwa mwaka 2024/ 2025. Katika mwaka 2025/2026, ruzuku ya Serikali ni Shilingi Bilioni 84.85 na mchango wa wakulima ni Shilingi Bilioni 289.3. Utekelezaji wa mpango huo, umewezesha kuongeza matumizi ya mbegu bora za mahindi ambapo jumla ya wakulima 531,903 wamenufaika.

75. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi hicho, tani 702.43 za mbegu bora za alizeti zimesambazwa kwa wakulima kwa mpango wa ruzuku na usambazaji unaendelea. Aidha, mbegu bora za ngano tani 500 na mpunga tani 500 zimesambazwa kwa wakulima katika mikoa ya uzalishaji. Pia, mbegu bora za ufuta tani 37.98, mbaazi tani 17.34, choroko tani 10.70, dengu tani nne (4) na soya tani moja (1) zimesambazwa kwa wakulima katika maeneo

ya uzalishaji. Mchanganuo wa usambazaji wa mbegu unaonekana katika **Kiambatisho Na 1**. Kadhalika, TOSCI imeainisha wazalishaji 75 watakaozalisha mbegu za kuazimia ubora (QDS) za mazao ya soya, dengu na mbaazi.

Uthibiti wa Ubora wa Mbegu

76. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha uthibiti wa ubora wa mbegu ili kukabiliana na changamoto ya mbegu zisizo na ubora, Wizara kupitia TOSCI imekagua mashamba ya mbegu 1,269 yenye ukubwa wa hekta 19,004.1. Kati ya hizo, hekta 18,636 zilikidhi vigezo vya uzalishaji wa mbegu na hekta 368.1 hazikukidhi vigezo. Wamiliki wa mashamba ambayo hayakukidhi vigezo walielekezwa kuzingatia taratibu za uzalishaji wa mbegu bora katika msimu ujao.

77. ***Mheshimiwa Spika***, ujenzi wa Maabara ya Taifa ya Mbegu iliyopo Makao Makuu ya TOSCI - Morogoro umefikia asilimia 95; na wakandarasi kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa maabara nne (4) za Kanda ya Ziwa – Mwanza, Kusini – Mtwara, Kaskazini – Arusha na Magharibi – Tabora wamesaini mikataba kwa ajili ya kuanza ujenzi. Kukamilika kwa maabara hizo kutaongeza kuthibiti ubora wa mbegu kwa kutumia teknolojia za kisasa na kuendelea kulinda taswira ya Tanzania katika viwango vya ubora wa mbegu kimataifa na kufungua fursa mpya kwa uwekezaji katika uzalishaji na biashara ya mbegu.

Ujenzi wa Maabara ya Taifa ya Mbegu iliyopo Makao Makuu ya TOSCI - Morogoro

78. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuongeza ufanisi wa uthibiti wa ubora wa mbegu, zabuni kwa ajili ya ununuzi wa mtambo wa kuchapisha lebo zitakazotumika katika vifungashio vya mbegu imetangazwa. Vilevile, lebo 30,882,500 za mbegu bora zimetolewa sawa na asilimia 96.5 ya lengo la kutoa lebo 32,000,000; na mafunzo kwa wakaguzi wa mbegu 144 yametolewa. Kati ya hao, 62 ni wakaguzi walioidhinishwa (ASI's) katika ngazi ya Halmashauri za Wilaya na 82 ni wakaguzi wa mbegu wa TOSCI.

Miundombinu ya uzalishaji mbegu

79. ***Mheshimiwa Spika***, katika kulinda mashamba ya mbegu dhidi ya uvamizi, ujenzi wa uzio katika mashamba ya Kilangali (km 20.8) umefikia asilimia 30, Mwele (km 14) asilimia 15, Namtumbo (km 33) asilimia 5 na mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa uzio katika shamba la Arusha (km 17) amekabidhiwa eneo kwa ajili ya kuanza ujenzi.

80. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara katika kuongeza ufanisi wa watumishi kwenye mashamba ya mbegu, imeendelea na ujenzi wa nyumba za watumishi ambapo ujenzi katika mashamba ya mbegu ya Msungura (nyumba 3) umefikia wastani wa asilimia 83, Kilimi (nyumba 2) asilimia 55, Mbozi (nyumba 6) asilimia 50, Arusha (nyumba 10) asilimia 35, Namtumbo (nyumba 3) asilimia 35 na Mwele (nyumba 4) asilimia 15. Pia, ujenzi wa ofisi moja (1) katika shamba la mbegu la Kilimi umefikia asilimia 80. Aidha, ujenzi wa karakana katika shamba la mbegu la Kilimi umekamilika. Karakana hiyo itatumika kwa ajili ya ukarabati wa mitambo inayotumika katika uzalishaji wa mbegu bora.

81. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuongeza ufanisi wa usambazaji wa mbegu bora na kuimarisha usimamizi, Wizara kupitia ASA imenunua magari matano (5) na malori matatu (3) yenye uwezo wa kubeba tani 30 za mbegu kila moja. Aidha, ili kuongeza uhifadhi na kuimarisha ubora wa mbegu, ujenzi wa ghala mbili (2) zenye uwezo wa kuhifadhi mbegu tani 2,500 katika shamba la BBT Ndogowe (tani 1,000) na shamba la mbegu la Arusha (tani 1,500) umefikia asilimia 10 na asilimia mbili (2), mtawalia.

82. ***Mheshimiwa Spika***, upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba saba (7) ya mbegu yenye ukubwa wa hekta 3,495 ya Namtumbo (1,000), Mbozi (600), Msimba (395), Kilimi (260), Arusha (340), Msungura (100) na Luhafwe (800) unaendelea.

83. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuongeza upatikanaji na ubora wa mbegu, Wizara kupitia ASA, imetangaza zabuni kwa ajili ya kumpata mkandarasi wa kununua na kusimika mitambo minne (4) ya kuchakata mbegu na mashine moja (1) ya kukausha mbegu. Aidha, mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa jengo la kuanikia mbegu katika shamba la Msimba amekabidhiwa eneo. Vilevile, zabuni kwa ajili ya kumpata mkandarasi wa ujenzi wa karakana itakayotumika kwa ajili ya matengezo ya mitambo na mashine katika shamba la mbegu la Msimba imetangazwa.

84. ***Mheshimiwa Spika***, ili kuongeza ufanisi wa kazi kwa watumishi kwa kuweka mazingira wezeshi, Wizara kupitia ASA imekamilisha ukarabati wa nyumba tano (5) za watumishi katika shamba la mbegu la Msimba. Aidha, mzabuni kwa ajili ya kusambaza tani 1,000 za chokaa zitakazotumika katika kuboresha afya ya udongo kweye mashamba ya mbegu ya Kilangali, Msimba na Dabaga ambayo yameathiriwa na tindikali amepatikana.

Uzalishaji wa Vipando

85. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha wakulima wanapata miche bora kwa gharama nafuu na kwa wakati, Wizara kupitia taasisi zake na kwa kushirikiana na wadau katika mwaka 2025/2026 imezalisha na kusambaza miche 37,502,071 kwa wakulima kwa mpango wa ruzuku katika mikoa ya uzalishaji. Kati ya hiyo, miche ya kahawa ni 27,702,090, mkonge 2,480,000, chai 1,634,250, parachichi 533,316, korosho 4,444,580, zabibu 342,000, migomba 314,412, kakao 40,044, karafuu 5,470, chikichi 4,491 na miembe 1,418. Aidha, pingili za muhogo 5,124,429 zimesambazwa kwa wakulima katika mikoa ya Kigoma, Kagera, Morogoro, Mwanza na Pwani.

Mhe: Daniel G. Chongolo (Mb), Waziri wa Kilimo akikagua kitalu cha uzalishaji wa miche ya korosho – TARI Naliendele

4.1.3 Uwekezaji kwenye Utoaji wa Ruzuku ya Mbolea na Viuatilifu

a) Upatikanaji wa Mbolea

86. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026, Wizara kupitia TFRA ilipanga kuratibu upatikanaji wa tani 1,500,000 za mbolea. Kati ya hizo, TFC ilipanga kununua na kusambaza mbolea tani 200,000 kwa ajili ya mazao ya chakula; kununua mbolea tani 133,000 kwa ajili ya zao la tumbaku na tani 500 kwa ajili ya zao la chai. Vilevile, Wizara ilipanga kununua tani 200,000 za mbolea na chokaa mazao tani 50,000 katika viwanda vya ndani. Pia, kuanza ujenzi wa kiwanda cha kuzalisha mbolea aina ya *Triple SuperPhosphate* – (TSP) na kuanzisha mradi wa kuchimba, kufungasha na kusambaza chokaa mazao katika eneo la Visiga Mkoa wa Pwani.

87. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, hadi Machi 2026, Wizara imetekeleza yafuatayo:-

88. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuratibu upatikanaji wa mbolea nchini ili kuwawezesha wakulima kupata na kutumia mbolea kwa lengo la kuongeza uzalishaji na tija ya mazao ya kilimo. Hadi Machi 2026, Wizara kupitia TFRA imeratibu upatikanaji

wa tani 1,254,203 sawa na asilimia 83.61 ya lengo la tani 1,500,000 katika mwaka 2025/2026. Kati ya kiasi kilichopatikana, tani 150,686 zimezalishwa ndani ya nchi, tani 869,840 zimeingizwa kutoka nje ya nchi na tani 233,677 ni bakaa ya msimu uliopita.

89. ***Mheshimiwa Spika,*** kati ya kiasi kilichopatikana, tani 674,686.24 za mbolea zenye thamani ya Shilingi 1,210,737,644,482 zimesambazwa kwa wakulima kwa mpango wa ruzuku katika mikoa yote na usambazaji unaendelea. Kati ya kiasi hicho, Shilingi 929,155,586,025 ni mchango wa wakulima na Shilingi 281,582,058,457 ni ruzuku ya Serikali. Hatua hiyo imeongeza kiwango cha matumizi ya mbolea kutoka kilo 19 za virutubisho mwaka 2021/2022 hadi kufikia wastani wa kilo 27 za virutubisho kwa hekta mwaka 2025/2026 ambayo ni sawa na asilimia 54 ya lengo la kilo 50 za virutubisho kwa hekta kulingana na azimio la CAADP.

90. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuiwezesha Kampuni ya Mbolea Tanzania (TFC) ili kuongeza upatikanaji wa mbolea nchini. Katika kutekeleza hilo, TFC imenunua tani 150,618 za mbolea, ambapo tani 126,345 zimesambazwa kwa wakulima kwa mpango wa ruzuku. Aidha, kati ya tani za mbolea zilizosambazwa, tani 69,751 ni kwa ajili ya mazao ya chakula na tani 56,594 ni kwa ajili ya tumbaku. Vilevile, ili kupunguza gharama za mbolea na uzalishaji wa mazao, TFC imenunua malori matano (5) yenye uwezo wa kubeba tani 10 kila moja kwa ajili ya kuwezesha usambazaji wa mbolea kwenda vijijini.

91. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha uhifadhi wa mbolea nchini kwa lengo la kuwa na mbolea yenye ubora na ya kutosha, Wizara kupitia TFC imekarabati ghala za kuhifadhi mbolea zilizopo katika mikoa ya Njombe (tani 18,000) na Ruvuma (tani 15,000). Ukarabati wa ghala hizo utaongeza uwezo wa uhifadhi na upatikanaji wa mbolea katika mikoa ya Njombe na Ruvuma.

92. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuongeza uzalishaji wa mbolea ndani ya nchi, usimikaji wa mitambo ya kuchanganya mbolea (Bulk Blending Facilities) katika Mkoa wa Dar es Salaam yenye uwezo wa kuchanganya tani 120 kwa saa, sawa na tani 300,000

kwa mwaka umefikia asilimia 50. Aidha, TFC kwa kushirikiana na TFRA imesaini mkataba wa awali na wazalishaji wa ndani wa mbolea nchini ili kuwawezesha kuzalisha tani 200,000 za mbolea na tani 50,000 za chokaa mazao.

93. ***Mheshimiwa Spika,*** pia, TFC imepata eneo lenye ukubwa ekari 97.3 katika eneo la viwanda lililopo Amboni, Kata ya Mzizima Mkoa wa Tanga, kwa ajili ya kuanzisha mradi wa kiwanda cha kuchimba, kufungasha na kusambaza chokaa mazao.

Mkurugenzi wa Kampuni ya Mbolea Bw. Samuel Mshote akiwa Bandari ya Dar es salaam akisimamia zoezi la ufungaji wa mbolea za TFC

94. ***Mheshimiwa Spika,*** ninapenda kutumia nafasi hii kuzishukuru kampuni zilizoanzisha viwanda vya kutengeneza mbolea hapa nchini kwa uwekezaji wao ambao umechangia kufikiwa kwa mafanikio tunayojivunia katika sekta ya kilimo mazao. Kwa namna ya kipekee ninaishukuru Halmashauri ya Wilaya ya Kinondoni kwa kuanzisha Kiwanda cha Mboji Mabwepande na Halmashauri ya Wilaya ya Moshi kwa kuanzisha Kiwanda cha Moshi Composit vinavyotengeneza mbolea hai kwa kutumia taka zilizooza. Mchango wao si tu unalenga kuimarisha uzalishaji na tija ya mazao ya kilimo bali unalenga pia kutunza na kuhifadhi mazingira.

Ninatoa rai kwa Halmashauri nyingine nchini kuiga mfano huo kwa kuwekeza kwenye viwanda vya kutengeneza mbolea hai kwa kutumia fursa ya taka ozo ambazo zinapatikana kwa wingi katika maeneo yao. Ikiwa na lengo pia la kusafisha na kutunza

mazingira. Kwa mfano Jiji la Dar Es Salaam kwenye dampo la Pugu, kwanza itasaidia kupunguza taka na kuzalisha mbolea hai.

b) Upatikanaji wa Viuatilifu na Udhibiti wa Visumbufu vya Mazao na Mimea

95. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2025/2026, ilipanga kununua lita 125,500 za viuatilifu kwa ajili ya kudhibiti milipuko ya visumbufu vya mimea na mazao. Vilevile, ilipanga kununua ndege moja (1) na ndege nyuki 20; kuzalisha wadudu rafiki na kusajili viuatilifu hai; kujenga Ofisi za TPHPA Makao Makuu; kukagua maduka 4,000 ya viuatilifu; na kuanzisha vituo vya kilimo anga katika mikoa ya Mwanza, Dodoma na Mbeya.

96. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, hadi Machi 2026, Wizara kupitia TPHPA imepata mzabuni kwa ajili ya ununuzi wa lita 58,757 za viuatilifu vya kudhibiti milipuko ya visumbufu vya mimea na mazao. Viuatilifu hivyo vinajumuisha lita 8,500 kwa ajili ya kudhibiti kwelea kwelea, lita 780 kwa ajili ya kudhibiti nzige, lita 46,227 kwa ajili ya kudhibiti viwavijeshi vamizi na lita 750 kwa ajili ya kudhibiti nzi wa matunda na kilogramu 2,500 kwa ajili ya kudhibiti panya.

97. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha udhibiti wa visumbufu vya mlipuko, Wizara kupitia TPHPA imeendelea kuwekeza katika upatikanaji wa vifaa na teknolojia ya udhibiti kwa njia ya anga. Katika kuhakikisha hilo, mzabuni kwa ajili ya ununuzi wa ndege nyuki 20 za udhibiti wa visumbufu vya mimea na mazao amepatikana.

98. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, imekamilisha usajili na kibali cha kuruka kwa ndege iliyonunuliwa ili kutoa huduma za kudhibiti visumbufu vya mimea na mazao mfano kwelea kwelea na nzige badala ya kutegemea ndege kutoka nje ya nchi. Ndege hiyo aina ya *Thrush 510P2+* ina uwezo wa kubeba lita 1,930 za viuatilifu pamoja na mbolea au mbegu mita za ujazo 1.9. Pia, ndege hiyo inauwezo wa kunyunyuzia viuatilifu kwenye eneo lenye ukubwa wa takriban hekta 3,000 kwa siku.

99. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha udhibiti wa visumbufu vya mazao na mimea kwa njia ya kibailojia kwa lengo la kupunguza matumizi ya viuatilifu vya viwandani, Wizara kupitia TPHPA imezalisha wadudu rafiki takriban 21,000 aina ya *Trichogramma* na *Telenomus remus spp*. kwa ajili ya udhibiti wa viwavijeshi vamizi; *Diadegma spp*. na *Cotesia spp*. kwa ajili ya kudhibiti nondomgongo almasi (DBM) ambao hushambulia mazao ya bustani aina ya kabichi na spinachi na funza wa mashina; na *Cyrtobagous salviniae* kwa ajili ya kudhibiti gugu la kariba na minyoo rafiki (EPNs) aina ya *Steinernema spp*. na *Heterorhabditis spp*. kwa ajili ya udhibiti wa viwavijeshi vamizi (Fally Armyworm), nondomgongo almasi (DBM) na funza wa *White grub*. Aidha jumla ya wakulima 2,300 na maafisa ugani 39 wamepatiwa mafunzo kuhusu udhibiti wa visumbufu vya mimea kwa njia ya kibaolojia.

100. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na uwepo wa viuatilifu bandia na chakavu nchini ambavyo vinaweza kusababisha madhara kwa wananchi, wanyama na mazingira. Wizara kupitia TPHPA, ilifanya mapitio ya kina ya viuatilifu vilivyosajiliwa nchini na kuainisha viuatilifu hatarishi vinavyoweza kusababisha madhara kwa binadamu, wanyama na mazingira. Wizara imeviondoa viuatilifu 130 vilivyobainika kuwa na viambata hatarishi na imebaini viuatilifu 675 ambavyo usajili wake haukuhuishwa. **Kiambatisho Na. 2**. Orodha ya viuatilifu vilivyoondolewa sokoni.

101. ***Mheshimiwa Spika,*** TPHPA imekagua maduka 1,404 na ghala 41 za viuatilifu na kubaini kuwa leseni za uendeshaji wa maduka 59 zimeisha muda. Hivyo, maduka hayo yamesitishiwa utoaji wa huduma hadi watakapohuisha leseni za uendeshaji wa maduka hayo.

Nitoe rai kwa wafanyabiashara wa viuatilifu nchini kuhakikisha wanafuata Sheria, taratibu na kanuni inayosimamia biashara ya viuatilifu nchini. Serikali haitasita kuchukua hatua kali za kisheria kwa mfanyabiashara atakayeuza viuatilifu visivyothibitishwa, visivyokidhi ubora au kufanya biashara ya viuatilifu bila ya vibali ili kuwalinda wananchi, wanyama na mazingira.

4.1.4 Usajili wa Wakulima na Urasimishaji wa Shughuli za Kilimo

102. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2025/2026 ilipanga kuendelea kurasimisha shughuli za kilimo kwa kusajili wakulima, wafanyabiashara wa mazao ya kilimo, watoa huduma za ugani, ghala na pembejeo za kilimo. Vilevile, Wizara kupitia TFRA ilipanga kuendelea kutoa hatimiliki na kadi za kielektroniki (smart card) kwa wakulima 10,000.

103. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, hadi Machi 2026, wakulima 686,794 wamesajiliwa katika mfumo wa kielektroniki wa Ruzuku ya Pembejeo (Agricultural Inputs Subsidy System) na kufanya idadi ya wakulima waliosajiliwa kufikia 5,433,147 kati ya hao, wanawake 1,942,869 na usajili unaendelea. Kati ya waliosajiliwa, wakulima 12,833 kati ya hao wanawake 3,191 wamepewa hatimiliki na kadi za kielektroniki (smart card) kwa ajili ya kuwawezesha kupata huduma mbalimbali ikiwemo ununuzi wa pembejeo. Aidha, utoaji wa hatimiliki na kadi za kieletroniki unaendelea.

104. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha usambazaji wa mbolea kwa wakulima nchini, Wizara kupitia TFRA imesajili katika mfumo wa kielektroniki (Agricultural Inputs Subsidy System) waagizaji (Kampuni za mbolea) 70, mawakala wa mbolea 8,785 na Vyama vya Ushirika 2,571 kuwa mawakala wa mbolea. Pia, jumla ya vituo 14,480 vya mauzo ya mbolea vimefunguliwa katika mikoa yote nchini. Kadhalika, wafanyabiashara wa mazao ya kilimo 2,452 wamesajiliwa kwa lengo la kuwatambua na kuimarisha usimamizi wa biashara za mazao.

105. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha viwango vya kitaalamu, ushirikiano na wakulima, ufuatiliaji na uwajibikaji kwa Maafisa ugani nchini unaimarishwa, Wizara imesajili watoa huduma za ugani 8,472. Kati ya hao, 6,618 ni Maafisa Ugani wa Serikali na 1,854 ni Maafisa Ugani wa sekta binafsi na usajili unaendelea.

Nitoe rai kwa maafisa ugani wa sekta binafsi kuendelea kujisajili katika mfumo ili kutambulika na kuendelea kutoa huduma kwa wakulima wakiwa rasmi.

106. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuratibu hifadhi ya chakula nchini na kuboresha miundombinu ya uhifadhi, Wizara imesajili ghala 2,431. Kati ya hizo, ghala 637 ni za Serikali na ghala 1,794 ni za sekta binafsi na usajili unaendelea.

4.1.5 Kuwekeza kwenye Ujuzi kwa Wataalam wa Ndani

107. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2025/2026, ilipanga kuwawezesha watumishi 151 kupata mafunzo ya muda mrefu na mfupi katika vyuo vya ndani na nje ya nchi. Ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, hadi Machi 2026, watumishi 583 wamepatiwa mafunzo mbalimbali ili kuendana na mahitaji ya taaluma. Kati ya hao, watumishi 71 wamejiunga na mafunzo ya muda mrefu na watumishi 512 ni wa mafunzo ya muda mfupi. Aidha, watumishi wanaohudhuria mafunzo ya muda mrefu wamegawanyika katika makundi yafuatayo:- Shahada ya uzamivu 43, Shahada ya uzamili 23, Shahada ya kwanza wawili (2) na Stashahada watatu (3).

4.1.6 Uwekezaji kwenye Huduma za Ugani

108. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026, Wizara ilipanga kununua na kusambaza vitendea kazi kwa Maafisa Ugani ikiwemo magari 100, vishikwambi 3,000 na mavazi maalum ya utambulisho 5,000; kuendelea na ujenzi wa miundombinu kwenye viwanja vya maonesho ya wakulima vya Dkt. John Samuel Malecela (Dodoma) na John Mwakangale (Mbeya); na kuanza ujenzi wa uzio katika viwanja vya Ipuli (Tabora). Aidha, Wizara ilipanga kukamilisha taratibu za uanzishaji wa Wakala wa Huduma za Ugani wa Taifa (NAESA) na kuanzisha mfumo wa huduma za ugani wa kidijiti ili kuwezesha upatikanaji wa huduma za ugani kwa sekta binafsi.

109. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ilipanga kujenga nyumba 50 za Maafisa Ugani; kuendelea kuimarisha vituo vinane (8) mahiri vya

usambazaji na uhaulishaji wa teknolojia; kushirikiana na VETA na CAMARTEC kutoa mafunzo kuhusu uhaulishaji na matumizi ya teknolojia za zana za kilimo; kukarabati miundombinu ya vituo vya uhaulishaji wa teknolojia za kilimo; kujenga miundombinu ya Chuo cha Taifa cha Sukari Kidatu; kutoa mafunzo kwa wakulima 20,000; kutoa mafunzo rejea kwa Maafisa Ugani 7,000; na kugharamia mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi 1,920 wa ngazi ya Stashahada.

110. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, hadi Machi 2026 Wizara imetekeleza yafuatayo:-

111. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha utoaji wa huduma za ugani kwa wakulima nchini, Wizara imeanza ununuzi wa vitendea kazi kwa Maafisa Ugani ambapo magari 18 kati ya 60 yamenunuliwa. Vilevile, taratibu za ununuzi wa vishikwambi na mavazi maalum ya Maafisa Ugani zinaendelea. Aidha, ujenzi wa awamu ya kwanza ya miundombinu kwenye viwanja vya maonesho vya Nanenane vya Dkt. John Samuel Malecela - Dodoma umefikia asilimia 75 na katika viwanja vya John Mwakangale – Mbeya umefikia asilimia 12. Kukamilika kwa ujenzi wa viwanja hivyo kutawezesha kutoa mafunzo kwa wakulima na wadau wengine kwa mwaka mzima. Aidha, maboresho ya viwanja vingine yanaendelea.

112. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha utoaji wa huduma za ugani, Wizara inaendelea kukamilisha taratibu za kuanzisha Wakala ya Taifa wa Huduma za Ugani Kilimo (National Agricultural Extension Services Agency - NAESA) ambao inatarajiwa kuanza rasmi tarehe 01 Julai, 2026. Wakala huo, utawezesha kuongeza ufanisi wa huduma za ugani, kuratibu na kusimamia shughuli za ugani na kuhaulisha teknolojia kutoka kwa watafiti na wadau wengine kwenda kwa Maafisa Ugani na wakulima. Pamoja na uanzishaji wa NAESA, Wizara imeendelea kuboresha mfumo wa kutoa huduma za ugani kidijiti ambao umewawezesha wakulima kutumia simu za mkononi kupata ushauri wa kitaalam kuhusu uendelezaji wa mazao ya kilimo nchini.

113. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuimarisha vituo mahiri vya uhaulishaji wa teknolojia za kilimo vya TARI kwa kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika vituo viwili (2) vya Dkt. John Samuel Malecela - Dodoma na Mwl. Julius Kambarage Nyerere – Morogoro. ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika vituo sita (6) vya uhaulishaji na usambazaji wa teknolojia katika viwanja vya Fatuma Mwasa - Tabora, John Mwakangale - Mbeya, Nyakabindi - Simiyu, Nyamuhongolo - Mwanza, Themi - Arusha na Ngongo – Lindi umefikia wastani wa asilimia 20. Hatua hiyo itawawezesha wakulima na watoa huduma za kilimo kupata ujuzi na maarifa kuhusu kilimo kwa kipindi cha mwaka mzima.

114. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea kuboresha mazingira ya utendaji kazi wa maafisa ugani ambapo ujenzi wa nyumba 29 za Maafisa Ugani katika mikoa ya Kigoma, Pwani, Tanga, Singida, Tabora, Mbeya, Kilimanjaro, Njombe, Ruvuma, Shinyanga, Arusha, Dar es Salaam, Songwe na Simiyu umekamilika. Aidha, ujenzi wa nyumba 21 umefikia wastani wa asilimia 90 na fedha kwa ajili ya ujenzi wa nyumba 34 katika mikoa 19 zimepelekwa katika Halmashauri husika ili kuanza ujenzi. Ujenzi wa nyumba hizo utawezesha upatikanaji wa huduma za ugani kwa wakati, kujenga uhusiano wa karibu na wakulima, kupunguza gharama za uendeshaji na kuongeza hamasa na ari ya kazi. Vilevile, jitihada za kuimarisha matumizi ya vituo vya Rasilimali za Kilimo vya Kata zinaendelea ikiwemo kutumika kama vituo vya zana jumuishi za kilimo na mafunzo kwa wakulima.

115. ***Mheshimiwa Spika,*** pia, Wizara kwa kushirikiana na sekta binafsi imetoa mafunzo kuhusu uhaulishaji na matumizi sahihi ya zana za kilimo kwa wasimamizi na waendesha mitambo 662 katika mikoa 17 ya Tanzania. Katika kuboresha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia, Wizara inaendelea na ukarabati wa miundombinu ya Kituo cha Mafunzo kwa Wakulima Mkindo ambapo ukarabati umefikia asilimia 55. Kadhalika, wakandarasi kwa ajili ya kuanza ukarabati wa miundombinu katika Vyuo vya Mafunzo ya Kilimo vya Igurusi na Mlingano wamekabidhiwa maeneo kwa ajili ya kuanza kazi. Pia, mkandarasi kwa ajili ya

kuanza ujenzi wa bweni la kisasa la Chuo cha Taifa cha Sukari Kidatu amekabidhiwa eneo kwa ajili ya kuanza ujenzi.

116. *Mheshimiwa Spika,* Wizara imetoa mafunzo kwa wakulima 23,444 kuhusu uzalishaji wa mazao ya kilimo kibiashara kupitia vituo vya mafunzo ya kilimo; na mafunzo rejea kwa Maafisa Ugani 1,753 kuhusu utoaji wa huduma za ugani kidijiti kupitia *e-kilimo*. Aidha, wanafunzi 2,075 wa ngazi ya Astashahada na Stashahada wamegharamiwa mafunzo kwa vitendo katika Vyuo vya Mafunzo ya Kilimo.

4.1.7 Kupima Afya ya Udongo kwa Wakulima Wadogo na Wakubwa

117. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2025/2026, Wizara ilipanga kuendelea na upimaji wa afya ya udongo na kuchora ramani za kidijiti zinazoonesha hali ya afya ya udongo; kununua na kusambaza *soil scanner* 43; na kujenga ofisi tatu (3) za usimamizi na mipango ya matumizi ya ardhi ya kilimo.

118. ***Mheshimiwa Spika***, ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Machi 2026, Wizara imetekeleza yafuatayo:-

119. ***Mheshimiwa Spika***, ili kuwawezesha wakulima kujua aina sahihi ya mbolea ya kutumia na mazao yanayotakiwa kupandwa kwenye maeneo yao, Wizara inaendelea na upimaji wa afya ya udongo nchini. Ili kutekeleza lengo hilo, Wizara imekusanya sampuli za udongo katika eneo la kilimo lenye ukubwa wa hekta 30,261,888.47 katika mikoa 15. Hatua hii imewezesha kuongezeka kwa eneo lililochukuliwa sampuli kufikia hekta 40,134,605.80 katika mikoa 19 ya Singida, Shinyanga, Dodoma, Simiyu, Geita, Mwanza, Mara, Kagera, Kigoma, Lindi, Pwani, Mtwara, Morogoro, Tabora, Tanga, Arusha, Manyara, kilimanjaro na Ruvuma. Aidha, uchukuaji wa sampuli unaendelea katika mikoa iliyobaki ya Tanzania Bara, na ukamilishaji wa ramani za awali za afya ya udongo unaendelea. Mchanganuo wa maeneo yaliyochukuliwa sampuli

za afya ya udongo unapatikana katika **Kiambatisho Na. 3**.

Maafisa kutoka wizara ya kilimo kwa kushirikiana na Maafisa kutoka TARI wakichukua sampuli ya udongo kwa ajili ya utafiti, katika Mkoa wa Singida

120. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha utoaji wa huduma ya upimaji wa afya ya udongo kwa kila Halmashauri nchini, Wizara imetangaza, zabuni kwa ajili ya ununuzi wa vipima afya ya udongo (soil scanner) 43. Sambamba na upimaji wa afya ya udongo, Wizara imebaini uwepo wa tindikali katika udongo kwenye baadhi ya maeneo inayoathiri tija na uzalishaji wa mazao ya kilimo. Hivyo, Wizara imetoa mafunzo kuhusu kurejesha afya ya udongo kwa Maafisa Ugani 185 na wakulima 18,749 katika mikoa ya Njombe, Iringa na Katavi ikiwa ni maeneo ya majaribio kupitia **Mradi wa Ruzuku Makini kwa kutumia chokaa mazao**.

121. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha miundombinu kwa ajili ya huduma za usimamizi na matumizi sahihi ya ardhi ya kilimo kwa wakulima, Wizara inaendelea na usanifu wa michoro kwa ajili ya ujenzi wa ofisi za Usimamizi na Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Kilimo katika Kanda ya Ziwa (Mwanza) na Mashariki (Morogoro).

4.1.8 Uendelezaji wa Kilimo cha Umwagiliaji

122. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji katika mwaka 2025/2026 ilipanga kuendelea na utekelezaji wa miradi 768 kati ya 780 iliyoanza kutekelezwa

mwaka 2022/2023 hadi 2024/2025. Miradi hiyo inahusisha ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika skimu mpya 60 (hekta 147,433.46); ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji katika skimu 41 (hekta 72,175); ujenzi wa mabwawa 19 (mita za ujazo 326,449,973); kuanza ujenzi wa mabwawa 28 (mita za ujazo 487,361,277); kuendelea na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa mabwawa 65; ujenzi wa skimu katika mabonde 14 ya kimkakati na kukamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa mabonde nane (8).

123. *Mheshimiwa Spika,* vilevile, ilipanga kujenga miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba matatu (3) ya Membe, Ndogowe na Chinangali; kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa mashamba matatu makubwa katika mikoa ya Kigoma, Kagera na Njombe; na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa skimu 429 na kuanza ujenzi/ukarabati wa skimu 98 ambazo upembuzi na usanifu umekamilika.

124. *Mheshimiwa Spika,* pia, Tume ilipanga kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika mabonde ya mto Ngono na Bugwema yenye jumla ya hekta 22,770; kuendelea na ujenzi wa mabwawa ya Mbakiamtuli na Ngorongo katika bonde la Rufiji yenye jumla ya mita za ujazo 57,548,653; kuanzisha mfumo wa usimamizi wa mashamba ya Mbarali Estate (ekari 6,437.5), Membe (ekari 2,500), Bugwema (ekari 7,500), Madibira (ekari 8,000) na Lumpungu (ekari 18,045); na kujenga mabwawa mawili (2) ya Dudumizi na Mambi katika shamba la Mbarali Estate.

125. *Mheshimiwa Spika,* vilevile, Wizara ilipanga kukamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na kuanza ujenzi wa miradi ya umwagiliaji kwa ajili ya kutumia maji ya Ziwa Victoria na Tanganyika kwa shughuli za kilimo; kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa sita (6); kukamilisha ujenzi wa Ofisi ya Umwagiliaji ya Makao Makuu; kuendelea na ujenzi wa Ofisi za mikoa 19 na Wilaya 13 na ukarabati wa ofisi nne (4) za mikoa; kununua pikipiki 100, magari 30 na mitambo mitatu (3); na kujenga maabara moja (1) ya uhakiki wa ubora wa ujenzi katika Mkoa wa Dodoma.

126. *Mheshimiwa Spika,* Wizara kupitia Tume ilipanga, kutoa mafunzo ya uendeshaji, usimamizi na matunzo ya miundombinu ya umwagiliaji kwa wakulima viongozi 3,000 na kusajili Vyama vya Umwagiliaji 300.

127. *Mheshimiwa Spika,* ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Machi 2026, Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imetekeleza yafuatayo:-

Ujenzi na ukarabati wa skimu na mabwawa

128. *Mheshimiwa Spika,* Wizara kupitia Tume imekamilisha ujenzi wa miradi 28 ya umwagiliaji inayohusisha ujenzi wa skimu mpya 10 zenye uwezo wa kumwagilia eneo lenye ukubwa wa hekta 10,300; ukarabati wa skimu tisa (9) zenye uwezo wa kumwagilia ukubwa wa hekta 10,760; na ujenzi wa mabwawa saba (7) yenye mita za ujazo milioni 53.2 yenye uwezo wa kumwagilia eneo lenye ukubwa wa hekta 10,141. Pia, ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika shamba la Ndogowe (hekta 2,000) na Chinangali I (hekta 88) umekamilika. Miradi iliyokamilika itanufaisha jumla ya wakulima 98,500 kwa kuwawezesha kulima kwa kipindi chote cha mwaka.

129. *Mheshimiwa Spika,* vilevile, Tume inaendelea na ujenzi wa miradi 118 ambapo, kati ya hiyo miradi 18 utekelezaji umefikia zaidi ya asilimia 50; miradi 52 utekelezaji upo chini ya asilimia 50 na miradi 48 ipo katika hatua za awali za utekelezaji. Orodha ya miradi ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji iliyotekelezwa imeoneshwa kwenye **Kiambatisho Na. 4.**

Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa skimu na mabwawa

130. *Mheshimiwa Spika*, Tume imekamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa skimu 120, mabwawa 51, mabonde ya kimkakati 15 na mashamba ya pamoja matatu (3). Vilevile, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa sita (6) ya Dabalo, Buigiri, Hombolo, Kimagai, Kidete na Ikowa umefikia wastani wa asilimia 25. Mabwawa hayo

yatatumika kuzuia mafuriko katika reli ya kati na kutumika katika shughuli za kilimo cha umwagiliaji.

131. ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, Tume imekamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa skimu mbili (2) za Mbakiamtuli na Ngorongo kati ya skimu sita (6) zilizopo katika bonde la Rufiji ambapo zabuni kwa ajili ya kuwapata wakandarasi wa ujenzi wa skimu hizo zimetangazwa. Aidha, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa skimu zilizobaki katika bonde la Rufiji pamoja na mabonde ya Manonga – Wembere, Ruhuhu, Malagarasi, Kalilankululu, Songwe na Kiru – Magara umefikia wastani wa asilimia 54.3. Kadhalika, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa skimu 389 umefikia wastani wa asilimia 36 na mabwawa 49 umefikia wastani wa asilimia 38. Orodha ya miradi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina imeoneshwa kwenye **Kiambatisho Na. 5.**

132. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume imekamilisha taratibu za umiliki wa Shamba la Bugwema na kupata hatimiliki ya shamba hilo. Aidha, mkandarasi amekabidhiwa shamba kwa ajili ya kuanza ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji. Vilevile, mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa skimu katika bonde la Mto Ngono amepatikana.

133. ***Mheshimiwa Spika,*** kadhalika, Wizara kupitia Tume imeingia makubaliano na Halmashauri ya Kibondo kuhusu ujenzi, uendeshaji na usimamizi wa Shamba la Lumpungu. Aidha, mkandarasi wa ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika shamba hilo amepatikana. Pia, tathmini ya shamba la Mbarali Estate imekamilika na taratibu za malipo ya fidia zinaendelea. Vilevile, Tume imehamasisha uanzishwaji wa umoja wa wakulima kwa ajili ya uendeshaji na usimamizi wa shamba la Membe.

134. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inaendelea kuhakikisha kuwa wakulima wa nchi hii wananufaika na rasilimali ya maji iliyopo kwa ajili ya shughuli za kilimo ili kuongeza uzalishaji na kukuza Uchumi wao. Katika kufanikisha azma hiyo, Wizara inaendelea kushirikiana na Wizara ya Maji kuhakikisha azma ya Serikali ya kutumia maji ya Ziwa Victoria na Tanganyika kwa ajili ya shughuli za umwagiliaji inatekelezwa. Kukamilika kwa ujenzi wa mradi huo utanufaisha

wakulima wa mikoa 12 ya Simiyu, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Kigoma, Mwanza, Geita, Mara, Kagera, Rukwa na Katavi, Wilaya 69, Kata 192 na Vijiji 943.

135. ***Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa ofisi ya Makao Makuu ya Tume iliyopo Mkoa wa Dodoma - Njedengwa umefikia asilimia 98; ujenzi wa ofisi nne (4) za mikoa ya Kilimanjaro, Kigoma, Iringa na Songwe umefikia wastani wa asilimia 10.5; na ujenzi wa ofisi 14 za wilaya za umwagiliaji katika wilaya za Chamwino (1), Mbulu (2), Ngorongoro (1), Tunduru (1), Morogoro (1), Chalinze (1), Momba (1), Musoma (1), Igunga (1), Nzega (1), Kwimba (1), Uyui (1) na Masasi (1) umefikia wastani wa asilimia 13.8. Aidha, Tume imenunua *supporting truck* 16 na *semi trailer* mbili (2) kwa ajili ya kubeba vifaa vya uchimbaji wa visima. Usanifu kwa ajili ya ujenzi wa maabara ya uhakiki wa ubora wa ujenzi katika Mkoa wa Dodoma umekamilika.

136. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Tume imetoa mafunzo ya uendeshaji, usimamizi na matunzo ya miundombinu ya umwagiliaji kwa wakulima 2,073 katika skimu 13. Aidha, Tume imesajili Vyama vya Umwagiliaji 99 na kufanya jumla ya vyama vilivyosajiliwa kufikia 1,013.

4.1.9 Uanzishaji wa Vituo vya kutoa Huduma na Ununuzi wa Zana za Kilimo

137. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026, Wizara ilipanga kuanzisha vituo 1,000 vya kutoa huduma ya zana za kilimo kwa wakulima; kununua trekta 10,000, *power tiller* 10,000 na mashine za kuvunia na kukaushia; na kutoa mafunzo kuhusu uendeshaji na usimamizi wa zana za kilimo kwa waendesha mitambo, wasimamizi wa vituo na watoa huduma 500.

138. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Machi 2026, Wizara imeanzisha vituo 79 vya kutoa huduma ya zana za kilimo kwa wakulima ambapo trekta 360 na zana zake zimesambazwa katika vituo hivyo na kuanza kutoa huduma kwa wakulima. Aidha, Wizara imenunua mashine mbili (2) zeye uwezo wa kukausha mazao ya nafaka (mahindi na

mpunga) tani 10 kwa saa na kuzisimika katika mikoa ya Mbeya (Mbarali) na Tanga (Korogwe).

139. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha usimamizi na utendaji kazi wa zana za kilimo zilizosambazwa, Wizara imeweka dirisha katika mfumo wa *e - Kilimo* kwa ajili ya kufuatilia utendaji kazi wa zana za kilimo katika vituo vya kutoa huduma za zana za kilimo ili kuhakikisha kuwa zana hizo zinatumika kwa ufanisi katika shughuli za kilimo. Aidha, kupitia mfumo huo, wakulima wataweza kuomba huduma za zana za kilimo, kufanya malipo ya huduma na kutoa taarifa ya utendaji kazi wa zana za kilimo ikiwemo masaa ya kazi na ukubwa wa eneo lililohudumiwa.

140. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuleta ufanisi na uendelevu wa matumizi ya zana hizo katika vituo vilivyanzishwa na vitakavyoanzishwa, Wizara imeandaa Mwongozo wa Uendeshaji wa Vituo vya Kutoa Huduma za zana za Kilimo kwa wakulima. Mwongozo huo utatumika kama nyenzo ya uendeshaji na usimamizi wa vituo hivyo.

Mkutano wa Afrika wa Matumizi Endelevu ya Zana za Kilimo

141. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhamasisha matumizi ya zana za kilimo nchini, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Chakula na Kilimo (FAO) iliratibu mkutano wa kwanza wa Afrika wa Matumizi Endelevu ya Zana za Kilimo uliofanyika Februari 3 - 6, 2026, Jijini Dar es Salaam. Pamoja na mambo mengine wakati wa Mkutano huo, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa, Dkt. Mwigulu L. Nchemba (Mb). alizindua Mkakati wa Pili wa Taifa wa Zana za Kilimo wa Mwaka 2025/2026 – 2035/2036 ambao umeweka Dira inayoonesha malengo na maeneo ya kipaumbele katika kuendeleza matumizi ya zana za kilimo nchini. Pia, Mkutano huo uliazimia mambo yafuatayo:-

a. Kuimarisha mifumo ya utoaji wa huduma za zana za kilimo ikijumuisha upatikanaji wa vipuri, matengenezo pamoja na huduma baada ya mauzo kwa kuzingatia mahitaji ya soko;

b. Kuimarisha majukwaa ya kubadilishana maarifa kwa kuunganisha taasisi za utafiti, watekelezaji, sekta binafsi na watunga Sera ili kubadilishana uzoefu wa maamuzi ya utekelezaji na Sera; na

c. Kuimarisha ushiriki wa vijana na wanawake katika huduma za zana za kilimo kupitia maendeleo ya ujuzi yanayolenga upatikanaji wa mitaji na teknolojia zinazorahisisha kazi ili kuchangia ajira zenye staha.

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb) akikabidhi ndege nyuki Wizara ya Kilimo

4.1.10 Kuendeleza Shoroba za Kilimo na Uzalishaji

142. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo ilipanga kuendelea kuimarisha shoroba nne (4) za kuendeleza kilimo Tanzania (AGCOT) kulingana na ikolojia za kilimo.

143. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, katika mwaka 2025/ 2026, Ofisi ya Mageuzi ya Kilimo (ATO) imeendesha na kuratibu mikutano ya uhamasishaji wa uendelezaji wa shoroba mpya tatu (3) za Kati, Kaskazini na Mtwara. Lengo kuu la mikutano hiyo ni kujenga uelewa wa pamoja kwa Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Makatibu

Tawala wa Mikoa, Wakurugenzi wa Halmashauri, Madiwani, sekta binafsi, na wadau wengine kuhusu dhana ya Shoroba za Kilimo. Kupitia mikutano hiyo, ATO imeimarisha ushiriki wa wadau, kuboresha uratibu wa utekelezaji katika ngazi za mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, na kuhakikisha shoroba zinakuwa kichocheo cha mageuzi ya kilimo nchini.

144. ***Mheshimiwa Spika,*** pia, Wizara kupitia ATO imeandaa rasimu ya Mwongozo wa Uwekezaji, Miundombinu na Vipaumbele vya Mnyororo wa Thamani wa Mazao (Investment Blue Print) na Uwekezaji unaolenga Utunzanji na Uhimilivu wa Mazingira (Investment Green Print). Miongozo hii inalenga kuvutia uwekezaji wa sekta binafsi, washirika wa maendeleo, taasisi za fedha, ushirikishwaji wa Wizara zingine na taasisi zake.

Uzalishaji wa Mazao kwa Mwaka 2025/2026

145. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ilipanga kuendelea kusimamia mikakati ya uzalishaji wa Mazao Asilia ya Biashara, Mazao ya Bustani, Mazao ya Chakula, Mazao ya Mafuta na mazao yenye mahitaji makubwa yanayoagizwa nje ya nchi ili kuongeza tija katika uzalishaji.

Mazao Asilia ya Biashara

146. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026 Wizara ilipanga kuongeza uzalishaji wa mazao asilia ya biashara ikiwemo pamba, kahawa, mkonge, korosho, tumbaku, pareto, kakao na chai kutoka jumla ya tani 1,451,694.11 zilizozalishwa mwaka 2024/2025 hadi tani 2,225,000.

147. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, hadi Machi 2026, uzalishaji wa mazao asilia ya biashara umefikia tani 1,599,945.66 sawa na asilimia 71.9 ya lengo la kuzalisha tani 2,225,000 na ongezeko la asilimia 10.0 ikilinganishwa na tani 1,451,694,11 zilizozalishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2024/2025. Mchanganuo wa malengo na uzalishaji wa mazao asilia ya biashara umebainishwa katika **Jedwali Na. 5**.

Jedwali Na. 5: Malengo na Uzalishaji wa Mazao Asilia ya Biashara (Tani) katika Mwaka 2025/2026

Na.	MAZAO	2025/2026	
		Malengo	Uzalishaji
1	Korosho	700,000	617,683.77
2	Pamba	400,000	222,014
3	Pareto	5,000	2,780*
4	Kahawa	85,000	74,663.60
5	Tumbaku	200,000	185,776
6	Chai	40,000	11,631.48*
7	Mkonge	80,000	64,321.77*
8	Sukari	700,000	410,979.04
9	Kakao	15,000	10,096*
JUMLA		**2,225,000**	**1,599,945.66**

Chanzo: *Wizara ya Kilimo 2026 * Uzalishaji unaendelea*

Zao la Pamba

148. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Bodi ya Pamba Tanzania ilipanga kuongeza uzalishaji wa zao la pamba kufikia tani 400,000 mwaka 2025/2026; kusambaza mbegu bora za pamba tani 28,000, chupa (acrepacks) 12,000,000 na vinyunyizi 100,000 kwa wakulima wa pamba; kununua mashine 20 za kupulizia viuatilifu; kuajiri Maafisa kilimo 2,000 kupitia programu ya BBT; kuzalisha na kusambaza kwa wakulima mbolea hai lita 12,000,000; na kununua na kusimika mtambo wa kuchakata mbegu wenye uwezo wa kuchakata tani 15,000 kwa mwaka.

149. ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi kwa kushirikiana na Tume ya Maendeleo ya Ushirika ilipanga kuratibu ufufuaji wa *Ginnery* mbili (2) zilizopo Mhunze na Uzogole; kushirikiana na MSD na vyama vya ushirika kuanzisha kiwanda cha kuchakata na kutengeneza pamba za hospitali na nyuzi kwa ajili ya kufungia tumbaku; kuanzisha kongani ya pamba (industrial park) katika Mkoa wa Simiyu; kuanza majadiliano na Wizara ya Nishati kuanzisha ruzuku ya umeme kwa kongani ya pamba; kuanza majadiliano na Wizara ya Fedha, Wizara ya Viwanda na Biashara na wadau wa pamba kutengeneza mfumo wa kodi (tax regime); kununua na

kusimika mitambo miwili (2) ya kuzalisha nishati ya kupikia inayotokana na masalia ya miche ya pamba na mitambo minane (8) ya kusokota nyuzi za pamba na kuzalisha vikoi na mitandio. Pia, Bodi ilipanga kuboresha kituo cha mafunzo ya wakulima cha Nyakabindi.

150. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, hadi Machi 2026, uzalishaji wa Pamba umefikia tani 222,014, sawa na asilimia 55.5 ya lengo la tani 400,000. Kutofikiwa kwa malengo ya uzalishaji kumetokana na mtawanyiko wa mvua usioridhisha katika maeneo ya uzalishaji hali iliyosababisha vitumba kudondoka. Aidha, kwa kiasi kikubwa uzalishaji uliopatikana ulitokana na juhudi zilizofanyika za kusambaza pembejeo zenye thamani ya jumla ya Shilingi 61,825,419,000 kwa wakulima 510,919. Pembejeo hizo zinahusisha mbegu bora za pamba tani 21,051 sawa na asilimia 75.18 ya lengo la tani 28,000, chupa (acrepacks) 9,568,258 sawa na asilimia 80 ya lengo la chupa (acrepacks) 12,000,000 na vinyunyizi 80,000 sawa na asilimia 80 ya lengo la vinyunyizi 100,000. Aidha, katika kuongeza uzalishaji wa pamba hai inayozalishwa nchini, Bodi imesambaza mbolea hai lita 408,000 zenye uwezo wa kunyunyuzia hekta 10,200 kwa wakulima wa zao la pamba.

151. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Bodi imenunua mashine 16 za kupulizia viuatilifu (self propelled boom sprayer) sawa na asilimia 80 ya lengo la kununua mashine 20. Mashine hizo zitawezesha wakulima kupunguza adha ya kunyunyuzia viuatilifu kwa kutumia vinyunyizi vya kubeba mgongoni.

Vilevile, katika kuimarisha upatikanaji na utoaji wa huduma za ugani kwenye zao la pamba, Bodi kwa kushirikiana na kampuni zinazonunua pamba, imetoa ajira kwa Maafisa Ugani 761 kupitia programu ya BBT.

Baadhi ya Vijana wa BBT ugani wakiwa na mashine ya kupulizia viuatilifu (self propelled boom sprayer) kwenye Zao la Pamba

152. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha uongezaji thamani wa zao la pamba nchini Bodi, inaratibu upatikanaji wa eneo lenye ukubwa wa ekari 260 katika Halmashauri ya Itilima kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda cha kuchakata na kutengeneza pamba za hospitali na nyuzi kwa ajili ya kufungia tumbaku (cotton twine). Vilevile, tathmini ya awali ya uthaminishaji na uhakiki wa ardhi ya maeneo ya wananchi watakaolipwa fidia ili kupisha ujenzi wa kongani ya pamba (industrial park) imekamilika ambapo jumla ya ekari 342.93 zitafidiwa kwa wananchi 190 katika Kijiji cha Nyamatara, Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi. Pia, eneo kwa ajili ya kusimika mtambo wa kuchakata mbegu za pamba limepatikana katika Halmashauri ya Igunga. Hatua hizo zinalenga kuongeza ajira kupitia uzalishaji wa zao la pamba, thamani na mauzo ya pamba iliyoongezwa thamani.

153. ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi kwa kushirikiana na Tume ya Maendeleo ya Ushirika, imeanza taratibu za ufufuaji wa *Ginnery* ya Mhunze ambapo andiko la mradi kwa ajili ya kupata fedha za ufufuaji limewasilishwa Benki ya Ushirika Tanzania.

Aidha, chama kikuu cha NYANZA kimeingia mkataba wa miaka mitatu (3) na Kampuni ya Mashati Oil Investiment kwa ajili ya kuendeleza *Ginnery* ya Uzogole. Uwepo wa *Ginnery* hizo utawawezesha wakulima wa pamba kuwa na soko la uhakika na kuongeza uzalishaji wa zao hilo.

154. *Mheshimiwa Spika,* Bodi kwa kushirikiana na *International Trade Centre*- ITC imenunua na kusambaza mashine tatu (3) kwa vikundi vya vijana na wanawake vilivyopo Halmashauri ya Ulanga. Mashine hizo zinatumika kusokota nyuzi za pamba; kutengeneza vikoi na mitandio.

Zao la Chai

155. *Mheshimiwa Spika,* katika mwaka 2025/2026, Wizara kupitia Bodi ya Chai Tanzania ilipanga kuongeza uzalishaji wa chai kavu kufikia tani 40,000; kutoa mafunzo kwa wakulima wadogo wa chai 8,000; kufufua mashamba ya chai yenye ukubwa wa hekta 56 katika Wilaya ya Kilolo; kujenga vituo sita (6) vya mizani kwenye maeneo mapya ya uzalishaji wa chai; kubadili mfumo wa uuzaji wa chai wa wakulima wadogo kutoka kuuza chai majani mabichi na kuanza kuuza chai nyeusi; kuwezesha shughuli za mnada wa chai Tanzania; kununua mashine mbili (2) za kuchakata na kuchanganya chai; kuanzisha viwanda sita (6) vya kuchakata chai kavu nyeusi na chai ya kijani; na kuendelea na majadiliano na wamiliki wa kiwanda cha Mvyulu.

156. *Mheshimiwa Spika,* pia, Bodi ilipanga kuwezesha upatikanaji wa hati ya kimataifa (ithibati) ya *Rain Forest Alliance* kwa wakulima wadogo wa chai; kuzalisha na kusambaza miche 2,350,000; kuanzisha maeneo mapya kwa ajili ya uzalishaji wa miche ya chai; na kujenga uzio katika ghala la kuhifadhia chai lililopo Kipawa.

157. *Mheshimiwa Spika,* ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Machi 2026, uzalishaji wa chai kavu umefikia tani 11,631.48. Wizara kupitia Bodi ya Chai Tanzania inaendelea na juhudi za kuendeleza tasnia ya chai nchini, ambapo imeanzisha viwanda viwili (2) vyenye uwezo wa kuchakata tani 150 za chai kavu nyeusi kwa siku na viwanda viwili (2) vya kuchakata tani 20 za chai maalum kwa siku katika Wilaya za Kilolo na Njombe. Viwanda hivyo, vitachochea uzalishaji wa chai na kuimarisha bei ya chai ya mkulima.

158. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Bodi imeendelea na majadiliano na wamiliki wa kiwanda cha Chai cha Lupembe na shamba lenye ukubwa wa ekari 200 katika Mkoa wa Njombe kwa ajili ya kulipa fidia ya kiwanda hicho chenye uwezo wa kuchakata tani 15 za majani mabichi kwa siku ili kurejeshwa na kuendeshwa na wakulima wadogo wa chai. Pia, imefufua mashamba ya chai yenye ukubwa wa hekta 34 katika Wilaya ya Kilolo na hekta 802 za Kampuni ya Eastern Usambara (EUTCO) katika Mkoa wa Tanga.

159. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha chai inayozalishwa nchini inakidhi viwango vinavyohitajika, Bodi imetoa mafunzo kuhusu kanuni za kilimo bora cha zao la chai kwa wakulima wadogo wa chai 24,183. Vilevile, imefanya tathmini kwa ajili ya ujenzi wa vituo viwili (2) vya mizani kwenye maeneo mapya ya uzalishaji wa chai katika Wilaya ya Kilolo ili kuimarisha upimaji wa chai inayovunwa. Pia, imezalisha na kusambaza miche 246,870 ya chai katika Wilaya za Kilolo (64,870) na Mufindi (182,000).

160. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha bei ya chai kavu, Bodi ya Chai Tanzania pamoja na timu ya washauri elekezi inafanya mapitio ya mjengeko wa bei ya majani mabichi ya chai. Aidha, Bodi imeendelea kuratibu uendeshaji wa mnada wa chai unaofanyika kwa njia ya mtandao (Digital Online Tea Auction - DOTA), ambapo bei ya chai kavu imeongezeka kutoka Dola za Marekani 0.98 sawa na Shilingi 2,450 hadi kufikia Dola za Marekani 1.6 sawa na Shilingi 4,000 kwa kilo moja ya chai kavu.

161. ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi imefanya tathmini na kubaini kuwa viwanda 13 vyenye jumla ya uwezo wa kuchakata chai tani 34,510 vimesitisha uchakataji wa majani mabichi ya chai kutoka kwa wakulima. Katika kuhakikisha uchakataji wa chai unaendelea, Serikali imeendelea na juhudi mbalimbali ikiwemo kuhakikisha viwanda hivyo vinaendelea na uzalishaji, kutafuta wawekezaji wapya wa viwanda vya chai na kujenga viwanda vipya. Juhudi hizo zimefanikisha kufunguliwa kwa viwanda vitano (5) kati ya 13 vilivyositisha huduma.

Mheshimiwa Spika, nitoe rai kwa wamiliki wa viwanda vya chai nchini kuendelea kuchakata chai ya wakulima kwa kuwa Serikali inaendelea na mikakati madhubuti ya kufufua na kuendeleza zao la chai. Kwa wale ambao viwanda vyao vitakuwa bado vimesitisha uzalishaji, Serikali itapitia upya mikataba yao ya ubinafsishaji na kuchukua hatua stahiki kwa mujibu wa Sheria.

Zao la Kahawa

162. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Bodi ya Kahawa Tanzania ilipanga kuongeza uzalishaji wa zao la kahawa kufikia tani 85,000; kutoa mafunzo kwa wakulima 20,000 na Maafisa Ugani 500; kuzalisha na kusambaza miche 30,000,000 ya kahawa; kuweka mfumo wa kusimamia uandaaji, usambazaji na utunzaji wa miche; kuwezesha uanzishaji wa mashamba ya kahawa yenye ukubwa wa hekta 4,000; kuchimba visima katika mashamba makubwa ya kahawa (block farm); na kujenga maabara za Tissue culture katika vituo vya TaCRI vya Maruku na Mbozi.

163. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Machi 2026, uzalishaji wa kahawa umefikia tani 74,663.60 sawa na asilimia 87.8 ya lengo la tani 85,000. Uzalishaji huo umefikiwa kwa kutoa mafunzo kuhusu kanuni za kilimo bora cha zao la kahawa na mbinu za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa wakulima 3,360 na Maafisa Ugani 112 katika maeneo ya uzalishaji; na kuchimba visima kumi (10) katika Mkoa wa Songwe (Mbozi) kwa ajili ya umwagiliaji kwenye mashamba ya kahawa ya wakulima wadogo ili kukabiliana na athari za ukame.

164. ***Mheshimiwa Spika***, Bodi kwa kushirikiana na TARI imezalisha na kusambaza miche 27,702,090 ya kahawa kwa mpango wa ruzuku kwa wakulima katika mikoa 17 inayozalisha kahawa nchini, sawa na asilimia 92.3 ya lengo la kuzalisha miche 30,000,000. Lengo ni kuongeza maeneo mapya ya uzalishaji wa kahawa na kuondoa miche ya zamani kwenye mashamba ya muda mrefu. Vilevile, Bodi imewezesha kuanzisha wa mashamba ya kahawa yenye ukubwa wa hekta 347.4 katika mikoa ya Kigoma (hekta 118.2), Ruvuma (hekta 112), Kilimanjaro (hekta 80), Arusha (hekta

20) na Songwe (hekta 17.2). Pia, Wizara imeendelea kuimarisha bustani za kuzalisha mbegu katika vituo vya utafiti vya TARI - TaCRI kwa kuviwekea miundombinu ya umwagiliaji ili kuviwezesha kuzalisha kiasi cha mbegu kinachokidhi mahitaji ya uzalishaji wa miche.

Zao la Korosho

165. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Bodi ya Korosho Tanzania katika mwaka 2025/2026 ilipanga kuongeza uzalishaji wa korosho kufikia tani 700,000; kununua na kusambaza viuatilifu vya korosho tani 30,000 za *Sulphur* na lita 3,800,000 za viuatilifu vya maji; kutoa mafunzo kupitia mashamba darasa 30 kwa wakulima 1,000 na Maafisa Ugani 200; kuzalisha na kusambaza mbegu za korosho tani 150; kuweka mfumo wa kusimamia uandaaji, usambazaji na utunzaji wa mbegu; kuendelea na ujenzi wa viwanda vya kubangua korosho pamoja na kuongeza thamani bidhaa nyingine zitokanazo na korosho katika kongani la viwanda Maranje Wilaya ya Nanyamba; na kutengeneza mfumo wa upatikanaji wa malighafi kwa wabanguaji wadogo.

166. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha uhifadhi na ubora wa korosho, Bodi kwa kushirikiana na Vyama Vikuu vya korosho ilipanga kujenga ghala tatu (3) zenye uwezo wa kuhifadhi jumla ya tani 15,000 katika vyama vya TANECU, MAMCU na CORECU.

167. ***Mheshimiwa Spika***, ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Machi 2026, uzalishaji wa zao la korosho umefikia tani 617,683.77 sawa na asilimia 88.24 ya lengo la tani 700,000. Uzalishaji huo umechangiwa na upatikanaji wa pembejeo kwa wakati zilizonunuliwa kwa fedha za ushuru wa korosho ghafi baada ya mabadiliko ya Sheria ya Tasnia ya Korosho. Wizara imenunua viuatilifu vya korosho vya *Sulphur* ya unga tani 44,177.18 na lita 2,142,874.5 na kuvisambaza kwa wakulima 549,936 kwa ajili ya kudhibiti visumbufu vya zao hilo katika maeneo ya uzalishaji. Kuongezeka kwa uzalishaji kulichangiwa na kuimarika kwa huduma bora za ugani zilizotolewa na vijana walioajiriwa kupitia mradi wa BBT.

168. ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, Bodi kwa kushirikiana na TARI imetoa mafunzo kuhusu kanuni za kilimo bora cha zao la korosho na matumizi sahihi ya viuatilifu kupitia mashamba darasa 500 kwa wakulima 222,332 na Maafisa Ugani 2,699 katika mikoa ya Mtwara, Lindi, Ruvuma, Pwani, Tanga, Singida, Katavi, Kigoma, Mbeya, Njombe, Rukwa, Morogoro, Shinyanga, Tabora, Iringa, Songwe na Dodoma.

169. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha upatikanaji wa miche ya korosho, Bodi kwa kushirikiana na TARI imezalisha na kusambaza mbegu bora za korosho tani 22 zenye uwezo wa kuzalisha miche takriban 3,000,000 kwa wakulima 100,000 katika Halmashauri za Rufiji, Manispaa ya Lindi, Mtama, Nachingwea, Ruangwa, Liwale, Tunduru, Namtumbo, Manispaa ya Mtwara, Mtwara Vijijini, Chunya, Kyela, Mbarali, Momba, Songwe, Nanyamba Mji, Tandahimba, Newala na Ludewa.

170. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhamasisha uwekezaji, upatikanaji wa masoko na uongezaji thamani wa zao la korosho, ujenzi wa kiwanda cha kubangua korosho chenye uwezo wa kubangua tani 50,000 kwa mwaka katika kongani ya viwanda iliyopo Maranje Halmashauri ya Wilaya ya Nanyamba umefikia wastani wa asilimia 55. Vilevile, ujenzi wa viwanda vitatu (3) vya kubangua korosho vyenye uwezo wa kubangua tani 230,000 kwa mwaka vinajengwa kupitia wawekezaji ambao ni Mateak Holdings (tani 100,000), Dorado Cashew Ltd (tani 100,000) na Korosho Investment (tani 30,000). Pia, Bodi imetengeneza mfumo wa upatikanaji wa malighafi kwa wabanguaji wadogo kupitia ghala zinazojengwa katika kongani ya viwanda ya Maranje ambapo wabanguaji watapata malighafi kupitia soko la awali.

171. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha uhifadhi na ubora wa korosho Chama Kikuu cha Ushirika cha TANECU kinaendelea na ujenzi wa ghala tatu (3) zenye uwezo wa kuhifadhi tani 5,000 kila moja. Ujenzi wa ghala hizo umefikia wastani wa asilimia 31. Vilevile, mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa ghala mbili (2) za Chama Kikuu cha Ushirika MAMCU zenye uwezo wa kuhifadhi tani 5,000 kila moja katika Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara amepatikana.

Zao la Mkonge

172. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Bodi ya Mkonge Tanzania katika mwaka 2025/2026, ilipanga kuhamasisha wakulima kuongeza uzalishaji wa zao la mkonge kufikia tani 80,000; kutoa mafunzo ya uongezaji thamani wa mkonge; kuanzisha mashamba makubwa ya pamoja yenye ukubwa wa hekta 2,000; kuwezesha umiliki wa ardhi ya kilimo yenye ukubwa wa hekta 6,000; kuanzisha Chama Kikuu cha Ushirika cha Mkonge; kununua na kusimika mashine 10 za kuchakata mkonge (dikotiketa); kurejesha viwanda na mashamba yaliyokuwa chini ya kampuni ya Sisalana; na kuendelea na ujenzi wa kituo cha uzalishaji wa nzi chuma.

173. ***Mheshimiwa Spika***, ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Machi 2026, uzalishaji wa zao la mkonge umefikia tani 64,321.77 sawa na asilimia 80.4 ya lengo la tani 80,000 na uzalishaji unaendelea. Uzalishaji huo umechangiwa kwa kutoa mafunzo kuhusu uzalishaji wa mkonge na uongezaji thamani wa zao hilo kwa wadau 6,853 na Maafisa Ugani 44 katika mikoa ya Tanga, Morogoro, Pwani, Shinyanga, Simiyu, Tabora, Mara, Singida, Kilimanjaro na Arusha.

174. ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, Bodi imeanzisha mashamba makubwa ya pamoja ya mkonge ya wakulima wadogo yenye ukubwa wa hekta 9,211 katika mikoa ya Morogoro (hekta 1,519), Pwani (hekta 343), Tanga (hekta 6,411) na Kilimanjaro (hekta 938) na imeendelea kuwezesha umiliki wa ardhi ya kilimo yenye ukubwa wa hekta 21,625.5 katika mikoa ya Tanga (hekta 16,027.50), Morogoro (hekta 3,797.50) na Arusha (hekta 1,800). Mashamba hayo yanatarajiwa kuongeza uzalishaji wa mkonge tani 120,000 ifikapo mwaka 2030.

Shamba kubwa la pamoja la zao la mkonge lililopo Wilaya ya Handeni -Tanga

175. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuongeza thamani na uzalishaji wa mkonge nchini, Wizara kupitia Bodi ya Mkonge Tanzania imeanzisha kiwanda kimoja (1) cha kuchakata mkonge chenye uwezo wa kuchakata tani tano (5) kwa siku katika Mkoa wa Tanga. Aidha, mzabuni kwa ajili ya kuanzisha viwanda viwili vya kuchakata mkonge katika Wilaya za Handeni na Mkinga, Mkoa wa Tanga amepatikana. Pia, Bodi imewezesha usajili wa Chama Kikuu cha Mkonge Mkoa wa Tanga (Tanga Sisal Cooperative Union Ltd) kitakacho hudumia vyama vyote vya msingi vinavyojishughulisha na zao la mkonge.

176. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea na ujenzi wa kituo cha uzalishaji wa nzi chuma (Blacksoldier flies) kwa kutumia mabaki ya mkonge (Sisal waste) ili kutengeneza protini kwa matumizi ya mifugo. Aidha, taratibu za urejeshaji wa viwanda na mashamba yaliyokuwa chini ya Kampuni ya Sisalana kwa ajili ya kuongeza uzalishaji na kuwezesha uchakataji wa mkonge zinaendelea.

Zao la Tumbaku

177. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Bodi ya Tumbaku Tanzania ilipanga kuongeza uzalishaji wa zao la tumbaku kufikia tani 250,000 mwaka 2025/2026; kutoa mafunzo kwa wakulima 5,000 na Maafisa Ugani 200 katika maeneo ya uzalishaji; kuratibu ununuzi na usambazaji wa viuatilifu lita 183,571, pakiti 1,468,568 na chupa 2,202,852; kujenga mabani 2,500 ya kukaushia tumbaku na kuanza kutumia teknolojia ya jua na umeme; kununua mitambo

minne (4) ya kuchimba mabwawa na visima katika mashamba ya wakulima; kukamilisha ujenzi wa ofisi; kuratibu ujenzi wa kiwanda cha kuchakata tumbaku; na kuanzisha bandari kavu kwa ajili ya kufungasha tumbaku.

178. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Machi 2026, uzalishaji wa zao la tumbaku umefikia tani 185,776 sawa na asilimia 74 ya lengo la tani 250,000. Uzalishaji huo umechangiwa kwa kutoa mafunzo kuhusu kanuni za kilimo bora cha zao la tumbaku kwa wakulima 5,200 na Maafisa Ugani 182 katika maeneo ya uzalishaji; kununua na kusambaza kwa wakulima viuatilifu aina ya *Flumetralin* lita 130,071 *Imidacloprid* (30g/pkt) pakiti 922,213 na *Deltamethrin* (20ml/chupa) chupa 798,135 kwa ajili ya kudhibiti visumbufu vya zao la tumbaku.

179. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Bodi imejenga mabani mapya 57,282 na kukarabati mabani 2,629 kwa ajili ya kukaushia tumbaku katika mikoa ya Tabora, Shinyanga, Katavi, Ruvuma, Songwe, Mbeya, Geita, Kigoma, Singida na Iringa; na kwa kushirikiana na TARI na Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Nelson Mandela imefanya majaribio ya kukausha tumbaku kwa mitambo inayotumia nishati ya jua katika Halmashauri ya Manispaa ya Tabora na kubaini kuwa viwango vya ubora vya tumbaku iliyokaushwa kwa jua havitofautiani na tumbaku iliyokaushwa kwa kutumia kuni.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nitoe rai kwa wakulima katika maeneo ya uzalishaji wa tumbaku kutumia nishati safi ya jua kwa ajili ya kukaushia tumbaku ili kulinda mazingira.

180. ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi kwa kushirikiana na wadau wa zao la Tumbaku imewezesha ununuzi wa mitambo miwili ya kuchimba visima kwa ajili ya wakulima wa tumbaku. Pia, imechimba visima 17 katika Wilaya ya Chunya na imejenga mabwawa matano (5) katika Wilaya ya Kaliua na Urambo kwa ajili ya kuwawezesha wakulima kupata maji ya kuhudumia vitalu vya tumbaku.

181. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Bodi inaendelea kuboresha mazingira ya kazi ambapo ujenzi wa ofisi za Kanda

katika Halmashauri ya Mpanda umekamilika na katika Halmashauri ya Kaliua umefikia wastani wa asilimia 95. Vilevile, katika kuimarisha uongezaji thamani wa zao la tumbaku, ujenzi wa jengo la kiwanda kinachomilikiwa na Kampuni ya Mkwawa Leaf chenye uwezo wa kuchakata tani 28 kwa siku katika Mkoa wa Tabora umefikia asilimia 75. Aidha, ununuzi wa mashine kwa ajili ya kiwanda hicho unaendelea.

Zao la Pareto

182. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia COPRA ilipanga kuongeza uzalishaji wa zao la pareto kufikia tani 5,000 mwaka 2025/2026; kutoa mafunzo kwa wakulima viongozi 19,000 na wakaguzi wa pareto 50; kupitia TARI kuzalisha mbegu bora za pareto tani mbili (2); kujenga makaushio 150; na kuanzisha kilimo cha mkataba katika zao la pareto na kuzuia usafirishaji wa unga wa pareto kwenda nje ya nchi.

183. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Machi 2026, uzalishaji wa zao la pareto umefikia tani 2,780 sawa na asilimia 55.6 ya lengo la tani 5,000 na uzalishaji unaendelea. Uzalishaji huo umechangiwa kwa kutoa mafunzo kuhusu kanuni za kilimo bora cha zao la pareto kwa wakulima viongozi 74 kupitia mashamba darasa 74 yaliyoanzishwa katika Halmashauri za Mbulu, Arusha Vijijini, Makete, Ileje, Mbeya Vijijini na Ludewa; na kwa kushirikiana na wadau imezalisha na kusambaza mbegu za pareto tani tisa (9) kwa wakulima katika mikoa ya Mbeya, Songwe, Njombe, Iringa na Arusha.

184. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha uongezaji thamani wa pareto inayozalishwa nchini, ujenzi wa makaushio 150 ya maua ya pareto katika Halmashauri za Mbulu (25), Arusha Vijijini (10), Makete (30), Ileje (35), Mbeya Vijijini (40) na Ludewa (10) umefikia wastani wa asilimia 20 na kilimo cha mkataba katika zao la pareto kimeanzishwa ili kuzuia usafirishaji wa unga wa pareto kwenda nje ya nchi kwa lengo la kuongeza thamani na kulinda viwanda vya ndani.

Zao la Kakao

185. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia COPRA katika mwaka 2025/2026, ilipanga kuhamasisha wakulima kuongeza uzalishaji wa kakao kufikia tani 15,000; kutoa mafunzo kwa wakulima viongozi 500 na Maafisa Ugani 45; kujenga miundombinu ya usindikaji na ukaushaji katika vituo saba (7) vya ukusanyaji wa kakao; kuhamasisha uongezaji thamani wa zao la kakao; kusajili wakulima 91,000 wa kakao; kuzalisha miche 1,000,000 na kuisambaza kwa wakulima; na kuwezesha kituo cha TARI Ifakara ili kukifanya kuwa kituo mahiri cha utafiti wa zao la kakao.

186. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Machi 2026, uzalishaji wa zao la kakao umefikia tani 10,069 sawa na asilimia 67.31 ya lengo la tani 15,000 na uzalishaji unaendelea. Uzalishaji huo umechangiwa kwa kutoa mafunzo kuhusu kanuni za kilimo bora kwa wakulima viongozi 456 na Maafisa Ugani 42 katika maeneo ya uzalishaji. Vilevile, ujenzi wa miundombinu ya kusindika na kukausha katika vituo saba (7) vya kukusanyia kakao vilivyopo Kyela (4), Mlimba (1), Mvomero (1) na Muheza (1) umefikia wastani wa asilimia 20. Kukamilika kwa miundombinu hiyo kutasaidia kuimarisha ubora wa uongezaji thamani wa zao la kakao.

187. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha matakwa ya soko la kimataifa la Ulaya, hususan kanuni za kuzuia ukataji wa miti za Umoja wa Ulaya (EUDR) kwa zao la kakao yanazingatiwa, wakulima 29,830 wa kakao na mashamba yao ya uzalishaji yenye jumla ya ekari 88,686 wamesajiliwa katika mikoa ya Tanga, Mbeya na Morogoro. Aidha, katika kuongeza mashamba ya uzalishaji wa kakao na kufidia miche iliyozeeka katika mashamba ya muda mrefu, TARI imezalisha na kusambaza miche 240,044 ya kakao kwa wakulima katika maeneo ya uzalishaji. Aidha, kituo cha TARI Ifakara kimekuwa kituo mahiri cha utafiti wa zao la kakao ambapo vinasaba 293 vya kakao vimekusanywa na kuhifadhiwa katika kituo hicho.

Mazao ya Bustani

188. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia COPRA kwa kushirikiana na wadau katika mwaka 2025/2026 ilipanga kuongeza uzalishaji wa mazao ya bustani kufikia tani 9,000,000; na kutoa mafunzo kwa Maafisa Ugani 1,500 na wakulima 5,000 katika maeneo ya uzalishaji. Ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Machi 2026, uzalishaji wa mazao ya bustani umefikia tani 9,781,236.74 mwaka 2024/2025 sawa na asilimia 108.68 ya lengo la kuzalisha tani 9,000,000; na mafunzo rejea kuhusu kilimo bora cha mazao ya bustani yametolewa kwa Maafisa Ugani 542 na wakulima 1,626 katika maeneo ya uzalishaji.

Mazao ya Bustani yenye Kipaumbele Zao la Parachichi

189. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2025/2026 ilipanga kuhamasisha wakulima kuongeza uzalishaji wa parachichi zinazouzwa nje ya nchi kufikia tani 40,000; kutoa mafunzo kwa wakulima 9,500 na Maafisa Ugani 200; kununua na kusambaza viuatilifu lita 3,000 za viuakuvu na lita 1,000 aina ya *Copper sulphate*; kuhamasisha wakulima kujiunga na Vyama vya Ushirika wa parachichi; kuandaa na kusambaza kwa wakulima mwongozo wa viwango vya uzalishaji wa parachichi na mazao ya viungo; na kutunga kanuni za kusimamia mnyororo wa thamani wa zao la parachichi.

190. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ilipanga pia, kuviwezesha viwanda vya uchakataji na utengenezaji wa bidhaa zitokanazo na parachichi; kusimamia mauzo ya parachichi; kujenga vituo 100 vya kukusanyia parachichi; kujenga vituo vitatu (3) vya kupanga madaraja na kufungasha parachichi; kuzalisha na kusambaza miche ya parachichi 2,100,000; na kuweka mfumo wa kusimamia uandaaji, usambazaji na utunzaji wa miche; na kuendelea kuwawezesha wakulima wadogo kupata miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba ya parachichi.

191. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, uzalishaji wa zao la parachichi ulifikia tani 201,354 katika mwaka 2024/2025. Kati ya hizo, parachichi zinazouzwa nje ya nchi

ni tani 37,871 sawa na asilimia 94.7 ya lengo la kuzalisha tani 40,000 ya parachichi zinazouzwa nje ya nchi. Uzalishaji huo umechangiwa kwa kutoa mafunzo kuhusu kanuni za kilimo bora cha zao la parachichi kwa wakulima 527 na Maafisa Ugani 50; kuandaa na kusambaza Mwongozo kuhusu Viwango vya Uzalishaji Endelevu wa zao la Parachichi na Mazao ya Viungo kwa wakulima 213; kutunga Kanuni za kusimamia mnyororo wa thamani wa zao la parachichi kwa kutambua wavunaji, kusajili wanunuzi, mawakala, kusimamia bei elekezi na kuweka madaraja ya matunda ya parachichi.

192. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TPHPA imetangaza zabuni kwa ajili ya ununuzi wa viuatilifu lita 3,000 za viuakuvu na lita 1,000 za *Copper sulphate* kwa ajili ya kudhibiti visumbufu katika zao la parachichi. Aidha, Tume ya Maendeleo ya Ushirika imehamasisha wakulima 54 wa parachichi wa Halmashauri ya Makete kuanzisha Chama cha Ushirika cha MANG'OTO AMCOS na wakulima 95 wa Wilaya ya Wanging'ombe kuanzisha chama cha Ulembwe AMCOS. Vyama hivyo vitasaidia kuongeza ushindani katika soko la parachichi na kuwezesha wakulima kuuza nje ya nchi.

Ufungashaji wa Parachichi kwa ajili ya kusafirisha nje ya nchi katika kiwanda cha Seasons Orchard - Njombe

193. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha uongezaji thamani wa zao la parachichi, ujenzi wa vituo nane (8) vya kukusanyia parachichi katika Mkoa wa Mbeya Halmashauri za Rungwe (6) na Busokelo (2) umefikia wastani wa asilimia 20. Vilevile, imesaini mikataba na mafundi na wasambazaji wa vifaa vya ujenzi kwa ajili ya ujenzi wa vituo 12 vya ukusanyaji wa parachichi katika mikoa ya Iringa vinne (4), Rukwa kimoja (1), Ruvuma viwili (2) na

Njombe vitano (5). Aidha, katika kuongeza maeneo ya uzalishaji wa parachichi, Wizara imesambaza miche ya parachichi 349,000 katika mikoa ya Mbeya, Songwe, Iringa na Njombe kwa mpango wa ruzuku na usambazaji unaendelea. Vilevile, Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imechimba visima vitatu (3) kwa ajili ya kuwawezesha wakulima wadogo kupata maji ya umwagiliaji katika maeneo yanayolima parachichi.

Zao la Viazi mviringo

194. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara katika mwaka 2025/2026, ilipanga kuongeza uzalishaji wa zao la viazi mviringo kufikia tani 2,570,061; kukarabati vitalu nyumba vinne (4); kujenga vitalu nyumba vitatu (3) katika vituo vya utafiti; kutoa mafunzo kwa wakulima wawezeshaji 500; na kuandaa na kusambaza mwongozo wa uzalishaji na uuzaji wa viazi mviringo.

195. ***Mheshimiwa Spika***, ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa uzalishaji wa viazi mviringo umefikia tani 2,961,414.82 sawa na asilimia 115 ya lengo la tani 2,570,061. Aidha, Wizara imefanya tathmini ya gharama kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa vitalu nyumba katika vituo vya utafiti vya Igeri (Njombe), Tengeru (Arusha), Uyole (Mbeya) na Nkundi (Rukwa) kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa mbegu bora za viazi mviringo. Vilevile, mafunzo kuhusu kanuni za kilimo bora na himilivu cha zao la viazi mviringo na uzalishaji wa mbegu bora za viazi kwa wakulima wawezeshaji 350 yametolewa katika mikoa ya Mbeya, Njombe, Morogoro, Tanga, Arusha, Kilimanjaro na Manyara. Pia, rasimu ya Mkakati wa Kuendeleza zao la Viazi mviringo nchini imeandaliwa.

Mazao yenye Mahitaji Makubwa

196. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuratibu uzalishaji wa mazao yenye mahitaji makubwa ambayo ni ngano, miwa na mazao ya mafuta yanayoagizwa kutoka nje ya nchi.

Zao la Ngano

197. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2025/2026, ilipanga kuongeza uzalishaji wa zao la ngano kufikia tani 300,000; kusambaza mbegu za ngano tani 1,000 kwa wakulima; kuanzisha vituo maalum vya kuzalisha mbegu za ngano; kuendelea na majaribio ya aina 82 za mbegu mpya za ngano; na kutoa mafunzo ya uzalishaji wa mbegu za kuazimia ubora (QDS) kwa wakulima 500.

198. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TARI ilipanga kufanya utafiti wa mbegu za ngano zenye kukidhi sifa ya mahitaji ya soko; kuhamasisha Vyama vya Ushirika kuanzisha mashamba makubwa ya ngano na viwanda vidogo vya kuchakata ngano; na kuwezesha upatikanaji wa mitaji kwa wakulima watakaoendesha mashamba hayo kupitia dirisha za *equity* na *guarantee scheme* litakaloanzishwa katika Benki ya Ushirika Tanzania.

199. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa uzalishaji wa zao la ngano ulifikia tani 115,826 mwaka 2024/2025. Aidha, tani 500 za mbegu bora za ngano zimesambazwa kwa wakulima katika maeneo ya uzalishaji kupitia mpango wa ruzuku; na mbegu za ngano aina tatu (3) zimewasilishwa TOSCI kwa ajili ya majaribio ya utambuzi na umahiri.

200. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia TARI imeendelea kufanya majaribio ya aina 82 ya mbegu mpya za ngano na imeendelea kufanya tathmini ya mashamba kwa ajili ya kuzalisha mbegu za ngano. Pia, Wizara kupitia TOSCI imetoa mafunzo ya uzalishaji wa mbegu za kuazimia ubora (QDS) kwa wakulima 415 ili kuwezesha uzalishaji wa mbegu za ngano nchini.

201. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika imehamasisha Vyama vya Ushirika 14 kuanzisha mashamba makubwa ya ngano na viwanda vidogo vya kuchakata ngano katika mikoa ya Manyara, Kilimanjaro na Njombe. Aidha, Benki ya Ushirika Tanzania imeanzisha dirisha za

equity na *guarantee scheme* kwa ajili ya kuwezesha upatikanaji wa mitaji yenye riba nafuu kwa wakulima.

Zao la Miwa na Uzalishaji wa Sukari

202. *Mheshimiwa Spika,* Wizara kupitia Bodi ya Sukari Tanzania katika mwaka 2025/ 2026, ilipanga kuongeza uzalishaji wa zao la miwa kutoka tani 4,713,907.89 zilizozalisha sukari tani 431,736.74 mwaka 2024/2025 hadi tani 7,000,000 za miwa zitakazozalisha sukari tani 700,000; kusimamia upanuzi wa kiwanda cha sukari cha Mtibwa na mashamba ya miwa ya kiwanda yaliyopo Dakawa yenye ukubwa wa hekta 12,000; kusimamia upanuzi wa mashamba yenye ukubwa wa hekta 13,000 ya kiwanda cha sukari Kagera na kusimamia utekelezaji wa mradi wa upanuzi wa kiwanda cha sukari cha Kilombero K4.

203. *Mheshimiwa Spika* vilevile, ilipanga kusimamia uanzishaji wa vitalu vya kuzalisha miche ya miwa kwenye eneo lenye ukubwa wa hekta 100 katika bonde la Kilombero; kuratibu uanzishaji wa viwanda vya sukari vya Rai Group na Lake Agro; TARI kuanzisha kitalu cha miche ya miwa kwenye eneo la ukubwa wa ekari 10; na kuzalisha mbegu za miwa tani 10.

204. *Mheshimiwa Spika*, ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Machi 2026, uzalishaji wa zao la miwa umefikia tani 4,351,673.1 zilizozalisha sukari tani 410,979.04 sawa na asilimia 62 na 59 ya lengo la kuzalisha miwa tani 7,000,000 na sukari tani 700,000, mtawalia. Uzalishaji huo umetokana na upanuzi wa kiwanda cha sukari cha Mtibwa na mashamba ya miwa ya kiwanda yaliyopo Dakawa yenye ukubwa wa hekta 12,000 ambapo upanuzi umefikia wastani wa asilimia 54. Aidha, upanuzi wa mashamba yenye ukubwa wa hekta 13,000 ya kiwanda cha sukari Kagera umefikia wastani wa asilimia 96; na upanuzi wa kiwanda cha sukari cha Kilombero K4 umekamilika. Upanuzi huo utaongeza uzalishaji wa miwa kutoka tani 600,000 hadi tani 1,500,000 kwa mwaka.

205. *Mheshimiwa Spika*, kitalu cha miche ya miwa kwa ajili ya wakulima wadogo kimeanzishwa kwenye eneo lenye ukubwa wa

hekta 100 katika bonde la Kilombero. Aidha, Wizara kupitia Bodi imeratibu uanzishaji wa viwanda vya sukari vya Lake Agro Ltd - Pwani, Rai group - Kigoma na Golden Sugar Mill – Kagera. Aidha, vitalu A na B venye ukubwa wa hekta 20 na hekta 170, mtawalia vinaendelea na uzalishaji.

206. ***Mheshimiwa Spika***, pia, Wizara kupitia Bodi imeratibu uwekezaji wa uzalishaji wa bidhaa zitokanazo na sukari kwa kusajili ujenzi wa distillery ya Mara Nile – Pwani, upanuzi wa Illovo distillery katika kiwanda cha Kilombero na kiwanda cha TPC Ltd – Moshi ili kuongeza uzalishaji wa bidhaa zitokanazo na sukari; na imezalisha mbegu za miwa tani 210 katika Mikoa ya Pwani, Kagera na Morogoro.

Kiwanda cha sukari cha Kilombero K4 – Morogoro

Mazao ya Mafuta

207. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ilipanga kuongeza uzalishaji wa mazao ya mafuta kufikia tani 2,200,000 mwaka 2025/2026; kuwezesha uchakataji wa mafuta yanayotokana na alizeti na chikichi kwa kuviwezesha viwanda vidogo; kuwawezesha wakulima wakubwa wa alizeti kwa kuwapatia mashamba makubwa ya pamoja; kuendelea kushauriana na Wizara ya Fedha kuweka sera za fedha ikiwemo kuongeza ushuru kwenye mafuta ya kula yanayotoka nje ya nchi; kusambaza mbegu bora za alizeti tani 2,150 kwa wakulima kwa mpango wa ruzuku; kuzalisha na kusambaza miche ya chikichi 10,000,000 kwa wakulima; na kuzalisha na kusambaza mbegu bora za karanga tani 20.1 na mbegu za ufuta tani 40.

208. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa uzalishaji wa mazao ya mafuta ulifikia tani 2,248,046.24 mwaka 2024/2025 na kuchangia uzalishaji wa mafuta ya kula nchini kufikia tani 305,906. Uzalishaji huo ni pungufu kwa asilimia 58 ya mahitaji ya mafuta ya kula ya tani 731,974 kwa mwaka. Aidha, mbegu bora za alizeti tani 741 zimesambazwa kwa wakulima kwa mpango wa ruzuku; miche ya chikichi 4,491 imezalishwa na kusambazwa kwa wakulima katika maeneo ya uzalishaji; na mbegu bora za karanga tani 24.3 na mbegu za ufuta tani 24.56 zimezalishwa na kusambazwa kwa wakulima katika maeneo ya uzalishaji. Kadhalika, Wizara imekamilisha Kanuni za Usimamizi wa Mafuta ya Kula ambazo zinalenga kuchagiza uzalishaji wa ndani na nchi kujitosheleza kwa mafuta ya kula ifikapo mwaka 2030.

4.2 Kuongeza Ajira zenye Staha na Ushiriki wa Vijana na Wanawake kwenye Kilimo 4.2.1 Kuwezesha Upatikanaji wa Ardhi ya Kilimo na Uanzishaji wa Mashamba Makubwa ya Pamoja (BBT – Mashamba)

209. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026, Wizara ilipanga kutambua, kupima na kutwaa mashamba yenye ukubwa wa hekta 80,000; kuanza uwekezaji katika shamba la Mapogoro – Chunya (Mbeya) katika eneo la ekari 20,000; kujenga ghala nane (8) zenye uwezo wa kuhifadhi tani 1,000; kujenga chumba cha ubaridi chenye uwezo wa kuhifadhi tani 1,000; kujenga uzio wa umeme kuzunguka shamba la Mlazo/Ndogowe; na kununua mitambo ya kuandaa mashamba.

210. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Machi 2026, Wizara imetambua maeneo yenye ukubwa wa hekta 7,019 katika mikoa ya Pwani (Kisarawe, Rufiji, Mkuranga na Kibaha) na Tanga (Mkinga) kwa ajili ya kuanzisha mashamba makubwa ya pamoja. Vilevile, katika kuimarisha miundombinu katika mashamba makubwa ya pamoja, ujenzi wa barabara zenye urefu wa km 20 katika shamba la Mapogoro – Chunya (Mbeya) umefanyika kupitia TARURA na zabuni kwa ajili ya kumpata mkandarasi wa ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji na nyumba za shambani imetangazwa. Aidha, zabuni kwa ajili ya kumpata mkandarasi wa ujenzi wa uzio wa umeme

wenye urefu wa km 27 kuzunguka shamba la Mlazo/Ndogowe imetangazwa. Pia, Wizara imenunua trekta nane (8), *trailer* sita (6), mitambo miwili (2) ya kuchimba visima, *Bulldozer* tatu (3), *Excavator* mbili (2), *Wheelloader* tatu (3), *Motorgrader* tatu (3) na *Planter* sita (6) kwa ajili ya shughuli za mashamba ya Chinangali, Ndogowe na Mapogolo.

211. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha ubora na uhifadhi wa mazao yanayolimwa na vijana na wanawake wa BBT, zabuni kwa ajili ya kumpata mkandarasi wa ujenzi wa ghala zenye uwezo wa kuhifadhi tani 1,000 katika mashamba ya pamoja ya vijana ya Chinangali (ghala 4) na Mlazo/Ndogowe (ghala 4) imetangazwa. Vilevile, zabuni kwa ajili ya kumpata mkandarasi wa ujenzi wa chumba cha ubaridi (cold room) chenye uwezo wa kuhifadhi tani 1,000 za mazao ya kilimo katika shamba la Chinangali imetangazwa.

4.2.2 Kuwezesha Uendelezaji wa Programu ya BBT Ngazi ya Halmashauri

212. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026, Wizara ilipanga kuendelea kutekeleza mradi wa BBT katika Halmashauri 20 zitakazotenga maeneo yasiyopungua ukubwa wa hekta 200 kwa kila Halmashauri; kutoa mafunzo ya kilimo biashara kwa vijana na wanawake; na kuanzisha mashamba ya tumbaku yenye ukubwa wa ekari 150 katika Halmashauri za Uyui na Chunya.

213. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, katika kutekeleza Programu ya BBT ngazi ya Halmashauri hadi Machi 2026, Halmashauri 18 zimetenga maeneo ya kilimo kwa ajili ya vijana kuanzisha mashamba ya pamoja. Halmashauri hizo ni Chemba, Ikungi, Bahi, Kaliua, Manyoni, Madaba, Kibaha, Kilolo, Mpanda, Muleba, Kisarawe, Njombe Musoma, Kakonko, Chunya, Njombe Mji, Geita Mji na Missenyi. Kadhalika, Bodi ya Tumbaku imeanzisha mashamba ya tumbaku katika Halmashauri za Uyui na Chunya kwa ajili ya kutoa mafunzo ya zao la tumbaku kwa vijana na wanawake.

214. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha vijana na wanawake wanapata elimu ya kilimo biashara, Halmashauri za Muleba na Kaliua zimedahili vijana na wanawake 582 kwa ajili ya kupata mafunzo ya kilimo biashara yanayoendana na shughuli za kilimo zinazofanyika katika Halmshauri hizo.

4.2.3 Kuwezesha Ujenzi wa Miundombinu ya Umwagiliaji kwa Wakulima wadogo (BBT visima)

215. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026, Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ilipanga kuchimba visima 500 vya umwagiliaji vitakavyomwagilia eneo lenye ukubwa wa hekta 30,393.39 katika Halmashauri 178 nchini ambavyo vitanufaisha wakulima 58,903.

216. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kuwezesha kilimo cha umwagiliaji kwa wakulima wadogo, ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Machi 2026, visima 345 vya umwagiliaji vyenye uwezo wa kumwagilia hekta 6,052 vimechimbwa katika mikoa 15 na kunufaisha takriban wakulima 12,545. Pia, Tume imenunua *surface pump* za umwagiliaji 1,000 na zitasambazwa kwa vikundi 740 vya wakulima wanawake na vijana kutoka kwenye maeneo ya pembezoni mwa Ziwa Victoria na Tanganyika. Orodha ya visima vilivyochimbwa umeainishwa katika **Kiambatisho Na. 6**. Aidha, uchimbaji wa visima unaendelea katika mikoa mingine.

217. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imenunua seti 1,250 za pampu, jenereta na mipira ambapo seti 250 zimesambazwa kwa wakulima na seti 1,000 zitaendelea kusambazwa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji kwa wakulima katika mikoa yenye vyanzo vya uhakika wa maji. Jumla ya wakulima 2,694 katika mikoa saba(7) ya Mara (468), Mwanza (398), Kagera (634), Ruvuma (483), Simiyu (74), Geita (292) na Tanga (345) wamenufaika. Matumizi ya vifaa hivyo yataongeza eneo linalomwagiliwa kwa hekta 19,200 au ekari 48,000.

4.2.4 Kuwezesha Upatikanaji wa Mikopo kwa Vijana na Wanawake (BBT mitaji)

218. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ilipanga kuiwezesha AGITF kiasi cha Shilingi Bilioni 6 kwa ajili ya kuwapatia mikopo vijana na wanawake; na kutenga Dola za Marekani Milioni 35 kwa kipindi cha miaka mitano (5) kupitia dirisha za *guarantee scheme*, *direct lending* na *equity fund* kwa ajili ya uongezaji thamani wa mazao ya kimkakati.

219. ***Mheshimiwa Spika,*** ninapenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Machi 2026, dirisha maalumu kwa ajili ya kuwezesha upatikanaji wa mitaji kupitia *guarantee scheme, direct lending* na *equity fund* limeanzishwa na kutoa mikopo yenye thamani ya Shilingi Bilioni 5.5 kwa riba nafuu isiyozidi asilimia saba (7%). Mikopo hiyo, imenufaisha wakulima katika mnyororo wa thamani wa kilimo. Vilevile, AGITF imeweka kiasi cha Shilingi Bilioni 3.5 kwenye dirisha la *guarantee scheme* litakalowezesha kutoa mikopo yenye thamani ya Shilingi Bilioni 7. Aidha, Kiasi cha Dola za Marekani milioni 35 zimetolewa kama *Guarantee Scheme* na Benki ya Maendeleo ya Afrika kwa taasisi za fedha zitakazokopesha vijana na wanawake mikopo yenye thamani ya zaidi ya Dola za Marekani Milioni 70.

4.2.5 Kuwezesha Vijana na Wanawake Kuongeza Thamani ya Mazao

220. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ilipanga kutekeleza mradi wa BBT kwa vijana na wanawake 200 kwa kuwapatia mafunzo ya kuongeza thamani ya zao la mkonge ili waweze kuzalisha bidhaa zitokanazo na zao hilo.

221. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Machi 2026, mafunzo atamizi kuhusu uongezaji thamani wa zao la mkonge yametolewa kwa vijana na wanawake 352 (wanawake 305 na wanaume 47) kupitia programu ya BBT Zanzibar na Mkoa wa Tanga. Pia, vijana na wanawake hao wamewezeshwa mashine 20 na tani tisa (9) za mkonge kwa ajili ya kutengeneza bidhaa. Vilevile, Bodi ya

Korosho Tanzania imenunua mashine 100 za kubangua korosho na kuwapatia vijana na wanawake 2,800 ili kuongeza thamani ya zao la korosho.

4.2.6 Kuwezesha Vijana na Wanawake kutoa Huduma za Ugani (BBT Ugani)

222. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ilipanga kuendelea kutekeleza Mpango wa Ugani (BBT – Agricultural Extension Enterpreneurship Scheme) kwa ajili ya kuwatengenezea ajira vijana na wanawake 500, kuimarisha utoaji wa huduma za ugani na kukuza ujuzi wa vijana wahitimu wa vyuo vya kilimo kwa kutoa huduma za ugani kwa wakulima; na kutekeleza Programu ya BBT – Miche kwa kuwawezesha vijana na wanawake kuzalisha miche ya mazao.

223. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Machi 2026, vijana na wanawake 1,434 wameajiriwa kwa ajili ya kutoa huduma za ugani. Kati ya hao, Bodi ya Pamba Tanzania imeajiri vijana 761; Bodi ya Korosho Tanzania imeajiri vijana 511; Bodi ya Kahawa Tanzania imeajiri vijana 112 na COPRA imeajiri vijana 50 kwa ajili ya zao la parachichi. Hatua hiyo, imesaidia kuimarisha utoaji wa huduma za ugani na kukuza ujuzi kwa vijana wahitimu wa vyuo vya kilimo kwa ajili ya kutoa huduma za ugani kwa wakulima.

Kilimo sasa ni fursa ya ajira kwa vijana na wanawake inayolenga kuchochea ubunifu, kuleta utajiri na kulisha Taifa kwa ujumla. Hii inasadifu shairi maarufu tulilokuwa tukilisoma shuleni la baba aliyekuwa akitoa wosia kwa watoto wake katika dakika za mwisho za uhai wake "kama mnataka mali mtaipata shambani"

4.3 Kuimarisha Usalama wa Chakula na Lishe

4.3.1 Uwekezaji kwenye Miundombinu ya Uhifadhi ili kufikia Uwezo wa Kuhifadhi tani 3,000,000 ifikapo Mwaka 2030

224. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha uhifadhi wa mazao nchini, Wizara kupitia NFRA ilipanga kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya uhifadhi yenye uwezo wa kuhifadhi tani 165,000 kupitia mradi wa kuongeza uhifadhi wa nafaka; kuanza ujenzi wa

miumbombinu yenye uwezo wa kuhifadhi tani 300,000; kukarabati ghala 46; kununua vifaa kwa ajili ya ghala 28; na kuanza ujenzi wa miundombinu ya uhifadhi wa mazao ya kilimo yenye uwezo wa kuhifadhi tani 30,000.

225. *Mheshimiwa Spika,* ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, hadi Machi 2026, mkandarasi amepatikana kwa ajili ya ukamilishaji wa ujenzi wa Mradi wa Kuongeza Uwezo wa Hifadhi unaojumuisha vihenge na ghala zenye uwezo wa kuhifadhi tani 165,000 katika Kanda za Songea, Makambako, Songwe, Shinyanga na Dodoma. Vilevile, wakandarasi wamekabidhiwa maeneo kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu yenye uwezo wa kuhifadhi tani 85,000 katika Kanda za Arusha, Sumbawanga, Dodoma, Shinyanga na Kipawa. Kukamilika kwa miradi hiyo kutaongeza uwezo wa Wakala wa kuhifadhi chakula kutoka tani 776,000 hadi tani 861,000. Aidha, zabuni kwa ajili ya kupata wakandarasi wa ukarabati wa ghala 20 imetangazwa. Pia, zabuni kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ghala 28 zilizojengwa katika Mkoa wa Ruvuma imetangazwa.

4.3.2 Kuiongezea NFRA Uwezo wa Kununua Mazao ya Wakulima ili Kuongeza Hifadhi

226. *Mheshimiwa Spika,* katika kuimarisha usalama wa chakula nchini, Wizara kupitia NFRA katika mwaka 2025/202,6 ilipanga kununua tani 1,140,000 za nafaka; na kuuza chakula ndani na nje ya nchi pindi kitakapohitajika.

227. *Mheshimiwa Spika,* ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Machi 2026, NFRA imenunua tani 135,290.394 za nafaka kwa lengo la kuimarisha usalama wa chakula nchini na kufanya hifadhi ya akiba ya chakula ya Taifa kufikia tani 553,077.376; na imeuza tani 95,872.887 za nafaka (mpunga tani 33,865.024, mahindi tani 55,867.957, mbaazi tani 5,652.479 na dengu tani 487.428).

Mh. Daniel Chongolo, Waziri wa Kilimo (kulia) akikagua ghala la kuhifadhia chakula linalopatikana Kipawa - Dar es Salaam, ghala hilo ni mali ya Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) kushoto ni Mkurugenzi Mtendaji wa Bw. Andrew Komba

4.3.3 Kuhamasisha Matumizi ya Mazao yaliyoongezewa Virutubishi ili Kukabiliana na Matatizo ya Lishe Nchini

228. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026, Wizara ilipanga kuendelea kutekeleza Mpango Kazi wa Lishe katika Kilimo (Nutrition Sensitive Agriculture Action Plan – NSAAP) ili kukabiliana na matatizo ya lishe yanayohusisha udumavu, ukondefu na upungufu wa wekundu wa damu; kuzalisha na kusambaza vipando vya viazi lishe 3,290,000; na kutoa mafunzo kuhusu kanuni za kilimo bora kwa wakulima wawezeshaji 2,500 na wazalishaji wa mbegu za viazi lishe 100.

229. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Machi 2026, Wizara kupitia TARI imezalisha vipando vya viazi lishe 25,401 na kuvisambaza katika mikoa ya Tabora, Kigoma, Singida, Katavi na Mwanza na uzalishaji unaendelea. Vilevile, TARI imetoa mafunzo kuhusu kanuni za kilimo bora kwa wakulima wawezeshaji 206 na wazalishaji wa mbegu bora za viazi lishe 1,054 katika Wilaya za Kakonko, Kasulu, Kibondo, Buhigwe, Uvinza, Tanganyika, Mpanda, Nsimbo, Mlele, Nkasi, Sikonge, Manispaa ya

Tabora, Kaliua, Uyui, Urambo, Nzega, Itigi, Manyoni, Manispaa ya Singida na Ikungi.

230. *Mheshimiwa Spika,* TARI imefanya utambuzi wa virutubisho kwa sampuli 69 za mazao ya mpunga, ngano, mahindi, maharage, kunde, mbaazi, soya, karanga, ufuta na alizeti ili kubaini muundo unaopatikana wa virutubisho kwa ajili ya kuongeza uelewa wa masuala ya lishe kwa watumiaji. Vilevile, imebuni *prototype* ambayo inatumika kukoboa nafaka ikiwemo mahindi, mtama, ngano, uwele na ulezi ambayo itawezesha wakulima kuchakata nafaka bila kuathiri virutubishi vilivyomo kwenye nafaka hizo.

4.4 Kuimarisha Upatikanaji wa Masoko, Mitaji na Mauzo ya Mazao Nje ya Nchi

4.4.1 Kujenga Miundombinu ya Masoko ya Mazao ya Kilimo kwa ajili ya Wakulima katika Halmashauri mbalimbali Nchini Masoko ya Kimkakati

231. *Mheshimiwa Spika,* katika kuendelea kuimarisha miundombinu ya masoko ya mazao ya kilimo, Wizara ilipanga kuendelea na ujenzi wa masoko matano (5) ya kimkakati. Ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Machi 2026, ujenzi wa masoko matano (5) ya kimkakati katika Halmashauri za Manispaa ya Kahama (Busoka), Ngara (Kabanga), Kyerwa (Nkwenda na Murongo) na Tarime (Sirari) umefikia wastani wa asilimia 81.

232. *Mheshimiwa Spika,* hatua ya ujenzi iliyofikiwa kwa kila soko ni kama ifuatavyo: - Soko la Nkwenda (asilimia 87), Kabanga (asilimia 85), Sirari (asilimia 83), Busoka (asilimia 75) na Murongo (asilimia 70). Kukamilika kwa ujenzi wa masoko hayo kutawezesha wakulima na wadau wengine kufanya biashara ya mazao ya kilimo katika mipaka ya nchi za Uganda, Kenya, Rwanda na Burundi.

Vituo vya Masoko (Market Sheds)

233. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026, Wizara ilipanga kuendelea na ujenzi wa vituo saba (7) vya masoko; kuanza ujenzi wa vituo vitatu (3) vya masoko (market sheds); na kuanzisha masoko manne (4) ya mazao ya kilimo kwenye mipaka ya Rusumo, Namanga, Kasumulo na Holili.

234. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Machi 2026, ujenzi wa vituo sita (6) vya masoko (market sheds) umefikia wastani wa asilimia 43.67. Vituo hivyo vya masoko ni Kibakwe (Mpwapwa) asilimia 98, Ushirika (Nzega Mji) asilimia 63, Endashangwet (Karatu) asilimia 42, Losirwa (Monduli) asilimia 37, Rombo (Mamsera) asilimia 20 na Hai (Masama Mula) asilimia 2. Kukamilika kwa ujenzi wa vituo hivyo, kutawezesha wakulima kukusanya na kuuza mazao yao sehemu rasmi zinazotambulika na mamlaka husika. Aidha, Wizara inaendelea na taratibu za kubainisha maeneo kwa ajili ya kuanzisha masoko manne (4) ya mazao ya kilimo kwenye mipaka ya Rusumo, Namanga, Kasumulo na Holili.

4.4.2 Kuimarisha Uongezaji Thamani kwa Kushirikisha Sekta Binafsi

235. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026, Wizara ilipanga kuendelea na ujenzi wa vituo jumuishi viwili (2); kujenga miundombinu ya kukaushia, kuchakata na kuhifadhi muhogo na tangawizi; kulipa fidia ya viwanda na ghala katika maeneo ya Mzizima (Dar es Salaam) na Isaka (Shinyanga); na CPB kununua tani 78,897 za nafaka na mazao mchanganyiko.

236. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Machi 2026, Wizara kupitia Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (CPB) imenunua tani 5,020.15 za nafaka. Kati ya hizo, tani 1,386.57 zimechakatwa na uchakataji unaendelea; na ujenzi wa vituo jumuishi vya kuchambua, kuhifadhi na kuchakata mazao ya bustani katika mikoa ya Iringa (Mufindi) na Mbeya (Rungwe) umefikia wastani wa asilimia 15.

237. *Mheshimiwa Spika,* zabuni kwa ajili ya ununuzi wa mashine ya kukaanga kahawa yenye uwezo wa kukaanga kilo 60 kwa siku imetangazwa; na mafunzo kuhusu uongezaji thamani wa mazao ya zabibu na korosho yametolewa kwa wakulima 250 na Maafisa Ugani 932 katika maeneo ya uzalishaji.

4.4.3 Kuongeza Mauzo ya Mazao ya Kilimo Ndani na Nje ya Nchi

238. *Mheshimiwa Spika,* katika mwaka 2025/2026, Wizara ilipanga kuongeza mauzo ya mazao nje ya nchi kutoka Dola za Marekani Bilioni 3.54 mwaka 2023/2024 hadi takriban Dola za Marekani Bilioni 4; TPHPA, kukamilisha mchakato wa ufunguzi wa masoko mapya 15; COPRA kuandaa na kusambaza miongozo kuhusu uuzaji, ununuzi, usindikaji, uhifadhi, usafirishaji na uingizaji wa mazao; kuandaa viwango vya uzalishaji wa mazao; kutoa mafunzo kuhusu viwango vya ubora wa mazao ya bustani kwa wakulima viongozi 4,500; kuwajengea uwezo wadau 5,350 kuhusu taratibu za usafirishaji wa mazao ya kilimo; na kuimarisha mifumo ya ununuzi na uuzaji wa mazao ya kilimo.

239. *Mheshimiwa Spika,* ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Machi 2026, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeendelea kusimamia mauzo ya mazao ya kilimo nje ya nchi na kuwezesha kuongeza thamani ya mauzo hayo kutoka Dola za Marekani Bilion 3.54 mwaka 2023/2024 hadi Dola za Marekani Bilioni 3.73 mwaka 2024/2025. Aidha, kupita mifumo rasmi ya kidigiti imewezesha uuzaji wa mazao ya kakao, choroko, dengu, mbaazi, soya na ufuta kuongeza kutoka tani 268,757.77 zenye thamani ya Shilingi Bilioni 896.91 mwaka 2024 hadi tani 713,618.72 zenye thamani ya Shilingi Trilioni 1.40 mwaka 2025.

240. *Mheshimiwa Spika,* vilevile, taratibu za ufunguzi wa masoko mapya 15 katika nchi 14 zipo katika hatua ya tathmini ya visumbufu hatarishi (Pest Risk Analysis - PRA) kwa masoko ya China (Vanilla na Nanasi), India (Vanila na Nanasi), Indonesia (Karafuu), Singapore (Karafuu), Israel (Parachichi), Malaysia (Parachichi), Canada (Pilipili Manga), Uturuki (Nanasi), Brazil (Nanasi), USA (Kakao), Afrika Kusini (Ndizi), Zambia (Viazi mviringo), Pakistan (Tumbaku) na Iraq (Tumbaku). Ufunguzi wa masoko hayo

utawezesha nchi yetu kuongeza mauzo ya mazao ya kilimo katika nchi hizo na hivyo kuongeza ajira na kukuza uchumi.

241. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha mauzo ya mazao nje ya nchi yanaendelea kuongezeka na kwa kuzingatia mahitaji makubwa ya zao la parachichi katika masoko ya Uingereza na Marekani, Wizara kupitia TPHPA imeanza kutekeleza operesheni maalum inayolenga kudhibiti kisumbufu cha kikarantini aina ya Nondo wa Matunda katika zao la parachichi. Lengo la operesheni hiyo inayotekelezwa katika mikoa ya Njombe, Iringa na Mbeya itaiwezesha Tanzania kukidhi kigezo muhimu na pekee kilichobaki ili kufungua masoko ya parachichi katika nchi za Uingereza na Marekani.

242. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha wakulima wanazalisha mazao yanayokidhi mahitaji ya soko, Wizara kupitia COPRA imeandaa na kusambaza miongozo ya uzalishaji wa mazao ya ufuta, mbaazi, dengu, choroko, soya na maharage. Aidha, COPRA imeandaa na kusambaza Miongozo ya Uuzaji na Ununuzi wa Mazao jamii ya mikunde, viungo, kakao na parachichi. Pia, imeandaa viwango vya uzalishaji wa mazao ya ufuta, mikunde (mbaazi, dengu, choroko, soya na maharage), viungo (mdalasini, iliki, pilipili manga na karafuu), kakao, parachichi na vitunguu maji.

243. ***Mheshimiwa Spika,*** COPRA imetoa mafunzo kuhusu viwango vya uzalishaji na ubora wa mazao ya ufuta na mikunde kwa Maafisa Ugani 3,214 katika mikoa ya Mtwara (693), Lindi (691), Ruvuma (418), Morogogo (353), Kilimanjaro (153), Tanga (150), Arusha (133), Rukwa (109), Pwani (102), Katavi (94), Singida (77),Manyara (73), Dodoma (60), Kigoma (49), Simiyu (27), Mwanza (13), Shinyanga (8), Mara (6) Tabora (4) na Geita (1). Aidha, imewajengea uwezo wadau 503 kuhusu kanuni za kilimo cha mkataba, udhibiti ubora, usajili, utoaji wa vibali na taratibu za usafirishaji wa mazao ya kilimo ndani na nje ya nchi.

4.4.4 Kuimarisha Upatikanaji wa Mitaji

244. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026, Wizara kupitia AGITF ilipanga kuanzisha dirisha la dhamana na mitaji kwa ajili ya

kuimarisha upatikanaji wa mitaji yenye riba nafuu kwa wakulima katika Benki ya Ushirika Tanzania; kuendelea kushirikiana na taasisi za fedha katika kuimarisha utoaji wa mikopo yenye riba nafuu kwenye sekta ya kilimo; TADB kuongeza idadi ya taasisi za fedha zinazotumia mfuko wa dhamana wa TADB kutoka taasisi 19 hadi 21; na kuendelea na ujenzi wa ofisi ya AGITF Makao Makuu katika Mkoa wa Dodoma.

245. *Mheshimiwa Spika,* ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Machi 2026, Wizara kupitia AGITF imetoa mikopo yenye riba nafuu yenye thamani ya Shilingi Milioni 100 kwa wakulima na Bilioni 5 zimepelekwa Benki ya Ushirika Tanzania kwa ajili ya kukopesha wakulima kupitia vyama vya ushirika; imeanzisha dirisha la dhamana na mitaji kwa ajili ya kuimarisha upatikanaji wa mitaji yenye riba nafuu kwa wakulima katika Benki ya Ushirika Tanzania; na ujenzi wa jengo la Ofisi ya AGITF Makao Makuu katika Mkoa wa Dodoma umefikia asilimia 65.

246. *Mheshimiwa Spika,* TADB imeongeza idadi ya taasisi za fedha zinazotumia mfuko wa dhamana kutoka taasisi 19 hadi 22. Ongezeko hilo limewezesha upatikanaji wa mikopo yenye riba nafuu katika shughuli za kilimo.

4.4.5 Kuziwezesha Maabara za Serikali ziweze kufikia Viwango vya Ubora vinavyotakiwa Kimataifa

247. *Mheshimiwa Spika,* Wizara kupitia TPHPA ilipanga kuanza ujenzi wa maabara ya kisasa katika Mkoa wa Njombe kwa ajili ya kupima ubora wa mazao; kuendelea kuimarisha maabara ya TPHPA Makao Makuu kwa kununua na kufunga vifaa vya kisasa vya maabara; TOSCI kukamilisha ukarabati wa maabara ya Makao Makuu na maabara ya kupima ubora wa mbegu iliyopo katika Mkoa wa Arusha; TARI kukamilisha ujenzi na ununuzi wa vifaa vya maabara ya magonjwa ya mimea na maabara ya kuzalisha miche kwa njia ya chupa katika kituo cha TARI Maruku; kununua vifaa vya maabara katika vituo vya TARI; na kukamilisha upatikanaji wa ithibati ya maabara ya udongo.

248. *Mheshimiwa Spika,* ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Machi 2026, ukarabati wa maabara ya Taifa ya Mbegu iliyopo TOSCI Makao Makuu katika Mkoa wa Morogoro umefikia asilimia 92. Kukamilika kwa maabara hiyo kutaongeza uwezo wa kuthibiti ubora wa mbegu kwa kutumia teknolojia za kisasa na kuendelea kulinda taswira ya nchi katika viwango vya ubora wa mbegu kimataifa na kufungua fursa mpya kwa uwekezaji katika uzalishaji na biashara ya mbegu. Vilevile, Wizara imeimarisha maabara ya TPHPA makao makuu kwa kukarabati, kununua na kufunga vifaa vya kisasa pamoja na kuwezesha upatikanaji wa ithibati ya kimataifa.

249. *Mheshimiwa Spika,* katika kuongeza uzalishaji wa miche itakayosambazwa kwa wakulima, ujenzi wa maabara ya kuzalisha miche kwa njia ya chupa katika kituo cha utafiti cha TARI Maruku umefikia asilimia 30; na ujenzi wa maabara ya kudhibiti visumbufu vya mimea (patholojia) katika Kituo cha Utafiti cha TARI Naliendele umefikia asilimia 67. Vilevile, ili kuimarisha ubora wa mazao, mshauri elekezi wa ujenzi wa maabara ya TPHPA kwa ajili ya kupima ubora wa mazao katika Mkoa wa Njombe amepatikana.

4.5 Kuimarisha Maendeleo ya Ushirika 4.5.1 Kuimarisha Mifumo ya Kidijiti kwenye Vyama vya Ushirika na Mamlaka za Usimamizi

250. *Mheshimiwa Spika,* katika mwaka 2025/2026, Wizara kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania ilipanga kuunganisha Mfumo wa MUVU na mifumo mingine ya TEHAMA; na kukagua mifumo ya TEHAMA inayotumiwa na Vyama vya Ushirika kwa lengo la kutathimini ufanisi wake.

251. *Mheshimiwa Spika,* ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Machi 2026, Tume imetengeneza *Portal* inayoonesha muhtasari (*Dashboard)* wa takwimu za kiushirika kupitia kiungo www.csmis.ushirika.go.tz/home. *Portal* hiyo inawezesha wananchi kupata taarifa za ushirika zikiwemo za usajili wa vyama, idadi ya wanachama, SACCOS, AMCOS, Vyama vya Upili na ukaguzi wa Vyama vya Ushirika. Vilevile, Tume imesajili vyama 6,545 vyenye

jumla ya wanachama 3,357,366 katika Mfumo wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika – MUVU kwa ajili ya kurahisisha utoaji wa huduma na usimamizi.

252. ***Mheshimiwa Spika,*** pia, imeunganisha mfumo wa MUVU na mifumo ya Wizara na Taasisi zingine za Serikali kupitia Mfumo Mkuu wa Serikali wa GovESB kwa ajili ya kurahisisha upatikanaji wa taarifa, kuondoa udurufu wa mifumo na kupunguza gharama za uendeshaji. Mifumo ambayo imeunganishwa ni pamoja na mfumo wa Wizara (e-Kilimo na Bodi ya Sukari (CANE GROWERS MIS), Mifumo ya eGA (GoveESB, ERMS, mGov, GMS), Mfuko wa Bima ya Afya (NHIF Online Self Services), Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari (NaPA), Wizara ya Fedha (GePG), Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEECMIS) na Soko la Bidhaa Tanzania (OTS). Mifumo mingine ni pamoja na SCULT (SOMA), ELCT ND SACCOS (Core Banking System), Rotai (Mkulima Hub) na Climbing Up (Shamba bora).

4.5.2 Kuimarisha Usimamizi na Udhibiti wa Vyama vya Ushirika

253. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume ilipanga kuendelea kuratibu na kusimamia utambuzi na uthaminishaji wa mali za Vyama vya Ushirika 5,973 na kuandaa Mpango wa Matumizi na Uendelezaji mali hizo; kuandaa kitabu kitakachoonesha fursa za uwekezaji zilizopo kwenye Vyama vya Ushirika; kufanya ufuatiliaji wa mali za Vyama vya Ushirika vilivyofutwa ikiwemo Chama Kikuu cha Ushirika cha Tanga (TARECU) na Shirikisho la Vyama vya Ushirika Tanzania.

253. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Machi 2026, utambuzi na uthaminishaji wa mali za kudumu za Vyama vya Ushirika unaendela kutekelezwa kupitia Kampuni ya World Map chini ya uratibu wa Shirikisho la Vyama vya Ushirika. Aidha, jumla ya Vyama vya Ushirika 5,934 katika mikoa ya Katavi (50), Mara (279), Geita (258), Mwanza (318), Simiyu (348), Njombe (206), Ruvuma (220), Pwani (184), Dar es Salaam (285), Morogoro (161), Arusha (158), Singida (134), Tanga (200), Lindi (182), Dodoma (99), Tabora (440), Manyara (119), Kagera (345), Mbeya (254), Kilimanjaro (215), Songwe (257),

Shinyanga (229), Simiyu (348), Mtwara (433) na Kigoma (212) vimefanyiwa uhakiki na uthaminishaji wa mali zao. Mali hizo ni ardhi, majengo, mitambo, mashine, mifumo ya TEHAMA na samani za ofisi.

255. ***Mheshimiwa Spika,*** pia, rasimu ya Mpango wa Matumizi na Uendelezaji wa Mali zinazomilikiwa na Vyama vya Ushirika pamoja na kitabu cha kuonesha fursa zilizopo kwenye Vyama vya Ushirika imeandaliwa na itakamilishwa baada ya utambuzi na uthaminishaji wa mali za Vyama vya Ushirika kukamilika. Vilevile, Tume imefanya ufuatiliaji wa mali za TARECU LTD na kubaini kuwa baadhi ya mali hazijauzwa ikiwemo ghala (6) na majengo (2) Pia, ufuatiliaji wa mali za Shirikisho la Vyama vya Ushirika (TFC) unaendelea.

4.5.3 Kuhamasisha Vyama vya Ushirika Kujiendesha Kibiashara na Kuviwezesha kupata Mitaji

256. *Mheshimiwa Spika,* Tume ya Maendeleo ya Ushirika kwa kushirikiana na Benki ya Ushirika Tanzania ilipanga kuendelea kuwezesha Vyama vya Ushirika kuingia katika mfumo rasmi wa kifedha kwa kuhamasisha Vyama Vikuu kuwa mawakala wa Benki na kufungua matawi; kusimamia Chama Kikuu cha Tandahimba na Newala (TANECU) kujenga kiwanda kipya cha kubangua korosho chenye uwezo wa kubangua tani 3,500; kufufua kiwanda cha kuchakata pamba cha Manawa na kulipa fidia za hisa za Serikali; na kufufua viwanda vya kuchakata pamba vya Buyagu na Magu.

257. *Mheshimiwa Spika,* Tume ilipanga kusimamia Chama Kikuu cha Ushirika cha Kahama (KACU) kujenga kiwanda cha kukamua mafuta ya kula; kusimamia Chama Kikuu cha Tabora (WETCU) kujenga kiwanda cha kutengeneza nyuzi za kusukia tumbaku; kuendelea kuimarisha mifumo rasmi na jumuishi ya biashara na masoko ya mazao katika Vyama vya Ushirika; na kuhamasisha Vyama vya Ushirika kuendelea kuuza mazao ya kilimo kupitia mifumo rasmi.

258. *Mheshimiwa Spika,* ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, hadi Machi 2026, Wizara kupitia Tume imehamasisha Vyama Vikuu vya Ushirika na SACCOS kubwa 52 kuwa mawakala wa Benki ya Ushirika Tanzania. Aidha, Vyama vya Ushirika 6,545 vimehamasishwa kuendelea kuwekeza katika Benki ya Ushirika Tanzania. Uhamasishaji huo umewezesha Vyama 1,540 kuwekeza kiasi cha Shilingi Bilioni 19 katika Benki ya Ushirika Tanzania. Pia, matawi manne (4) ya Benki ya Ushirika yaliyonzishwa katika mikoa ya Dodoma, Kilimanjaro, Tabora na Mtwara yanaendelea na utoaji wa huduma.

259. *Mheshimiwa Spika*, katika kuhamasisha Vyama vya Ushirika kuongeza thamani ya mazao, Tume imeendelea kuratibu ujenzi wa kiwanda cha kubangua korosho cha TANECU chenye uwezo wa kubangua tani 3,500 kwa mwaka katika Wilaya ya Tandahimba. Vilevile, Tume inaendelea na ufufuaji wa kiwanda cha Magu ambapo utekelezaji umefikia asilimia 52. Pia, tathmini ya ufufuaji wa kiwanda cha Manawa imefanyika ambapo gharama ya ufufuaji wa kiwanda hicho ni Shilingi Bilioni 3.5 ambayo inahusisha fidia za hisa za wawekezaji ili kimilikiwe na ushirika. Baada ya kukamilisha malipo ya fidia, Chama Kikuu cha NYANZA kitaendelea kuratibu ufufuaji wa kiwanda hicho. Kadhalika, ufufuaji wa kiwanda cha Buyagu umepangwa kufanyika baada ya ufufuaji wa Kiwanda cha Magu kukamilika.

260. *Mheshimiwa Spika*, ujenzi wa kiwanda cha Chama Kikuu cha KACU chenye uwezo wa kuchakata mafuta tani 10,800 kwa mwaka umefikia asilimia 90. Pia, eneo lenye ukubwa wa mita za mraba 12,000 katika Wilaya ya Nzega kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda cha kutengeneza nyuzi za kusukia tumbaku limepatikana. Mradi huo utatekelezwa kupitia TCJE.

261. *Mheshimiwa Spika*, Tume kwa kushirikiana na wadau imeendelea kuhamasisha Vyama vya Ushirika kuuza mazao kupitia mifumo rasmi ikiwemo mfumo wa Soko la Bidhaa Tanzania (TMX) ambapo hadi Machi 2026, umewezesha kuuza kilo 1,501,744,164 za mazao zenye thamani ya Shilingi 3,740,335,430,188. Hatua hiyo, imeongeza uwazi, kuimarisha ushiriki

wa wanachama katika maamuzi ya kibiashara, kupunguza biashara isiyo rasmi na kuongeza mapato.

4.5.4 Kuhamasisha Ushirika kwenye Sekta Mbalimbali na Makundi Maalum

262. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume katika mwaka 2025/2026, ilipanga kuhamasisha vikundi 105 vinavyotekeleza shughuli za kiuchumi katika Sekta ya Kilimo, Mifugo, Uvuvi, Madini, Viwanda na Fedha ili kuunda Vyama vya Ushirika; kuratibu uanzishwaji wa Kampuni ya Bima ya Ushirika; kuhamasisha Vyama vya Ushirika kujiunga na Bima mbalimbali; kuhamasisha wanaushirika kujiunga na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii; kuandaa Mpango wa Maendeleo wa Sekta ya Ushirika; na kuanzisha SACCOS kwenye AMCOS.

263. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, hadi Machi 2026, Wizara kupitia Tume imehamasisha vikundi 25 vya vijana vyenye jumla ya wanachama 1,307 kuanzisha Vyama vya Ushirika 25 vikiwemo vya kilimo (12), mifugo (4), uvuvi (3), madini (1), viwanda (2) na fedha (3) katika mikoa ya Dar es Salaam, Tabora, Dodoma, Mwanza, Pwani na Arusha Aidha, Tume kupitia Shirikisho la Vyama vya Ushirika (TFC) imeratibu uanzishwaji wa Kampuni ya Bima ya Ushirika na taratibu kwa ajili ya kupata leseni ya uendeshaji kutoka TIRA zinaendelea.

264. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume kwa kushirikiana na Shirikisho la Vyama vya Ushirika Tanzania inaendelea kuratibu upatikanaji wa bima ya afya, bima ya mazao na hifadhi ya kinga ya jamii. Katika kuhakikisha upatikanaji wa bima katika zao la tumbaku, jumla ya wakulima 32,822 wamesajiliwa katika Halmashauri za Uyui, Nzega, Urambo na Manispaa ya Tabora. Kadhalika, Tume inaendelea na majadiliano na NSSF kwa lengo la kuingia makubaliano rasmi ya kuwezesha vyama vya ushirika kupata mafao mbalimbali ya hifadhi ya jamii. Pia, rasimu ya Mpango Kabambe wa Maendeleo ya Ushirika imeandaliwa ili kuwezesha utekelezaji wa Dira 2050 katika maeneo yanayohusu ushirika.

265. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume imehamasisha Vyama Vikuu vya *Kagera Cooperative Union - KCU, Karagwe District Cooperative*

Union - KDCU, Lindi Mwambao, *Arusha Cooperative Union - ACU,* Mirambo na Juhudi AMCOS kuanzisha SACCOS kwa lengo la kuongeza mitaji na kuwawezesha wanachama kupata mikopo yenye riba nafuu.

4.6 Kuimarisha Matumizi ya Mifumo ya TEHAMA Katika Uendelezaji wa Sekta ya Kilimo

4.6.1 Kuwekeza kwenye Matumizi ya Mifumo ya Kidijiti katika Sekta ya Kilimo

266. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026, Wizara ilipanga kuendelea kuimarisha mfumo wa *e – Kilimo* kwa kuendelea kujenga moduli ya taarifa za kilimo na taarifa za mifumo ya kijiografia; kuboresha mawasiliano na njia ya kubadilishana taarifa na wadau wa kilimo; kuanzisha maktaba ya kidijiti (e-library) kwa ajili ya kutunza kumbukumbu za kilimo; kuendelea kutoa huduma za ugani kwa wakulima kidijiti; TPHPA kuanzisha moduli ya kufuatilia mazao; na kuanzisha *e-phyto*.

267. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Wizara kupitia COPRA ilipanga kuendelea kusajili ghala, masoko, vituo vya ukaguzi wa mazao na wafanyabiashara wa mazao ya kilimo; AGITF kuboresha mfumo wa kidijiti kwa ajili ya usimamizi wa mikopo; na kuendelea kununua vifaa vya TEHAMA kulingana na teknolojia mpya na za kisasa.

268. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, hadi Machi 2026 Wizara imekamilisha ujenzi wa moduli ya mbolea, ghala na mashamba ya wakulima; kuendelea kujenga na kufanya majaribio ya moduli ya taarifa za kilimo na kijiografia zinazopatikana kwa lugha nyepesi; imeboresha mawasiliano na njia ya kubadilishana taarifa za wadau wa kilimo (agriculture data digitalization value chain) kwa kuunganisha mfumo wa *e – kilimo* na mifumo mbalimbali ikiwemo TFRA kwa taarifa za usajili wa wakulima, TMA kwa takwimu za hali ya hewa, TRA kwa ajili ya masuala ya kodi na namba za utambulisho za mlipakodi. Vilevile, Wizara inaendelea na uunganishaji wa mfumo wa NIDA kwa ajili ya utambulisho wa mkulima.

269. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara ipo katika hatua za mwisho za kukamilisha mfumo wa *e – phyto* kwa ajili ya kuwezesha ubadilishanaji wa vyeti vya usafi wa mimea na *traceability* ili kuwezesha ufuatiliaji wa viuatilifu vinavyoingia nchini na mazao ya kilimo ambayo hayajakidhi vigezo katika soko la kimataifa. Pia, imetoa mafunzo kuhusu ufuatiliaji wa vigezo vya kuingiza na kusafirisha mazao ya kilimo nje ya nchi kwa wakaguzi na Maafisa TEHAMA 70 katika moduli hizo.

270. ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, kupitia mfumo wa *Crop Stock Dynamic System* - CSDS imesajili ghala 637 na kufanya jumla ya ghala zilizosajiliwa kufikia 2,431; imesajili masoko 20 na kufanya jumla ya masoko yaliyosajiliwa kufikia 398; imesajili vituo vya ukaguzi vitano (5) na kufanya jumla ya vituo vilivyosajiliwa kufikia 160 na imesajili wafanyabiashara wa mazao ya kilimo 1,798 na kufanya jumla ya wafanyabiashara waliosajiliwa kufikia 2,414.

271. ***Mheshimiwa Spika***, Kituo cha Huduma kwa Wateja (Kilimo Call Center) kimetoa huduma kwa wadau 9,837 ikiwemo uzalishaji na utunzaji wa mazao na matumizi sahihi ya pembejeo; taarifa za bei za mazao na masoko na matumizi sahihi ya zana za kilimo; na imeimarisha mawasiliano ya ugani kwa kujenga moduli ya kuwawezesha wakulima kupata huduma za ugani kilimo kutoka kwa maafisa ugani waliopo karibu yao.

4.6.2 Kuimarisha Mifumo ya Kidijiti itakayowezesha Upatikanaji wa Taarifa Sahihi kwa Wakati

272. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026, Wizara ilipanga kuendelea kuboresha mfumo wa *e – Kilimo* wa Wizara kwa kuunganisha na mifumo mingine ya Serikali; na kuanzisha kituo cha teknolojia za kilimo cha TEHAMA (AgriTech Hub).

273. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, hadi Machi 2026, Wizara imeunganisha mfumo wa *e – Kilimo* na mfumo wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) kwa ajili ya taarifa za ruzuku, Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC) kwa ajili ya kupata taarifa za wakulima kupitia ushirika wa mazao, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA)

kwa takwimu za hali ya hewa na mfumo wa HCMIS (Utumishi) kwa uhakiki wa Maafisa Ugani.

274. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, imeunganisha na mfumo wa Serikali wa mGov kwa huduma ya jumbe fupi (Bulk SMS), mfumo wa TRA wa namba za utambulisho za mlipakodi (TIN) na mfumo wa forodha (TANCIS) kwa sehemu ya vibali vya biashara (Import and Export), mfumo wa BRELA pamoja na mfumo wa malipo wa Serikali (GePG).

MAENEO MENGINE MUHIMU YALIYOTEKELEZWA NA WIZARA
Kuongeza Matumizi ya Teknolojia na Mbinu za Kilimo Kinachohimili Mabadiliko ya Tabianchi

275. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi, hususan kwa wakulima wa nyanda kame, Wizara kupitia TARI ilipanga kujenga uwezo wa kituo cha TARI - Hombolo kuwa kituo mahiri cha tafiti za mazao ya nyanda kame na mabadiliko ya Tabianchi; kuendelea kujenga Ofisi na miundombinu ya kisasa; kuendelea na utafiti wa zao la Tende; kuendelea na utekelezaji wa Mpango wa Sekta wa Usimamizi na Utunzaji wa Mazingira pamoja na Mpango wa Sekta wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi.

276. ***Mheshimiwa Spika,*** pia, ilipanga kuendelea kufanya tathmini ya athari ya mazingira na jamii kwenye mashamba makubwa 10; kuandaa Mipango ya Usimamizi wa Mazingira; kutoa mafunzo kuhusu utunzaji na usimamizi wa mazingira, mbinu na teknolojia za kilimo kinachohimili mabadiliko ya tabianchi ili kuwa na kilimo endelevu na himilivu kwa wakulima 800 katika mikoa ya Dodoma, Singida, Manyara na Tanga.

277. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, hadi Machi 2026, Wizara imegundua na kutoa mbegu himilivu aina 54 za mazao ya choroko (mungbean), maharage, mbogamboga, mpunga, karanga, mtama na muhogo kwa lengo la kuongeza uhimilivu na uzalishaji wa mazao katika maeneo mbalimbali ya nchi kulingana na ikolojia husika.

278. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imekiwezesha kituo cha TARI – Hombolo kuwa Kituo Mahiri cha Utafiti wa Mazao ya Nyanda Kame na Teknolojia za Uhimilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi ikiwemo kujenga kitalu nyumba (screen house) na miundombinu ya umwagiliaji. Kutokana na jitihada hizo, kituo kimeendelea kufanya utafiti wa mbegu bora za zao la tende kwa kuanzisha mashamba darasa manne (4) ya zao hilo na kusambaza miche 1,166 kwa wakulima 53 katika Vijiji vya Mita, Hombolo, Mvumi na Chalinze Nyama.

279. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha Wizara na wadau wa kilimo, wanatekeleza majukumu kwa kuzingatia sheria ya mazingira ya mwaka 2004, na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ambayo yana athiri utekelezaji wa shughuli za kilimo, Wizara imeandaa mpango wa pili wa usimaizi wa mazingira wa sekta ya kilimo ili kutekeleza Dira ya Taifa 2050 inayotuelekeza kuzingatia utunzaji wa mazingira kwa kilimo endelevu.

280. ***Mheshimiwa Spika,*** pia, Wizara imeendelea kuratibu tathmini ya athari ya mazingira na jamii katika miradi inayoendelea 24. Kadhalika, Wizara imeendela kutoa mafunzo kuhusu uhifadhi na usimamizi wa mazingira na kilimo himilivu kwa wanufaika 23,403 wakiwemo wakulima, maafisa ugani, maafisa mipango, maafisa mazingira, maendeleo ya jamii, watafiti, wasimamizi wa mashamba ya mbegu, wakaguzi na wasambazaji wa mbegu katika mikoa ya Arusha, Dodoma, Geita, Iringa, Katavi, Kigoma, Mwanza, Morogoro, Mtwara, Njombe, Pwani, Shinyanga, Tabora na Tanga. **Kiambatisho Na. 7**. Orodha ya miradi iliyofanyiwa Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii.

Masuala ya Jinsia

281. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026, Wizara ilipanga kuendelea kuhakikisha uzingatiaji wa masuala ya jinsia katika kilimo cha mazao mbalimbali; kukamilisha mwongozo wa ujumuishaji wa masuala ya jinsia katika mnyororo wa thamani wa kilimo; kuendelea kuhakikisha kuwa masuala ya jinsia yanazingatiwa katika utoaji wa pembejeo za kilimo; kutoa

mafunzo kupitia vikundi vya wakulima katika mashamba darasa; na kuendelea kutekeleza shughuli kwa kuzingatia usawa wa jinsia.

282. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Machi 2026, Wizara imekamilisha Mwongozo wa Ujumuishaji wa Masuala ya Jinsia katika Mnyororo wa Thamani wa Kilimo. Vilevile, imetoa mafunzo kuhusu jinsia na ukatili wa kijinsia kwa wadau wa kilimo 2,751 (wanawake 1,146 na wanaume 1,605) katika mikoa ya Tanga, Mbeya, Tabora, Iringa, Arusha, Kilimanjaro pamoja na taasisi za TARI, ASA na TOSCI; na imeendelea kuhakikisha ujumuishwaji wa jinsia unapewa kipaumbele katika utekelezaji wa shughuli za kilimo.

283. ***Mheshimiwa Spika,*** pia, maafisa ugani 1,877 wamepatiwa mafunzo ya kilimo himilivu ambapo kati ya hao 573 ni wanawake. Vilevile, wakulima 18,749 wameshiriki katika mradi wa ruzuku makini (majaribio ya pembejeo na ushauri wa kushusha kemikali ya udongo) na kuwajengea uelewa kuhusu mbinu za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi katika mikoa ya Katavi, Iringa, Mwanza, Shinyanga, Geita na Njombe kati ya hao wanawake 8,002.

284. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeanzisha madawati tisa (9) ya jinsia katika ngazi ya Wizara makao makuu na taasisi zilizo chini ya Wizara (NiRC, TARI, TOSCI na ASA). Pia, imefanya utambuzi wa watoa huduma 251 katika mikoa 18 iliyojumuisha Wilaya 37 kwa ajili ya waathirika wa masuala ya ukatili wa kijinsia katika maeneo yote ya utekelezaji wa Miradi iliyopo chini ya Wizara ya Kilimo.

Afya na Ustawi wa Watumishi

285. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026, Wizara ilipanga kuendelea kutoa huduma ya lishe na dawa kwa watumishi tisa (9) wanaoishi na VVU na UKIMWI; kuhamisha watumishi kushiriki michezo mbalimbali ili kupunguza athari za Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza kwa ajili ya kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya Wizara; kuratibu vikao vinne (4) vya waelimisha rika; kutoa elimu ya VVU, UKIMWI, Afya ya Akili na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza; kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa

watumishi kwa kuwapatia vitendea kazi, motisha na stahiki zao kwa mujibu wa Sheria, Kanuni, miongozo na taratibu; na kuwapatia nafasi za watumishi kujiendeleza kitaaluma.

286. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Machi 2026, Wizara imeendelea kutoa huduma ya lishe na dawa kwa watumishi wanaoishi na VVU na UKIMWI; imehamasisha watumishi 347 kushiriki michezo mbalimbali ili kupunguza athari za Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza kwa ajili ya kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya Wizara; imeratibu vikao viwili (2) vya waelimisha rika kwa lengo la kubadilishana taarifa na kutathmini hali ya utekelezaji wa afua za VVU, UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza mahala pa kazi katika Utumishi wa Umma; imetoa elimu ya VVU, UKIMWI, Afya ya Akili na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza kwa watumishi 428 kwa kushirikiana na Wizara ya Afya.

287. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuimarisha utendaji kazi wa watumishi kwa kuwapatia watumishi 640 kompyuta mpakato, magari 55 yamenunuliwa kwa ajili ya shughuli za ofisi sambamba na kutoa motisha na stahiki zao kwa mujibu wa sheria, taratibu, kanuni na miongozo.

5 MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2026/ 2027

288. ***Mheshimiwa Spika***, takwimu za Benki ya Dunia za mwaka 2023 zinaonesha kuwa wastani wa Shilingi 9,540 zinahitajika ili kukidhi kiwango cha kipimo cha maisha kwa siku kwa mwananchi mmoja mmoja ambapo ni sawa na Shilingi 3,482,100 kwa mwaka. Aidha, takwimu za Ofisi ya Taifa ya Takwimu zinaonesha kuwa kipato cha mtanzania kwa mwaka ni wastani wa Shilingi 3,000,000 ambacho kimechochewa na jitihada za Serikali tangu uhuru kupitia Sekta ya Kilimo.

289. ***Mheshimiwa Spika***, katika kufikia kiwango cha kipimo cha maisha kwa siku kinachohitajika kwa mwananchi mmoja mmoja kwa kuzingatia takwimu za Benki ya Dunia za mwaka 2023, Mpango na Bajeti ya Wizara ya Kilimo katika mwaka 2026/2027 umebeba maono mapana ya Serikali kupitia kilimo ambayo ni

msingi na dira itakayoiwezesha Tanzania kufikia hadhi ya nchi ya kipato cha kati cha juu ifikapo mwaka 2050.

290. ***Mheshimiwa Spika,*** Mpango na Bajeti ya Wizara ya Kilimo ya mwaka 2026/2027 umezingatia Dira ya Maendeleo ya Taifa (2050); Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2026/2027 – 2030/2031); Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2026/2027; Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2025 - 2030; Hotuba ya Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoitoa wakati wa Ufunguzi wa Bunge la 13 tarehe 14 Novemba, 2025 Jijini Dodoma; Sera ya Taifa ya Kilimo ya mwaka 2013; Sera ya Taifa ya Umwagiliaji ya mwaka 2010; Sera ya Maendeleo ya Ushirika ya mwaka 2002; na Mpango Kabambe wa Mageuzi ya Kilimo 2050 (Tanzania Agriculture Master Plan 2050) itakayotekelezwa kupitia Agenda 10/30 na Mpango Mkakati wa Wizara ya Kilimo wa mwaka 2026/2027 - 2030/2031.

291. ***Mheshimiwa Spika,*** pia, umezingatia Agenda za Kikanda na Kimataifa ikiwemo Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) na Azimio la Kampala kuhusu Programu ya Kuendeleza Kilimo Barani Afrika (CAADP 2026 - 2035); Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2026/2027; Maoni na Ushauri wa Kamati za Kudumu za Bunge; Maoni ya Baraza la Rais la Ushauri wa Kilimo na wadau wa maendeleo; masuala mtambuka ya jinsia, mazingira, lishe, mabadiliko ya tabianchi, vijana na kutokomeza ajira kwa watoto katika Sekta ya Kilimo, Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza, VVU na UKIMWI.

292. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027, Wizara itaendelea kutekeleza vipaumbele sita (6), ambavyo ni: Kuongenza Tija na Uzalishaji; Kuchangia Kuongeza Ajira zenye Staha na Ushiriki wa Vijana na Wanawake Kwenye Kilimo; Kuimarisha Usalama wa Chakula na Lishe; Kuimarisha Upatikanaji wa Mitaji, Masoko na Mauzo ya Mazao Nje ya Nchi; Kuimarisha Maendeleo ya Ushirika; na Kuimarisha Matumizi ya Mifumo ya TEHAMA katika Uendelezaji wa Sekta ya Kilimo.

293. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha kuwa vipaumbele vilivyopangwa vinafikiwa, Wizara imepanga kutekeleza mikakati 30 kama ifuatavyo:-

i. Kuongeza Tija na Uzalishaji;

294. ***Mheshimiwa Spika***, mikakati itakayozingatiwa katika eneo hili ni pamoja na:-

a) Utafiti wa Kilimo;
b) Uzalishaji na usambazaji wa mbegu bora na miche;
c) Kutoa ruzuku ya mbolea, mbegu na viuatilifu;
d) Usajili wa wakulima na urasimishaji wa shughuli za kilimo;
e) Kuimarisha huduma za ugani;
f) Kuanzisha mashamba makubwa ya pamoja na kupima afya ya udongo;
g) Uendelezaji wa kilimo cha umwagiliaji; na
h) Uanzishaji wa vituo vya kutoa huduma za zana za kilimo.

ii. Kuchangia Kuongeza Ajira zenye Staha na Ushiriki wa Vijana na Wanawake kwenye Kilimo

295. ***Mheshimiwa Spika***, kwa kuzingatia changamoto ya upatikanaji wa ajira hususan kwa vijana na wanawake, Wizara imepanga kutekeleza mikakati ifuatayo:-

a) Kuwezesha uendelezaji wa programu ya BBT ngazi ya Halmashauri;
b) Kuwezesha ujenzi wa miuondombinu ya umwagiliaji kwa wakulima wadogo (BBT visima);
c) Kuwezesha upatikanaji wa mikopo kwa vijana na wanawake (BBT mitaji);
d) Kuwezesha vijana na wanawake kuzalisha miche (BBT miche);
e) Kuwezesha vijana na wanawake kuongeza thamani ya mazao; na
f) Kuwezesha vijana na wanawake kutoa huduma za ugani (BBT Ugani).

iii. Kuimarisha Usalama wa Chakula na Lishe

296. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027, Wizara itaendelea kuimarisha hifadhi ya chakula ili kuwezesha nchi kuendelea kujitosheleza katika usalama wa chakula na lishe. Katika eneo hili, mikakati itakayotekelezwa ni pamoja na:-

a) Uwekezaji kwenye Miundombinu ya Uhifadhi ili Kufikia Uwezo wa Kuhifadhi tani 3,000,000 ifikapo Mwaka 2030
b) Kuiongezea NFRA uwezo wa kununua mazao ya wakulima ili kuongeza hifadhi ya chakula; na
c) Kuhamasisha matumizi ya mazao yaliyoongezewa virutubishi ndani ya nchi ili kukabiliana na matatizo ya lishe nchini.

iv. Kuimarisha Upatikanaji wa Mitaji, Masoko na Mauzo ya Mazao Nje ya Nchi

297. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha wananchi wananufaika zaidi na shughuli za kilimo, Wizara imepanga kutekeleza mikakati inayolenga kuimarisha kipato cha wananchi na kuondoa umaskini.
Mikakati hiyo ni pamoja na:-

a) Kujenga miundombinu ya masoko ya mazao ya kilimo katika Halmashauri mbalimbali;
b) Kuimarisha uongezaji thamani kwa kushirikisha Sekta Binafsi;
c) Kuongeza mauzo ya mazao ya kilimo ndani na nje ya nchi;
d) Kuimarisha upatikanaji wa mitaji; na
e) Kuziwezesha maabara za Serikali kufikia viwango vya ubora unaotakiwa kimataifa.

v. Kuimarisha Maendeleo ya Ushirika

298. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027, Wizara imepanga kutekeleza mikakati ifuatayo ili kuimarisha maendeleo ya ushirika nchini:-

a) Kuimarisha ukaguzi na usimamizi wa uendeshaji wa vyama vya ushirika;
b) Kuimarisha ushirika kwenye sekta mbalimbali na makundi maalum; na
c) Kuhamasisha vyama vya ushirika kujiendesha kibiashara.

vi. Kuimarisha Matumizi ya Mifumo ya TEHAMA katika Uendelezaji wa Sekta ya Kilimo

299. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika shughuli za kilimo, Wizara imepanga kutekeleza mikakati ifuatayo:-
a) Kuimarisha mifumo ya kidijiti itakayowezesha upatikanaji wa taarifa sahihi kwa wakati; na
b) Kuwekeza kwenye matumizi ya mifumo ya kidijiti katika Sekta ya Kilimo.

KAZI ZITAKAZOTEKELEZWA KWA KUZINGATIA VIPAUMBELE VYA MWAKA 2026/2027

5.1 Kuongeza Tija na Uzalishaji

5.1.1 Utafiti wa Kilimo

300. *Mheshimiwa Spika,* utafiti ni msingi wa ukuaji wa Sekta ya Kilimo unaowezesha ugunduzi na matumizi ya teknolojia za kisasa ikiwemo mbegu bora, matumizi ya udongo na maji, udhibiti wa visumbufu vya mimea na mazao na kuongeza thamani ya mazao ili kuongeza uzalishaji na tija.

301. *Mheshimiwa Spika,* katika kuhakikisha matokeo ya tafiti yanamnufaisha mkulima wa kitanzania na kuendeleza teknolojia za kilimo kwa mwaka 2026/2027, Wizara kupitia TARI itakamilisha ugunduzi na kusajili aina 73 za mbegu bora za mazao ya kimkakati ya nafaka, jamii ya mikunde, biashara, mizizi, matunda na mafuta kwa lengo la kuongeza aina mpya za mbegu zinazoendana na mahitaji ya soko. Vilevile, itaendelea na ugunduzi wa teknolojia 20 za kanuni za kilimo bora kwa mazao ya nafaka, jamii ya mikunde, biashara, mizizi, matunda na mafuta

kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa mazao, kuongeza ufanisi wa matumizi ya rasilimali na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

302. ***Mheshimiwa Spika,*** TARI itaendelea na tafiti 28 za teknolojia za afya ya udongo kwa mazao ya kimkakati ya nafaka, jamii ya mikunde, biashara, mizizi, matunda na mafuta. Kukamilika kwa tafiti hizo kutawezesha mapendekezo ya matumizi sahihi ya mbolea. Vilevile, itakamilisha uchambuzi wa sampuli 34 za udongo zilizokusanywa kwa ajili ya utafiti wa afya ya udongo ili kubaini kiwango sahihi cha uwekaji wa mbolea ya kupandia na kukuzia kwa tumbaku ya mvuke katika wilaya za Uyui, Kaliua, Uvinza, Kasulu, Tanganyika, Chunya, Namtumbo, Kahama, Mbogwe na Serengeti. Aidha, TARI itapokea sampuli za udongo 2,300 na sampuli 200 za mbolea kutoka kwa wadau kwa ajili ya kuzichambua na kushauri matumizi sahihi.

303. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha uzalishaji wa mbegu za utafiti, Wizara kupitia TARI itazalisha mbegu tani 1,870.5 za mazao ya nafaka, mikunde, mafuta na mazao ya bustani. Kati ya hizo, mbegu mama ni tani 53.12, mbegu za awali tani 343.3, mbegu za msingi tani 831.1 na mbegu zilizothibitishwa tani 642.98. Vilevile, itakusanya na kutunza nasaba 2,325 za mbegu za asili za mazao ya mahindi (132), mpunga (70), kunde (20), mbaazi (6) maharage (86), mbegu za mazao ya miti (11), ufuta (600), karanga (750), mtama (150), njugumawe (100), muhogo (200) na viazi vitamu (200).

304. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha matokeo ya utafiti yanawafikia wakulima, TARI itahaulisha teknolojia 381 zinazojumuisha teknolojia za mbegu bora (139); kanuni za kilimo bora (175); afya ya udongo (9); teknolojia za kuongeza thamani ya mazao (24) na teknolojia za kudhibiti wadudu, magonjwa na viuatilifu vya visumbufu vya mimea (34).

305. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha miundombinu ya utafiti nchini, TARI itaendelea na ujenzi wa maabara za kuzalisha miche kwa njia ya chupa (tissue culture lab) katika vituo vya TARI Maruku na TARI Tengeru. Vilevile, itakarabati maabara ya TARI Mikocheni na kununua vifaa kwa ajili ya maabara ya kituo cha TARI

Mlingano. Aidha, itajenga maabara mbili (2) za kuzalisha mbegu katika vituo vya TARI Ilonga na TARI Selian pamoja na kuendelea na ujenzi wa maabara ya kudhibiti visumbufu vya mimea katika kituo cha TARI Naliendele.

306. ***Mheshimiwa Spika,*** TARI itaendelea na ujenzi wa kituo cha *Bioscience* katika Mkoa wa Morogoro kwa ajili ya kutoa huduma za kisasa za kisayansi katika utafiti wa mbegu, wadudu, magonjwa, uhimilivu wa athari za mabadiliko ya tabianchi, udongo, uhandisi wa kibaolojia (Bio - engineering) na kanzidata za taarifa za kibaolojia (Bioinformatics). Vilevile, itaendelea na ujenzi wa Benki ya mbegu katika kituo cha TARI Selian, ujenzi wa Ofisi ya Makao Makuu (Njedengwa, Dodoma) na ujenzi wa nyumba tatu (3) za watumishi, jiko na hosteli katika Kituo cha Utafiti wa Kahawa cha Mwayaya (Buhigwe).

307. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kulinda mashamba ya utafiti wa mbegu dhidi ya uvamizi. TARI itaendelea na ujenzi wa uzio katika mashamba ya utafiti wa mbegu katika vituo vya TARI Uyole, TARI Kifyulilo, TARI Dakawa, TARI Hombolo, TARI Maruku, TARI Ifakara, TARI Kihinga, TARI Mlingano, TARI Ukiriguru na TARI Tumbi. Aidha, italipa fidia kwa wananchi watakaohamishwa katika kituo cha TARI Uyole ili kupisha ujenzi wa uzio. Pia, itaendelea na taratibu za upatikanaji wa hatimiliki katika vituo 17 na mashamba ya majaribio 18.

308. ***Mheshimiwa Spika,*** TARI itaendelea kukarabati nyumba 49 za watumishi katika vituo vya TARI Ilonga (24), TARI Mlingano (15) na TARI Tumbi (10) na ukarabati wa ofisi nne (4) katika vituo vya TARI Ilonga (3) na Tumbi (1). Aidha, itaendelea na ujenzi wa ofisi moja (1) katika kituo cha TARI Hombolo na ofisi ya TARI makao makuu Njedengwa - Dodoma.

309. ***Mheshimiwa Spika,*** TARI itaendelea na ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji itakayomwagilia eneo lenye ukubwa wa hekta 2,160.9 katika vituo 17 vya TARI Selian (145), TARI Kihinga (150), TARI Ilonga (215), TARI Hombolo (70), TARI Kifyulilo (26.5), TARI Dakawa (50), TARI Uyole (920), TARI Kibaha (20), TARI Maruku (32), TARI Tengeru (50), TARI Ifakara (36.4), TARI

Tumbi (60), TARI Naliendele (37), TARI Mikocheni (60), TARI Ukiriguru (247), TARI Mlingano (20) na TARI Uyole – Isimani (22).

310. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha uhifadhi wa mbegu za utafiti zinazozalishwa, Wizara kupitia TARI itaendelea na ujenzi wa ghala 11 zenye uwezo wa kuhifadhi tani 415 kila moja katika vituo vya TARI Tumbi - Tabora, TARI Selian - Arusha, TARI Hombolo - Dodoma, TARI Dakawa - Morogoro, TARI Naliendele - Mtwara, TARI Uyole - Mbeya, TARI Kifyulilo - Iringa, TARI Ifakara - Morogoro, TARI Ilonga - Morogoro, TARI Ukiriguru - Mwanza na TARI Maruku – Kagera.

311. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia TARI, imepanga kununua na kusimika mashine ya kukaanga kahawa yenye uwezo wa kukaanga kilo 60 kwa siku katika Kituo cha Utafiti wa Kahawa cha Mwayaya (Buhigwe). Aidha, itanunua zana za kilimo 15 kwa ajili ya shughuli za kilimo. Kati ya hizo, mashine za kuvunia mazao (2), kunyunyizia dawa (2), kupandia (2), trekta (3), *harrow* (2), *plough* (2) na *trailer* (2). Pia, itanunua magari (2), pikipiki (3) na mashine za *seed treatment*, *cold rooms facilities* na *seed graders.* Ununuzi wa vitendea kazi hivyo utaimarisha utendaji kazi katika vituo vya utafiti.

5.1.2 Uzalishaji na Usambazaji wa Mbegu Bora na Miche Uzalishaji wa Mbegu

312. ***Mheshimiwa Spika***, mahitaji ya mbegu bora nchini kwa mwaka ni tani 127,650. Katika mwaka 2026/2027, Wizara kwa kushirikiana na Sekta Binafsi imepanga kuongeza upatikanaji wa mbegu bora kutoka tani 79,214.48 mwaka 2025/2026 hadi tani 127,650. Vilevile, Wizara itaongeza uzalishaji wa mbegu bora ndani ya nchi kutoka tani 47,702.45 mwaka 2025/2026 hadi tani 105,000 mwaka 2026/2027.

313. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha upatikanaji wa mbegu bora nchini, ASA itazalisha mbegu bora tani 27,219 kupitia kilimo cha mkataba kwa kampuni na wakulima kwenye eneo lenye ukubwa wa hekta 12,470 katika mashamba ya mbegu ya ASA. Kati ya hizo, ufuta tani 490, mahindi tani 17,632, mpunga tani

5,108, maharage tani 412, choroko tani 110, mbaazi tani 160, mtama tani 300, alizeti tani 1,907 na ngano tani 1,100.

Miundombinu ya Uzalishaji Mbegu

314. ***Mheshimiwa Spika***, ASA itafungua mashamba mapya ya uzalishaji wa mbegu yenye ukubwa wa hekta 1,900 katika mashamba ya mbegu ya Mbozi (hekta 600), Msimba (hekta 500) na Luhafwe (hekta 800). Vilevile, ASA itaendelea na ujenzi wa ghala tano (5) zenye uwezo wa kuhifadhi mbegu tani 1,800 kila moja katika mashamba ya mbegu ya Msimba, Msungura, Dabaga, Namtumbo na Mbozi.

315. ***Mheshimiwa Spika***, ili kulinda mashamba ya mbegu dhidi ya uvamizi, ASA itaendelea na ujenzi wa uzio katika mashamba ya mbegu ya Namtumbo (km 33.3), Mwele (km 14), Kilangali (km 23), Luhafwe (km 13), Msungura (km 5), Mbozi (km 40), Dabaga (km 22), Bugaga (km 10) na Arusha (km 17).

316. ***Mheshimiwa Spika***, ASA itaendelea na ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika eneo lenye ukubwa wa hekta 3,000 katika mashamba ya mbegu ya Msimba (200), Mbozi (500), Namtumbo (1,000), Msungura (100), Arusha (240), Kilimi (160) na Luhafwe (800). Vilevile, itaendelea na ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba ya mbegu yenye ukubwa wa hekta 700 ya Mbozi (100), Namtumbo (400), Arusha (100) na Msimba (100).

317. ***Mheshimiwa Spika***, ASA itajenga makaushio matatu (3) ya mbegu katika mashamba ya mbegu ya Namtumbo, Luhafwe na Igunga. Vilevile, itakarabati ofisi mbili (2) katika mashamba ya mbegu ya Mwele na Mbozi. Pia, itajenga nyumba 29 za watumishi katika mashamba ya mbegu ya Namtumbo (3), Bugaga (3), Arusha (3), Kilangali (3), Mbozi (3), Msimba (3), Dabaga (3), Mwele (3) na Kilimi (5) ili kuimarisha utendaji kazi wa watumishi katika mashamba ya mbegu.

Uthibiti wa Ubora wa Mbegu

318. ***Mheshimiwa Spika***, msingi wa mapinduzi ya kilimo unaanza na mbegu bora ambapo hubeba hatma ya mavuno yetu na kiini cha tija na usalama wa chakula na nchi kwa ujumla. Serikali imekuwa ikipokea malalamiko kutoka kwa baadhi ya wakulima kuhusu uwepo wa mbegu zisizo na ubora za mazao mbalimbali kutoka kwa wafanyabiashara wasio waaminifu.

319. ***Mheshimiwa Spika***, katika kukabiliana na changamoto iliyopo ya uuzaji wa mbegu zisizo na ubora, jambo ambalo ni hujuma ya wazi dhidi ya mkulima, Wizara katika mwaka 2026/2027, itatoa mafunzo kwa vitendo (Demonstration) kwa wakulima na wauzaji wa mbegu yatakayolenga kuwawezesha kutofautisha mbegu zisizo na ubora na mbegu bora.

Nitoe wito kwa wafanyabiashara wasio waaminifu wanaouza mbegu zisizo na ubora kufahamu kuwa mkono wa sheria hautawaacha salama. Niwasihi wakulima wa nchi hii kuwa macho na kuhakikisha wananunua mbegu bora kutoka kwa mawakala waliosajiliwa na kukagua kwa makini nembo za uthibiti ubora kwenye vifungashio na siyo vinginevyo.

320. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha uthibiti wa ubora wa mbegu nchini, TOSCI itanunua mtambo wa kuchapisha lebo zinazotumika katika vifungashio vya mbegu kwa lengo la kuongeza ufanisi na kujenga uwezo wa utoaji wa lebo za kuthibiti ubora, kuepuka vihatarishi vya kiusalama na kuhakikisha upatikanaji wa mbegu bora kwa wakulima kwa wakati. Vilevile, itanunua maeneo kwa ajili ya ujenzi wa maabara za mbegu katika mikoa ya Dodoma, Geita na Mbeya.

321. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia TOSCI, itanunua vifaa vya kisasa kwa ajili ya Maabara ya Taifa ya Mbegu yenye uwezo wa kufanya uchambuzi wa kikemikali na lishe, vifaa vya ofisi na magari sita (6). Vilevile, itanunua na kusimika Mtambo wa kuchapisha lebo za ubora zitakazotumika katika vifungashio vya mbegu na kutoa lebo za ubora wa mbegu 45,000,000. Pia, itaendelea na ukarabati wa maabara ya Kanda ya Kaskazini

(Arusha) pamoja na ujenzi wa maabara tatu (3) katika Kanda ya Magharibi (Tabora), Kusini (Mtwara) na Kanda ya Ziwa (Mwanza).

322. ***Mheshimiwa Spika***, TOSCI itaendelea na ukaguzi wa mashamba 1,669 ya mbegu yenye ukubwa wa hekta 26,600, miche 20,000,000, maduka 2,800 na ghala za kuhifadhi mbegu 167. Vilevile, itatoa mafunzo kwa wakaguzi wa mbegu walioidhinishwa 115 katika ngazi ya Halmashauri, wakulima 890 wa mbegu katika Mfumo wa Ubora wa Mbegu Uliobainishwa na Mkulima (UMBEGU-QDS), na wafanyabiashara wa mbegu 6,500. Pia, itakusanya sampuli za mbegu 4,820 kwa ajili ya majaribio ya ubora wa mbegu ili kuongeza mbegu zilizothibitishwa ubora.

323. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha upatikanaji wa aina mpya za mbegu nchini na kumwezesha mkulima kuwa na chaguo la aina za mbegu, TOSCI itafanya majaribio ya utambuzi wa aina mpya za mbegu 80, majaribio ya umahiri wa aina mpya za mbegu 30, majaribio ya uhalisia wa mbegu zilizopo katika uzalishaji 250, pamoja na tafiti za kiuchunguzi juu ya mahitaji ya mbegu nchini. 324. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha upatikanaji wa takwimu na taarifa za mbegu bora nchini, TOSCI itaboresha Mfumo wa *TOSCI Online Application Services* (TOAS) ili kuwawezesha wakulima na wadau wengine wa tasnia ya mbegu nchini kupata taarifa za mbegu bora kwa urahisi na kwa wakati.

Uzalishaji wa Vipando

325. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha miche inazalishwa na kusambazwa kwa wakulima, Wizara itaimarisha ufuatiliaji na usimamizi wa miche kwa lengo la kuhakikisha miche hiyo inawafikia wakulima kwa wakati ili kuongeza uzalishaji na tija katika mazao ya kilimo. Pia, itahamasisha vikundi vya vijana na wanawake kushiriki katika uzalishaji wa miche ambao utachangia upatikanaji wa ajira na kupunguza upotevu wa miche.

326. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2026/2027, Wizara kwa kushirikiana na sekta binafsi itazalisha miche 46,603,721 ya mazao ya kakao (559,500), karafuu (508,563), parachichi (1,727,400), chikichi (2,000,000), korosho (5,000,000), kahawa (30,000,000),

migomba (750,758), zabibu (700,000), miembe (17,500), michungwa (20,000), minazi (111,000), mkonge (3,500,000), tufaha (600,000), iliki (109,000) na chai (1,000,000). Pia, TARI itazalisha na kusambaza vipando vya viazi lishe 3,400,000 na pingili za muhogo 5,670,000.

5.1.3 Utoaji wa Ruzuku ya Mbolea, Mbegu na Viuatilifu

a) Upatikanaji wa mbolea

327. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027, Wizara kupitia Mamlaka ya Mbolea Tanzania (TFRA) imepanga kuratibu upatikanaji wa mbolea nchini kufikia tani 1,500,000 za mbolea. Kati ya hizo, TFC itanunua na kusambaza mbolea tani 220,500 ikiwemo tani 150,000 kwa ajili ya mazao ya chakula, tani 70,000 kwa ajili ya zao la tumbaku na tani 500 kwa ajili ya zao la chai. Pia, itasimika mitambo ya kuchanganya mbolea (Bulk Blending Facilities) katika Mkoa wa Dar es Salaam yenye uwezo wa kuchanganya tani 300,000 kwa mwaka kwa ajili ya mazao ya parachichi, chai na mazao mengine kulingana na mahitaji ya wakulima na hali ya afya ya udongo kwenye maeneo mbalimbali.

328. ***Mheshimiwa Spika,*** TFC itanunua na kusambaza tani 50,000 za mbolea kutoka kwa wazalishaji wa ndani ili kuviwezesha viwanda vya ndani kuongeza uzalishaji na kupunguza utegemezi wa uagizaji mbolea kutoka nje ya nchi. Pia, itanunua malori matano (5) yenye uwezo wa kubeba mbolea tani 30 kila moja ili kuwezesha usambazaji wa mbolea.

329. ***Mheshimiwa Spika,*** TFC itaanzisha kiwanda cha kutengeneza chokaa mazao chenye uwezo wa kuzalisha tani 250,000 hadi 500,000 kwa mwaka katika eneo lenye ukubwa wa hekta 39 Kata ya Mzizima, Halmashauri ya Jiji la Tanga, Mkoa wa Tanga. Vilevile, itajenga ghala mbili (2) zenye uwezo wa kuhifadhi tani 5,000 za mbolea kila moja katika mikoa ya Tanga (Tanga Jiji) na Ruvuma (Tunduru).

330. ***Mheshimiwa Spika,*** TFC itakarabati ghala nne (4) za kuhifadhi mbolea zenye uwezo wa kuhifadhi tani 55,000 zilizopo katika mikoa ya Mbeya (15,000), Mwanza (5,000), Tabora (20,000) na Rukwa (15,000). Pia, itaendelea kutafuta mbia kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda cha kuzalisha mbolea aina ya *Triple Super Phosphate* – TSP, *Single Super Phosphate* – SSP, MAP, Urea na DAP kwa kutumia madini ya makaa ya mawe na *phosphate* katika Mkoa wa Songwe.

b) Ruzuku ya Mbegu

331. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027, Wizara kupitia COPRA imepanga kusambaza mbegu bora za alizeti tani 120 na tani 480 za mazao ya mikunde na mafuta ikiwemo ufuta 100, choroko 100, dengu 100, soya 20 na mbaazi 160 kwa mpango wa ruzuku kwa lengo la kuwawezesha wakulima kupata mbegu bora kwa bei nafuu na kuongeza tija na uzalishaji. Mpango huu unalenga kuwafikia wakulima 139,000 katika maeneo ya uzalishaji nchini.

c) Upatikanaji wa Viuatilifu na Udhibiti wa Visumbufu vya Mazao na Mimea

332. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania (TPHPA) katika mwaka 2026/2027, itaendelea kuimarisha matumizi sahihi ya viuatilifu ili kudhibiti magonjwa na wadudu waharibifu wa mazao na mimea na hivyo kuwezesha usalama wa chakula pamoja na kukuza soko la bidhaa za kilimo ndani na nje ya nchi. Katika kufanikisha hayo Wizara itatekeleza yafuatayo:-

333. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuhakikisha uzalishaji wa mazao ya kilimo unaongezeka na kupunguza upotevu wa mazao kabla ya kuvuna, Wizara kupitia TPHPA, itanunua na kusambaza lita 100,000 za viuatilifu kwa ajili ya udhibiti wa milipuko ya visumbufu vya mimea na mazao na kwa kutumia wadudu rafiki. Aidha, katika maeneo yasiyofikika kwa urahisi na yenye athari za milipuko ya visumbufu vya mimea na mazao, TPHPA itadhibiti visumbufu hivyo kwa kutumia teknolojia mbalimbali ikiwemo udhibiti kwa njia ya

anga ambapo itatumia ndege ya kilimo na ndege nyuki za kunyunyizia viuatilifu.

334. ***Mheshimiwa Spika,*** TPHPA itazalisha aina 10 za wadudu rafiki kwa ajili ya udhibiti wa visumbufu kwenye mazao ya muhogo, mahindi na baadhi ya mazao ya bustani. Vilevile, itasajili wafanyabiashara wa viuatilifu nchini ili kupunguza viuatilifu feki. Aidha, itaendelea na ukarabati wa Ofisi ya Makao Makuu, Ofisi tatu (3) za Kanda za Magharibi, Nyanda za Juu Kusini na Mashariki ili kupeleka huduma karibu na wananchi. Pia, itaanza ujenzi wa maabara ya ubora wa mazao katika Mkoa wa Njombe ili kuimarisha uchunguzi na udhibiti wa visumbufu vya mazao na kuongeza upatikanaji wa masoko ya kimataifa.

335. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha mazao yanayouzwa nje na ndani ya nchi yanakidhi viwango ili kulinda afya ya mlaji, mazingira na kukuza biashara, TPHPA itakagua tani 1,500,000 za mazao na mimea. Aidha, itapima viwango vya mabaki ya viuatilifu (Maximum Residual Limits – MRLs) kwa mazao ya chakula. Pia, itatoa mafunzo kwa wakulima 9,000, wafanyabiashara wa pembejeo za kilimo 252 na Maafisa Ugani 6,748 kuhusu utambuzi, ufuatiliaji na mbinu bora za kudhibiti visumbufu vamizi kwa lengo la kuongeza tija.

336. ***Mheshimiwa Spika,*** TPHPA itafanya majaribio 1,000 ya ufanisi wa kibaiolojia wa viuatilifu vipya kwa ajili ya usajili. Vilevile, itaendelea na ukaguzi wa maduka ya pembejeo za kilimo na ghala za kuhifadhi viuatilifu 4,000 kwa ajili ya kudhibiti ubora wa viuatilifu. Aidha, ili kuhakikisha katika mipaka yote tunakuwa na vituo kwa ajili ya kutoa huduma kwa wafanyabiashara na kulinda afya ya mimea, TPHPA itafungua ofisi za ukaguzi wa mazao na mimea katika vituo 14 vya mipakani katika Kanda ya Ziwa, Kaskazini, Magharibi, Nyanda za Juu Kusini, Mashariki na Kusini.

337. ***Mheshimiwa Spika,*** TARI itaendelea na tafiti 18 za visumbufu vya mimea (magonjwa na wadudu) kwa mazao ya korosho, mitende, miwa, maharage, viazi mviringo, soya, mbogamboga, ngano, pamba, kahawa, minazi na miti ya miyombo ili kudhibiti visumbufu na kuongeza tija katika uzalishaji.

5.1.4 Usajili wa Wakulima na Urasimishaji wa Shughuli za Kilimo

338. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kurahisisha upatikanaji wa huduma za kilimo kidijiti, Wizara katika mwaka 2026/2027, itaendelea na usajili wa wakulima, wafanyabiashara wa mazao ya kilimo, watoa huduma za ugani, ghala na pembejeo za kilimo. Vilevile, kupitia TFRA itaendelea kutoa hatimiliki na kadi za kielektroniki (smart card) kwa wakulima 10,000 kwa lengo la kurahisisha upatikanaji wa huduma mbalimbali ikiwemo kununua pembejeo za kilimo.

5.1.5 Kuimarisha Huduma za Ugani Vitendea Kazi na Miundombinu ya Kujifunzia

339. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuimarisha utoaji wa huduma za ugani nchini, Wizara katika mwaka 2026/2027, imepanga kununua na kusambaza vitendea kazi kwa Maafisa Ugani ikiwemo magari 107, pikipiki 1,000 na mavazi maalum ya utambulisho 2,021. Vilevile, katika kuimarisha uhaulishaji wa teknolojia za kilimo kwa wakulima ili kuongeza tija na uzalishaji, Wizara itaendelea na ujenzi wa miundombinu katika viwanja vya maonesho ya wakulima ya Nanenane vya Dkt. John Samuel Malecela (Dodoma) na John Mwakangale (Mbeya).

340. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TARI itaendelea kuimarisha vituo sita (6) mahiri vya usambazaji na uhaulishaji wa teknolojia kwa kuviwekea miundombinu ya umwagiliaji katika viwanja vya maonesho ya nanenane vya Nyakabindi, Themi, Nyamuhongolo, Fatuma Mwasa, Ngongo na John Mwakangale. Lengo ni kuwezesha utoaji wa huduma na uhaulishaji wa teknolojia za kilimo mwaka mzima.

341. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia, Wizara itaendelea kukarabati miundombinu ya vituo vinne (4) vya uhaulishaji wa teknolojia za kilimo vya MATI Mtwara, Mlingano, Igurusi na Ichenga. Vilevile, itaendelea na ukarabati wa vituo vinne (4) vya Rasilimali za Kilimo vya Kata katika mikoa ya Dodoma, Singida, Tanga na Tabora. Pia, itajenga mabwawa matano (5) katika Vyuo vya Mafunzo ya Wakulima vya MATI – Ilonga, MATI Tumbi, MATI Ukiriguru, MATI

Igurusi na MATI Uyole kwa ajili ya kuvuna maji ya mvua kwa lengo la kutoa mafunzo ya kilimo kinachokabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

342. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha huduma za ugani zinasogezwa karibu na wakulima, Wizara itakamilisha ujenzi wa nyumba 55 za Maafisa Ugani katika mikoa 19 nchini. Vilevile, itaendelea na ujenzi na ukarabati wa vituo vitano (5) vya Rasilimali za Kilimo vya Kata (Ward Resource Centres – WARC's) ili kuwezesha wakulima kupata mafunzo na huduma za kilimo katika vituo hivyo.

343. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea na ujenzi wa miundombinu ya Chuo cha Taifa cha Sukari Kidatu ili kuwa kituo mahiri cha tasnia ya sukari katika ukanda wa SADC na kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia. Lengo ni kuzalisha wataalamu mahiri katika tasnia ya sukari ili kuongeza tija na uzalishaji katika tasnia ya sukari nchini.

Mafunzo ya Kilimo

344. ***Mheshimiwa Spika,*** ukombozi wa kweli wa mkulima haupatikani kwa kutoa vitendea kazi pekee, bali kwa kupatiwa mafunzo ili kukuza ujuzi na maarifa. Wizara katika mwaka 2026/2027, itaendesha programu za uhaulishaji teknolojia za kilimo ikiwemo kutoa mafunzo ya kanuni za kilimo bora, uendeshaji na usimamizi wa matumizi endelevu ya zana za kilimo, kilimo biashara na teknolojia himilivu kwa wakulima 1,200,000. Vilevile, itagharamia mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi 2,320 wa ngazi ya Astashahada na Stashahada kupitia vituo vya kuhaulisha teknolojia za kilimo kwa ajili ya kuwajengea wanafunzi umahiri kwenye mnyororo wa uzalishaji na usimamizi wa mazao mahsusi.

345. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na kiongozi mahiri Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itaendelea kutekeleza azma ya kumuinua mkulima kupitia mafunzo ambayo yatatolewa na maafisa ugani. Ili kufikia lengo hilo Wizara itaendelea kutoa

mafunzo rejea kwa Maafisa Ugani 1,200 ili kuendana na mahitaji na mabadiliko ya teknolojia ambazo watazifikisha kwa wakulima.

5.1.6 Kuanzisha Mashamba Makubwa ya Pamoja na Kupima Afya ya Udongo

346. ***Mheshimiwa Spika***, wengi wetu tunatambua kuwa ardhi ni mali na asili ya utajiri wetu na hatuwezi kuupata utajiri huo kwa kiwango chake kwa kuendeleza uzalishaji katika mashamba madogo. Ni lazima ardhi tuifanye iseme kwa lugha ya mafanikio kupitia mashamba makubwa. katika mwaka 2026/2027, Wizara itakamilisha uchoraji wa ramani za kidijiti zinazoonesha hali ya afya ya udongo nchini na kutoa mapendekezo ya matumizi sahihi ya pembejeo za kilimo katika maeneo yote yanayotumika kwa kilimo katika ngazi za vijiji. Vilevile, Wizara itatambua, itapima na itawezesha umiliki wa mashamba yenye ukubwa wa ekari 80,000 kwa ajili ya uwekezaji wa kilimo biashara kwa mazao ya kimkakati ya chikichi na ngano.

347. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara itanunua na kusambaza *soil scanner* 43 kwa ajili ya kupima afya ya udongo katika Halmashauri 43 ili kuhakikisha matumizi sahihi ya pembejeo za kilimo kwa wakulima. Aidha, Wizara itaendelea na ujenzi wa ofisi mbili (2) za usimamizi na mipango ya matumizi ya ardhi ya kilimo katika Kanda ya Ziwa (Mwanza) na Mashariki (Morogoro) kwa ajili ya kusogeza huduma karibu na wakulima.

5.1.7 Uendelezaji wa Kilimo cha Umwagiliaji

348. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027, Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji itaendelea na ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji katika miradi 118 kama ifuatavyo: -

i. Ujenzi wa skimu 55 za umwagiliaji zenye jumla ya hekta 124,626;
ii. Ujenzi wa mabwawa 23 yenye mita za ujazo 100,629,958;
iii. Ukarabati wa skimu 39 za umwagiliaji zenye jumla ya hekta 106,480; na

iv. Ufungaji wa miundombinu ya umwagiliaji katika shamba la Chinangali awamu ya pili lenye ukubwa wa hekta 620.8.

349. *Mheshimiwa Spika,* vilevile, Tume itaendelea na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa skimu za umwagiliaji 389, mabwawa 49 na mabonde ya kimkakati saba (7) yenye ukubwa takriban hekta 168,796.

350. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027, Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji itaendelea na ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika shamba la Bugwema lenye jumla ya hekta 3,000. Vilevile, Tume itaanza ujenzi wa mabwawa ya Mbakiamtuli na Ngorongo katika bonde la Rufiji yenye jumla ya mita za ujazo 57,548,653 zitakazomwagilia eneo lenye jumla ya hekta 64,800; na kuanza ujenzi wa skimu katika Bonde la mto Ngono lenye jumla ya hekta 20,470.

351. *Mheshimiwa Spika,* Wizara itaendelea kushirikiana na Wizara ya Maji kuhakikisha mradi wa kutumia maji ya Ziwa Victoria na Tanganyika (mradi wa Gridi ya Taifa ya Umwagiliaji) kwa ajili ya umwagiliaji unatekelezwa. Mradi wa Gridi ya Taifa ya umwagiliaji utanufaisha wakulima wa mikoa ya Simiyu, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Kigoma, Mwanza, Geita, Mara, Kagera, Rukwa na Katavi, Wilaya 69, Kata 192 na Vijiji 943.

352. *Mheshimiwa Spika,* katika kuhakikisha uendelevu wa miradi ya umwagiliaji, Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji itaendelea kuimarisha usimamizi wa miundombinu ya umwagiliaji kwa kusajili vyama vya umwagiliaji 100; kutoa mafunzo ya uendeshaji na utunzaji wa miundombinu ya umwagiliaji kwa wakulima 5,000; itaingia mikataba na vyama vya umwagiliaji 500 kuhusu uendeshaji, usimamizi na matunzo ya miundombinu; na kutoa mafunzo ya ukusanyaji wa ada ya huduma za umwagiliaji kwa vyama vya umwagiliaji 500.

5.1.8 Uanzishaji wa Vituo vya kutoa Huduma na Ununuzi wa Zana za Kilimo

353. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027, Wizara itaanzisha vituo 100 vya kutoa huduma ya zana za kilimo kati ya vituo 1,000 vinavyotarajiwa kuanzishwa ifikapo mwaka 2030. Aidha, Wizara itanunua trekta 500, *power tiller* 200 na mashine 50 za kuvuna na kukausha nafaka kwa ajili ya shughuli za kilimo. Vilevile, itaanzisha Kituo cha Zana za Kilimo cha Taifa (National Mechanization Centre) ambacho kitakuwa na zana zote za msingi kwa ajili ya kusafisha na kusawazisha mashamba, uchimbaji wa visima na mabwawa na kutoa mafunzo.

Uzalishaji wa Mazao kwa Mwaka 2026/2027

354. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027, Wizara itaendelea kusimamia na kutekeleza mikakati ya uzalishaji wa mazao ya kilimo kulingana na mahitaji ili kuongeza tija katika uzalishaji. Mazao hayo yanahusisha Mazao Asilia ya Biashara, Mazao ya Bustani, Mazao ya Chakula, Mazao ya Mafuta na mazao yenye mahitaji makubwa yanayoagizwa nje ya nchi.

Mazao Asilia ya Biashara

355. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea kuhamasisha wakulima kuongeza uzalishaji wa mazao asilia ya biashara ikiwemo pamba, kahawa, mkonge, korosho, tumbaku, pareto, kakao na chai kutoka jumla ya tani 1,599,945.66 mwaka 2025/2026 hadi tani 2,118,000 mwaka 2026/2027 kama inavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 6**.

Jedwali Na. 6: Malengo ya Uzalishaji wa Mazao Asilia ya Biashara (Tani) katika Mwaka 2026/2027

Na.	Mazao	2025/2026	2026/2027
		Uzalishaji	**Malengo**
1	Korosho	617,683.77	750,000
2	Pamba	222,014	400,000
3	Pareto	2,780*	3,000
4	Kahawa	74,663.60	85,000
5	Tumbaku	185,776	205,000
6	Chai	11,631.48*	30,000
7	Mkonge	64,321.77*	80,000
8	Sukari	410,979.04	550,000
9	Kakao	10,096*	15,000
Jumla		**1,599,945.66**	**2,118,000**

* *Uzalishaji unaendelea*

356. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kufikia malengo hayo, mikakati ya uzalishaji kwa kila zao ni kama ifuatavyo:-

Zao la Pamba

357. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Bodi ya Pamba Tanzania itaendelea kuhamasisha wakulima kuongeza uzalishaji wa zao la pamba kutoka tani 222,014 mwaka 2025/2026 hadi tani 400,000 mwaka 2026/2027. Uzalishaji huo utafikiwa kwa kusambaza mbegu bora za pamba tani 18,000, chupa (acrepacks) 10,000,000 navinyunyizi 20,000. Vilevile, Bodi kwa kushirikiana na wadau itazalisha na kusambaza mbolea hai lita 7,200,000 zenye uwezo wa kunyunyuzia hekta 360,000 pamoja na kuimarisha huduma za ushauri wa kitaalamu katika maeneo ya uzalishaji.

358. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Bodi ya Pamba itaandaa mradi maalum wa *Complete Cotton Village* kwa kuhamasisha vyama vya ushirika vinne (4) katika uongezaji thamani wa zao la pamba katika Mkoa wa Simiyu. Vilevile, itanunua na kusimika mtambo wa kuchakata mbegu wenye uwezo wa kuchakata tani 15,000 kwa mwaka ili kupunguza gharama na kuongeza uendelevu wa upatikanaji wa mbegu. Aidha, Bodi itaendelea

kutafuta mbia wa kuanzisha kiwanda cha kuchakata na kutengeneza pamba za hospitali na nyuzi kwa ajili ya kufungia tumbaku (cotton twine) katika Mkoa wa Simiyu. Hatua hiyo itasaidia kupunguza matumizi ya fedha za kigeni kutokana na uagizaji wa vifaa tiba vinavyotokana na pamba.

359. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea kuratibu ujenzi wa kongani ya pamba (industrial park) kwenye eneo la ekari 1,000 katika Mkoa wa Mwanza. Aidha, itaanzisha mashamba makubwa ya pamoja ya pamba yenye ukubwa wa ekari 20,000 kwa ajili ya vijana na wanawake katika mikoa ya Simiyu, Singida na Kigoma. Vilevile, itaendelea kuboresha vituo vya mafunzo ya wakulima katika mikoa ya Simiyu - Nyakabindi na Tabora - Igunga ili kuviwezesha kutoa huduma za zana za kilimo.

360. ***Mheshimiwa Spika,*** Aidha, itanunua na kusimika mitambo miwili (2) ya kuzalisha nishati ya kupikia inayotokana na masalia ya mashina ya pamba na mitambo nane (8) ya kusokota nyuzi za pamba na kuzalisha vikoi na mitandio. Pia, Bodi kwa kushirikiana na Tume ya Maendeleo ya Ushirika itaendelea kuratibu ufufuaji wa *Ginnery* mbili (2) zilizopo Mhunze na Uzogole.

Zao la Chai

361. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha tasnia ya chai nchini, Wizara kupitia Bodi ya Chai Tanzania itahamasisha wakulima kuongeza uzalishaji wa chai kavu kutoka tani 11,631.48 mwaka 2025/2026 hadi tani 30,000 mwaka 2026/2027. Vilevile, katika kuimarisha masoko na uongezaji thamani wa zao la chai, Bodi kwa kushirikiana na wadau wa sekta binafsi itaratibu uanzishwaji wa viwanda vitatu (3) vya kuchakata na kuchanganya chai. Aidha, Bodi itatoa mafunzo kuhusu matumizi ya mifumo ya kilimo mtandao kwa wakulima 15,000 wa zao la chai katika mikoa ya Iringa, Mbeya na Njombe.

362. ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi ya Chai itaendelea kuratibu uendeshaji wa mnada wa chai wa Dar es Salaam na kuwezesha mnada huo kufanyika kwa njia ya mtandao ili kupata masoko mapya ya kimataifa na kuimarisha bei ya chai kavu. Vilevile,

itawezesha utekelezaji na usimamizi wa viwango endelevu vya hiari (Voluntary Sustainability Standards – VSS) na uthibitishaji wa mazingira, jamii na utawala bora (Enviromental Social and Governance – ESG) ikiwemo ajira zenye staha na hifadhi za bioanuai katika mashamba ya chai kwa wakulima wa chai 4,040 wa Mufindi na Lupembe.

Zao la Kahawa

363. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027, Wizara kupitia Bodi ya Kahawa Tanzania itahamasisha wakulima kuongeza uzalishaji wa zao la kahawa kutoka tani 74,663.60 mwaka 2025/2026 hadi tani 85,000. Vilevile, itatoa mafunzo kuhusu kanuni za kilimo bora cha zao la kahawa na mbinu za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa wakulima 2,300 na Maafisa Ugani 217 kwenye maeneo ya uzalishaji. Pia, itaweka mfumo wa kusimamia uandaaji, usambazaji na utunzaji wa miche inayozalishwa.

364. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuongeza uzalishaji wa zao la kahawa, Bodi ya Kahawa kwa kushirikiana na TARI itazalisha na kusambaza miche ya kahawa 30,000,000. Vilevile, itawezesha uanzishaji wa mashamba mapya ya kahawa yenye ukubwa wa hekta 4,000 katika Halmashauri 54 zinazozalisha kahawa.

365. ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi itanunua na kusimika mashine nne (4) za kumenya kahawa kwa ajili ya vyama vya ushirika vilivyopo katika wilaya za Mbinga na Mbozi kwa lengo la kuongeza thamani ya zao la kahawa. Kadhalika, itachimba visima 10 katika mashamba makubwa ya kahawa (block farm) katika maeneo ya uzalishaji ili kuwezesha wakulima kupata maji ya uhakika kwa ajili ya umwagiliaji.

Zao la Korosho

366. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027 Wizara kupitia Bodi ya Korosho Tanzania, itahamasisha wakulima kuongeza uzalishaji wa korosho kutoka tani 617,683.77 mwaka 2025/2026 hadi tani 750,000. Lengo hilo litafikiwa kwa kuendelea kutoa

mafunzo kuhusu kanuni za kilimo bora cha zao la korosho kwa wakulima 2,000 katika maeneo ya uzalishaji. Vilevile, Bodi itanunua na kusambaza viuatilifu vya *Sulphur* ya unga tani 30,000 na viuatilifu vya maji lita 1,500,000 kwa ajili ya udhibiti wa visumbufu vya zao la korosho.

367. ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi ya Korosho, itaanzisha mashamba ya pamoja ya korosho yenye ukubwa wa hekta 3,520 katika mikoa ya Pwani (2,600), Singida (120), Lindi (200), Katavi (200) na Mbeya (400). Kadhalika, itaendelea na ujenzi wa miundombinu ikiwemo, kuchimba visima - 5, kujenga zahanati - 1, jengo la utawala - 1, nyumba- 5 na ghala - 1 katika kongani la viwanda la Maranje.

368. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha upatikanaji wa miche ya korosho, Bodi kwa kushirikiana na TARI na sekta binafsi itazalisha na kusambaza miche ya korosho 5,000,000. Vilevile, itawatambua na kuwasajili wazalishaji 3,000 wa miche ya korosho na kuendelea kuhuisha kanzidata ya wakulima wa korosho.

369. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuhamasisha uwekezaji na upatikanaji wa masoko ya zao la korosho, Bodi itanunua vifaa na mashine za viwandani katika kongani la viwanda la Maranje. Vilevile, itaendelea na ujenzi wa viwanda vitatu (3) vya kubangua korosho vyenye uwezo wa kubangua tani 230,000 kwa mwaka vitavyojengwa kupitia wawekezaji wa Kampuni ya Mateak Holding LTD (tani 100,000), Dorado Cashew Ltd. (tani 100,000) na Korosho Investment (tani 30,000).

370. ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi itaendelea na ujenzi wa ghala nne (4) zenye uwezo wa kuhifadhi tani 38,000 katika Halmashauri za Mkinga (tani 10,000), Tunduru (tani 10,000), Mkuranga (tani 10,000) na Mtwara (tani 8,000). Vilevile, itahamasisha Vyama Vikuu vya Ushirika vya TANECU, MAMCU na CORECU kuendelea na ujenzi wa ghala tatu (3) zenye uwezo wa kuhifadhi jumla ya tani 15,000 za korosho kwa lengo la kuongeza thamani ya zao la korosho.

Zao la Mkonge

371. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Bodi ya Mkonge Tanzania itahamasisha wakulima kuongeza uzalishaji wa zao la mkonge kutoka tani 64,321.77 mwaka 2025/2026 hadi tani 80,000 mwaka 2026/2027. Vilevile, itasambaza miche ya mkonge 3,500,000 kwa wakulima. Aidha, Bodi kwa kushirikiana na TARI itatoa mafunzo kuhusu uzalishaji wa mkonge na uongezaji thamani wa zao hilo kwa wadau 200 na Maafisa Ugani 50.

372. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuhamasisha uongezaji thamani wa zao la mkonge, Bodi itaendelea na ununuzi na usimikaji wa mashine 10 za kuchakata mkonge (dikotiketa) zenye uwezo wa kuchakata tani mbili (2) kwa siku katika mikoa ya Tanga (6), Morogoro (2), Shinyanga (1) na Tabora (1). Aidha, itakamilisha ujenzi wa vituo viwili (2) vya kuchakata zao la mkonge katika Wilaya ya Mkinga na Handeni.

373. ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi ya Mkonge itaanzisha vituo 13 vya ukusanyaji na uuzaji wa mkonge kwa ajili ya wakulima wadogo na kuweka miundombinu ya uongezaji thamani *(brushing & baling)* katika mikoa ya Singida, Pwani na Tanga ili kuimarisha upatikanaji wa masoko ya zao la mkonge.

374. ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi itakamilisha ujenzi wa ghala, ofisi na miundombinu ya maji taka katika viwanda vya Taula na Kibaranga vilivyopo katika Halmashauri za Wilaya za Handeni na Muheza. Pia, itakamilisha malipo ya mashine saba (7) za kuchakata mkonge zinazomilikiwa na Kampuni ya Sisalana katika mashamba matano (5) ya Hale (1), Magoma (2), Magunga (1), Ngombezi (1) na Mwelya (2).

Zao la Tumbaku

375. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Bodi ya Tumbaku Tanzania itaendelea kuhamasisha wakulima kuongeza uzalishaji wa zao la tumbaku kutoka tani 185,776 mwaka 2025/2026 hadi tani 200,000 mwaka 2026/ 2027 kulingana na mikataba kati ya wakulima na makampuni ya tumbaku. Vilevile, itahamasisha na kutoa mafunzo

kuhusu kanuni za kilimo bora cha zao la tumbaku kwa wakulima 8,000 na Maafisa Ugani 250 kutoka kwenye kampuni za tumbaku, Vyama vya Ushirika na Halmashauri za Wilaya katika maeneo ya uzalishaji. Aidha, itaanzisha shamba darasa moja (1) lenye ukubwa hekta 40 katika Halmashauri ya Chunya, Mkoa wa Mbeya.

376. *Mheshimiwa Spika,* Bodi itakamilisha ujenzi wa ofisi katika Halmashauri za Kaliua na Manispaa ya Songea na kununua magari mawili (2) kwa ajili ya kuratibu na kuwezesha utekelezaji wa shughuli za Bodi. Aidha, itajenga Ofisi mbili (2) za Kanda katika mikoa ya Tabora (Sikonge) na Kigoma (Kasulu) na kununua vifaa vya ofisi. Kukamilika kwa shughuli hizo, kutawezesha Bodi kuimarisha utekelezaji wa majukumu yake.

377. *Mheshimiwa Spika,* ili kuongeza thamani ya zao la tumbaku, Bodi kwa kushirikiana na wadau itasimamia ujenzi wa mabani 750 ya tumbaku kwa ajili ya kukaushia tumbaku katika mikoa ya Tabora, Shinyanga, Katavi, Kigoma, Mbeya, Songwe, Geita, Kagera, Singida, Ruvuma na Iringa. Vilevile, itanunua na kusimika makaushio matatu (3) ya tumbaku (Curing hubs) yanayotumia nishati ya jua na itajenga ghala moja (1) la kuhifadhia tumbaku katika Mkoa wa Morogoro.

378. *Mheshimiwa Spika,* Pia, Bodi kwa kushirikiana na wadau itaendeleza jitihada za kuhamasisha upandaji wa miti kwa kila mkulima, matumizi ya matawi ya miti badala ya magogo pamoja na nishati mbadala ya kukaushia tumbaku ikiwemo majani tembo na makaa ya mawe ili kupunguza ukataji wa miti na kuendeleza jitihada za uhifadhi wa mazingira.

379. *Mheshimiwa Spika,* Bodi kwa kushirikiana na *Tumbaku Cooperative Joint Enterprise* (TCJE) itaratibu ununuzi na usambazaji wa viuatilifu aina ya *Flumetralin* lita 142,857.14 *Imidacloprid* (30g/pkt) pakiti 1,142,857.14 na *Deltamethrin* (20ml/chupa) chupa 1,714,285.71 kwa ajili ya kudhibiti visumbufu vya zao la tumbaku.

Zao la Pareto

380. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko (COPRA), itaendelea kuhamasisha wakulima kuongeza uzalishaji wa zao la pareto kutoka tani 2,780 mwaka 2025/2026 hadi tani 3,000 mwaka 2026/2027. Vilevile, itatoa mafunzo kuhusu kanuni za kilimo bora cha zao la pareto kwa wakulima viongozi 450 na wakaguzi wa pareto 50 kupitia mashamba darasa 100 yatakayoanzishwa katika maeneo ya uzalishaji kwa kushirikiana na wadau wa zao la pareto.

381. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha ubora wa pareto inayozalishwa nchini inakidhi viwango vya kimataifa, Wizara kupitia COPRA itaendelea na ujenzi wa makaushio 150 ya maua ya pareto katika Halmashauri za Makete (30), Ileje (35), Mbeya Vijijini (40), Ludewa (10), Mbulu (25) na Arusha Vijijini (10). Vilevile, itaendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika uongezaji thamani ya zao la pareto ili kuongeza mauzo nje ya nchi. Kadhalika, COPRA itasajili wakulima 20,000 wa zao la pareto kwa kuchukua taarifa zao na majira ya nukta ya mashamba yao kwa lengo la kuwatambua na kuwapa huduma stahiki.

382. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuhakikisha upatikanaji wa mbegu za pareto kwa wakati kwa wakulima, COPRA na TARI kwa kushirikiana na wadau itazalisha na kusambaza mbegu za pareto tani tano (5) katika maeneo ya uzalishaji.

Zao la Kakao

383. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027, Wizara kupitia COPRA itahamasisha wakulima kuongeza uzalishaji wa kakao kutoka tani 10,096 mwaka 2025/2026 hadi tani 15,000. Uzalishaji huo utafikiwa kwa kutoa mafunzo kuhusu kanuni za kilimo bora cha zao la kakao kwa wakulima viongozi 500 na Maafisa Ugani 45 katika Halmashauri za Kyela, Rungwe, Busokelo, Mlimba na Mvomero. Vilevile, COPRA kwa kushirikiana na TARI itazalisha na kusambaza miche 559,500 ya kakao kwa wakulima katika mikoa ya Tanga, Kigoma, Kagera na Morogoro.

384. *Mheshimiwa Spika,* ili kuimarisha uongezaji thamani na kuhakikisha kakao inafikia viwango vya soko la kimataifa, COPRA itaendelea na ujenzi wa miundombinu ya usindikaji na ukaushaji katika vituo saba (7) vya ukusanyaji wa kakao vya Mlimba (1), Kyela (4), Mvomero (1) na Muheza (1) kwa ajili ya uongezaji thamani wa zao la kakao. Tume ya Maendeleo ya Ushirika itahamasisha chama kikuu cha KYECU kuanzisha kiwanda cha kusindika kakao.

Mazao ya Bustani

385. *Mheshimiwa Spika,* katika mwaka 2026/2027, Wizara kupitia COPRA na kwa kushirikiana na wadau itaendelea kuhamasisha na kusimamia utekelezaji wa mikakati ya kuendeleza mazao ya bustani itakayowezesha kuongeza uzalishaji wa mazao hayo kutoka tani 9,781,236.74 mwaka 2024/2025 hadi tani 10,000,000. Uzalishaji huo utafikiwa kwa kutoa mafunzo rejea kuhusu kilimo bora cha mazao ya bustani kwa Maafisa Ugani 1,500 na wakulima 4,000 katika maeneo ya uzalishaji.

386. *Mheshimiwa Spika*, Wizara itaendelea na ujenzi wa vituo jumuishi viwili (2) vya kuchambua, kufungasha na kuhifadhi mazao ya bustani katika Halmashauri za Mufindi (Iringa) na Rungwe (Mbeya) ili kuongeza thamani na kukidhi viwango vya soko la ndani na nje ya nchi.

387. *Mheshimiwa Spika,* mazao ya bustani yameendelea kuwa sehemu muhimu katika kuchochea ajira kwa vijana na wanawake, kuongeza kipato kwa mkulima na kukuza uchumi wa nchi. Serikali inaendelea kuweka mikakati madhubuti ili kuendeleza mazao hayo yakiwemo:-

Zao la Parachichi

388. *Mheshimiwa Spika,* kutokana na fursa kubwa iliyopo ya soko la parachichi ndani na nje ya nchi, Wizara katika mwaka 2026/2027 itahamasisha wakulima kuongeza uzalishaji wa zao la parachichi kutoka tani 201,354 mwaka 2024/2025 hadi tani 235,000. Kati ya hizo, parachichi zinazouzwa nje ya nchi

zinatarajiwa kufikia tani 40,000. Uzalishaji huo utafikiwa kwa Wizara kutoa mafunzo kuhusu kanuni za kilimo bora cha zao la parachichi kwa wakulima 9,500 na Maafisa Ugani 500 katika maeneo ya uzalishaji.

389. *Mheshimiwa Spika,* katika kuhakikisha wakulima wanaongeza mashamba ya parachichi ili kuongeza uzalishaji na kipato, Wizara kupitia TARI na COPRA kwa kushirikiana na wadau itaviwezesha vikundi vya vijana na wanawake kuzalisha na kusambaza miche ya parachichi 1,727,400 kwa mpango wa ruzuku. Hatua hiyo si tu inalenga kuongeza uzalishaji wa parachichi bali ni nia ya dhati ya kuwawezesha vijana kupata ajira zenye staha kupitia kilimo. Aidha, Wizara itaweka mfumo wa kusimamia uandaaji, usambazaji na utunzaji wa miche ya parachichi.

390. *Mheshimiwa Spika,* ili kuimarisha uongezaji thamani na upatikanaji wa masoko ya zao la parachichi, Wizara kupitia COPRA itaendelea na ujenzi wa vituo 20 vya kukusanyia parachichi katika mikoa ya Mbeya nane (8), Iringa vinne (4), Rukwa kimoja (1), Ruvuma viwili (2) na Njombe vitano (5). Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na wadau itaendelea kuhamasisha uzalishaji wa mafuta ya parachichi katika viwanda vya ndani kwa kuwa hadi sasa kuna viwanda vya kati na vikubwa nane (8) vya kuzalisha mafuta ya parachichi.

Zao la Viazi Mviringo

391. *Mheshimiwa Spika*, kutokana na umuhimu mkubwa wa zao la viazi mviringo katika kuchangia usalama wa chakula nchini na chanzo kikubwa cha kipato kwa wananchi. Wizara katika mwaka 2026/2027, imepanga kuongeza uzalishaji wa zao la viazi mviringo kutoka tani 2,961,414.82 mwaka 2024/2025 hadi tani 3,000,000. Katika kufikia lengo hilo, Wizara kwa kushirikiana na wadau itatoa mafunzo kuhusu kanuni za kilimo bora na himilivu cha zao la viazi mviringo kwa wakulima 5,000.

392. *Mheshimiwa Spika*, Wizara kupitia TARI kwa kushirikiana na wadau itatoa mafunzo kuhusu uzalishaji wa mbegu bora za viazi

mviringo kwa wakulima wawezeshaji 500 katika mikoa ya Mbeya, Njombe, Morogoro, Tanga, Arusha, Kilimanjaro na Manyara. Vilevile, Wizara itakamilisha uandaaji wa Mkakati wa Kuendeleza Zao la Viazi Mviringo wenye lengo la kuimarisha uzalishaji wa kibiashara wa zao hilo. Kadhalika, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara itaendelea kutoa elimu kwa wadau wa tasnia ya viazi mviringo kuhusu ufungashaji unaozingatia vipimo kwa mujibu wa sheria zilizopo ili kumlinda mkulima.

393. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuimarisha uzalishaji wa mbegu bora za viazi mviringo, Wizara kupitia TARI itajenga vitalu nyumba viwili (2) katika vituo vya utafiti vya Igeri (Njombe) na Uyole (Mbeya) na kukarabati kitalu nyumba kimoja (1) katika kituo cha TARI Tengeru (Arusha).

Zao la Tufaha (Apples)

394. ***Mheshimiwa Spika***, kwa muda mrefu nchi yetu imekuwa ikitegemea matunda ya tufaha kutoka nje ya nchi licha ya uwepo wa fursa ya kutosha ya uzalishaji wa zao hilo hususan katika maeneo ya Kanda ya Kaskazini, Kati na Kanda ya Nyanda za Juu Kusini yanayofaa kwa uzalishaji wa tufaha zinazokidhi viwango vya ubora wa kimataifa. Hadi Machi 2026, takriban tani 1,481.98 za tufaha ziliingizwa kutoka nje ya nchi. Hali hiyo, inaonesha mahitaji ya zao hilo ni makubwa ndani ya nchi.

395. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2026/2027, Wizara imepanga kuhamasisha wakulima kuongeza uzalishaji wa zao hilo ili kukidhi mahitaji. Kilimo hiki, si tu alama ya mabadiliko ya kifikra bali ni chanzo kipya cha kukuza uchumi wa mkulima mmoja mmoja hususan vijana na wanawake, kuliingizia Taifa fedha za kigeni na kupunguza utegemezi wa bidhaa hiyo kutoka nje ya nchi.

396. ***Mheshimiwa Spika,*** katika safari hii ya kipekee, Wizara kupitia TARI na COPRA itazalisha na kusambaza miche 600,000 ya tufaha kwa wakulima katika maeneo ya uzalishaji. Aidha, itatoa mafunzo kuhusu kanuni za kilimo bora cha zao la tufaha kwa wakulima

2,400 na Maafisa ugani 50 katika maeneo ya uzalishaji. Vilevile, Wizara kupitia COPRA itasajili wakulima 8,261 wa zao la tufaha kwa lengo la kuwatambua na kurahisisha utoaji wa huduma.

397. ***Mheshimiwa Spika,*** jitihada hizo ni kielelezo cha dhamira ya dhati ya kuhakikisha tunatumia fursa zilizopo kuzalisha tufaha ndani ya nchi yetu.

Nitoe wito kwa vijana, wanawake na wawekezaji kuchangamkia kilimo cha tufaha na fursa zilizopo katika mnyororo wake mzima. Tufaha si tu tunda linalotumika kuonesha upendo pekee, bali ni biashara yenye tija na faida ya muda mrefu na ni urithi tunaoweza kuuacha kwa vizazi vijavyo.

Mazao yenye Mahitaji Makubwa

398. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kupunguza matumizi ya fedha za kigeni zinazotumika kuagiza mazao na bidhaa za ngano, sukari na mafuta ya kula kutoka nje ya nchi, Wizara itaendelea kuhamasisha wakulima kuongeza uzalishaji wa mazao hayo kwa kuweka na kutekeleza mikakati mbalimbali ikiwemo kununua ardhi yenye ukubwa usiopungua ekari 80,000 kwa ajili ya kuanzisha mashamba makubwa ya pamoja kwa mazao ya ngano, alizeti na chikichi na kuwapatia wakulima wakubwa na wadogo ili kuongeza uzalishaji. Aidha, mikakati kwa kila zao ni kama ifuatavyo:-

Zao la Ngano

399. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027, Wizara imepanga kuongeza uzalishaji wa zao la ngano kutoka tani 115,826 mwaka 2024/2025 hadi tani 200,000. Lengo hilo litafikiwa kwa kusambaza mbegu za ngano tani 700 kwa wakulima kupitia mpango wa ruzuku na kuanzisha vituo maalum vya kuzalisha mbegu za ngano katika mashamba makubwa ya pamoja. Vilevile, COPRA itatoa mafunzo ya mbinu za kilimo bora cha ngano kwa wakulima 2,000 na maafisa ugani 100 kwenye mikoa ya uzalishaji.

400. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kupata mbegu zinazostahimili hali ya joto kwa lengo la kuongeza uzalishaji, TARI itaendelea na majaribio ya aina 82 za mbegu mpya za ngano katika mikoa ya Morogoro na Tanga. Pia, TARI itaendelea na tafiti za mbegu za ngano zenye kukidhi sifa ya mahitaji ya soko na tija katika uzalishaji. Vilevile, katika kuhakikisha upatikanaji wa mbegu za ngano, TOSCI itatoa mafunzo ya uzalishaji wa mbegu za kuazimia ubora (QDS) kwa wakulima 500 katika Wilaya za Nkasi, Babati, Hanang, Songwe, Mbinga, Siha na Makete. Kadhalika, Wizara kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika itaendelea kuhamasisha vyama vya ushirika kuanzisha mashamba makubwa ya ngano na viwanda vidogo vya kuchakata ngano.

Zao la Miwa na Uzalishaji wa Sukari

401. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027, Wizara kupitia Bodi ya Sukari Tanzania itaongeza uzalishaji wa zao la miwa kutoka tani 4,351,673.1 zilizozalisha sukari tani 410,979.04 mwaka 2025/2026 hadi tani 5,500,000 za miwa zitakazozalisha sukari tani 550,000. Vilevile, Wizara kupitia TARI itaanzisha shamba la kuzalisha mbegu za miwa lenye ukubwa wa ekari 10 katika Halmashauri ya Kilosa ambalo litakuwa na uwezo wa kuzalisha jumla ya tani 400 za mbegu za miwa. Pia, itazalisha mbegu za miwa tani 200 kutoka kwenye shamba la ekari 5 la Mvomero.

402. ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi kwa kushirikiana na TARI itaanzisha vitalu vya kuzalisha miche ya miwa kwenye eneo lenye ukubwa wa hekta 100 katika bonde la Kilombero kwa ajili ya wakulima wadogo wa miwa.

403. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuongeza uwekezaji katika zao la miwa, Wizara kupitia Bodi ya Sukari itaandaa maeneo kwa ajili ya uwekezaji wa kilimo cha miwa nchini ikihusisha eneo la Bonde la Mto Pangani (Korogwe, Muheza, Handeni na Pangani) lenye hekta 146,704.6 na kwenye sehemu ya Bonde la Wembere (Tabora) lenye hekta 15,218 lililopo katika Wilaya za Uyui na Igunga kwa ajili ya uzalishaji wa sukari.

404. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara itaendelea kuratibu uanzishaji wa viwanda viwili (2) vya sukari katika mikoa ya Pwani na Kigoma. Kadhalika, itaratibu uwekezaji wa kujenga viwanda vitatu (3) katika Mkoa wa Tanga ambapo kimoja ni kwa ajili ya sukari ya viwandani na viwili (2) ni kwa ajili ya sukari ya kawaida itakayotumika kama malighafi ya kuzalisha sukari ya viwandani.

Mazao ya Mafuta

405. ***Mheshimiwa Spika,*** mahitaji ya mafuta ya kula nchini ni takriban tani 731,974 ikilinganishwa na uzalishaji wa tani 305,906 kwa mwaka. Uzalishaji huo ni pungufu kwa tani 426,068 ambapo huilazimu nchi kutumia fedha nyingi za kigeni kuagiza mafuta ya kula nje ya nchi kwa ajili ya kufidia pengo hilo.

406. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kupunguza utegemezi wa mafuta ya kula kutoka nje ya nchi, Wizara katika mwaka 2026/2027, itahamasisha wakulima kuongeza uzalishaji wa mazao ya mafuta kutoka tani 2,248,046.24 mwaka 2024/2025 hadi tani 2,300,000 kwa kutoa mafunzo kuhusu kanuni za kilimo bora cha mazao ya mafuta kwa wakulima katika maeneo ya uzalishaji. Vilevile, itaanzisha mashamba makubwa ya pamoja yenye ukubwa wa hekta 48,000 kwa ajili ya zao la chikichi na alizeti katika mikoa ya Kigoma, Morogoro, Singida na Dodoma.

407. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itasambaza mbegu bora za alizeti tani 120 kwa wakulima kwa mpango wa ruzuku pamoja na kuzalisha na kusambaza miche ya chikichi 2,000,000 kwa wakulima katika maeneo ya uzalishaji. Kadhalika, itaratibu upatikanaji na usambazaji wa mbegu bora za karanga tani 20.1 na mbegu za ufuta tani 100. Wizara itakamilisha na kuanza utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Mafuta ya Kula (National Edible Oil Strategy), wenye lengo la kuongeza uzalishaji na kujitosheleza kwa mafuta ya kula nchini.

5.2 Kuchangia Kuongeza Ajira zenye Staha na Ushiriki wa Vijana na Wanawake kwenye Kilimo

408. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea kutekeleza kipaumbele cha kuchangia kuongeza ajira zenye staha kwa vijana na wanawake kufikia 3,000,000 ifikapo mwaka 2030. Ajira hizo zitatokana na utekelezaji wa programu ya BBT katika miradi ya mashamba makubwa katika maeneo walipo vijana na wanawake ngazi ya Halmashauri; kuendelea kuwezesha ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji kwa wakulima wadogo (BBT visima); upatikanaji wa mikopo kwa vijana na wanawake (BBT mitaji); na kuongeza thamani ya mazao na kutoa huduma za ugani (BBT Ugani).

5.2.1 Kuwezesha Uendelezaji wa Programu ya BBT Ngazi ya Halmashauri

409. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea kutekeleza Programu ya BBT katika Halmashauri 20 zilizotenga maeneo yasiyopungua ukubwa wa ekari 200 katika mikoa ya Dodoma, Singida, Tabora, Njombe, Mbeya, Iringa, Pwani, Mara, Katavi, Rukwa, Kagera na Geita. Vilevile, Wizara itawajengea uwezo vijana 2,000 watakaochaguliwa na Halmashauri zao kuhusu kilimo biashara kupitia program ya BBT kwenye vyuo na vituo vya mafunzo ya kilimo. Wizara itaanza ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji, barabara na hifadhi ya mazao ya kilimo katika shamba la Mapogolo Wilaya ya Chunya.

410. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea na ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji na uhifadhi katika mashamba ya Ndogowe na Chinangali katika Wilaya ya Chamwino. Vilevile, itaendelea kufungua mashamba na kuweka miundombinu muhimu ya uzalishaji katika mashamba 20 ya Halmashauri. Kadhalika, upembuzi yakinifu utafanyika kwa ajili ya kuweka miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba makubwa ya pamoja matano (5) yaliyopo katika mikoa ya Tabora, Singida, Mbeya na Dodoma.

411. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaratibu utekelezaji wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii (TAM) katika mashamba matano (5) ya pamoja. Vilevile, itajenga ghala nane (8), chumba cha ubaridi, uzio na kuweka miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba ya BBT Ndogowe na Chinangali. Pia, wizara imepanga kusafisha ekari 1,800 katika shamba la BBT Ndogowe.

5.2.2 Kuwezesha Ujenzi wa Miundombinu ya Umwagiliaji kwa Wakulima Wadogo (BBT Visima)

412. ***Mheshimiwa Spika,*** kilimo cha umwagiliaji ni nguzo muhimu katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Ili kuendeleza kilimo cha umwagiliaji nchini, Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji katika mwaka 2026/2027, itachimba visima 846 vya umwagiliaji katika mikoa 25 nchini kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji na kufunga mifumo ya umwagiliaji katika Halmashauri 178 nchini; na itanunua *surface pump* za umwagiliaji 1,000 kwa ajili ya makundi ya wanawake na vijana kutoka kwenye maeneo ya pembezoni mwa Ziwa Victoria na Tanganyika.

5.2.3 Kuwezesha Upatikanaji wa Mikopo kwa Vijana na Wanawake (BBT Mitaji)

413. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Mfuko wa Dhamana wa Pembejeo za Kilimo (AGITF) itawezesha upatikanaji wa mikopo yenye riba nafuu ya Shilingi Bilioni 5 kwa vijana na wanawake. Vilevile, itaweka kiasi cha Dola za Marekani Milioni 35 kwenye Benki za biashara kwa ajili ya *guarantee scheme* zitakazowezesha vijana na wanawake kupata mikopo yenye riba nafuu mara mbili au zaidi ya fedha hizo.

5.2.4 Kuwezesha Vijana na Wanawake Kuongeza Thamani ya Mazao

414. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Bodi ya Mkonge itaendelea kutoa mafunzo ya kuongeza thamani ya zao la mkonge kwa vijana na wanawake 200 ili waweze kuzalisha bidhaa zitokanazo na zao hilo; na Bodi ya Korosho Tanzania

itanunua mashine 100 za kubangua korosho na kuwapatia vijana na wanawake ili kuongeza thamani ya zao la korosho.

5.2.5 Kuwezesha Vijana na Wanawake kutoa Huduma za Ugani (BBT Ugani)

415. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha utoaji wa huduma za ugani na kukuza ujuzi wa vijana wahitimu wa vyuo vya mafunzo ya kilimo kwa kutoa huduma za ugani kwa wakulima, Wizara kupitia Bodi za mazao kwa kushirikiana na Chuo Kikuu Cha Sokoine cha Kilimo na sekta binafsi itaendelea kutekeleza Mpango wa Ugani (BBT – Agricultural Extension Enterpreneurship Scheme) kuzalisha ajira kwa vijana na wanawake 1,700. Vilevile, kupitia Bodi za mazao, vijana na wanawake watahamasishwa kushiriki katika uzalishaji wa miche ya mazao mbalimbali kulingana na mahitaji.

5.3 Kuimarisha Usalama wa Chakula na Lishe

416. ***Mheshimiwa Spika,*** usalama wa chakula na lishe nchini ni nguzo muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu katika nyanja za uchumi, kijamii na kisiasa. Katika mwaka 2026/2027, Wizara itaendelea kuwekeza katika miundombinu ya uhifadhi wa chakula, kuiongezea NFRA uwezo wa kununua mazao pamoja na kuhamasisha matumizi ya mazao yaliyoongezewa virutubishi ili kukabiliana na matatizo ya lishe nchini.

5.3.1 Uwekezaji kwenye Miundombinu ya Uhifadhi ili Kufikia Uwezo wa Kuhifadhi tani 3,000,000 ifikapo Mwaka 2030

417. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha uwezo wa kuhifadhi, kupunguza upotevu wa mazao ya kilimo baada ya kuvuna na kuimarisha usalama wa chakula, Wizara kupitia NFRA itaendelea na ujenzi wa miundombinu ya uhifadhi yenye uwezo wa kuhifadhi tani 165,000 kupitia Mradi wa Kuongeza Uhifadhi wa Nafaka katika Kanda za Songea, Makambako, Dodoma, Shinyanga na Songwe. Vilevile, itaendelea na ujenzi wa miundombinu yenye uwezo wa kuhifadhi tani 85,000 na kuanza ujenzi wa miundombinu yenye uwezo wa kuhifadhi tani 65,000 katika Kanda za Arusha, Sumbawanga, Songea, Makambako, Songwe, Kipawa,

Shinyanga na Dodoma. Kukamilika kwa miradi hiyo kutaongeza uwezo wa hifadhi na kufanya Taifa kuwa kitovu cha chakula katika Bara la Afrika.

418. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itakarabati ghala 46 katika mikoa ya Shinyanga, Geita, Kigoma, Tabora, Rukwa, Katavi, Mwanza, Manyara na Songwe. Vilevile, itanunua vifaa kwa ajili ya ghala 79 katika mikoa ya Ruvuma, Iringa, Geita, Morogoro, Katavi, Rukwa, Songwe, Manyara, Tabora, Kigoma, Dodoma, Mtwara na Mwanza ili kuongeza uwezo wa hifadhi.

5.3.2 Kuiongezea NFRA Uwezo wa Kununua Mazao ya Wakulima ili Kuongeza Hifadhi

419. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuimarisha hifadhi ya mazao nchini kwa mwaka 2026/2027, Wizara kupitia NFRA, itaendelea kununua nafaka kutoka kwa wakulima kwa lengo la kuhakikisha usalama wa chakula na upatikanaji wa bei ya uhakika kwa wakulima inaendelea kuimarishwa.

5.3.3 Kuhamasisha Matumizi ya Mazao yaliyoongezewa Virutubishi (Biofortified) ili Kukabiliana na Matatizo ya Lishe Nchini

420. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027, Wizara itaendelea kutekeleza Mpango Kazi wa Lishe katika Kilimo (Nutrition Sensitive Agriculture Action Plan – NSAAP) ili kukabiliana na matatizo ya lishe yanayohusisha udumavu, ukondefu na upungufu wa wekundu wa damu. Vilevile, Wizara kupitia TARI itazalisha na kusambaza vipando vya viazi lishe 3,400,000 kwa lengo la kuhamasisha matumizi katika mikoa ya Mwanza, Geita, Tabora, Katavi, Kigoma, Shinyanga, Simiyu, Kagera na Mara.

421. ***Mheshimiwa Spika,*** TARI itatoa mafunzo kuhusu kanuni za kilimo bora kwa wakulima wawezeshaji 2,518 na wazalishaji wa mbegu za viazi lishe 100 katika Halmashauri za Bukombe, Geita, Misungwi, Misenyi na Bukoba. Pia, itaandaa fomula ya kutengeneza unga lishe wenye mchanganyiko wa ngano, mahindi ya provitamini A, maharage yenye madini ya chuma na *zinc*. Unga huo utasaidia kuimarisha lishe nchini.

422. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itatoa mafunzo kwa Maafisa Ugani 200 na wakulima viongozi 1,000 katika mikoa ya Njombe, Mbeya na Ruvuma kuhusu ukadiriaji wa mazao ya chakula yakiwemo nafaka, mikunde na mizizi kwa ajili ya hifadhi katika ngazi ya kaya. Vilevile, itatoa mafunzo kuhusu ujumuishaji na utekelezaji wa mipango ya lishe katika kilimo kwa Maafisa Ugani (250), Maafisa Lishe (12) na Maafisa Mipango (10) katika mikoa ya Lindi na Mtwara. Pia, itatoa mafunzo kuhusu kanuni za kilimo bora kwa wakulima wawezeshaji 2,518 na wazalishaji wa mbegu 100 katika Halmashauri za Bukombe, Geita, Misungwi, Misenyi na Bukoba.

5.4 Kuimarisha Upatikanaji wa Masoko, Mitaji na Uongezaji Thamani

423. ***Mheshimiwa Spika,*** dhamira ya Serikali si tu kuona wakulima wanazalisha mazao ya kutosha, bali ni kuhakikisha kuwa jasho lao linalindwa kupitia mifumo thabiti ya masoko na mitaji kwa kuimarisha mazingira wezeshi na kuweka mifumo itakayowezesha mauzo ya mazao ya kilimo kwa bei ya soko. Hivyo, Serikali ya Awamu ya Sita inajenga daraja kati ya wazalishaji na walaji ambalo litawezesha upatikanaji wa mitaji yenye riba nafuu hususan kwa wakulima wadogo.

424. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027, Wizara kwa kushirikiana na wadau itaendelea kuimarisha upatikanaji wa masoko, mitaji na uongezaji thamani kwa kutekeleza mikakati ifuatayo:-

5.4.1 Kujenga Miundombinu ya Masoko ya Mazao ya Kilimo

425. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha miundombinu ya masoko ya mazao ya kilimo, Wizara itakamilisha ujenzi wa masoko matano (5) ya kimkakati katika Halmashauri za Manispaa ya Kahama (Busoka), Ngara (Kabanga), Kyerwa (Nkwenda na Murongo) na Tarime (Sirari). Ujenzi wa masoko hayo utawezesha kuendeleza biashara ya mazao ya kilimo katika mipaka ya nchi za Uganda, Kenya, Rwanda na Burundi.

426. *Mheshimiwa Spika,* Wizara imepanga kujenga masoko matano (5) kwenye maeneo ya mipakani na maeneo ya kimkakati katika Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Kanda ya Ziwa na Kanda ya Mashariki ambayo ni malango muhimu ya biashara kati ya Tanzania na nchi za jirani ambapo shughuli nyingi za kiuchumi na kijamii zinafanyika.

427. *Mheshimiwa Spika,* Wizara itaendelea na ujenzi wa vituo vya masoko (market sheds) vya Endashangwet (Karatu), Kibakwe (Mpwapwa), Losirwa (Monduli), Ushirika (Nzega Mji), Mamsera (Rombo), Mula (Hai), Kigoma (Kibondo), Moshi (Himo), Halmashauri ya Wilaya ya Singida (Merya) na Manispaa ya Mpanda (Mpanda hoteli). Ujenzi wa vituo hivyo, utawezesha wakulima kukusanya na kuuza mazao sehemu rasmi zinazotambulika na mamlaka husika.

5.4.2 Kuongeza Mauzo ya Mazao ya Kilimo Ndani na Nje ya Nchi

428. *Mheshimiwa Spika,* katika kuongeza mauzo ya mazao ya kilimo ndani na nje ya nchi, Wizara katika mwaka 2026/2027, itaendelea kushirikiana na sekta binafsi kuimarisha biashara ya mazao ya kilimo kwa kusimamia mikakati ya uzalishaji na kuongeza mauzo ya mazao nje ya nchi kutoka Dola za Marekani Bilioni 3.54 mwaka 2023/2024 hadi takriban Dola za Marekani Bilioni 4 mwaka 2026/2027. Vilevile, Wizara itakamilisha taratibu za ufunguzi wa masoko mapya 15 katika nchi 14 kwa ajili ya mazao ya nafaka, bustani, mikunde na tumbaku.

429.*Mheshimiwa Spika,* Wizara itatoa elimu ya stakabadhi za shala na minada ya kidijiti kwa wakulima 3,200 ili kuimarisha biashara ya mazao ya kilimo. Vilevile, Wizara itaongeza mazao ya mahindi, njugumawe, kunde, pilipili manga, karafuu, iliki, vitunguu na mdalasini katika mifumo rasmi ya biashara kupitia Mfumo wa Stakabadhi ya Ghala, mfumo wa vituo rasmi vya mauzo na mfumo wa kilimo cha mkataba.

5.4.3 Kuimarisha Uongezaji Thamani kwa Kushirikisha Sekta Binafsi

430. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027, Wizara itaendelea na ujenzi wa vituo jumuishi viwili (2) katika mikoa ya Iringa (Mufindi) na Mbeya (Rungwe) ili kuwezesha kuchambua, kuhifadhi na kuchakata mazao ya bustani. Vilevile, itaendelea na ujenzi wa miundombinu ya kukaushia, kuchakata na kuhifadhi muhogo katika Halmashauri za Kakonko na Kibondo na tangawizi katika Halmashauri ya Buhigwe.

431. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea na ujenzi wa vituo 20 vya ukusanyaji wa parachichi na mazao mengine ya bustani pamoja na kuweka miundombinu stahiki ili kuimarisha shughuli za ukusanyaji, uhifadhi na upatikanaji wa masoko ya mazao hayo katika mikoa ya Mbeya, Njombe, Iringa, Rukwa, Ruvuma, Tanga, Kilimanjaro, Kagera, Kigoma na Songwe.

432. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TARI itatafiti teknolojia tatu (3) za usindikaji na uongezaji thamani wa zao la korosho, mahindi na ufuta na utengenezaji wa ethanoli. Vilevile, itaendelea na utafiti wa aina 13 za teknolojia za kuongeza thamani ya mazao ya nyanya, muhogo, mtama, choroko, ulezi, uwele, viazi lishe, soya, kunde, mbaazi, migomba, zabibu na matunda ya asili. Aidha, COPRA itanunua mashine 100 za kusafisha, kuchambua na kupanga madaraja ya mazao ya jamii ya mikunde na nafaka. Mashine hizo zitakabidhiwa kwa AMCOS kwa ruzuku katika mikoa ya Rukwa, Katavi na Songwe.

5.4.4 Kuimarisha Upatikanaji wa Mitaji

433. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2026/2027, itaendelea kushirikiana na taasisi za fedha katika kuimarisha utoaji wa mikopo yenye riba nafuu kwenye sekta ya kilimo. Vilevile, TADB itashirikiana na taasisi za fedha 22 zinazotumia mfuko wa dhamana wa TADB ili kurahisisha utoaji wa mikopo yenye riba nafuu katika shughuli za kilimo yenye thamani ya Shilingi Bilioni 330.

434. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia AGITF itatoa mikopo yenye thamani ya Shilingi 21,470,000,000 kupitia dhamana ya

mikopo, mkulima nafuu *loan*, mkulima *loan* na *wholesale lending*. Kadhalika, itaendelea na ujenzi wa ofisi ya AGITF Makao Makuu katika Mkoa wa Dodoma.

5.4.5 Kuziwezesha Maabara za Kilimo Kufikia Viwango vya Ubora Vinavyotakiwa Kimataifa

435. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TPHPA itaanza ujenzi wa maabara ya kisasa katika Mkoa wa Njombe kwa ajili ya kupima ubora wa mazao ili kusogeza huduma karibu na wadau wa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini na mikoa ya jirani. Vilevile, TOSCI itakamilisha ukarabati wa maabara ya Makao Makuu katika Mkoa wa Morogoro na maabara ya kupima ubora wa mbegu iliyopo katika Mkoa wa Arusha. Pia, itajenga na kukarabati vyumba vya ubaridi katika maabara ya mbegu iliyopo Mkoa wa Mbeya na Arusha.

436. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itakamilisha ujenzi na ununuzi wa vifaa vya maabara ya magonjwa ya mimea (Patholojia) katika kituo cha TARI Naliendele na maabara ya kuzalisha miche kwa njia ya chupa katika kituo cha TARI Maruku. Vilevile, Wizara itaimarisha maabara za kuzalisha miche kwa njia ya chupa kwa kununua vifaa vya maabara katika vituo vya TARI Tengeru, TARI Mikocheni na TARI Mlingano. Pia, itakamilisha upatikanaji wa ithibati ya maabara ya udongo katika kituo cha TARI Mlingano.

5.5 Kuimarisha Maendeleo ya Ushirika

437. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ya Awamu ya Sita inatambua kuwa nguvu ya wakulima ipo katika uzalishaji, usindikaji, mitaji na masoko kupitia AMCOS na SACCOS. Hivyo, kuimarisha maendeleo ya ushirika si bahati mbaya bali ni kipaumbele chetu cha msingi katika kuwawezesha wakulima kuwa na sauti moja yenye maamuzi sokoni.

438. ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na umuhimu huo katika mwaka 2026/2027, Wizara kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika itaimarisha ukaguzi na usimamizi wa uendeshaji wa vyama vya ushirika; itahamasisha ushirika kwenye sekta mbalimbali na

makundi maalum; na kuhamasisha vyama vya ushirika kujiendesha kibiashara. Ili kufikia malengo hayo, Wizara kupitia Tume itatekeleza yafuatayo:-

5.5.1 Kuimarisha Ukaguzi na Usimamizi wa Uendeshaji wa Vyama vya Ushirika

439. *Mheshimiwa Spika,* katika kuimarisha utendaji kazi wa vyama vya ushirika, Wizara kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) kwa mwaka 2026/2027, itafanya ukaguzi wa mara kwa mara katika vyama vya ushirika 6,545 na COASCO itafanya ukaguzi wa vitabu vya hesabu vya vyama vya ushirika 6,545 vilivyosajiliwa katika mfumo wa MUVU. Aidha, Tume itatoa mafunzo kuhusu usimamizi wa vyama vya ushirika kwa Maafisa Ushirika 80. Vilevile, Tume itawapatia vitendea kazi Maafisa Ushirika 60 ikiwemo Kompyuta (60) na Pikipiki (60) kwa ajili ya kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Kadhalika, Tume itatoa mafunzo kuhusu utunzaji wa kumbukumbu na uandaaji wa vitabu vya hesabu kwa vyama vya ushirika 6,545 kwa lengo la kuwawezesha kuzingatia Sheria na taratibu katika uendeshaji.

440. *Mheshimiwa Spika,* Tume itatathmini na kuvipanga vyama vya ushirika wa mazao 4,894 katika madaraja kulingana na umiliki wa mali za kudumu na utendaji ili kubaini aina ya usimamizi unaotakiwa katika chama husika. Vilevile, itaendesha kampeni ya **Linda Ushirika Chagua Uadilifu** kwa ajili ya kuelimisha wadau wakiwemo vyama vya ushirika, mahakama, polisi, TAKUKURU na wanasheria kuhusu ushirika, uadilifu na utatuzi wa migogoro.

5.5.2 Kuhamasisha Vyama vya Ushirika Kujiendesha Kibiashara na Kuviwezesha Kupata Mitaji

441. *Mheshimiwa Spika,* Tume kupitia *Ushirika Joint Enterprise (UJE)* kwa kushirikiana na Benki ya Ushirika Tanzania itaendelea kuhamasisha vyama vya ushirika kuendelea kununua hisa katika Benki ya Ushirika kutoka asilimia 45 hadi 51. Vilevile, itahamasisha vyama vikuu vya ushirika 25 kuwa mawakala wa Benki na kufungua matawi katika mikoa ya Kagera, Dar es Salaam, Mwanza, Mbeya, Katavi na Ruvuma.

442. *Mheshimiwa Spika,* ili kuongeza thamani ya zao la korosho Tume itaendelea kuratibu ujenzi wa kiwanda cha kubangua korosho chenye uwezo wa kubangua tani 3,500 kwa mwaka katika Wilaya ya Tandahimba ambacho kitajengwa na Chama Kikuu cha Tandahimba na Newala (TANECU). Vilevile, Tume itaendelea kuratibu ufufuaji wa kiwanda cha kuchakata pamba cha Magu kinachomilikiwa na Chama Kikuu cha Ushirika NYANZA.

443. *Mheshimiwa Spika,* Tume itaendelea kuratibu ujenzi wa kiwanda cha kukamua mafuta ya kula na kusimika mitambo ya kukamua mafuta kinachomilikiwa na Chama Kikuu cha Ushirika cha Kahama (KACU) ili kuongeza thamani na kukidhi mahitaji ya soko.

444. *Mheshimiwa Spika,* katika mwaka 2026/2027, Tume itaendelea kuratibu ukarabati na ufufuaji wa kiwanda cha kuchakata pamba kinachomilikiwa na Chama Kikuu cha Pamba Mara. Vilevile, itaratibu ukarabati wa kiwanda cha maziwa kinachomilikiwa na Chama cha Ushirika CHAWAKIM katika Mkoa wa Pwani. Pia, itaendelea kuratibu Chama Kikuu cha Tabora (WETCU) kujenga kiwanda cha kutengeneza nyuzi za kusukia tumbaku katika kongani ya viwanda vya pamba itakayojengwa katika Mkoa wa Simiyu.

445. *Mheshimiwa Spika,* Tume kwa kushirikiana na wadau itaendelea kuhamasisha vyama vya ushirika kuuza mazao kupitia mifumo rasmi na jumuishi ya biashara na masoko ya mazao. Lengo ni kuongeza ushindani, uwazi na mauzo ya mazao ndani na nje ya nchi.

5.5.3 Kuhamasisha Ushirika kwenye Sekta mbalimbali na Makundi Maalum

446. *Mheshimiwa Spika,* Tume itahamasisha uanzishaji wa vyama vya ushirika 26 vya vijana katika ngazi za mikoa ili kuwezesha kupata fursa mbalimbali za kiuchumi ikiwemo kupata mitaji ili viweze kujiendesha. Pia, itahamasisha vikundi 127 vya wafugaji na wavuvi ili kuanzisha ushirika wa wafugaji na wavuvi kwa ajili ya

kuwezesha udhibiti wa malisho na kuongeza masoko ya mazao ya mifugo na uvuvi.

447. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Tume itafanya uhamasishaji kwa wakulima wa mazao ya chikichi, viazi mviringo ngano na tufaha ili waweze kujiunga na ushirika. Aidha, Tume, itawezesha uchakataji wa zao la chikichi kwa kutoa mashine 18 za kuongeza thamani ya zao hilo kwenye vyama 18 vilivyoanzishwa.

448. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Tume itaratibu maandalizi ya Kongamano la Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo Barani Africa (SACCA CONGRESS) litakalofanyika Oktoba, 2026 kwa mara ya kwanza nchini Tanzania. Vilevile, Tume itahamasisha vyama vya ushirika kutumia Kampuni ya Bima ya Ushirika inayomilikiwa na wanaushirika. Lengo ni kutoa huduma za bima zitakazowakinga na vihatarishi vya aina mbalimbali ikiwemo kushuka kwa bei za mazao, majanga yanayotokana na mabadiliko ya tabia nchi na magonjwa ya mazao na binadamu. Pia, Tume itaendelea kuhamasisha uanzishwaji wa SACCOS kwenye AMCOS zinazosimamiwa na vyama vikuu ili kurahisisha upatikanaji wa mikopo kwa wanachama.

5.6 Kuimarisha Matumizi ya Mifumo ya TEHAMA katika Uendelezaji wa Sekta ya Kilimo

449. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027, Wizara itaendelea kuimarisha mifumo ya TEHAMA itakayowezesha wadau wa mnyororo wa kilimo kubadilishana taarifa zinazohusiana na kilimo. Hatua hii si tu itaongeza tija, bali italeta ufanisi na kuhakikisha wakulima wanapata huduma kwa wakati na kukuza uchumi. Ili kufanikisha azma hiyo, Wizara itatekeleza mikakati ifuatayo:-

5.6.1 Kuimarisha Mifumo ya Kidijiti itakayowezesha Upatikanaji wa Taarifa Sahihi kwa Wakati

450. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027, Wizara itaendelea na ujenzi wa moduli ya taarifa za kilimo za kijiografia zitakazopatikana kwa kutumia ramani kwa lengo la kuwezesha

upatikanaji wa taarifa kwa wakati. Vilevile, itaendeleza mawasiliano na kubadilishana taarifa za wadau wa mnyororo wa thamani wa takwimu za kilimo za kidijiti (*Agriculture data exchange and digitalization in value chain*).

451. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TPHPA itaendelea kufuatilia mazao (*crop traceability system*) yanayosafirishwa nje ya nchi ili kulinda soko la mazao ya kilimo. Vilevile, Wizara kupitia COPRA itasajili ghala 10,000 za kuhifadhia nafaka na mazao mchanganyiko na kufanya ufuatiliaji wa mazao (stock monitoring) katika mikoa ya Ruvuma, Mbeya, Katavi, Rukwa, Morogoro na Songwe. Aidha, Wizara itaendelea kutumia mifumo ya kidijiti kutoa huduma za ugani kwa wakulima ili kupanua wigo wa utoaji wa huduma hizo. Pia, Wizara itaendelea kuboresha huduma za ugani kwa kutumia teknolojia ya akili unde ambayo itasaidia kuboresha mawasiliano kati ya wakulima, wadau wa kilimo na Wizara.

5.6.2 Kuwekeza kwenye Matumizi ya Mifumo ya Kidijiti katika Sekta ya Kilimo

452. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TPHPA, itaendelea kujenga moduli ya afya ya mimea kwa ajili ya kukusanya na kutunza taarifa, kutoa vibali vya uingizaji na usafirishaji wa mazao na mimea nje ya nchi na vibali vya matumizi ya viuatilifu vya mimea na mazao. Vilevile, Wizara itaendelea kuboresha moduli ya mnyororo wa thamani wa mbegu kwa ajili ya upatikanaji wa taarifa zikiwemo za uchakataji, ukusanyaji, utunzaji na usambazaji wa mbegu bora.

453. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea na taratibu za kuanzisha kituo cha teknolojia za kilimo cha TEHAMA (AgriTech Hub) kilichopo katika Mkoa wa Dodoma (Mtanana) ili kusaidia wakulima ikiwemo vijana kujifunza na kufanya ubunifu wa kutumia teknolojia za kidijiti. Pia, Wizara kupitia AGITF itaboresha mfumo wa kieletroniki kwa ajili ya usimamizi wa mikopo ili kuongeza wigo wa upatikanaji wa mikopo.

454. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha na kurahisisha huduma kwa wananchi kupitia Mifumo ya Kidijiti, Wizara kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika, imepanga kusimamia matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika vyama vya ushirika 290. Aidha, imepanga kujenga Mfumo wa Akili Unde (AI) na Taarifa ya Huduma ya Ziada Isiyoundwa - *Unstructured Supplementary Service Data* (USSD) kwa ajili ya kurahisisha matumizi ya Mifumo na kupata taarifa katika sekta ya ushirika. Vilevile, itajenga mfumo wa kurahisisha taratibu za ajira na kutoa taarifa za ajira katika vyama vya ushirika sambamba na kuunganisha mifumo 12 ya vyama vya ushirika na Taasisi za Serikali.

MAENEO MENGINE MUHIMU YATAKAYOTEKELEZWA NA WIZARA
Kuimarisha Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira, pamoja na Matumizi ya Mbinu na Teknolojia za Kilimo Himilivu

455. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi, hususan kwa wakulima wa Nyanda Kame, Wizara itaendelea kukijengea uwezo kituo cha TARI - Hombolo kuwa kituo mahiri cha Utafiti wa Mazao ya Ukame na Teknolojia za Uhimilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi (Centre for Dryland Crops and Climate Change Research) katika maeneo ya: agronomia, uboreshaji wa mbegu, ulinzi wa mazao, usimamizi wa baada ya mavuno (uchakataji, ongezeko la thamani na matumizi), rasilimali asilia, matumizi ya miumbombinu ya kisasa (automated screenhouse and irrigation) na masuala ya kijamii na kiuchumi.

456. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea kuratibu maandalizi na utekelezaji wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii (TAM) kwa miradi na mashamba makubwa ya pamoja 20 kwa mujibu wa matakwa ya sheria, kanuni na miongozo ya usimamizi wa mazingira.

457. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imepanga kuendelea kutoa mafunzo kwa wadau 40,000 wa sekta ya kilimo kuhusu mbinu bora za usimamizi wa taka zitokanazo na shughuli za kilimo ikiwa ni njia rafiki ya utunzaji wa mazingira. Vilevile, itatoa mafunzo ya

matumizi ya maji kwa ufanisi katika kilimo cha umwagiliaji na matumizi ya nishati mbadala katika shughuli za kilimo.

Masuala ya Jinsia

458. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuendelea kuhakikisha masuala ya kijinsia yanazingatiwa katika kilimo, Wizara itakamilisha mwongozo wa ujumuishaji wa masuala ya jinsia katika mnyororo wa thamani wa kilimo na kusambaza kwa wadau mbalimbali kwenye mnyororo wa thamani. Vilevile, Wizara itahakikisha kuwa masuala ya kijinsia yanazingatiwa katika utoaji wa pembejeo za kilimo ikiwemo utoaji wa ruzuku ya mbegu na mbolea pamoja na utoaji wa mafunzo kupitia vikundi vya wakulima katika mashamba darasa ya miradi mbalimbali ya Wizara.

459. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea kutoa mafunzo jumuishi ya masuala ya jinsia kwa Maafisa Ugani, Maendeleo ya Jamii, Mazingira na Mipango kutoka katika Halmashauri 26. Pia, Wizara itaendelea kuanzisha madawati ya Jinsia katika taasisi na bodi za mazao zilizopo chini ya Wizara.

Afya na Ustawi wa Watumishi

460. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027, Wizara itaendelea kutoa huduma ya lishe kwa watumishi wanaoishi na VVU watakaojitokeza. Vilevile, Wizara itaendelea kuhamamisha watumishi kushiriki michezo mbalimbali ili kuimarisha afya na kupunguza athari za Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza kwa ajili ya kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

461. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaratibu vikao vinne (4) vya waelimisha rika kwa lengo la kubadilishana taarifa na kutathmini hali ya utekelezaji wa afua za VVU, UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza mahala pa kazi katika Utumishi wa Umma. Vilevile, Wizara itaendelea kutoa elimu ya VVU, UKIMWI, Afya ya Akili na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza.

462. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027, Wizara itaendelea kutoa elimu ya mapambano dhidi ya rushwa mahali

pa kazi na kuratibu vikao vinne (4) vya masuala ya rushwa na uzingatiaji wa maadili. Vilevile, Wizara itaendelea kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa watumishi kwa kuwapatia vitendea kazi, kununua mabasi mawili (2) ya watumishi pamoja na kutoa motisha na stahiki zao kwa mujibu wa Sheria, Kanuni, Miongozo na Taratibu za utumishi wa umma. Pia, Wizara itahakikisha watumishi wote wenye sifa wanapatiwa nafasi za kujiendeleza kitaaluma kwa kadri ya mahitaji ya Wizara kwenye maeneo mahsusi.

Kuwekeza kwenye Ujuzi kwa Wataalam wa Ndani

463. *Mheshimiwa Spika,* katika mwaka 2026/2027, Wizara kupitia mpango wake wa kuendeleza mafunzo itawawezesha watumishi 1,059 kupata mafunzo ya muda mrefu na mfupi katika vyuo vya ndani na nje ya nchi ili kuendana na mahitaji ya taaluma. Kati ya hao, Shahada ya uzamivu (41), Shahada ya uzamili (188), Shahada (40) na Stashahada (3) na mafunzo ya ujuzi maalum (797).

Wajibu kwa Jamii (Corporate Social Responsibility – CSR)

464. *Mheshimiwa Spika,* katika kuimarisha mahusiano na jamii (Corporate Social Responsibility – CSR), Wizara kupitia taasisi zake itatekeleza miradi itakayolenga kuimarisha uzalishaji wa mazao kwenye maeneo mbalimbali nchini kwa lengo la kuhamasisha na kutoa motisha kwa jamii husika kushiriki katika shughuli za kilimo hususan vijana na wanawake.

Hitimisho na Shukrani

465. *Mheshimiwa Spika,* katika kuhitimisha hotuba yangu mbele ya Bunge lako Tukufu, ninapenda kuwakumbusha Watanzania wote kuwa kilimo ni biashara na mkulima ni mwekezaji. Serikali ya Awamu ya Sita kupitia uongozi mahiri wa Dkt. Samia Suluhu Hassan, umetafsiri dhana hiyo kwa vitendo kwa kuendesha **Kampeni ya Mali Shambani** yenye lengo la kuhakikisha kuwa mkulima wa kitanzania anahama kutoka kilimo cha mazoea na

cha kujikimu na kuingia katika kilimo biashara chenye tija, endelevu, uhakika wa soko na manufaa kwa mkulima.

466. ***Mheshimiwa Spika,*** lengo si tu kujitosheleza kwa chakula kwa asilimia 100 bali tunalenga kuwa ghala la chakula kwa ukanda wa EAC, SADC na Afrika kwa ujumla, jambo litakaloongeza fedha za kigeni na kuimarisha thamani ya Shilingi yetu.

467. ***Mheshimiwa Spika,*** malengo hayo hayawezi kufikiwa bila ushirikiano wa karibu na sekta binafsi, hivyo, Wizara inaendelea kuwakaribisha wawekezaji wa ndani na nje kwenye mnyororo wa kilimo ili kuzalisha ajira na kuwa na bidhaa zenye chapa ya *Made in Tanzania*.

468. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa unyenyekevu mkubwa nitumie nafasi hii ya kipekee kumshukuru tena Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, ambaye ameendelea kuweka nguvu kubwa katika kusaidia sekta ya kilimo na wakulima nchini. Aidha, nitumie nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuwa pamoja na wakulima na kuendelea kuhamasisha shughuli za kilimo katika majimbo yao.

469. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba nitumie fursa hii kuzishukuru nchi ambazo zimeendelea kuunga mkono juhudi za Serikali katika kutekeleza shughuli za kilimo nchini. Nchi hizo ni pamoja na:- Serikali za Japan, Marekani, Uingereza, China, Urusi, Indonesia, Korea Kusini, India, Italia, Misri, Kuwait, Israel, Saudi Arabia, Thailand, Iran, Ukraine, Ubelgiji, Ujerumani, Ufini, Norway, Brazil, Uholanzi, Ireland, Malaysia, Denmark, Austria, Ufaransa, Romania, Belarus, Vietnam, Sweden, Canada, Poland, Qatar, Oman, Uturuki pamoja na Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika, Umoja wa nchi za Afrika, Umoja wa Ulaya, Jumuiya ya Madola na Umoja wa Falme za Kiarabu.

470. ***Mheshimiwa Spika,*** ninayashukuru mashirika mbalimbali ya kitaifa na kimataifa ikiwemo Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, JICA, IMF, IFAD, FAO, WFP, AGRA, KOICA, Care International, World Vision, UNIDO, UNDP, TAHA, World Vegetable Centre, SAT, SUGECO, AGCOT, Aspires Tanzania, CIAT, RIKOLTO,

HELVATAS, ENABEL, CAMFED, BIVAC, IRRI, Agriedo, Mazao Hub, Global Community, TASTA, GAIN, NORAD, IITA, AATI, AMDT, SNV, FSDT, ANSAF, MVIWATA, SWISS AID, TOAM, GIZ, UN Women, ESAFF, IFC, ESRF, PASS Trust, Action Aid Tanzania, EAGC, Global Crop Diversity Trust na EFTA.

471. *Mheshimiwa Spika,* ninapenda kuzishukuru taasisi za fedha ikiwemo CRDB, NMB, Benki ya Ushirika Tanzania, TADB, TIB, TCB, Azania Bank, Akiba Commercial Bank, Stanbic, NBC, PBZ, Equity Bank na Mwanga Hakika kwa kuendelea kuwezesha upatikanaji wa mitaji katika shughuli za kilimo.

472. *Mheshimiwa Spika,* ninapenda kuzishukuru taasisi zote za elimu ya juu na taasisi za utafiti. Vilevile, ninapenda kushukuru kampuni na wafanyabiashara wote wa mazao ya kilimo ambao tumekuwa tukishirikiana nao katika kutoa soko la uhakika kwa wakulima. Ninawashukuru pia wafanyabiashara na wasambazaji wa pembejeo za kilimo kwa kuhakikisha pembejeo zinawafikia wakulima kwa wakati.

473. *Mheshimiwa Spika,* ninapenda pia kuzishukuru kampuni za mawasiliano nchini ikiwemo TTCL, Airtel, Vodacom, Yas na Halotel. Ninawashukuru pia kwa umuhimu wa kipekee wamiliki na wahariri wa vyombo vya habari vyote nchini pamoja na wanahabari wote wa vyombo vyote ikiwemo mitandao ya kijamii kwa kushirikiana nasi katika kuhabarisha umma na kutoa elimu kwa wakulima. Pia, ninawashukuru wasanii wote nchini kwa kuendelea kushirikiana nasi katika kutoa elimu kwa wakulima.

474. *Mheshimiwa Spika,* ninawashukuru sana viongozi wa dini kwa kuendelea kutuombea na kutushauri katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

6 MAOMBI YA FEDHA MWAKA 2026/2027

FUNGU 43, 24 na 05

6.1 Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli

475. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2026/2027, inatarajia kukusanya Shilingi **28,600,000,000.00** kupitia Fungu 43, Fungu 24 na Fungu 05. Kati ya fedha hizo, Shilingi **25,000,000,000.00** zitakusanywa kutokana na ukaguzi wa mazao, kodi za majengo na uuzaji wa nyaraka za zabuni kupitia Fungu 43 na Shilingi **3,600,000,000.00** zitakusanywa kutokana na ada za huduma ya umwagiliaji na ukodishaji wa mitambo kupitia Fungu 05.

6.2 Fedha za Matumizi kwa Mafungu yote

476. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027, Wizara ya Kilimo inaliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi **1,105,950,115,000.00** kupitia Fungu 43, Fungu 24 na Fungu 05.

6.2.1 Fedha kwa Fungu 43

477. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027, Shilingi **698,985,584,000.00** kinaombwa. Kati ya fedha hizo, Shilingi **567,345,730,000.00** ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ambapo Shilingi **360,678,811,000.00** ni fedha za ndani na kiasi cha Shilingi **206,666,919,000.00** ni fedha za nje. Aidha, Shilingi **131,639,854,000.00** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambapo Shilingi **84,956,697,000.00** ni mishahara na Shilingi **46,683,157,000.00** ni matumizi mengineyo ya Wizara, Bodi na Taasisi.

6.2.2 Fedha kwa Fungu 05

478. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inaomba kuidhinishiwa jumla ya Shilingi **384,290,761,000.00**. Kati ya fedha hizo, Shilingi **308,721,961,000.00** ni fedha za maendeleo na Shilingi **75,568,800,000.00** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha za maendeleo zinazoombwa, Shilingi **259,617,801,000.00** ni fedha za ndani na Shilingi

49,104,160,000.00 ni fedha za nje. Aidha, kati ya Shilingi **75,568,800,000.00** ya fedha za matumizi ya kawaida zinazoombwa, Shilingi **65,148,830,000.00** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na Shilingi **10,419,970,000.00** ni kwa ajili ya mishahara.

6.2.3 Fedha kwa Fungu 24

479. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/2027, Tume ya Maendeleo ya Ushirika inaomba kuidhinishiwa jumla ya Shilingi **22,673,770,000.00.** Kati ya fedha hizo, Shilingi **21,976,594,000.00** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Shilingi **697,176,000.00** ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya Fedha za matumizi ya kawaida zinazoombwa, Shilingi **8,130,236,000.00** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na Shilingi **13,846,358,000.00** ni kwa ajili ya mishahara.

480. ***Mheshimiwa Spika,*** NINAOMBA KUTOA HOJA**.**

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Waziri, hoja imeungwa mkono. Tunakushukuru Mheshimiwa.

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea tunao wageni waliokaa Jukwaa la Spika ambao ni wageni wa Mheshimiwa Dkt. Daniel Godfrey Chongolo, Waziri wa Kilimo ambao ni Mheshimiwa Albert Chalamila, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam; Mheshimiwa Rosemary Senyamule, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma; Mheshimiwa Jabir Makame, Mkuu wa Mkoa wa Songwe; Prof. Sifuni Mchome, Mwenyekiti wa Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko; Dkt. Abdulmajid Nsekela, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya *CRDB* na Mwenyekiti wa Tume ya Ushirika Nchini, na Mwenyekiti wa Bodi ya Chai. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni wengine wa Mheshimiwa Dkt. Godfrey Chongolo, Waziri wa Kilimo, ambao ni Wakurugenzi na Wakuu wa

Vitengo kutoka Wizarani na taasisi zake; wapo pia wataalamu wa kilimo wa Wizara na taasisi zake; wapo wadau wa maendeleo wa ndani kutoka taasisi mbalimbali; zipo pia taasisi za kifedha; pamoja na Waheshimiwa Madiwani kutoka Makambako Mkoani Njombe. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo pia wageni wa Waheshimiwa Wabunge ambao ni wageni 56 wa Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, ni Wanakwaya kutoka Kanisa la Moravian la Jijini Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaendelea. Ninaomba nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo, na Mifugo, Mheshimiwa Deodatus Mwanyika. *(Makofi)*

MHE. DEODATUS P. MWANYIKA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO, NA MIFUGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninamshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu ili niwasilishe Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo, na Mifugo kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Kilimo ya mwaka wa fedha 2025/2026, pamoja na Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara Hiyo kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaomba taarifa yote ya Kamati iwekwe kwenye kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)* kama ilivyowasilishwa Mezani kwako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukidhi matakwa ya Kanuni ya 121(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, taarifa hii imegawanyika katika sehemu zifuatazo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya kwanza inatoa maelezo ya jumla kuonesha msingi na Muundo wa Taarifa pamoja na namna Kamati ilivyofanya kazi; Sehemu ya Pili ni uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti wa ofisi hii kwa mwaka wa fedha 2025/2026;

Sehemu ya Tatu ni uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027; Sehemu ya nne inahusu maoni na ushauri wa Kamati; na Sehemu ya Tano ni hitimisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mawanda ya uchambuzi; Taarifa ya utekelezaji wa bajeti na makadirio ya mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo inagusa mafungu matatu. Fungu 43 ambalo ni Wizara ya Kilimo, Fungu 24 – Tume ya Maendeleo ya Ushirika, na Fungu 05 – Tume ya Taifa ya Umwagiliaji. Ninaomba kutoa taarifa mbele ya Bunge lako Tukufu kuwa, Kamati ilichambua taarifa ya utekelezaji wa bajeti na makadirio ya mapato na matumizi kwa mafungu yote matatu tarehe 19 hadi 23 Machi, 2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu matokeo ya uchambuzi na tathmini ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026. Katika vikao vya Kamati vilivyoketi tarehe 19 na 23 ya mwezi Machi, 2026, Kamati ilipokea, kujadili, na kuchambua taarifa ya Wizara ya Kilimo zilizohusu, pamoja na mambo mengine, utekelezaji wa bajeti ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Taarifa hiyo iliwasilishwa na Mheshimiwa Dkt. Daniel Godfrey Chongolo, Waziri wa Kilimo. Uchambuzi wa Kamati kuhusu taarifa hizo umeangazia maeneo makuu manne yafuatayo:-

(a) Makusanyo ya maduhuli kuanzia Julai, 2025 – Februari, 2026;

(b) Mwenendo wa upatikanaji wa fedha za bajeti za matumizi ya kawaida na mendeleo kwa kipindi cha Julai, 2025 – Februari, 2026;

(c) Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026; na

(d) Uzingatiaji wa ushauri wa Kamati Bungeni uliotolewa na Bunge wakati wa kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo hayo yanatoa taswira muhimu kwa Bunge kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025; taarifa ya utekelezaji wa bajeti na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Kilimo inajumuisha mafungu matatu, Wizara ya Kilimo – Fungu 43, Tume ya Maendeleo ya Ushirika – Fungu 24, na Tume ya Taifa ya Umwagiliaji – Fungu 05.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa taarifa ya fedha zilizovuka mwaka 2024/2025. Katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wizara ya Kilimo (Fungu 43) iliomba kibali cha kuvuka na jumla ya shilingi bilioni 48.79 ili kutekeleza kazi mbalimbali za maendeleo zikiwemo kugharamia ununuzi wa mbolea, ruzuku za mbolea, ununuzi wa nafaka na kugharamia madeni yalitotokana na biashara ya pamba msimu wa kilimo 2019/2020. Aidha, kwa upande wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji – Fungu 05 fedha zilizovuka mwaka 2024/2025 ni shilingi bilioni 23.03 ambapo fedha hizo zilitumika kulipa madai ya wakandarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu makusanyo ya maduhuli kwa Wizara ya Kilimo – Fungu 43; katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 Wizara ya Kilimo (Fungu 43) ililenga kukusanya maduhuli ya jumla ya shilingi bilioni 8.66 kutoka mapato ya Mfuko Mkuu wa Serikali na shilingi bilioni 24.21 kutoka katika Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi Februari, 2026, Wizara ya Kilimo ilikuwa imekusanya shilingi bilioni 42.25 sawa na 128.48%. Ukusanyaji huo wa mapato unaonyesha kuwa umevuka malengo ambayo Wizara ilijiwekea. Mchanganuo wa makusanyo hayo unaonekana katika jedwali namba moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwenendo huu ni wazi kuwa Wizara inaweza kufanya tathmini na kuongeza lengo la makusanyo kwa mwaka wa fedha 2026/2027 kwa kuimarisha

matumizi ya Mfumo wa *e-Kilimo* katika ukusanyaji wa mapato na kudhibiti utoroshaji wa mazao mipakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika makusanyo ya maduhuli kwa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji – Fungu 5; kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ilijiwekea lengo la kukusanya jumla ya shilingi shilingi 3.6. Hadi kufikia mwezi Februari, 2026 Tume ya Umwagiliaji ilikuwa imekusanya shilingi bilioni 1.9 sawa na 53.02% ya lengo lililokusudiwa. Mchanganuo wa makusanyo hayo unaonekana katika jedwali namba mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makusanyo ya maduhuli kwa Fungu 5 yamefikia asilimia 53.2% ya lengo kwa mwaka. Kwa kiwango hicho cha makusanyo siyo cha kuridhisha, kwani hadi Februari, 2026 kiwango cha makusanyo kilipaswa kufikia 75%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kushindwa kukusanya maduhuli kwa kiwango kinachotosheleza kunapunguza uwezo wa Tume kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Ili kuondokana na athari hizo, ni rai ya Kamati kuwa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji iongeze kasi ya kubuni mikakati itakayowezesha ukusanyaji wa maduhuli kupitia mifumo madhubuti ili kufikia lengo lililokusudiwa katika mwaka wa fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida; katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara ya Kilimo imeidhinishiwa jumla ya shilingi trilioni 1.19 kupitia Fungu 43, Fungu 05, na Fungu 24.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Wizara ya Kilimo – Fungu Na. 43; katika mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara ya Kilimo, iliidhinishiwa na Bunge bajeti ya shilingi bilioni 135.98 kwa ajili ya matumizi ya kawaida, na fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo ilikuwa shilingi bilioni 652.27. Hadi kufikia Februari, 2026 Wizara ilipokea jumla ya shilingi bilioni 65.18 kwa ajili ya matumizi ya kawaida, sawa na 47.93% ya bajeti iliyotengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa fedha za maendeleo, Wizara ilipokea jumla ya shilingi bilioni 361.29 sawa na 55.39%. Mchanganuo unaonekana katika jedwali namba mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini ya mapokezi ya fedha za matumizi ya kawaida siyo ya kuridhisha, kwani ni 47.93% ya fedha iliyotengwa imepokelewa. Endapo hali hiyo itaendelea hadi itakapofika mwezi Juni, 2026 wakati wa kuhitimisha mwaka huu wa fedha, ni dhahiri kuwa Wizara itashindwa kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi uliofanywa na Kamati umebaini mambo mbalimbali kuhusu utekelezaji wa bajeti ya miradi ya maendeleo kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiasi cha fedha kilichopokelewa kwa miradi ya maendeleo ni 55.39% ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Jenga Kesho iliyo Bora *(BBT)* uliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 16, fedha za ndani. Hadi kufikia Februari, 2026, fedha zilizopokelewa ni shilingi bilioni sita tu, sawa na 37.50% ya Bajeti. Utolewaji huu wa fedha umeathiri utekelezaji wa miradi ya *BBT* na hivyo kupelekea kushindwa kufikia malengo ya kuongeza ajira zenye staha na ushiriki wa vijana na wanawake kwenye kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi mingine ya maendeleo iliyoathirika kutokana na mtiririko huu wa fedha ni Mradi wa Upatikanaji wa Pembejeo za Kilimo Nchini, Programu ya Maendeleo ya Kilimo ambayo tayari ipo kwenye hatua mbalimbali za utekelezaji wake, jambo linaloathiri utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi kilichoahidi kuendelea kusimamia mapinduzi ya kilimo ili kuhakikisha kinaendelea kuwa chenye tija na kinachotumia teknolojia ya kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Tume ya Taifa ya

Umwagiliaji – Fungu 5 iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 73.41 kwa ajili ya matumizi ya kawaida, na fedha za maendeleo ni shilingi 308.72. Hadi kufikia mwezi Februari, 2026, fedha za matumizi ya kawaida ziliyopokelewa ni shilingi bilioni 9.41 sawa na 14% ya fedha iliyoidhinishwa; na fedha ya maendeleo kiasi cha shilingi bilioni 141.25 sawa na 45.7%. Mchanganuo wa upokeaji wa fedha unaonekana katika jedwali namba tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini inaonesha kuwa, hadi Februari, 2026, upatikanaji wa fedha za bajeti katika Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo hauridhishi. Aidha, kutolewa kwa fedha za matumizi ya kawaida kwa 14.45% tu kwa kiasi kikubwa kunakwamisha uendeshaji wa majukumu ya Tume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokupokelewa kikamilifu kwa fedha za miradi iliyotengwa kuna athari kwa Tume ya kushindwa kutekeleza azma yake ya kuongeza uzalishaji wa chakula na usimamizi wa mipango iliyokusudiwa kutekelezwa. Ni maoni ya Kamati kuwa, fedha za maendeleo, hususan fedha zilizotengwa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya sekta ya umwagilaji zitolewe ili kukamilisha miradi iliyokusudiwa kutekelezwa na kupunguza malimbikizo ya madeni ya wakandarasi na wazabuni, jambo linalopelekea kuongezeka kwa madeni kutokana na riba na hivyo kupelekea hasara kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika, kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Tume ya Taifa ya Maendeleo ya Ushirika – Fungu 24 iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 21.87 kwa ajili ya matumizi ya kawaida, na fedha za maendeleo shilingi 697. Hadi kufikia Februari, 2026, fedha za matumizi ya kawaida ziliyopokelewa ni shilingi bilioni 9.4 sawa na 58.30% ya fedha iliyoidhinishwa, na fedha ya maendeleo kiasi cha shilingi milioni 278 sawa na 40%. Mchanganuo wa upokeaji wa fedha unaonekana katika jedwali namba sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini ya mapokezi ya fedha kwa Fungu 24 – Tume ya Maendeleo ya Ushirika inaonekana kuwa siyo ya kuridhisha kwa upande wa fedha za maendeleo. Endapo

hali hiyo itaendelea hadi itakapofika mwezi Juni, 2026 wakati wa kuhitimisha mwaka wa fedha wa 2025/2026, ni dhahiri kuwa miradi iliyotengewa fedha katika mwaka huu haitatekelezwa; kama vile mradi wa kuimarisha ushirika wa bustani za mazao ya mbogamboga ambao ulitengenewa shilingi milioni 418 na hakuna fedha iliyopokelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri kuwa, fedha zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo zitolewe ipasavyo ili wananchi waweze kunufaika na miradi iliyopangwa kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo, katika Wizara ya Kilimo na Mafungu yake matatu, Kamati ilitembelea na kukagua miradi miwili iliyopo Morogoro na Dodoma kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 120 (1) ya Kanuni za Bunge. Kamati ilitembelea na kukagua miradi ifuatayo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, Mradi wa Ukarabati wa Maabara ya Taifa ya Mbegu *TOSCI* – Morogoro; Kamati ilitembelea na kukagua Mradi wa Ukarabati wa Maabara ya *TOSCI* – Morogoro. Ukarabati huo ulilenga kuongeza ukubwa wa maabara kutoka meta za mraba 825 na kufikia meta za mraba 1,715. Mradi huu ulianza tarehe 19 Septemba, 2024 na ulitarajiwa kukamilika tarehe 17 Machi, 2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilielezwa kuwa, mradi huu hadi kukamilika kwake unatarajiwa kugharimu jumla ya shilingi bilioni 1.98, ikiwa ni fedha za ufadhili kutoka Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo. Hadi kufikia tarehe 2 Machi, 2026, jumla ya shilingi bilioni 1.2 na utekelezaji wa mradi umefikia 86%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati iliridhishwa na hatua ya utekelezaji wa mradi huu na inaona kuwa kukamilika kwa mradi huu utaongeza uwezo wa kudhibiti ubora wa mbegu kwa kutumia teknolojia za kisasa na kuendelea kulinda taswira ya Tanzania katika viwango vya ubora wa mbegu kimataifa na kufunga fursa mpya kwa uwekezaji katika uzalishaji na biashara ya mbegu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mradi wa Ujenzi wa Miundombinu ya Umwagilijaji katika Kituo cha *TARI* – Hombolo Dodoma; Kamati ilielezwa kuwa *TARI* kupitia kituo cha *TARI* Hombolo ilitekeleza Mradi wa Ujenzi wa Miundombinu ya Umwagiliaji wenye ukubwa wa hekta 70. Mradi huu ni sehemu ya mradi wa umwagiliaji wa vituo 11 vya *TARI* na unatarajia kugharimu shilingi bilioni 17.81. Mradi huu ulianza kutekelezwa mwezi Mei, 2024 na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2026. Utekelezaji wa mradi umefikia 90%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu utatekelezwa kwa ujenzi wa miundombinu ya kutoa maji katika Bwawa la Hombolo na kusafirisha mpaka mashamba ambako kunajengwa na kusimikwa miundombinu ya umwagiliaji aina ya *Centre Pivot* na *Gun Sprinkler System*. Kukamilika kwa mradi huu kutaimarisha kazi za utafiti wa kilimo kwa kuwezesha majaribio kufanyika kwa mwaka mzima, kuongeza eneo la uzalishaji mbegu kutoka hekta 3.6 hadi 73.6, kuongeza mapato ya ndani yanayotokana na mauzo ya mbegu kutokana na ongezeko la uzalishaji wa mbegu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inampongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jitihada zake za kuwekeza kwenye miundombinu ya umwagiliaji na utafiti itakayosaidia Wizara kupitia taasisi zake kugundua, kubuni, na kuongeza upatikanaji wa teknolojia zinazojibu changamoto za kilimo nchini. Teknologia hizi zitawafanya wakulima kuongeza tija katika uzalishaji na hivyo kuchangia kuondoa umaskini na kukuza uchumi wa mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uzingatiaji wa ushauri wa Kamati, wakati wa uchambuzi wa bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Kamati ilitoa maoni, ushauri na mapendekezo mbalimbali ili kuboresha utekelezaji wa bajeti ya hiyo. Ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, kwa sehemu kubwa Serikali imezingatia maoni na ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya utekelezaji huo mzuri, upatikanaji wa fedha usioridhisha umeendelea kuwa kikwazo kwa

Wizara, na hivyo kushindwa kuzingatia ipasavyo baadhi ya ushauri wa Kamati. Kamati inaendelea kusisitiza kuwa, maagizo yenye mwendelezo wa utekelezaji yaendelee kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 120 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge 2025, mnamo tarehe 23 Machi Kamati ilipokea, kuchambua, na kujadili Taarifa ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. Uchambuzi wa Kamati ulijikita katika maeneo makuu mawili ambayo ni makadirio ya makusanyo ya maduhuli na makadirio ya matumizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini ya uchambuzi kuhusu maeneo hayo ni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara ya Kilimo – Fungu 43 inaomba kuidhinishiwa kukusanya mapato jumla ya shilingi bilioni 61 ikiwa ni ongezeko la 85% ikilinganishwa na makadirio ya makusanyo kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Mchanganuo wa makusanyo ya fungu unaonekana katika jedwali namba saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini inaonyesha kuwa, makadirio ya maduhuli kwa mwaka wa fedha 2026/2027 yameongezeka kwa 85% ikilinganishwa na lengo la makusanyo kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Hata hivyo, uzoefu wa ukusanyaji wa mwaka wa fedha unaoishia, ilionesha kumudu kukusanya 128.48% hadi kipindi cha robo ya tatu ya kipindi cha utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kufikia 85% Kamati inaamini kuwa upo uwezekano wa kufikia na kuvuka lengo la makusanyo lililowekwa kwa mwaka wa fedha 2026/2027 endapo Wizara itaimarisha ukusanyaji wa tozo za mazao na kudhibiti utoroshaji wa mazao sehemu za mipaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Fungu 05, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inakadiriwa kukusanya jumla ya shilingi bilioni

3.6 ambayo ni sawa na lengo la maduhuli kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Jedwali namba nane linaonesha mchanganuo huo wa makadirio hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi unaonesha kwamba kwa ujumla makadirio ya maduhuli kwa mwaka 2026/2027 ni sawa na lengo la maduhuli ya mwaka wa fedha 2025/2026. Kamati inashauri, Tume kuweka mikakati thabiti itakayowezesha kuongeza makusanyo ya mapato, ikiwa ni pamoja na kutumia mifumo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa matumizi ya kawaida. Katika mwaka wa fedha 2026/2027 Wizara ya Kilimo inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi trilioni 1.1 kupitia Fungu 43, Fungu 05 na Fungu 24, ikiwa ni punguzo la asilimia saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2026/2027 Fungu 43, Wizara ya Kilimo inaomba kuidhinishiwa bajeti ya shilingi bilioni 131.63 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kiasi hicho ni punguzo la 3.19% ikilinganishwa na bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026. Aidha, fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni shilingi bilioni 567.34 ikiwa ni punguzo la 13%. Mchanganuo unaoneshwa kwenye jedwali namba tisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya mwaka 2026/2027 ya Wizara ya Kilimo kwa mafungu yote matatu imepungua kwa kiasi cha shilingi bilioni 86.91 sawa na punguzo la asilimia saba ikilinganishwa na bajeti ya 2025/2026. Uchambuzi umebaini ya kuwa punguzo hilo linatokana pia na kupungua kwa fedha za matumizi ya kawaida kwa Fungu 43 Wizara ya Kilimo ambapo imepungua kwa 11.32%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufanisi wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo hususan usambazaji wa mbolea pamoja na pembejeo za kilimo unategemea upatikanaji wa fedha za kutosha na kwa wakati. Kamati inaona ipo haja ya kuongeza bajeti ya kilimo ili kukidhi mahitaji ya sekta hii na kuhakikisha tija inaongezeka katika kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuongezeka kwa bajeti kutaboresha miundombinu ya umwagiliaji, ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya hifadhi ya mazao, kuimarisha vituo vya utafiti, upatikanaji wa pembejeo, kuimarisha huduma za ugani pamoja na kuimarisha usimamizi na ukaguzi wa vyama vya ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Tume ya Taifa Umwagiliaji, Fungu 05 kwa mwaka wa fedha 2026/2027, inaomba kuidhinishiwa na Bunge bajeti ya shilingi bilioni 75.56 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kiasi hicho ni ongezeko la asilimia tano nukta sita tatu ikilinganishwa na bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026. Aidha, fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni shilingi bilioni 308.72 na hakuna ongezeko lolote kwenye fedha za maendeleo. Mchanganuo unaonesha kwenye jedwali namba 10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Taifa ya Maendeleo ya Ushirika, Fungu 24 katika mwaka wa fedha 2026/2027 inaomba kuidhinishiwa na Bunge bajeti ya shilingi bilioni 21.97 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kiasi hicho ni punguzo la asilimia sifuri nukta nne mbili ikilinganishwa na bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026. Aidha, fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni shilingi milioni 697 na hakuna ongezeko lolote. Mchanganuo unaoneshwa kwenye jedwali namba tisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa jumla unaonesha kwamba bajeti ya matumizi ya kawaida kwa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji na Tume ya Maendeleo ya Ushirika, imepungua ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2025/2026. Aidha, fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo haijaongezeka. Punguzo la bajeti inawezekana kuathiri kufikia malengo yaliyowekwa katika mpango wa kuendelea kuongeza tija na uzalishaji katika sekta ya kilimo. Kamati inashauri Serikali kuendelea kuongeza bajeti ya tume hizi ili ziweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia majadiliano ya kina yaliyofanywa na Kamati kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2025/2026 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka wa fedha 2026/2027 ili kusaidia katika utekelezaji mzuri wa bajeti hiyo, Kamati ina maoni yafuatayo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni ya jumla. Kamati inatoa maoni, ushauri na mapendekezo ya jumla kwa mafungu yote Wizara ya Kilimo kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokupatikana kwa wakati kwa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya miradi ya maendeleo, kunasababisha utekelezaji wa miradi hiyo kusuasua. Kutokana na hali hiyo, miradi mbalimbali imeathirika kutokana na kuongezeka kwa madeni ya wazabuni wanaosambaza mbolea kwa mpango wa ruzuku, wakandarasi wa miradi ya umwagiliaji, kupungua kwa ufanisi wa ufanyaji utafiti wa kilimo pamoja na uzalishaji wa mbegu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali itoe fedha za miradi ya maendeleo kwa wakati na kwa kiwango kilichokusudiwa ili kukidhi matarajio ikiwa ni pamoja na kulipa madeni ya kampuni zinazouza mbegu za mahindi kupitia programu ya ruzuku ya kiasi cha shilingi bilioni 54.91. Aidha, Serikali ijielekeze zaidi kwenye kutumia vyanzo vya ndani vya mapato katika kutekeleza miradi ya maendeleo kutokana na uzoefu kuwa upatikanaji wa fedha za nje umekuwa wa kusuasua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupungua kwa fedha zilizotengwa kwa Wizara ya Kilimo Fungu 43 kwa mwaka wa fedha 2026/2027 kwa asilimia saba kunakinzana na makubaliano ya utekelezaji wa Azimio la Maputo la 2023 na Malabo 2014 yanazozitaka nchi wanachama kutenga 10% ya bajeti ya Taifa kwa sekta ya kilimo. Kamati inaendelea kushauri kwamba Serikali iendelee kuongeza bajeti ya kilimo ili kufikia malengo yaliyokusudiwa na kutekeleza makubaliano ya maazimio ambayo nchi yetu imeingia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makusanyo hafifu ya maduhuli kutoka kwenye baadhi ya vyanzo vya mapato ya Wizara hii yanatokana na changamoto ya udhibiti usiotosheleza wa maeneo ya mipaka ambapo unapelekea baadhi ya mazao kutoka nchi za nje bila kukaguliwa katika vituo vya mipakani, hivyo kupoteza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri Wizara kuhakikisha inashirikiana na mamlaka nyingine za Serikali katika utoaji wa tozo za mazao ili kuimarisha maduhuli ya Serikali na vilevile kuongeza wakaguzi wa mazao katika vituo vya mipakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusimama kwa mchakato wa kutunga sheria ya Kitaifa ya kusimamia rasilimali ya nasaba za mimea kwa takribani miaka 18, kumepelekea wakulima kutokuwa na sheria inayolinda mbegu za asili na haki za wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kukamilisha mchakato wa utungaji wa sheria hii ili mbegu za asili ziweze kutambulika na kulinda haki za mkulima wa mbegu. Aidha, kuwepo kwa sheria kutasaidia kuongezeka kwa uzalishaji wa mbegu za asili na hivyo kusaidia upatikanaji wa lishe bora na kuchangia kujitosheleza kwa virutubisho na kupunguza ulazima wa uhitaji wa virutubisho vya viwandani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na athari zilizowekwa, zinazoweza kujitokeza kwenye tasnia ya mbolea nchini kufuatia na migogoro inayoendelea kati ya Marekani, Israel na Iran, jambo ambalo litapelekea kupanda kwa bei ya mbolea pamoja na kuvurugika kwa mnyororo wa ugavi na hivyo kupelekea kupanda kwa gharama za uzalishaji kwa wakulima nchini, Kamati inashauri Serikali kufanya yafuatayo: -

(i) Kuviwezesha viwanda vinavyozalisha mbolea na visaidizi vya mbolea ndani ya nchi kwa kutekeleza mpango maalumu wa ruzuku ili kupunguza gharama za uzalishaji;

(ii) Kuwa na mpango mahususi wa kuhakikisha mbolea inapatikana kwa wakati, ni pamoja na kuwezesha kampuni zinazoagiza mbolea nchini kuingiza mbolea kutoka maeneo mbalimbali yanayozalisha mbolea duniani; na

(iii) Kulipa madai ya kampuni zinazouza mbolea kupitia programu ya ruzuku kiasi cha shilingi bilioni 398.32. Kati ya kiasi hicho, *Tanzania Fertilizer Company* inadai takribani shilingi bilioni 43.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kufungwa kwa viwanda vingi vya chai nchini, soko la chai limekuwa changamoto kubwa, jambo linalopelekea kuinyima sekta ya kilimo fursa ya kuchangia ipasavyo katika uchumi ikiwa ni pamoja na kuwakatisha tamaa wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri Serikali kuchukua hatua mahususi na madhubuti, ikiwa ni pamoja na kutafuta wawekezaji wenye uwezo wa kuwekeza na kuendesha viwanda vya chai nchini na kutafuta masoko ya nje. Aidha, Serikali iandae mkakati mahususi wa kuinua zao la chai nchini kwa kutatua changamoto mbalimbali ili wananchi waendelee kulima zao la chai. Vilevile Serikali iweke mkakati wa kuwawezesha wakulima kuwa na viwanda vidogo vidogo vya kusindika chai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya zana za kilimo bado ni changamoto kwa wakulima wengi nchini. 44% ya wakulima bado wanatumia jembe la mkono, jambo linalowapelekea wakulima wengi kuzalisha bila tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri Serikali kuongeza upatikanaji wa huduma za zana za kilimo za kisasa kwa kununua matrekta na *powertillers* pamoja na zana nyingine na vile vile kuongeza vituo vya kutoa huduma za zana za kilimo ili kuongeza upatikanaji wa huduma za zana za kilimo kwa wakulima na kupunguza gharama za uzalishaji na kuongeza tija. Aidha, Kamati inaishauri Serikali iandae mwongozo maalum wa usimamizi wa utekelezaji wa vituo hivyo kwa kutoa huduma za zana za kilimo kwa kuwa uzoefu unaonesha zana hizi kukosa usimamizi na kuharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi yasiyo sahihi ya pembejeo za kilimo (mbegu bora, viuatilifu na mbolea) yanapelekea wakulima wengi kupunguza uzalishaji, uharibifu wa udongo, na ubora mdogo wa mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali iendelee kutoa elimu kwa wakulima kuhusu matumizi sahihi ya pembejeo

za kilimo ili kufikia lengo la kuongeza uzalishaji na ukuaji wa kilimo kufikia 10% ifikapo 2030.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutotolewa kwa fedha za miradi ya Jenga Kesho Iliyo Bora *(BBT)* ambapo kiasi cha fedha kilichotolewa ni shilingi bilioni sita sawa na 37.5% ya fedha ya ndani zilizotengwa. Jambo hili limeathiri utekelezaji wa miradi ya *BBT*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kutoa kiasi cha fedha kilichobaki kabla ya mwaka huu wa fedha kwisha ili kufanikisha utekelezaji wa mradi kutokana na umuhimu wa mradi huu katika kuongeza ajira zenye staha na ushiriki wa vijana na wanawake na hatimaye kufikia lengo la kutengeneza ajira milioni tatu kwa vijana na wanawake ifikapo 2030.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maendeleo ya sekta yoyote yanatokana na tafiti za kutosha kutoka sekta husika. Sekta ya Kilimo inakumbwa na changamoto ya watafiti kuondoka na kwenda kufanya kazi ambazo siyo za kitafiti, jambo ambalo linaathiri utekelezaji wa shughuli za kilimo. Kamati inaishauri Serikali kuwekeza mazingira wezeshi kwa watafiti ikiwemo kuboresha maslahi ya watafiti na mazingira ya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji Fungu 05: kutotolewa kwa fedha za miradi ya sekta ya umwagiliaji kumepelekea kuchelewa kwa malipo ya wakandarasi washauri elekezi, jambo ambalo limeathiri utekelezaji wa miradi ya sekta ya umwagiliaji. Baadhi ya athari hizo ni pamoja na miradi 51 iliyopangwa kutekelezwa katika mwaka 2025/2026 kutoanza utekelezaji wake hadi tarehe 25 Machi, 2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakandarasi wanaotekeleza miradi ya umwagiliaji wanadai jumla ya shilingi bilioni 109.1 na miradi 101 iliyokuwa itekelezwe kabla ya mwaka 2025/2026 imesimama jambo ambalo litaisababishia Serikali hasara kwa sababu mvua zinazoendelea nchini zinaweza kuathiri miradi hiyo na hivyo Serikali kuingia gharama mara mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kulipa hati zote za madai ambazo zimewasilishwa Wizara ya Fedha za jumla ya shilingi bilioni 100.9. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kukwamua miradi yote iliyokwama ili kudhibiti hasara inayoweza kujitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ione umuhimu wa kuongeza bajeti katika miradi ya sekta ya umwagiliaji ili kuweza kujenga miundombinu ya umwagiliaji kwenye mabonde ikiwemo mwagiliaji mdogo mdogo na kwa kutumia maji ya maziwa, visima na mito isiyokauka ili kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula kama vile ngano, mchele, miwa na kadhalika. Kamati inaishauri Serikali kutafuta fedha maalumu kwa ajili ya miradi mikubwa ya umwagiliaji wa kimkakati katika mabonde makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ninapenda kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa uongozi wenu na kwa kutupa nafasi ya kuwasilisha taarifa hii hapa Bungeni. Aidha, kwa dhati kabisa ninapenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, ambao maoni na ushauri na ushirikiano wao umewezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na hatimaye kukamilisha taarifa hii. Ninaomba majina yao yaingizwe kwenye taarifa za *Hansard* kama ilivyowasilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati, ninapenda kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuona umuhimu wa Sekta ya Kilimo kwa kipindi chote cha uongozi wake. Pia, ninapenda kuwapongeza Mheshimiwa Daniel Godfrey Chongolo, Waziri wa Kilimo na Mheshimiwa David Ernest Silinde, Naibu Waziri wa Kilimo kwa ushirikiano mkubwa wanaoipa Kamati ambao kwa sehemu kubwa umechangia kuiwezesha Kamati kutekeleza shughuli zake kikamilifu. Ninawashukuru pia watendaji wote wa Wizara ya Kilimo na taasisi zote zilizopo chini ya Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu Bwana Gerald Godfrey Mweli, akisaidiwa na Naibu Makatibu: Profesa Peter Msofe na *Engineer* Athumani Kilundumya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee ninamshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Baraka Leonard kwa kuwaongoza vyema Watumishi wa Ofisi ya Bunge katika utaratibu na usimamizi wa shughuli za Kamati kwa ujumla hadi kukamilika kwa ripoti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo sasa, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo Fungu 43, Fungu 24 na Fungu 05 kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA KILIMO KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

SEHEMU YA KWANZA

1.0 MAELEZO YA JUMLA

1.1 Utangulizi

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 121 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2025, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, pamoja na Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/ 2027.

Mheshimiwa Spika, ili kukidhi matakwa ya Kanuni ya 121(9) ya Kanuni za Bunge, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu zifuatazo: -

(a) Sehemu ya Kwanza inatoa maelezo ya jumla kuonesha msingi na Muundo wa Taarifa pamoja na namna Kamati ilivyofanya kazi;
(b) Sehemu ya Pili ni uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti wa Ofisi hii kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026;
(c) Sehemu ya Tatu ni uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027;
(d) Sehemu ya Nne inahusu maoni na ushauri wa Kamati; na
(e) Sehemu ya Tano ni hitimisho.

1.2 Msingi wa Taarifa

Mheshimiwa Spika, Msingi wa taarifa hii ni majukumu ya Kamati kwa mujibu wa Kifungu cha 6(1)(b) na Kifungu cha 7(1) (a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, pamoja na masharti ya Kanuni ya 121 (4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Kanuni hizo kwa pamoja zimeweka masharti yanayohusu uchambuzi wa Taarifa ya Utekekezaji na Makadiriro ya Matumizi ya Wizara ya Kilimo kabla ya kujadiliwa Bungeni. Kwa masharti hayo Kamati ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo ilifanya uchambuzi na kupata maudhui ya Taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, sambamba na uchambuzi na uchambuzi huo, Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni ya 120(1) ya Kanuni za Bunge yanayohusu kutembelea na kukagua utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha unaokwisha. Kazi hiyo ilifanyika kati ya tarehe 15 na 18 Machi 2026 katika Mikoa ya Morogoro na Dodoma. Napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 ulitumia matokeo ya ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Wizara ya Kilimo.

1.3 Mawanda ya Uchambuzi

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo inagusa mafungu matatu. **Fungu 43** ambalo ni Wizara ya Kilimo, **Fungu 24** - Tume ya Maendeleo ya Ushirika na **Fungu 05** - Tume ya Taifa ya

Umwagiliaji. Naomba kutoa taarifa mbele ya Bunge lako Tukufu kuwa, Kamati ilichambua taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mafungu yote matatu tarehe 19 na 23 Machi 2026.

SEHEMU YA PILI

2.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI NA TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026.

2.1 Ufafanuzi wa Jumla

Mheshimiwa Spika, Katika vikao vya Kamati vilivyoketi tarehe 19 na 23 ya Mwezi Machi, 2026. Kamati ilipokea, kujadili na kuchambua Taarifa ya Wizara ya Kilimo zilizohusu pamoja na mambo mengine Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa fedha 2025/2026. Taarifa hiyo iliwasilishwa na **Mhe. Daniel Godfrey Chongolo Mb**, Waziri wa Kilimo. Uchambuzi wa Kamati kuhusu Taarifa hizo umeangazia maeneo makuu manne yafuatayo;

(a) Makusanyo ya maduhuli kuanzia Julai, 2025 hadi Februari, 2026;
(b) Mwenendo wa Upatikanaji wa fedha za Bajeti za Matumizi ya kawaida na Mendeleo kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Februari 2026;
(c) Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026; na
(d) Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati Bungeni uliotolewa na Bunge wakati wa kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, mambo hayo yanatoa taswira muhimu kwa Bunge kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

2.2 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo inajumuisha mafungu matatu, Wizara ya Kilimo - **Fungu 43**, Tume ya Maendeleo ya Ushirika - **Fungu 24** na Tume ya Taifa ya Umwagiliaji - **Fungu 05**.

2.2.1Taarifa ya Fedha zilizovuka Mwaka 2024/2025

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara ya Kilimo (Fungu 43) iliomba kibali cha kuvuka na jumla ya **Shilingi 48,791,570,661** ili kutekeleza kazi mbalimbali za maendeleo zikiwemo kugharamia ununuzi wa mbolea, ruzuku za mbolea, ununuzi wa nafaka na kugharamia madeni yalitotokana na biashara ya Pamba msimu wa kilimo 2019/2020. Kampuni ya Mbolea TanzaniaTFC **Shilingi 15,000,000,000**, Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania – TFRA **Shilingi 15,000,000,000,** Wakala wa Taifa wa Hifadhi za Chakula-NFRA **Shilingi 4,000,000,000** na Bodi ya Pamba Tanzania-TCB **Shilingi 14,791,570,661.** Hadi kufikia Februari 2026 fedha zote **Shilingi 48,791,570,661** zilipokelewa. Aidha kwa upande wa **Tume ya Taifa ya Umwagiliaji-Fungu 05** fedha zilizovuka mwaka 2024/2025 ni **Shilingi 23,035,020,861.95** ambapo fedha hizo zilitumika kulipa madai ya wakandarasi.

2.2.2 Makusanyo ya Maduhuli kwa Wizara ya Kilimo – Fungu 43

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 Wizara ya Kilimo Fungu 43 ililenga kukusanya maduhuli jumla ya **Shilingi 8,665,370,000** kutoka Mapato ya Mfuko Mkuu wa Serikali ambayo yanatokana na Ukaguzi wa Mazao, Kodi za Mazao na Uuzaji wa Nyaraka za Zabuni na **Shilingi 24,219,196,666.66** kutoka Mfuko wa Mendeleo ya Kilimo.

Hadi kufikia Mwezi Februari, 2026 Wizara ya Kilimo ilikuwa imekusanya **12,962,023,810.69** sawa na **Asilimia 149.58** ya malengo yaliyokusudiwa kutoka kwenye Mapato ya Mfuko Mkuu

wa Serikali na **Shilingi 29,288,658,829.92** sawa na **Asilimia 120.93** kutoka Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo. Mchanganuo wa makusanyo hayo unaonekana katika **Jedwali Na.01.**

Jedwali Na: 1 Fungu 43 - Makadirio na Makusanyo katika Mwaka wa Fedha 2025/2026

MAKADIRIO NA MAKUSANYO 2025/2026			
Chanzo	**Makadirio (tsh.)**	**Makusanyo (tsh.)**	**Asilimia**
Mapato ya Mfuko Mkuu wa Serikali	8,665,370,000	12,962,023,810.69	149.58
Mapato ya Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo	24,219,196,666.66	29,288,658,829.92	120.93
Jumla	**32,884,566,666.66**	**42,250,682,640.61**	**128.48**

Chanzo: Randama ya bajeti ya 2026/2027 fungu 43

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa makusanyo ya maduhuli unaonesha kwamba mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli unaonesha kuwa jumla ya **Shilingi 42,250,682,640.61** sawa na **Asilimia 128.48** ya makusanyo yote yalikusanywa katika kipindi hicho. Ukusanyaji huo wa mapato unaonyesha kuwa umevuka malengo ambayo Wizara ilijiwekea.

Mheshimiwa Spika, kwa uchambuzi huu ni wazi kuwa Wizara inaweza kufanya tathmini na kuongeza lengo la makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 kwa kuimarisha matumizi ya Mfumo wa e-kilimo katika ukusanyaji wa mapato na kuthibiti utoroshaji wa mazao Mipakani.

2.2.3 Makusanyo ya Maduhuli kwa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji – Fungu 05

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa Fedha 2025/2026, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ilijiwekea lengo la kukusanya jumla ya **Shilingi 3,600,000,000**. Hadi kufikia mwezi Februari, 2026 Tume ya Umwagiliaji ilikuwa imekusanya **Shilingi 1,908,588,429.88** sawa

na **asilimia 53.02** ya lengo lililokusudiwa. Mchanganuo wa makusanyo hayo unaonekana katika Jedwali namba 2.

Jedwali Na: 2: Fungu 05 - Makadirio na Makusanyo katika Mwaka wa Fedha 2025/2026

MAKADIRIO NA MAKUSANYO 2025/2026			
Chanzo	**Makadirio (tsh.)**	**Makusanyo (tsh.)**	**Asilimia**
Fungu 05	3,600,000,000	1,908,588,429.88	53.02

Chanzo: Randama ya bajeti ya 2026/2027 fungu 05

Mheshimiwa Spika, makusanyo ya maduhuli kwa fungu 05 yanaonesha kwamba, kiasi kilichokusanywa katika Fungu hili hadi kufikia Mwezi Februari 2026 ni Shilingi **1,908,588,429.88** sawa na **asilimia 53.02** ya lengo kwa mwaka. Kiwango hicho cha makusanyo si cha kuridhisha, kwani hadi Februari, 2026 kiwango cha makusanyo kilipaswa kufikia **asilimia 75.**

Mheshimiwa Spika, Kushindwa kukusanya maduhuli kwa kiwango kinachotosheleza cha asilimia, kuna punguza uwezo wa Tume kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. **Ili kuondokana na athari hizo, ni rai ya Kamati kuwa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji iongeze kasi na kubuni mikakati itakayowezesha ukusanyaji wa maduhuli kupitia mifumo mathubuti ili kufikia lengo lililokusudiwa katika mwaka wa fedha 2026/2027**.

2.2.4 Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka Fedha 2025/2026 Wizara ya Kilimo imeidhinishiwa jumla ya **Shilingi 1,192,975,075,000** kupitia Fungu 43, Fungu 05 na Fungu 24.

2.2.4.1 Fungu Na.43 Wizara ya Kilimo

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, **Fungu 43 -** Wizara ya Kilimo, iliidhinishiwa na Bunge Bajeti ya **Shilingi 135,983,889,000.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo **Shilingi 81,447,048,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara

ya Wizara, Bodi na Taasis na **Shilingi 54,536,841,000.00** kwa ajili ya matumizi mengineyo kwa Wizara, Bodi na Taasisi. Aidha fedha kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ilikuwa **Shilingi 652,275,933,000** kati ya fedha hizo **Shilingi 424,328,013,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 227,947,920,000** ni fedha za nje.

Hadi kufikia Februari, 2026 Wizara ilipokea jumla ya **Shilingi 65,180,207,771.44** kwa ajili ya Matumizi ya kawaida sawa na **asilimia 47.93** ya bajeti iliyotengwa. Kati ya fedha hizo **Shilingi 14,549,642,218.88** matumizi mengineyo na **Shilingi 50,630,565,552.56** ni kwa ajili ya mishahara.

Kwa upande wa fedha za maendeleo hadi kufikia mwezi Februari, 2026 Wizara ilipokea jumla ya **Shilingi 361,292,488,068.57** sawa na **Asilimia 55.39**. kati ya fedha hizo **Shilingi 197,639,844,258.98** sawa na **Asilimia 46.58** ni fedha za ndani na **Shilingi 163,652,643,809.59** sawa na **Asilimia 71.79** ni fedha za nje. Jedwali namba 3 linaonesha mwenendo wa upatikanaji wa fedha wa Fungu 43 kwa Mwaka 2025/2026.

Jedwali Na: 3: Fungu 43 Mapokezi ya Fedha za Matumizi ya Kawaida 2025/2026

MAPOKEZI YA FEDHA ZA MATUMIZI YA KAWAIDA 2025/202				
Matumizi		**Fedha iliyotengwa 2025/2026**	**Fedha zilizopokelewa**	**Asilimia ya mapokezi**
Mishahara		**81,447,048,000.00**	**50,630,565,552.56**	62.16
Oc		**54,536,841,000.00**	**14,549,642,218.88**	26.68
Jumla ndogo (matumizi ya kawaida)		**135,983,889,000.00**	**65,180,207,771.44**	**47.93**
Maendeleo	**Ndani**	**424,328,013,000**	**197,639,844,258.98**	**46.58**
	Nje	**227,947,920,000**	**163,652,643,809.59**	**71.79**
Jumla Kuu		**788,259,822,000**	**426,472,695,840.01**	**54.10**

Chanzo: Randama ya Wizara Fungu 43

Jedwali Na: 4: lifuatalo linaonyesha miradi ya maendeleo iliyotengewa Fedha na kupokelewa kwa kila mradi

MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA 2025/2026						
Namba na jina la mradi	**Bajeti iliyotengwa 2024/2025**		**Mapokezi ya fedha hadi kufikia Februari 2026**		**Asilimia ya mapokezi**	
	Fedha za ndani	**Fedha za nje**	**fedha za ndani**	**fedha za nje**	**Ndani**	**Nje**
4429: Programu ya Maendeleo ya Kilimo na Uvuvi(AFDP)		31,246,503,540	0	8,334,783,893		26.67
4430: Mradi wa kuwezesha upatikaji wa pembejeo za Kilimo Tanzania (TAISP)	221,800,000,000,	40,000,000,000	61,000,000,000	6,506,899,505	37.50	16.27
4431 Mradi wa Jenga kesho iliyo Bora (BBT)	16,000,000,000	41,009,000,000	6,000,000,000	14,502,899,505	37.50	35.36
4403 Program ya Mifuko himilivu ya Chakula Tanzania (TFSRP)	185,071,116,400	130,736,000,000	129,882,960,658	128,232,558,184	70.18	98.09
4497 Mradi wa kuongeza uwezo wa uhifadhi	700,000,000	28,880,000,000	0	0	0	0
4499 Mradi wa kudhibiti Sumukuvu Tanzania (TANIPAC)	756,883,600	6,076,396,460	756,883,600	6.076,396,459	100	100
Jumla Kuu	**424,328,000,000**	**277.947,900,000**	**197,639,844,259**	**163,652,643,810**	**46.58**	**58.88**

Chanzo. *Randama ya Bajeti 2026/2027 Fungu 43*

Mheshimiwa Spika, tamthimi ya mapokezi ya fedha za matumizi ya kawaida si wa kuridhisha kwani ni **asilimia 47.93** ya fedha iliyotengwa imepokelewa. Endapo hali hiyo itaendelea kuwa si kuridhisha hadi itakapofika mwezi Juni 2026 wakati wa kuhitimisha mwaka huu wa fedha, ni Dhahiri kuwa Wizara itashindwa kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi uliofanywa na Kamati umebaini mambo mbalimbali kuhusu utekelezaji wa bajeti ya miradi ya Maendeleo kama ifuatavyo;

(a) Kiasi cha fedha kilichopokelewa kwa Miradi ya Maendeleo ni **Asilimia 55.39** ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili hiyo.

(b) Mradi wa Jenga Kesho iliyo Bora (BBT) uliidhinishiwa jumla ya Shilingi **16,000,000,000** fedha za ndani, hadi kufikia Februari, 2026 fedha zilizopokelewa ni **Shilingi 6,000,000,000** sawa na **asilimia 37.50** ya Bajeti. Utolewaji huu wa fedha umeathiri utekelezaji wa miradi ya BBT na hivyo kupelekea kushindwa kufikia malengo ya kuongeza ajira zenye staha na ushiriki wa vijana na wanawake kwenye Kilimo.

(c) Mtiririko huu wa fedha kwenye miradi ya maendeleo unaathiri utekelezaji wa majukumu ya Wizara hasa kwenye mradi wa Upatikananaji wa Pembejeo za Kilimo Tanzania, Program ya Maendeleo ya Kilimo, ambayo tayari ipo kwenye hatua mbalimbali za utekelezaji wake. Jambo linaloathiri utekelezaji Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi kilichoahidi kuendelea kusimamia mapinduzi ya kilimo ili kuhakikisha kinaendelea kuwa chenye tija na kinachotumia teknolojia ya kisasa.

2.2.4.2 Tume ya Taifa ya Umwagiliaji

Mheshimiwa Spika, Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji - **Fungu – 05** iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 73,416,447,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo **Shilingi 8,267,617,000** kwa ajili ya mishahara na **Shilingi 65,148,830,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha Fedha za Maendeleo ni **Shilingi 308,721,961,000**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 259,617,801,000** fedha za ndani na **Shilingi 49,104,160,00**0 ni fedha za nje.

Hadi kufikia mwezi Februari, 2026, fedha za matumizi ya kawaida iliyopokelewa ni **Shilingi 9,415,070,368.75** sawa na **asilimia 14** ya fedha iliyoidhinishwa na Fedha za Maendeleo kiasi

cha **Shilingi 141,259,519,828.31** sawa na **asilimia 45.7.** Mchanganuo wa upokeaji wa fedha unaonekana katika **Jedwali Na. 5**.

Jedwali Na: 5: Fungu 05 Mapokezi Fedha za Matumizi ya Kawaida

MAPOKEZI YA FEDHA ZA MATUMIZI YA KAWAIDA 2025/2026				
Matumizi		**Fedha iliyotengwa 2025/2026**	**Fedha zilizopokelewa**	**Asilimia ya mapokezi**
Mishahara		8,267,617,000	5,784,281,500	69.96
Oc		65,148,830,000	3,430,788,869	5.2
Jumla ndogo (matumizi ya kawaida		**73,416,447,000**	**9,415,070,368.75**	**14.45**
Maendeleo	**Ndani**	**259,617,801,000**	**102,082,179,525.32**	**39.32**
	Nje	**49.104,160,000**	**39,187,340,303**	**79.80**
Jumla Kuu		**382,138,408,000**	**150,684,590,192**	**39.43**

Chanzo: Randama ya Wizara Fungu 05

Mheshimiwa Spika, tathmini inaonesha kuwa, hadi februari, 2026, upatikanaji wa fedha za bajeti katika Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo hauridhishi. Uchambuzi zaidi wa Kamati unaonesha kuwa, kiasi kikubwa cha fedha za maendeleo zililenga kutekeleza miradi ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji. Aidha kutolewa kwa fedha za Matumizi ya kawaida kwa **asilimia 14.45** tu kwa kiasi kikubwa kunakwamisha uendeshaji wa majukumu ya Tume.

Mheshimiwa Spika, kutokupokelewa kwa fedha za miradi iliyotengwa kikamilifu, kuna athari kwa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ya kushindwa kutekeleza azma yake ya kuongeza uzalishaji wa chakula na usimamizi wa mipango iliyokusudiwa kutekelezwa.

Ni maoni ya Kamati kuwa, fedha za maendeleo hususan fedha zilizotengwa kutekeleza miradi ya sekta ya umwagilaji

zitolewe ili kukamilisha miradi iliyokusudiwa kutekelezwa na kupunguza malimbikizo ya madeni ya wakandarasi na wazabuni jambo linalopelekea kuongezeka kwa madeni kutokana na riba na hivyo kupelekea hasara kwa serikali.

2.2.4.3 Tume ya Maendeleo ya Ushirika

Mheshimiwa Spika, Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Tume ya Taifa ya Maendeleo ya Ushirika - **Fungu – 24** iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 21,879,669,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo **Shilingi 12,846,074,000** kwa ajili ya mishahara na **Shilingi 9,033,595,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Aidha Fedha za Maendeleo ni **Shilingi 697,176,000**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 418,305,600** fedha kwa ajili ya kuimarisha ushirika wa Bustani za mazao mbogamboga (TCDC) na **Shilingi 49,104,160,00**0 ni fedha za ukarabati wa Ofisi za COASCO.

Hadi kufikia mwezi Februari, 2026, fedha za matumizi ya kawaida iliyopokelewa ni **Shilingi 9,415,070,368.75** sawa na **asilimia 58.30**ya fedha iliyoidhinishwa na Fedha za Maendeleo kiasi cha **Shilingi 278,880,000 (COASCO)** sawa na **asilimia 40** kilipokelewa**.** Mchanganuo wa upokeaji wa fedha unaonekana katika **Jedwali Na. 5**.

Jedwali Na: 6: Fungu 15 Mapokezi ya Fedha za Matumizi ya Kawaida 2025/2026

MAPOKEZI YA FEDHA ZA MATUMIZI YA KAWAIDA 2025/2026			
Matumizi	**Fedha iliyotengwa 2025/2026**	**Fedha zilizopokelewa**	**Asilimia ya mapokezi**
Mishahara	12,846,074,000	10,472,835,670	81.52
Oc	9,033,595,000	2,284,053,472.26	47.44
Maendeleo	697,176,000	278,870,400	40
Jumla	22,576,845,000	13,035,759,542	57.73

Chanzo: *Randama ya Bajeti 2026/2027 Fungu 24*

Mheshimiwa Spika, tathmini ya mapokezi ya fedha kwa Fungu 24- Tume ya Maendeleo ya Ushirika inaonekana kuwa si ya kuridhisha kwa upande wa fedha za maendeleo. Endapo hali hiyo itaendelea kuwa si ya kuridhisha hadi itakapofika mwezi Juni, 2026 wakati wa kuhitimisha mwaka wa fedha wa 2025/2026, ni dhahiri kuwa miradi iliyotengewa fedha katika mwaka huu haitatekelezwa mathalani mradi wa kuimarisha ushirika wa Bustani za mazao mbogamboga(TCDC) ambao ulitengenewa **Shilingi 418,305,600** na hakuna fedha iliyopokelewa.

Kamati inashauri kuwa fedha zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo zitolewe ipasavyo ili wananchi waweze kunufaika na miradi iliyopangwa kutekelezwa.

2.2.5 Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

Mheshimiwa Spika, Katika Wizara ya Kilimo na Mafungu yake matatu. Kamati ilitembelea na kukagua miradi miwili iliyopo Morogoro na Dodoma kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 120 (1) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilitembelea na kukagua miradi ifuatayo: -

i. **Mradi Namba 6260 – Mradi wa Ukarabati wa Maabara ya Taifa ya Mbegu TOSCI – Morogoro.**

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitembelea na kukagua Mradi wa Ukarabati wa Maabara ya Taifa ya Mbegu TOSCI- Morogoro. Ukarabati huo ulilenga kuongeza ukubwa kutoka Mita za Mraba 825 na kufikia Mita za Mraba 1,715 jambo linaloongeza Maabara Mahsusi kutoka tatu na kufikia 4, Ofisi za Wataalam 7 na kufikia 19. Mradi huu ulianza tarehe 19 Septemba 2024 na ulitarajiwa kukamilika tarehe 17 Machi 2026.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa mradi huu hadi kukamilika unatarajiwa kugharimu jumla ya **Shilingi 1,988,144,792.79** ikiwa ni fedha za ufadhili kutoka Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo. Hadi kufikia tarehe 2 Machi 2026 jumla ya **Shilingi 1,224,059,637.51** zimetumika kwa shughuli za

utekelezaji wa mradi saw ana asilimia 61.6 ya bajeti ya mradi. Aidha utekelezaji wa mradi umeikia **asilimia 86.**

Mheshimiwa Spika, Kamati ililidhishwa na hatua ya utekelezaji wa mradi huu na inaona kuwa kukamilika kwa mradi huu utaongeza uwezo wa kudhibiti ubora wa mbegu kwa kutumia teknolojia za kisasa na kuendelea kulinda taswira ya Tanzania katika viwango vya ubora wa mbegu kimatifa na kufunga fursa mpya kwa uwekezaji katika uzalishaji na biashara ya mbegu.

ii. **Mradi Na. 4486 – Mradi wa Ujenzi wa Miundombinu ya Umwagilijaji katika Kituo cha TARI- Hombolo Dodoma.**

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa TARI kupitia kituo cha TARI Hombolo inatekeleza mradi wa Ujenzi wa Miundombinu ya Umwagiliaji wenye ukumbwa wa hekta 70. Mradi huu ni sehemu ya mradi wa umwagiliaji wa vituo 11 vya TARI na unatarajia kugharimu 17,818,629,997.28. Mradi huu ulianza kutekelezwa Mwezi Mei 2024 na unatarajia kukamilika Mwezi Juni 2026, utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 90.

Mheshimiwa Spika, Mradi huu unatekelezwa kwa ujenzi wa Miundombinu ya kutoa maji katika Bwawa la Hombolo na kusafirisha mpaka mashambani ambako kunajengwa na kusimikwa miundombinu ya umwagiliaji aina ya *Centre Pivot* na *Gun Springler system*. Kukamilika kwa mradi huu kutaimarisha kazi za utafiti wa kilimo na kuwezesha majaribio kufanyika kwa mwaka mzima,kuongeza eneo la uzalishaji mbegu kutoka hekta 3.6 hadi 73.6, kuongeza mapato ya ndani yanayotokana na mauzo ya mbegu kutokana na ongezeko la uzalishaji wa mbegu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inampongeza **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jitihada zake za kuwekeza kwenye miundombinu ya umwagiliaji na utafiti itakayosaidia Wizara kupitia Taasisi zake kugundua, kubuni na kuongeza upatikanaji wa teknolojia zinazojibu changamoto za Kilimo Nchini. Teknologia hizi zitawafanya Wakulima kuongeza tija katika uzalishaji na hivyo**

kuchangia kuondoa umaskini na kukuza uchuni wa mtu mmojammoja na Taifa kwa Ujumla

2.2.6 Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati

Mheshimiwa Spika, Wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Kamati ilitoa maoni, ushauri na mapendekezo mbalimbali ili kuboresha utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi hiyo. Naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kwamba kwa sehemu kubwa Serikali imezingatia maoni na ushauri wa Kamati. Licha ya utekelezaji huo mzuri, upatikanaji wa fedha usioridhisha umeendelea kuwa kikwazo kwa Wizara na hivyo kushindwa kuzingatia ipasavyo baadhi ya ushauri wa Kamati, Kamati inaendelea kusisitiza kuwa maagizo yenye muendelezo wa utekelezaji yaendelee kutekelezwa

SEHEMU YA TATU

3.0 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 120(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025, mnamo tarehe 23 Machi, 2026; Kamati ilipokea, kuchambua na kujadili Taarifa ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ta Kilimo kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Uchambuzi wa Kamati ulijikita katika maeneo makuu mawili ambayo ni Makadirio ya makusanyo ya maduhuli na makadirio ya matumizi. Tathmini ya uchambuzi kuhusu maeneo hayo ni kama ifuatavyo: -

3.1 Uchambuzi wa Makadirio ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

Mheshimiwa Spika,katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, Wizara ya Kilimo - Fungu 43 inaomba kuidhinishiwa kukusanya mapato jumla ya **Shilingi 61,000,000,000**. Kati ya fedha hizo Shilingi 25,000,000,000 maduhuli kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali na Shilingi 36.000.000.000 kutoka Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo. Fedha inayotarajiwa kukusanywa ni ongezeko la **asilimia 85**

ikilinganishwa na makadirio ya makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. Mchanganuo wa lengo la makusanyo kwa fungu unaonekana katika **Jedwali Na.7.**

Jedwali Na: 7: Ulinganisho katika Makusanyo ya Maduhuli Fungu 43

ULINGANISHO WA MAKUSANYO YA MADUHULI KWA MWAKA 2025/2026 NA 2026/2027				
Chanzo	**Makadirio Mwaka 2025/2026**	**Makadirio Mwaka 2026/2027**	**PUNGUFU/ ONGEZEKO**	**Asilimia**
Mapato ya Mfuko Mkuu wa Serikali	8,665,370,000	25,000,000,000	16,334,630,000	188.72
Mapato ya Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo	24,219,196,666.66	36,000,0000,000		35.82
Jumla	**32,884,566,666.66**	**42,250,682,640.61**	**11,780,803,334**	**85**

Chanzo: Randama ya bajeti ya 2026/2027 fungu 43

Mheshimiwa Spika, Tathmini inaonyesha kuwa makadirio ya maduhuli kwa mwaka wa fedha 2026/2027 yameongezeka kwa **asilimia 85** ikilinganishwa na lengo la makusanyo kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Hata hivyo uzoefu wa ukusanyaji kwa Mwaka wa Fedha unaoisha ulionesha kumudu kukusanya **asilimia 128.48** hadi kipindi cha robo tatu ya kipindi cha utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kufikia **asilimia 85** ndani ya robo tatu ya Mwaka. Kamati ina amini kuwa upo uwezekano wa kufikia na kuvuka lengo la makusanyo lililowekwa kwa mwaka wa fedha 2026/2027 endapo Wizara itaimarisha ukusanyaji wa tozo za mazao na kuthibiti utoroshaji wa mazao sehemu za mipakani jambo linalopelekea upotevu wa mapato.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa **Fungu 05 -** Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inakadiriwa kukusanya jumla ya **Shilingi 3,600,000,000** ambayo ni sawa na lengo la maduhuli kwa mwaka

wa fedha 2025/2026. **Jedwali Na. 6** linaonesha mchanganuo wa makadirio hayo.

Jedwali Na: 8: Ulinganisho katika Makusanyo ya Maduhuli Fungu 05

ULINGANISHO WA MAKUSANYO YA MADUHULI KWA MWAKA 2025/2026 NA 2026/2027				
Chanzo	**Makadirio 2025/2026 (tsh.)**	**Makadirio 2025/2026 (tsh.)**	**Ongezeko/ Pungufu**	**Asilimia**
Mfuko wa NIDF	3,600,000,000	3,6,000,000,000	0	0

Chanzo: Randama ya bajeti ya 2026/2027 fungu 05

Mheshimiwa Spika, uchambuzi unaonesha kwamba, kwa ujumla makadirio ya maduhuli kwa mwaka 2026/2027 ni sawa na lengo la maduhuli ya mwaka wa fedha 2025/2026. Kamati inaishauri Tume kuweka mikakati thabiti itakayowezesha kuongeza makusanyo ya mapato ikiwa ni pamoja kutumia Mifumo.

3.2 Uchambuzi wa Matumizi ya Kawaida

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka Fedha 2026/2027 Wizara ya Kilimo inaomba kuidhinishiwa jumla ya **1,106,064,979,995** kupitia Fungu 43, Fungu 05 na Fungu 24. Ikiwa ni punguzo la **asilimia 7**.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2026/2027, **Fungu 43 -** Wizara ya Kilimo, inaomba kuidhinishiwa na Bunge Bajeti ya **Shilingi 131,639,854,000** kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo **Shilingi 84,956,697,000** ni kwa ajili ya Mishahara ya Wizara, Bodi na Taasis na **Shilingi 46,683,157,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo kwa Wizara, Bodi na Taasisi. Kiasi hicho ni punguzo ya **asilimia 3.19** ikilinganishwa na bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Aidha fedha kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ni **Shilingi 567,345,730,000**. Kiasi hicho ni punguzo la **asilimia 13** Mchanganuo kama unavyoonyesha kwenye jedwali Na.7

Jedwali Na: 9: Makadirio ya Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2025/2026

ULINGANISHO WA MAKUSANYO YA MADUHULI KWA MWAKA 2025/2026 NA 2026/2027					
Matumizi		**Makadirio 2025/2026**	**Makadirio 2026/2027**	**Ongezeko/ punguzo**	**Asilimia**
Mishahara		**81,447,048,000.00**	**84,956,697,000**	3,509,649,000	4.30
Oc		**54,536,841,000.00**	**46,683,157,000**	-7,853,684,000	14.40
Jumlandogo(matumizi ya kawaida		**135,983,889,000.00**	**131,639,854,000**	**-4,344,035,000**	**-3.19**
Maendeleo	**Ndani**	**424,328,013,000**	**360,678,811,000**	**-63,649,202,000**	**-15**
	Nje	**227,947,920,000**	**206,666,919,000**	**-21,281,001,000**	**-9.33**
Jumla Kuu		**788,259,822,000**	**698,985,575,000**	**-89,274,247,000**	**-11.32**

Chanzo: Randama ya Wizara Fungu 43

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Mwaka 2026/2027 ya Wizara ya Kilimo kwa mafungu yote matatu imepungua kwa kiasi cha **Shilingi 86,910,095,005** sawa na punguzo la **asilimia 7** ikilinganishwa na bajeti ya 2025/2026. Uchambuzi umebaini kuwa punguzo hilo linatokana pia kupungua kwa fedha za matumizi ya kawaida kwa Fungu 43- Wizara ya Kilimo ambapo imepungua kwa **asilimia 11.32.**

Mheshimiwa Spika, Ufanisi wa utakelezaji wa miradi ya maendeleo hususani usambazaji wa mbolea pamoja na pembejeo za kilimo, unategemea upatikanaji wa fedha za kutosha na kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaona ipo haja ya kuongeza bajeti ya kilimo ili kukidhi mahitaji ya sekta hii na kuhakikisha tija inaongezeka katika kilimo. Kuongezeka kwa bajeti kutaboresha miundombinu ya umwagiliaji, ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya hifadhi ya mazao, kuimarisha vituo vya utafiti, upatikanaji wa pembejeo, kuimarisha huduma za ugani pamoja na kuimarisha Usimamizi na Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika.

Mheshimiwa Spika, Kwa Upande ya **Tume ya Taifa ya Umwagiliaji Fungu 05.** Katika Mwaka wa Fedha 2026/2027 **Tume**, inaomba kuidhinishiwa na Bunge Bajeti ya **Shilingi 75,568,800,000** kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo **Shilingi 10,419,970,000** ni kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi 65,148,830,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo. Kiasi hicho ni ongezeko la **a silimia 5.63** ikilinganishwa na bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Aidha fedha kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ni **Shilingi 308,721,961000**. Hakuna ongezeko lolote kwenye fedha za maendeleo. Mchanganuo kama unavyoonyesha kweny jedwali Na.10

Jedwali Na: 10: Makadirio ya Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2025/2026

ULINGANISHO WA MAKUSANYO YA MADUHULI KWA MWAKA 2025/2026 NA 2026/2027					
Matumizi		**Makadirio 2025/2026**	**Makadirio 2026/2027**	**Ongezeko /Pungufu**	**%**
Mishahara		8,267,617,000	**10,419,970,000**	2,152,353,000	26.03
Oc		65,148,830,000	**65,148,830,000**	0	0
Jumlandogo(matumizi ya kawaida		**73,416,447,000**	**75,568,800,000**	**2,152,353,000**	**2.93**
Maendeleo	**Ndani**	**259,617,801,000**	**259,617,801,000**	**0**	**0**
	Nje	**49.104,160,000**	**49,104,160,000**	**0**	**0**
Jumla Kuu		**382,138,408,000**	**384,290,761,000**	**2,152,353,000**	**5.63**

Chanzo: Randama ya Wizara Fungu 05

Mheshimiwa Spika,Tume ya Taifa ya Maendeleo ya Ushirika Fungu 24. Katika Mwaka wa Fedha 2026/2027 inaomba kuidhinishiwa na Bunge Bajeti ya **Shilingi 21,976,594,000** kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo **Shilingi 13,846,358,000** ni kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi 8,130,236,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo. Kiasi hicho ni punguzo la **asilimia 0.42** ikilinganishwa na bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Aidha fedha kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ni **Shilingi 697,176,000**. Mchanganuo kama unavyoonyesha kweny jedwali Na.9

Jedwali Na: 11: Makadirio ya Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2025/2026

ULINGANISHO WA MAKUSANYO YA MADUHULI KWA MWAKA 2025/2026 NA 2026/2027				
Matumizi	**Makadirio 2025/2026**	**Makadirio 2025/2026**	**Ongezeko/ Punguzo**	**%**
Mishahara	12,846,074,000	13,846,358,000	1,000,284,000	7.78
Oc	9,033,595,000	8,130,236,000	-903,359,000	9.99
Maendeleo	697,176,000	697,176,000		40
Jumla	22,576,845,000	13,035,759,542		57.73

Chanzo: *Randama ya Bajeti 2026/2027 Fungu 24*

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa jumla unaonesha kwamba Bajeti ya Matumizi ya Kawaida kwa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji na Tume ya Maendeleo ya Ushirika imepungua ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2025/2026. Aidha fedha kwaajili ya Miradi ya Maendeleo haijaongezeka.

Punguzo la bajeti inaweza kuathiri kufikia malengo yaliyowekwa katika mpango wa kuendelea kuongeza tija na uzalishaji katika sekta ya kilimo. Kamati inaishauri serikali kuendelea kuongeza bajeti ya Tume hizi ili ziweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

SEHEMU YA NNE

4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

Mheshimiwa Spika, kufuatia majadiliano ya kina yaliyofanywa na Kamati kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Mwaka 2025/2026 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya

Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, ili kusaidia katika utekelezaji mzuri wa bajeti hiyo, Kamati ina maoni yafuatayo:-

4.1 **Maoni ya Jumla**

Mheshimiwa Spika, Kamati inatoa maoni, ushauri na mapendekezo ya jumla kwa Mafungu yote yaliyo Wizara ya Kilimo kama ifuatavyo:

(i) Kutopatikana kwa wakati kwa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya miradi ya maendeleo kuna sababisha utekelezaji wa miradi hiyo kusuasua, Kutokana na hali hiyo miradi mbalimbali imeathirika kutokana na kuongezeka kwa madeni ya wazabuni wanaosambaza mbolea kwa mpango wa ruzuku, wakandarasi wa miradi ya umwagiliaji, kupungua kwa ufanisi wa ufanyaji wa tafiti za kilimo pamoja na uzalishaji wa mbegu. Kamati inaishauri Serikali itoe fedha za miradi ya maendeleo kwa wakati na kwa kiwango kilichokusudiwa ili kukidhi matarajio ikiwa ni pamoja na kulipa madeni ya Makampuni yanayouza mbegu za mahindi kupitia program ya Ruzuku ya mbegu kiasi cha **Shilingi 54,917,779.249**. Aidha Serikali ijielekeze zaidi kwenye kutumia vyanzo vya ndani vya mapato katika kutekeleza miradi ya maendeleo kutokana na uzoefu kuwa upatikanaji wa fedha za nje umekuwa wa kusuasua.

4.2 Wizara ya Kilimo – Fungu 43

(a) Kupungua kwa fedha iliyotengwa kwenye Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 kwa **asilimia 7** kunakinzana na makubaliano ya utekelezaji wa Azimio la Maputo (2003) na Malabo (2014) yanayozitaka nchi wanachama kutenga **asilimia 10** ya bajeti ya Taifa kwa ajili ya sekta ya kilimo. Kamati inaendelea kushauri kwamba Serikali iendelee kuongeza bajeti ya kilimo ili kufikia malengo yaliyokusudiwa na kutekeleza makubaliano ya maazimia ambayo nchi yetu imeingia.

(b) Makusanyo hafifu ya maduhuli kutoka kwenye baadhi ya vyanzo vya mapato ya Wizara hii yanatokana na changamoto ya udhibiti usiotosheleza wa maeneo ya mipaka ambapo

unapelekea baadhi ya mazao kutoka nje ya nchi bila kukaguliwa katika vituo vya mipakani hivyo kupelekea kupoteza mapato ya Serikali. Kamati inashauri Wizara kuhakikisha inashirikiana na mamlaka nyingine za Serikali katika utozaji wa tozo za mazao ili kuimarisha maduhuli ya Serikali na vilevile iongeze wakaguzi wa mazao katika vituo vya mipakani.

(c) Kusimama kwa mchakato wa kutunga Sheria ya Kitaifa Kusimamia Rasilimali za Nasaba za Mimea kwa takribani miaka 18 kumepelekea Wakulima kutokuwa na Sheria inayolinda Mbegu za Asili na Haki za Wakulima. Kamati inaishauri Serikali kukamilisha mchakato wa utungaji wa Sheria hii ili mbegu za asili ziweze kutambulika na kulinda haki za mkulima wa mbegu. Aidha kuwepo kwa sheria kutasaidia kuongezeka kwa uzalishaji wa mbegu za asili na hivyo kusaidia upatikanaji wa lishe bora na kuchangia kujitosheleza kwa virutubisho na kupunguza ulazima wa uhitaji wa virutubisho vya viwandani.

(d) Kutokana na athari zinazoweza kujitokeza kwenye Tasnia ya Mbolea nchini kufuatia migogoro inayoendelea kati ya Marekani/Israeli na Irani jambo ambalo litapelekea kupanda kwa bei ya mbolea pamoja na kuvurugika kwa mnyororo wa ugavi na hivyo kupelekea kupanda kwa gharama za uzalishaji kwa wakulima nchini. Kamati inaishauri Serikali kufanya yafuatayo:-

(i) Kuviwezesha viwanda vinavyozalisha mbolea na visaidizi vya mbolea ndani ya nchi kwa kutekeleza mpango Maalumu wa Ruzuku ili kupunguza gharama za uzalishaji.

(ii) Kuwa na Mpango Mahsusi wa kuhakikisha mbolea inapatikana kwa wakati ikiwa ni pamoja na kuwezesha Kampuni zinazoagiza mbolea nchini kuingiza mbolea kutoka maeneo mengine yanayozalisha mbolea Duniani.

(iii) Kulipa madai ya Makampuni yanayouza mbolea kupitia programu ya Ruzuku ya Mbolea kiasi cha **Shilingi 398,320,133,180,** kati ya kiasi hicho TFC inadai takribani **Shilingi 43,022,740,822.**

(e) Kutokana na kufungwa kwa Viwanda Vingi vya Chai Nchini, soko la zao la Chai limekuwa changamoto kubwa jambo linalopelekea kuinyima sekta ya kilimo fursa ya kuchangia ipasavyo katika uchumi ikiwa ni pamoja na kuwakatisha tamaa wakulima. Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua za makusudi ikiwa ni pamoja na kutafuta Wawekezaji wenye uwezo wa kuendesha Viwanda vya Chai Nchini na kutafuta masoko ya nje ya nchi. Aidha Serikali iandae mkakati mahsusi wa kuinuna zao la Chai nchini kwa kutatua changamoto mbalimbali ili Wananchi waendelee kulima zao la chai. Vilevile Serikali iweke Mkakati wa kuwawezesha Wakulima kuwa na Viwanda vidogovidogo vya kusindika Chai.

(f) Matumizi ya Zana za Kisasa za Kilimo bado ni changamoto kwa Wakulima wengi Nchini, asilimia 44 ya Wakulima bado wanatumia jembe la mkono jambo linalopelekea wakulima wengi kuzalisha bila tija. Kamati inaishauri Serikali kuongeza upatikanaji wa Huduma za Zana za Kisasa kwa kununua Matrekta na *Powertille*r pamoja na zana nyingine na vilevile kuongeza Vituo vya Kutoa Huduma za Zana za Kilimo ili kuongeza upatikanaji wa huduma za zana za kisasa kwa wakulima na, kupunguza gharama za uzalishaji na kuongeza tija. Aidha Kamati inaishauri Serikali iandae Mwongozo Maalum wa usimamizi na uendeshaji wa Vituo hivyo vya kutoa Huduma za Zana za Kilimo kwa kuwa uzoefu unaonyesha kuwa Zana hizi hukosa usimamizi na kuharibika. Aidha Serikali ihakikishe inatafuta wawekezaji wa Viwanda vya Zana za Kilimo Nchini ili kupunguza bei za zana hizo na kuongeza upatikanaji.

(g) Matumizi yasiyosahihi ya pembejeo za kilimo yaani mbegu bora, viuatilifu na mbolea vinapelekea wakulima wengi kupunguza uzalishaji, uharibifu wa udogo, ubora mdogo wa mazao. Kamati inaishauri Serikali iendelee kutoa elimu kwa wakulima kuhusu matumizi sahihi ya pembejeo za kilimo ili kufikia lengo la kuongeza uzalishaji na ukuaji wa kilimo na kufikia asilimia 10 ifikapo 2030 na vilevile kupunguza athari za viuatilifu kwa binadamu. Aidha Serikali iendelee kuboresha huduma za Ugani kwa kuwapatia vitendea kazi.

(h) Kutotolewa kwa fedha za mradi wa Jenga Kesho iliyo Bora (BBT) ambapo kiasi cha fedha kilichopokelewa ni **Shilingi 6,000,000,000** sawa na **asilimia 37.50** ya fedha za ndani zilizotengwa jambo ambalo limeathiri utekelezaji wa miradi ya BBT. Kamati inaishauri Serikali kutoa kiasi cha fedha kilichobaki kabla Mwaka huu wa fedha kuisha ili kufanikisha utekelezaji wa mradi kutokana na umuhimu wa mradi huu katika kuongeza ajira zenye staha na ushiriki wa vijana na wanawake na hatimaye kufikia lengo la kutengeneza ajira 3,000,000 za vijana na wanawake ifikapo 2030.

(i) Maendeleo ya Sekta yoyote yanatokana na tafiti za kutosha kuhusu sekta husika. Sekta ya kilimo inakumbwa na changamoto ya watafiti kuondoka na kwenda kufanya kazi ambazo siyo za kitafiti jambo ambalo linaathiri utekelezaji wa shughuli za kilimo. Kamati inaishauri Serikali kuweka mazingira wezeshi kwa watafiti ikiwemo kuboresha maslahi ya watafiti, mazingira ya kazi pamoja na kupata Hatimiliki za Ugunduzi.

4.3 Tume ya Taifa ya Umwagiliaji – Fungu 05

(a) Kutotolewa kwa fedha za miradi ya sekta ya umwagiliaji kumepelekea kuchelewa kwa malipo ya Wakandarasi, Washauri elekezi jambo ambalo limeathiri utekelezaji wa miradi ya sekta ya umwagiliaji. Baadhi ya athari hizo ni pamoja na Miradi **51** iliyopangwa kutekelezwa katika mwaka 2025/26 kutoanza utekelezaji wake hadi tarehe 25 Machi, 2026 wakandarasi wanaotekeleza miradi ya umwagiliaji wanadai jumla ya **shilingi 109,189,941,826.84 na** Miradi **101** iliyokuwa ikitekelezwa kabla ya mwaka 2025/2026 kusimama, jambo ambalo litaisababishia Serikali hasara kwa sababu mvua zinazoendelea nchini zinaweza kuathiri miradi hiyo na hivyo Serikali kuingia gharama mara mbili. Kamati inaishauri Serikali kulipa hati zote za madai ambazo zimewasilishwa Wizara ya Fedha zenye jumla ya **shilingi 109,189,941,826.84.** Aidha, Kamati inaishauri Serikali kukwamua miradi yote iliyokwama ili kudhibiti hasara inayoweza kujitokeza.

(b) Serikali ione umuhimu wa kuongeza bajeti katika miradi ya sekta ya umwagiliaji ili kuweza kujenga miundombinu ya umwagiliaji kwenye Mabonde, Umwagiliaji mdogo mdogo wa kutumia maji ya maziwa, visima na mito isiyokauka ili kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula kama vile Ngano, Mchele, Miwa yatakayoweza kutosheleza mahitaji ya ndani ya nchi na nje ya nchi, na hivyo kuongeza thamani ya mauzo ya nje ya nchi kutoka Dola za Marekani Billioni 1.2 hadi Dola za Marekeni Bilioni 5 ifikapo 2030. Kamati inaishauri Serikali kutafuta fedha maalumu kwa ajili ya miradi mikubwa ya umwagiliaji ya Kimkakati katika mabonde makubwa kama Kilombelo na Ruvu.

4.4 Tume ya Maendeleo ya Ushirika – Fungu 24

(a) Kutotolewa kwa fedha za Mradi wa Kuimarisha Ushirika wa Bustani za Mazao ya Mbogamboga (TCDC) kiasi cha **Shilingi 428,305,600.00** kumesababisha mradi huu kutotekelezwa kabisa. Kamati inaishauri Serikali kuona umuhimu wa kutoa fedha hizo ili kuongeza uzalishaji wa mazao ya bustani.

(b) Kukosekana kwa Mpango Madhubuti wa ufufuaji wa Viwanda vya Vyama vya Ushirika kunapelekea kukosekana kwa ushindani wa masoko nchini hasa katika zao la pamba, Kahawa, tumbaku na mazoa mengine. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuimarisha vyama vya ushirika kwa kuhakikisha mipango ya uwekezaji ikiwa pamoja na kufufua Viwanda vya Vyama vya Ushirika inatekelezwa ili vyama hivyo vijiendeshe kibiashara na kiushidani.

SEHEMU YA TANO

5.0 HITIMISHO

5.1 Maelezo ya Kuhitimisha

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa Uongozi wenu na kutupatia nafasi ya kuwasilisha taarifa hii hapa Bungeni. Aidha, kwa dhati kabisa, ninapenda kuwashukuru Wajumbe wote wa

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao yaingizwe kwenye taarifa rasmi za Bunge kama yalivyowasilishwa;

1. Mhe. Deodatus Philip Mwanyika, Mb – **Mwenyekiti**
2. Mhe. Mariam Ditopile Mzuzuri, Mb – **M/Mwenyekiti**
3. Mhe. Salma Rashid Kikwete, Mb – Mjumbe
4. Mhe. Prof. Sospeter Mwijarubi Muhongo, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Yustina Arcadius Rahhi, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Khadija Hassan Aboud, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Tauhida Galos Cassian, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Emmanuel Peter Cherehani, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Omar Marcus Msigwa, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Suma Ikenda Fyandomo, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Kabula Enock Shitobelo, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Dkt.Rita Enerpher Kabati, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Livingstone Joseph Lusinde Mb - Mjumbe
14. Mhe. Magreth Baraka Ezekiel, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Abubakar Alli Omari, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Kenneth Ernest Nollo, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Khalfan Issa Mohamed, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Jacqueline Kandidus Ngonyani Msongozi, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Khamis Hamad Yussuf, Mb - Mjumbe
20. Mhe. Amour Seif Abdalla, Mb - Mjumbe
21. Mhe. Khalid Mussa Nsekela, Mb - Mjumbe
22. Mhe. Ghati Zephania Chomete, Mb - Mjumbe
23. Mhe. Salum Khamis Salum, Mb - Mjumbe

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kumshukuru na kumpongeza **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kwa kuona umuhimu wa sekta ya kilimo kwa kipindi chote cha uongozi wake, Mhe. Daniel Godfrey Chongolo (Mb) - Waziri wa Kilimo na Mhe. David Ernest Silinde (Mb) – Naibu Waziri wa Kilimo, kwa ushirikiano mkubwa wanaoipatia Kamati ambao kwa sehemu kubwa umechangia kuiwezesha Kamati kutekeleza shughuli zake kikamilifu. Nawashukuru pia watendaji wote wa Wizara ya Kilimo na Taasisi zilizo chini ya Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu

Bwana Gerald Geofrey Mweli, akisaidiwa na Naibu Makatibu Prof. Peter Msoffe na Ndg. Athumani Kilundumya

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee namshukuru Katibu wa Bunge - Ndg. Baraka I. Leonard kwa kuwangoza vyema watumishi wa Ofisi ya Bunge katika uratibu na usimamizi wa shughuli za Kamati kwa ujumla hadi kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, Baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo (Fungu 43, 24 na 05), kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Deodatus Philip Mwanyika (Mb)
MWENYEKITI
KAMATI YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO

Aprili, 2026

MWENYEKITI: Tunakushukuru Mheshimiwa Mwenyekiti kwa uwasilishaji wa taarifa ya Kamati.

Waheshimiwa Wabunge, ninaomba niwataarifu kwamba Mheshimiwa Profesa Makame Mnyaa Mbarawa, ndiyo anayekaimu nafasi ya Mkuu wa Shughuli za Serikali hapa Bungeni, kuanzia leo tarehe 27 Aprili, 2026. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hapa tunao pia wageni wa Mheshimiwa Godfrey Chongolo, Waziri wa Kilimo, ambao ni Waheshimiwa Madiwani kutoka Makambako mkoani Njombe, karibuni sana Waheshimiwa Madiwani. *(Makofi)*

Waheshimiwa tunaanza na uchangiaji wa Wizara ya Kilimo. Tunaanza na Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mheshimiwa Salehe Mbwana Mhando ajiandae.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri ambayo anaifanya, hasa kwenye eneo la sekta ya kilimo. Tendo tu la kupeleka pembejeo zenye ruzuku, zimewasaidia sana wakulima waweze kuzalisha kwa kiwango kikubwa sana, tunampongeza sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumshukuru sana Mheshimiwa Chongolo, Waziri wa Kilimo kwa kazi nzuri ya kuisimamia Wizara ambayo anaifanya akishirikiana na msaidizi wake Mheshimiwa Naibu Waziri, wamefanya kazi nzuri. Wameendelea kuisimamia Wizara na ni wasikivu, wanasikiliza watu hasa tendo la kuwashirikisha wadau wote wa sekta ya kilimo, imefanya kila mtu ajenge imani kwenu ninyi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nianze mchango wangu kwenye zao la tumbaku. Zao la tumbaku limepata anguko la bei, ni eneo ambalo tunaiomba Serikali iangalie kwa kina. Zao la tumbaku limeporomoka kutoka bei ya awali iliyokuwepo mwaka 2025, leo hii zao la tumbaku linauzwa wastani wa dola 1.9 kutoka wastani wa dola 2.3 iliyokuwepo mwaka 2025. Ni anguko kubwa ambalo linapelekea wakulima wa zao la tumbaku washindwe kukidhi mahitaji yao na kushindwa kurejesha mikopo ambayo walikopa kupitia vyama vya ushirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishauri Wizara iangalie katika eneo hili, waangalie mjengeko wa bei ili waufumue, hasa kwenye gharama za uzalishaji ambazo zimekuwa kubwa sana kuliko kile ambacho mkulima anakitarajia kukipata. Wakulima wamekopa pembejeo za gharama ya juu sana mwaka huu, mfuko mmoja upo zaidi ya shilingi 160,000, ambao anakatwa mkulima kwenye eneo la uzalishaji, lakini bei anayoenda kuuza, ni ya chini kiasi kwamba hataweza kurejesha ule mkopo aliokopa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali iangalie, kwenye maeneo ambayo hasa gharama ambazo zinanufaisha kutoka

kwenye kilo inayozalishwa ya zao la tumbaku, vyama vya ushirika waangalie na wadau mbalimbali ili waweze kumsaidia huyu mkulima aweze kumudu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua, siyo jambo ambalo limetokea hapa tu kwetu, ni baada ya ongezeko la uzalishaji duniani limesababisha zao hili liweze kupata mtikisiko. Sasa mahala ambapo panapotokea mtikisiko lazima Serikali iweze kutengeneza fidia ya kumsaidia huyu mkulima ili aweze kurudi tena kwenye eneo la uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni zao la pamba. Mkulima wa zao la pamba bado hajanufaika kwa kiwango kikubwa. Bei anayopewa ni ndogo; anapata kati ya shilingi 1,000 na bei ya juu ni shilingi 1,060. Hata hivyo, bahati mbaya gharama ambazo anachangia huyu mkulima hasa kwenye mfuko wa pembejeo wa pamba ambao unapita bodi ya pamba, nilikuwa ninashauri kwenye eneo hili Mheshimiwa Waziri anajua pembejeo lazima mkulima apate. Hata hivyo, bado tuangalie gharama zile ambazo anazitumia huyu mzalishaji zinamwelemea, anashindwa kupata uzalishaji ambao utamfanya arejee kwenda kwenye kuzalisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba eneo hilo badala ya kutumia zile shilingi 300 kwa ajili ya mfuko wa pembejeo, tunashauri angalau nusu iende kwenye mfuko wa pembejeo na nyingine iende ikamfidie huyu mkulima aweze kupata fedha. Ni muhimu sana. Ukiangalia kwenye maeneo haya ya uzalishaji, yanaweza yakatupeleka kupata uzalishaji ambao ni mzuri na wananchi wakaneemeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala la miradi ya umwagiliaji. Miradi mingi ya umwagiliaji imefeli, haijakuwa vizuri na haiendi kwa sababu hakuna fedha ambayo imefika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mradi wa skimu ya umwagiliaji ya Karema ambayo ni ya muda mrefu. Tumetembea na Mawaziri wa kila aina; Waziri aliyeteuliwa kwenye Wizara ya Kilimo, amefika

kwenye eneo lile la mradi. Eneo lile ni kero kubwa kwa wananchi na aibu kwa sisi tunaoisimamia Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri, atakapokuwa anahitimisha hotuba yake, tunataka tupate mwafaka wa mradi wa skimu ya umwagiliaji ya Karema ambao bado haujafanyiwa kitu chochote. Awali kabla ya kuweka mradi ule, ulipokuwa umeanzishwa na Serikali, wakulima walikuwa wanufaika, wanapata fedha zao kwa ajili ya uzalishaji, lakini baada ya kuweka miundombinu mibovu ambayo haikuweza kukidhi mahitaji, ule mradi ulisababisha wakulima wengi kuanza kupata hasara kubwa kwa ajili ya mkondo wa maji kubadili uelekeo wake uliokuwepo awali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana kwenye eneo hili la miradi ya umwagiliaji Serikali ifanyie kazi na kwenda kuiona na kuhakikisha wanapeleka wakandarasi ambao wanaweza kufanya kazi vizuri wakawatumikia Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo tu huo mradi wa Skimu ya Karema, kwangu nina mradi mwingine wa skimu ya umwagiliaji ya Kabageni, Skimu ya Iloba, zote hizo bado hazijakamilika. Ninaomba sana, kwenye maeneo haya, yatatusaidia sana kuzalisha, na sisi tunayo mabonde mengi na tunazalisha mpunga kwa kiwango cha juu sana isipokuwa miundombinu ndiyo ambayo haipo sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba mwendelezo kwenye mabonde ya Mto Katuma, Mto Nyamasi tuweze kupata skimu za umwagiliaji ili ziweze kuwasaidia wananchi kwenye maeneo haya. Miradi ya umwagiliaji ndiyo pekee itakayoweza kuwasaidia wananchi waweze kujikwamua kwenye mfumo wa kilimo chenye uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo la masoko, Wizara tunahitaji ishughulike kuwasaidia wananchi kwenye maeneo hasa ya uzalishaji kwenye mazao yote ambayo yapo nchini. Korosho, pamba, chai, kahawa bado masoko siyo mazuri kwa sababu masoko haya hayasimamiwi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri, atengeneza mifumo ambayo itawasaidia Watanzania ili wananchi wanapokuwa wanazalisha wawe na uhakika wa masoko ya kwao. Mwaka huu tumezalisha mahindi mengi. Kwa kuwa Serikali imetambua uzalishaji ambao ni mkubwa karibu kila sehemu, ninaomba sasa Serikali ijikite kuwasaidia hawa wananchi waweze kupata masoko mazuri ambayo yatawasaidia kuwa na kipato kizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi, ninaunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Tunakushuru Mheshimiwa kwa mchango wako, nilimtaja Mheshimiwa Salehe Mbwana Mhando, ajiandae Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, ajiandae Mheshimiwa Ester Amos Bulaya.

MHE. SALEHE M. MHANDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nami nichukue fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kupata nafasi ya kuchangia hotuba ya Wizara ya Kilimo kwa siku ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami pia nianze kumpongeza Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa mapinduzi makubwa ambayo anaendelea nayo katika sekta hii ya kilimo hapa nchini. Hili halina ubishi, uwekezaji mkubwa unaofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita katika kutekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi inaonekana na mambo yanaendelea kwa kiwango ambacho kinaleta tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, niwapongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo Mheshimiwa Geodfrey Chokolo akisaidiwa kwa umahiri mkubwa na Naibu Waziri ndugu yangu Mheshimiwa Silinde, Katibu Mkuu pamoja na timu nzima ya Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nianze kwa kuunga mkono hoja ya hotuba ya Wizara ya Kilimo na ninaunga mkono kwa maana kwamba katika Taifa letu na katika nchi yetu

tumekubaliana kwamba kilimo ni uti, na Mheshimiwa Waziri ameboresha siyo uti wa mgongo, utii wa mgongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo ni kwamba, hapa leo tunazungumzia hatima ya maisha ya Watanzania, na hatima ya uchumi wa Taifa letu. Kwa maana kwenye kilimo kule ndiko kunakofanya tunaweza kuishi, kupata chakula, utoshelevu wa chakula, usalama wa chakula, halikadhalika, kilimo sasa hivi ni biashara. Kwa hiyo, hapa tunazungumzia uchumi wa wananchi wetu kwa mtu mmoja mmoja, Taifa na tunazungumzia suala la uchumi katika pato letu la Taifa kwa maana ya kuweza kuuza nje ya nchi na kupata fedha za kigeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na muktadha huu, ninaomba nichangie hotuba hii katika eneo muhimu sana ambalo limeelezwa na Waziri katika hotuba yake ya bajeti, lakini kwa msisitizo mkubwa nimeisikiliza sana hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge. Eneo ambalo tunatakiwa kuliwekea uzito sana katika suala la kilimo, mapinduzi ya kilimo, ni suala la umwagiliaji. Kilimo tunahitaji tutoke kwenye kilimo cha msimu twende kwenye kilimo cha mwaka mzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa hakuna njia nyingine zaidi ya uwekezaji kwenye miundombinu ya umwagiliaji. Katika miundombinu ya umwagiliaji, kwanza tukubaliane kwamba kupanga ni kuchagua, lazima fedha itoke iende kwenye eneo hilo. Miradi mingi tumeelezwa hapa, kwanza tuwe na miradi ya kimkakati tusipunguze miradi mingi, tukubaliane twende na miradi kadhaa ambayo tunaitekeleza mpaka ilete matokeo twende hatua nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano, kuna miradi kadhaa ambayo leo imeelezwa hapa, ukienda huwezi ukakuta kuna mradi ambao sasa hivi unazalisha mara mbili kwa msimu, haupo. Kwa hiyo, bado safari ni ndefu. Hapa, nilikuwa niombe na kuishauri Serikali kupitia Wizara ya Kilimo, mamlaka, na Wizara ya Fedha; kati ya jambo ambalo tunatakiwa kwenda kumwachia alama Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwenye nchi hii ni

kwenda kuitoa Tanzania kutoka kwenye kilimo cha msimu wa mvua kwenda kwenye kilimo cha msimu wa muda wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna fursa ya kuilisha Afrika, tuna fursa ya kuilisha dunia, na hata yanayoendelea duniani haya kwa upande mwingine kwa Tanzania sisi hii ni fursa. Leo hata hii miradi inayotekelezwa, tunatekeleza miradi ya kukinga maji ya mvua, baada ya mvua, ikiondoka, miradi ile na yenyewe haifanyi kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nashauri tuchague miradi. Kuna mabonde ambayo unajua kabisa ukisema Usangu, ukisema kule Mwamburu - Katavi, ukisema kule Morogoro, una hakika kwamba tukitengeneza miradi, Kilindi kule Tamota, miradi ambayo ukaweka miundombinu ya mabwawa, maji yakatengenezewa miundombinu ya umwagiliaji, tukazalisha kipindi cha mvua na kipindi cha kiangazi, haya ndiyo maana halisi ya miradi ya umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba hapa niweke msisitizo kwamba kilimo ni maji. Hakuna msamiati mwingine kwamba tutazalisha bila kuwa na maji. Kilimo ni maji na hili ninaomba niliwekee msisitizo kabisa kwamba hata nikiishia leo kuchangia hapa, nitakuwa nimesaidia Taifa letu kwamba kilimo ni maji na bahati mbaya sana tunapoteza maji. Mvua zinanyesha, tunalalamika hapa. Kuna jambo halijakaa sawa sawa kwenye mipango na kwenye utekelezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, twende tukatumie hii baraka ya Mwenyezi Mungu kutupa mvua kwa ajili ya faida ya uzalishaji wa mara mbili mara tatu kwa msimu tuwe sisi ndiyo ghala la chakula kama inavyoelezwa kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nilitaka kulichangia leo ni suala zima la zana za kilimo. Eneo la zana la kilimo nalo hili ni eneo muhimu sana katika kuleta mapinduzi ya kilimo hapa nchini, na nipongeze sana jitihada za Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na Wizara husika ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili ninaomba sana Jimbo la Kilindi, Wilaya ya Kilindi, lile ndiyo eneo la uzalishaji kwenye ukanda wa kaskazini likiungana na wenzake wa Kiteto. Ninaomba sana katika ule mpango wa kusambaza matrekta, *power tiller* maeneo haya yapewe kipaumbele kwa sababu ndiyo yanayolisha ukanda mzima wa kaskazini na nchi jirani ya Kenya na maeneo mengine. Ninaomba tulitumie hili eneo kuwekeza katika miundombinu au vitendea kazi kama matrekta, *power tiller* kwa wakulima wetu ili tuhakikishe kwamba tunakwenda kuongeza tija, kuongeza uzalishaji na mwisho wa siku kuinua pato la wananchi wetu na pato la Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitoe rai na nitoe ushauri kwamba pia katika eneo hili twende kwa maeneo tuangalie vipaumbele vya maeneo. Ninaomba tukubaliane, tukiamua kwenda kwa utaratibu wa kwamba hivi vitu tunatapanya, peleka huku kimoja peleka huku viwili, havitoi matokeo, hatupati tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba tukubaliane, tunaposema tunapeleka hapa, tupeleke kitu kilete matokeo, na yale matokeo yatoe tija, tuhamie sehemu nyingine. Tutafika kwenye maeneo yote, lakini kwa kwenda kwa utaratibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni suala la masoko, na hapa nilikuwa ninaomba kuzungumzia *NFRA*. Moja ya chombo ambacho kinaweza kikaleta na kikachachusha masoko ya ndani ni kupitia *NFRA*. Changamoto ya *NFRA;* mfumo wa upatikanaji wa fedha kwenye *NFRA* unabishana na masuala ya masoko kwa wakulima kule kwenye maeneo yetu. Ukipeleka fedha mwezi wa Tisa, hiyo fedha haimnufaishi mkulima. Kuna watu wamekusanya, wameweka kwenye *store* ndio wanaonufaika na fedha zile za *NFRA,* lakini mkulima ambaye amehangaika amejishughulisha na kilimo kwa miezi yote ile, anajikuta ameangukia kwenye walanguzi, amepata hela ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho wa siku unapokuja kupeleka *NFRA* fedha, zinakwenda kunufaisha watu ambao hatujakusudia. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan anakusudia kwenda kupeleka tabasamu kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa upatikanaji wa fedha za *NFRA* utazamwe, ikibidi apewe fedha mwezi wa Pili, au wa Tatu tayari kwa maandalizi. Mavuno yanaanza mwezi wa Tano na wa Sita, wawe wameshajiipanga, wahakikishe kwamba ule utaratibu tuliouweka wa kupeleka mifumo ya ukaushaji mazao tukawasaidie wakulima ili tuiwezeshe *NFRA* inunue mazao ambayo yamekaushwa vizuri, yanahifadhika, na pia kuweza kuwapa wananchi soko la uhakika na kuleta ushindani kwa wanunuzi binafsi kwa kipindi husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuchangia hayo, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Nakushukuru Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, ajiandae Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, Mheshimiwa Dkt. Ritta Enespher Kabati ajiandae.

MHE. DEODATUS P. MWANYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia kwenye bajeti hii ya Wizara ya Kilimo. Awali ya yote ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri sana aliyoitoa hapa inayotupa matumaini makubwa kwenye kilimo. Kwa kweli Wizara hii imefanya kazi kubwa na inafanya kazi kubwa kuendeleza kilimo. Mambo yanayofanyika ni mengi na tunawapongeza sana kwa kazi nzuri wanayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kuna maeneo machache ambayo niliona niyazungumze, ambayo mengi tumeyaongelea kwenye Kamati, lakini nime-*pick* machache ambayo ni muhimu kwangu na kwa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia uzalishaji wa mazao ya asili ya biashara, Wizara inafanya vizuri sana kwa ujumla, hasa kwenye uzalishaji. Masuala ya bei yana *complications* zake na bei zinapanda na kushuka, lakini kiuzalishaji, mazao mengi yanafanya vizuri sana. Ukienda kwenye korosho, inafanya vizuri sana kiuzalishaji, kahawa, mkonge unafanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaposema vizuri, ni malengo waliyojiwekea ukilinganisha na walipofikia. Kwa kiasi kikubwa, haya mazao kama korosho yapo 80%, kahawa 90%, mkonge 90%, pamba 60%, tumbaku wako 95%, hata sukari wako 70%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo yake ni kwamba kwa ujumla, amesema kwenye ripoti yake, mpango ulikuwa ni kuzalisha tani milioni 2.2 kwa ujumla kwa mazao hayo yote, lakini wameweza kufikia tani milioni 1.5. Kwa hiyo, *progress* ni nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kuna baadhi ya mazao ambayo kwa kweli ni tatizo kubwa sana. Zao ambalo linaongoza na lenye changamoto kubwa kwenye Wizara hii ni zao la chai. Zao la chai, tunavyoongelea sasa, uzalishaji wake umeendelea kuporomoka siku hadi siku. Malengo yalikuwa ni kuzalisha angalau tani 30,000, lakini mpaka Februari walikuwa tani 9,000 na ilikuwa inaonyesha wapo tani 10,000. Hali hii siyo nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwa karibu sana, utagundua kinachosababisha zao la chai kuporomoka, sababu kubwa ni viwanda kutozalisha, na viwanda kufungwa. Kuna viwanda nane ambavyo vimefungwa. Kama kiwanda kinazalisha chini ya asilimia tano ni sawa na kama kimefungwa, lakini kuna vile ambavyo vimefungwa kabisa havifunguliwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda ukaangalia viwanda vilivyofungwa, mfano Rungwe kuna viwanda kama vitatu vimefungwa. Ukija Njombe kuna viwanda vitatu vimefungwa, na Mufindi kuna viwanda viwili vimefungwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda ukaangalia zaidi vimefungwa kwa sababu gani? Cha kwanza utagundua kwamba vimefungwa kwa sababu kuna mwekezaji ambaye au hana uwezo ama hana nia ya kuendeleza zao la chai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaongea nikiwa nimeongozwa na *data* za uzalishaji wa viwanda hivyo. Ukiangalia hivi viwanda nilivyovitaja, vyote kwa pamoja, kimoja kinazalisha tani 8,000, kimoja 6,000, kimoja 2,000. Kuna uzalishaji wa viwanda

vinne au vitano vya mwekezaji mmoja ambaye ni *DL Group*, hawa peke yao wana uwezo wa kuzalisha tani 17,800.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko sana, uzalishaji wao sasa hivi ni tani 320, chini ya asilimia tatu. Sasa hili siyo jambo la kufumbia macho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Watanzania tuna jambo letu. jambo letu ni Dira. Dira inatuambia kwamba 2025 kwenda 2050, tunataka *private sector* ichangie 70% kwenye hiyo dola trilioni moja ambayo tunatakiwa tuwe nayo au tuizalishe na pato la mtu liwe dola 7,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwendo huu ambao tunakwenda kwenye viwanda, nchi yetu lazima iwe tayari kufanya maamuzi magumu. Nilikuwa ninatafuta neno zuri, "maamuzi magumu." Katika maamuzi magumu ni pamoja na kufanya *evaluation* ya aina ya uwekezaji ambao tunao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu inavutia wawekezaji, lakini tunapovutia wawekezaji kuna baadhi ya wawekezaji hawatufai. Ninalisema hili kwa sababu nimeongea ndani ya Bunge hili kwa miaka mitano pamoja na wenzangu kuhusiana na zao la chai kwenye maeneo ya Mufindi, Njombe mpaka Rungwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni kwamba tuna mwekezaji ambaye alipewa viwanda kwa nia njema na Serikali kupitia benki, lakini uwezo wake umeonesha kwamba ni mdogo kuendesha hivyo viwanda. Kama tunataka kufikia lengo letu la *private sector* kuwa ndiyo *engine* ya kutusaidia kule mbele ni lazima tuwe tayari kufanya maamuzi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2021 mwezi Machi, Mheshimiwa Majaliwa Majaliwa akiwa Waziri Mkuu alitembelea Njombe, akakaa na wadau wa chai na yaliyojitokeza yalikuwa wazi kwamba, mwekezaji huyu tunayemwongelea ambaye ni *DL Group* kutoka nchi ya mbele ya Mlima wa Kilimanjaro. Mwekezaji huyu ilionekana wazi na haya siyo maneno yangu ni maneno ya

Mheshimiwa Waziri Mkuu wa wakati ule kwamba, anatuhujumu. Ni mhujumu uchumi hapa nchini, kwa sababu hawezi kuendesha viwanda, wafanyakazi wengi kule wamepunguzwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, …

MHE. EDWIN E. SWALLE: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa Mheshimiwa Edwin Swalle.

TAARIFA

MHE. EDWIN E. SWALLE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ninataka nimpe taarifa Mheshimiwa Deo Philip Mwanyika anayechangia vizuri sana kuhusu zao la chai. Amerejea hotuba ya Waziri Mkuu Mstaafu, Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa ya tarehe 9 Machi, 2021 Njombe na mimi nilikuwepo. Waziri Mkuu alisema mwekezaji anayemiliki viwanda hivi vya Kibena, Lupembe na Luponde inaonekana kama anafanya *sabotaging* kwenye zao la chai hapa nchini. Hivyo ndiyo taarifa ambayo nilitaka nimwongezee Mheshimiwa Deo Mwanyika. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Deo Mwanyika, unaipokea taarifa hiyo?

MHE. DEODATUS P. MWANYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipokea taarifa hiyo. Ninamshukuru sana mdogo wangu Wakili Enosy Swalle. Matokeo ya jambo hili ni kwamba mapato ya Taifa, ya Serikali na halmashauri yameporomoka kwenye maeneo hayo yote, ajira zimepotea, fedha za kigeni tulizozitegemea hazipo tena, migomo ya wafanyakazi ni jambo la kawaida inaendelea, ilianza Mufindi baadaye imehamia Njombe, lakini pensheni za wafanyakazi hazilipwi na huyu mtu. Sisi tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kutambua nia nzuri ya kumwita mwekezaji, aliruhusu Wizara ifanye utaratibu wa kutafuta fedha angalau kumsaidia mwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, alipewa shilingi 10,000,000,000 siku za karibuni, mwaka jana. Pamoja na kupewa shilingi

10,000,000,000 hali bado ni mbaya, hakuna mwanga. Hizi fedha siyo fedha za kutoka huko anakotoka, hizi ni fedha za nchi yetu, za Benki yetu hapa ya *CRDB*. Kwa hiyo, niseme kwamba aina ya huu uwekezaji ni lazima tukubaliane. Ndiyo mambo aliyosema Profesa Kitila *lets try to do business unusual, let's do business unusual*. Tunataka wawekezaji ni kweli na sisi hatutaki kupeleka meseji mbaya kwa wawekezaji, lakini mwekezaji anayeturudisha nyuma, mwekezaji ambaye anarudisha umaskini kwa wananchi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, chai ni zao ambalo linaongeza ajira kwa watu wa kawaida. Chai ni zao ambalo watu wanauza, wanapata hela ya kwenda kulipa ada. Chai ni zao ambalo wanalipa hela ya matibabu. Leo hii watu hawawezi kufanya hayo mambo kwa sababu mwekezaji amefunga viwanda, hata chai yake anashindwa kuhudumia. Hawezi kuweka mbolea, hawezi kubadilisha mashine, hawezi kununua *spare*, hata umeme anashindwa kulipa. Hivi huyu mwekezaji wa aina hiyo, kwa nini Serikali isifanye maamuzi magumu ya kutatufa njia ya kuachana naye? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazo letu na wazo langu. Ni wakati sasa wa kutafuta wawekezaji wengine wa uhakika maana wapo. Wapo na tuombe sana benki ya *CRDB* itusaidie kwenye hilo, kwa sababu wao wame-*finance*, siamini kama wanaona mwanga kwenye jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huhitaji kuwa *financial* guru kujua kwamba *this is a failure business,* huhitaji, unaona namba zinajionesha wazi kabisa. Ukizalisha kwa uzalishaji huu na migomo inayoendelea deni la pensheni peke yake la wafanyakazi ni shilingi bilioni 4.7. Hata hivyo, analipa mishahara kwa kusuasua na hapeleki hata hizo pensheni bado kwa wafanyakazi. Kwa hiyo, hatuwezi kuendelea na hii hali, *we have to make a decision.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, nina matumaini makubwa kwamba analifahamu na nina uhakika sana kwamba Waziri wetu ana uwezo wa kutusukuma tukafika mahali pazuri kwenye jambo hili. Nimwombe sana

Mheshimiwa Waziri, sisi tuna matumaini makubwa naye, tunakutegemea sana kwenye jambo la chai. Bahati nzuri na yeye ni mkulima wa chai, ninayoyasema haya na yeye anayapitia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilipenda niongelee chai kwa uzito huo na niombe sana Serikali ifanye maamuzi. Wakati ninamshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia kwa kusababisha hawa wamepata pesa, lakini hizo pesa hawazitumii kama inavyotakiwa. Hata hivyo, wanafanya vizuri kwenye mazao mengi na zao la parachichi pamoja na mbogamboga, Wizara hii imelisimamia vizuri sana na linafanya vizuri sana. Tumeona hapa linakwenda vizuri, *production iko above the target* wanaongelea 108%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe sana bado kuna changamoto. Zao la parachichi ni *very delicate,* lakini linaweza lika-*transform* uchumi wa nchi hii. Unaposema ni *green gold, it's real means green gold.* Lina uwezo mkubwa wa ku-*transform* uchumi wa nchi hii na kubadilisha maisha ya wananchi wa kawaida. Niwaombe sana, kuna changamoto ndogondogo pale na ninawapongeza sana watu wa *COPRA* wamekuwa mstari wa mbele kushirikiana na wakulima kutatua changamoto, kwa hiyo, tuwatie moyo waendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwenye chai tuwaambie watu wa Bodi ya Chai wapo, kazi yao ni kusimamia zao hili. Tunapiga kelele miaka yote hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Waziri akiweza aanze na kubadilisha hiyo bodi. Hatuwezi kuwa na bodi ambayo hatuoni mwanga kwa miaka mitano. Ni vema tukatafuta watu wenye uwezo na walio na *commitment* ya kubadilisha zao la chai ambalo lina watu wa kawaida wengi sana wanaolitegemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu umwagiliaji. Tumesema hapa kwamba kwa kweli fedha zinakwenda kidogo kidogo na sisi tuombe, ukiangalia *statistics* za *success* kwa maeneo ambayo

yameshapata umwagiliaji. Niwaombe Wabunge pamoja na kwamba tuna matatizo kwenye umwagiliaji, lakini tukumbuke kwamba umwagiliaji ndiyo utakaotutoa nchi hii. Kwa *statistics* za haraka haraka, kwa kiasi ambacho tume-*invest* kwenye umwagiliaji kwa maeneo yale mpaka muda huu, tumeongeza eneo la umwagiliaji mpaka kufika hekta 800,000 kutoka hekta 400,000 mwaka 2015, lakini lengo letu ni kufika hekta milioni 1.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tija imeanza kusikika, mpunga, mahindi na vitunguu zote kwa pamoja zimeongeza uzalishaji kwa tani kwa kila hekta. Ukiangalia mpunga tulikuwa 1.5 *tons per hectare,* tupo *five* mpaka *seven.* Mahindi tulikuwa *1.5 tons per hectare* tupo *3.7* mpaka *5.0*. Nyanya tulikuwa *5.0 tons per hectare* tupo *18 tons per hectare* kwa sababu ya umwagiliaji. Vitunguu vilikuwa *13 tons* tuko *26 tons per hectare*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe sana bado tuna matumaini makubwa kwamba ni vizuri fedha zikatolewa. Tuombe kuna miradi mikubwa ambayo tunaweza kusema ni *game changer.* Miradi hii ni miradi ambayo itatusaidia sana na miradi hii, kwa vile *ceiling* yetu ya Wizara ni ndogo, tukiendelea kuiweka kwenye hiyo hatutaweza kufanikiwa, tuiweke kama miradi ya kimkakati ili tupate *financing* kutoka Serikalini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, ajiandae Mheshimiwa Dkt. Ritta Enespher Kabati.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Kabla sijaanza nikumbushie jimboni kidogo, kuna *scheme* ya umwagiliaji Mheshimiwa Waziri anaijua ya Balili, ilipata madhara ya mvua, sasa hivi imeharibika tunahitaji pesa ya dharura pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, nisisitize, mchangiaji aliyepita amezungumzia miradi ya umwagiliaji ya kimkakati. Kama

kweli tunataka tupige hatua kwenye kilimo, ile miradi 26 ambayo imezungumzwa kenye taarifa ya Kamati lazima tuifanye ya kimkakati kama ambavyo tumefanya Bwawa la Mwalimu Nyerere, kama ambavyo tumefanya *SGR* na maeneo mengine ya kimkakati, ndiyo tutatoka hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukifanya hivyo, tutakuwa na uhakika wa kutenga pesa za kutosha katika miradi ya umwagiliaji. Lazima iwe miradi ya kimkakati ili tuondokane na kilimo cha kutegemea mvua. Hilo Mheshimiwa Waziri lazima alichukue, ili ile ndoto ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kufanya kilimo, kiwe kilimo cha biashara na siyo watu waone kilimo ni mateso, waone kilimo ni starehe, kilimo pesa, kilimo mali, lazima tuwekeze katika kilimo cha umwagiliaji kwenye miradi ile 26 ya kimkakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nizungumzie zao la parachichi. Tunazungumza kila siku kwamba parachichi ni *green gold*. Parachichi duniani huko inahitajika kweli kweli na soko lake lipo wazi. Zao la parachichi halina msimu. Parachichi ukienda India, parachichi moja ya *Hass* unanunua kwa shilingi 10,000 au 15,000. Mheshimiwa Waziri anajua, bandari yetu haina miundombinu rafiki ya kusafirisha mazao ya mbogamboga na parachichi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama zao hili linailetea pesa za kigeni nchi yetu, kwa nini hatuwezi kutengeneza miundombinu katika bandari yetu? Leo hii wakulima wa parachichi wanatumia zaidi ya dola 6,500 kwenda kusafirisha kwa kulipia gari la kwenda kupeleka bandarini. Wanaenda Mombasa kwa sababu Bandari ya Mombasa kuna miundombinu mizuri kwa ajili ya kuwezesha wakulima kusafirisha matunda pamoja na mboga mboga. Tungekuwa tuna miundombinu yetu kwenye Bandari yetu ya Dar es Salaam, wakulima wangetumia dola 2,000 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa nini tusione kwamba ni wakati muafaka wa bandari yetu yenyewe iweze kujitosheleza, siyo tena wakulima wetu wa hapa wanaenda Bandari ya Tanga, kiuchumi haijakaa sawa. Yaani sisi tunaenda kunufaisha nchi

nyingine wakati tuna uwezo wa kutengeneza miundombinu yetu katika bandari yetu na wakulima wetu tukawaondolea mzigo mkubwa wa pesa kwa ajili ya lile gari la kusafirisha kwenda kupeleka parachichi bandarini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, Mheshimiwa Waziri anajua kwamba maeneo ambayo kuna mashamba ya parachichi, barabara zake ni mbovu. Zao la parachichi linahitaji uangalizi wa hali ya juu. Leo hii mkulima unaweza ukavuna parachichi *let say* tani tano au kumi, barabara ikiwa mbovu mpaka uende kwenye *park house,* unaweza ukaambiwa tani mbili zote, tani tatu zote ni parachichi ya kiwango cha pili. Unaambiwa *reject* ingawa sisi wakulima wa parachichi hatutaki suala la *reject*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa lazima Mheshimiwa Waziri, Wizara yake na Wizara ya Miundombinu kupitia kule *TARURA* kuhakikisha maeneo yote yenye mashamba ya kimkakati ya parachichi, barabara zinapitika muda wote, ili wakulima wa parachichi wawe na uhakika wakitoa zao kwenda kupeleka kwenye *park house*, basi tunda liwe na ubora. Likisafirishwa, lisafirishwe kwa kiwango kikubwa, mkulima apate pesa ya kutosha na Serikali ipate mapato. Hilo ni jambo la msingi sana na Mheshimiwa Waziri anayajua mashamba ya parachichi, kote barabara hazipitiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaenda kwenye msimu wa mwezi Agosti, ukienda kule Mgala, Kifanya na maeneo mengine Mafinga, barabara hazipitiki wakulima wa parachichi wanalalamika. Watashindwa kuvuna, wakishindwa kuvuna matunda yataoza. Parachichi ni *green gold,* wanaiacha *gold* inaoza shambani, kwa sababu miundombinu haipitiki? Hapana, lazima tuwe tuna mkakati wa kutosha. Mheshimiwa Waziri anajua dawa za kuulia wadudu za parachichi ni *very expensive,* wakulima wetu wengi hawawezi kumudu. Ni wakati muafaka sasa wa kupata ruzuku kwa ajili ya dawa za parachichi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutoe elimu kwa wakulima wetu wadogo, kwa sababu usipowapa ruzuku wanashindwa kuwahi

kupuliza dawa kwa wakati. Hawezi kupata mazao ya kutosha yenye ubora. Utakuta anakuwa na maparachichi ambayo hayana *standards* ambazo zinatakiwa kwenye soko huko duniani, lakini tukiwapa ruzuku wakulima wa parachichi, wakalima vizuri na tukatoa elimu ya kutosha kwa wakulima wadogo wadogo, ninaamini kabisa parachichi yetu itaenda mbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niwaambie kwa Afrika, Tanzania parachichi yetu ni bora sana sana na ndiyo maana kuna hila za kiuchumi ya nchi jirani hapo, kutaka kuonesha parachichi letu ni baya lakini tuna parachichi bora na linatoka Njombe, lazima kama Watanzania tupige…

MHE. ELIBARIKI I. KINGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa, Mheshimiwa Elibariki Kingu.

TAARIFA

MHE. ELIBARIKI I. KINGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mchango wa kizalendo sana unaotolewa na Mheshimiwa Bulaya, ninaomba nimpe taarifa kwamba, pamoja na kwamba anawaombea wakulima waweze kupewa ruzuku ya viuatilifu, lakini kwa sababu duniani maparachichi yanabidi yatumie mbolea ya *organic* ni wakati muafaka kwa Serikali kuingiza mbolea ya *organic* katika ruzuku ili wakulima wa Tanzania wapate *access* ya masoko duniani. Ninaomba kutoa taarifa. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ester Bulaya, unaipokea taarifa hiyo?

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipokea taarifa ya Mbunge bingwa kabisa. Kwa hiyo, kwenye parachichi Mheshimiwa Waziri amenielewa. Nimesoma hotuba yake amesema kabisa mbegu ni usalama wa nchi na amezungumzia mbegu ni chakula. Tuna Taasisi ya Serikali ya *ASA,* ninaomba waiwezeshe, inahitaji hekta 60,000 ili waweze kumaliza changamoto ya mbegu ili tusitegemee watu wanaoagiza mbegu

nje. Amezungumza vizuri kabisa mbegu yetu ya *ASA* inastahimili ukame, mazingira yetu sisi Watanzania kuliko mbegu za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii wana ardhi hekta 17,000 na kwenye hiyo hekta 3,000 tu ndiyo ina miundombinu ya umwagiliaji. Hivi tukiwawezesha hawa wakahakikisha wanalima kwa msimu mara mbili kwa mwaka, hatutakuwa na shida ya mbegu, yaani tutakuwa tuna mbegu zetu wenyewe. Watu waliotumia mbegu za *ASA* leo hii hawataki kutumia mbegu nyingine na mbegu zao ni bei rahisi, shilingi 7,000 tofauti na watu wengine ambao wanaleta mbegu zingine ambazo siyo nzuri zaidi ya 15,000. Kwa nini tusiiwezeshe taasisi yetu ya Serikali? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine Mheshimiwa Waziri tunaomba wawalipe wakulima ambao wameingia mikataba, wanalima mbegu. Hivi tunavyozungumza wanadai zaidi ya shilingi 3,000,000,000. Mkulima anakopa benki, anatakiwa ajiandae vizuri kwenda kwenye msimu mpya mpaka sasa hivi wanadai shilingi 3,000,000,000. Tunaenda kuvuna, tunaanza mwezi Juni mwishoni, Julai, mpaka kuhakikisha mbegu zimechakatwa, tunaenda mwezi Septemba, mpaka Oktoba, anatakiwa ajiandae, lakini hajalipwa bado! (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawezaje kuhakikisha tuna mbegu zetu wenyewe tunazozizalisha nchini, kama huyu mkulima nyinyi mnampa shamba, hela ya kwake na bado wanachelewa kumlipa atawezaje kuwaletea mbegu? Tumeshasema sisi wenyewe tuna uwezo wa kuzalisha mbegu bora. Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Waziri wa Fedha yupo hapa, wakulima wanadai, mbegu ni usalama wa nchi, tuna taasisi yetu wenyewe, kwa nini tusiiwezeshe tukawa na uhakika. Mbegu ni chakula, chakula ndiyo usalama wa nchi. *Why* tutegemee nje wakati tuna taasisi yetu ina mbegu ambazo zinaendana na mazingira yetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine Mheshimiwa Waziri ni kuhusiana na ushirika. Nimeambiwa wana mizani ya kidijiti, wametumia zaidi ya shilingi 15,000,000,000 kuinunua; zaidi ya mizani 4,000 na wameisambaza, ila kuna fitina kwa watu kule, viongozi wa ushirika kule hawataki, kwa sababu hii inadhibiti

kuwaibia wakulima. Ninaomba washikilie hapo hapo, wakatoe elimu, mizani hii itumike na wawaondoe vishoka kwenye vyama vya ushirika wanaowadhulumu wakulima huku. Kuna wizi mkubwa sana na ndiyo hiyo yote inaondoa sifa ya vyama vya ushirika kuonekana vibaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ile mizani wameijaribu imefanya vizuri, wale viongozi hawawezi ku-*temper* nayo, tunaomba wawaelimishe wakulima itumike ili mkulima asiibiwe…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, la msisitizo hilo nililokwambia Waziri la pamba jimboni kwangu, aliangalie kwanza, tunahitaji mabomba 1,200 kwa ajili ya kunyunyuzia wadudu kwenye wakulima wa pamba. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ninakushukuru Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Dkt. Ritta Enespher Kabati, ajiandae Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani.

MHE. DKT. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia. Ninaomba nimtangulize Mwenyezi Mungu katika mchango wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Chongolo; Naibu Waziri; Katibu Mkuu, Mr. Mweli; Naibu Makatibu Wakuu; na viongozi wote waliopo katika Wizara ya Kilimo kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya katika Wizara yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya 90% ya wananchi wa Kilolo ni wakulima, wanategemea kilimo. Hivyo niiombe Serikali sasa hizi Wizara ziweze kusomana. Niiombe Serikali kuhakikisha kwamba Wizara zetu zinasomana ili barabara zote za kiuchumi na za kilimo ziweze kupitika wakati wote, ili pembejeo ziweze kufika kwa wakati kwa wananchi, lakini vilevile, mazao yaweze kufika sokoni kwa wakati ili uchumi wetu uweze kukua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba vilevile nichangie zao la chai. Ninaungana na Mheshimiwa Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Kilimo kuhusiana na zao la chai. Kwanza ninapongeza Serikali, ilikuwa na nia nzuri kabisa hii Awamu ya Sita kuhakikisha kwamba, wanafufua viwanda vya chai, lakini bahati mbaya sana Kilolo na sisi tumepata mwekezaji, ambaye hawezi kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya miaka 30 wakulima wa zao la chai wa Kilolo walikuwa wanasubiri kwa hamu kuona sasa wanapata mkombozi wapate mwekezaji, ambaye atawasaidia, lakini bahati mbaya yule mwekezaji wa Kichina tuliyempata ni changamoto kubwa sana. Wananchi wanalia, wanasema yule mwekezaji anataka auziwe chai yao iliyochumwa kwa sindano, wakati wananchi wanachuma chai yote kwa hiyo, hawana pa kupeleka, hawana soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunategemea kwamba, soko la wakulima wa chai ni kiwanda. Mheshimiwa Waziri kwa hiyo, nakuomba, kwanza uje uwatembelee Wananchi wa Kilolo uone wewe mwenyewe jinsi yule mwekezaji anavyowatesa wananchi wa Kilolo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba, ipo *AMCOS* ambayo ina uwezo na kuna wakulima wana uwezo kuliko huyu mwekezaji ambaye yupo. Tushukuru sana ushirika unawezesha hivi vyama viweze kuendesha viwanda vyetu. Kwa hiyo, ninaomba aje Kilolo na tunaomba kiwanda cha chai ili wananchi wa Kilolo wapate soko; walikuwa wanataka hata kuondoa kabisa, ili waweze kulima kilimo kingine kwa sababu, ukiangalia waliolima parachichi wameshazungusha mara tatu, mara nne. Waliolima miti wameweza kuvuna mara tatu, mara nne, lakini wao miaka zaidi ya 30, hakuna walichopata. Kwa hiyo, ninamwomba Waziri, Mwenyekiti wetu ameongea sana, zao la chai sasa liweze kupata suluhu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua Waziri pia, amekulia katika hili zao la chai. Kwa hiyo, tunajua atakuwa suluhisho kuhakikisha sasa hili zao linawasaidia wakulima, linaleta ajira na linaleta uchumi mkubwa katika hii nchi. Atakapokuwa anahitimisha hoja

hebu sema neno moja, kwa ajili ya Kilolo waweze kupona. Tupate kiwanda kitakachowasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba vilevile nizungumze kuhusiana na ushirika kwa kweli, yapo mambo mazuri. Benki ya Ushirika pia, itawasaidia sana wakulima wetu, tunaomba iwezeshwe, wakulima wengi waende kwenye hivi vyama, waweze kukopa kwa kiasi kikubwa, ili kilimo chetu kiwe na tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapongeza vilevile tumeona wamezindua, "Linda Ushirika Chagua Uadilifu." Ninaamini kabisa vyama vyetu vingi vilikuwa vinakufa kwa sababu, kulikuwa kuna ubadhirifu mkubwa. Kwa hiyo, kutokana na hii kampeni yao tunategemea sasa vyama vingi vitafanya vizuri na vitawezeshwa, ili viweze kufanya vizuri katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaungana na wote kwamba, Tume ya Umwagiliaji ipewe pesa ya kutosha, ili miradi ya umwagiliaji ile iliyoanzishwa ikamilike iweze kuleta tija, tunaomba sana. Katika Kamati yetu tumezungumzia sana, miradi mingi imeanzishwa haikamiliki kwa hiyo, gharama ya hii miradi inakuwa kubwa sana kama haikamiliki kwa wakati. Tuombe sana Tume ya Uwekezaji ikamilishe miradi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Kilolo tumepata mradi wa shilingi bilioni 4.4 katika Kata ya Ruaha Mbuyuni, tunashukuru sana, lakini pia, tuna mradi wa shilingi bilioni 23.9. Hii miradi tuna imani sasa inakwenda kukamilika, leteni pesa ikamilike, ili wananchi wa Kilolo na sisi tuweze kutumia miradi hii kuhakikisha kwamba, kilimo chetu kinakuwa na tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie vilevile kuhusu zao la parachichi. Kwa kweli, ninapongeza sana zao hili sasa hivi ni la mkakati kupitia *COPRA,* mtendaji wake dada Irene tunamshukuru sana, ameweza kufanya vizuri sana. Sasa hivi kutakuwa kuna miche ya ruzuku kwa Mikoa ya Iringa, Mbeya, Njombe na Songwe, kwa hiyo, tunaomba sasa hii ruzuku igawiwe vizuri na ikiwezekana hata katika shule zetu sasa hivi wajifunze kuwa na hili

zao liweze kuwasaidia, ili wanapokua pia, waendelee kujua kwamba, ukitaka mali utaipata shambani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tushukuru pia kwamba, sasa hivi tutakuwa na *collection center* katika kata mbili katika Wilaya yetu ya Kilolo. Tunawashukuru sana *COPRA,* endeleeni hivyo tuhakikishe kwamba, zao hili pia linachangia uchumi wa kutosha *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba viwanda vyetu vya mbolea viwezeshwe, ili mbolea tutegemee viwanda vya ndani, sasa hivi kuwe na mpango maalum kabisa wa kupunguza gharama ya ruzuku. Tukiwa na viwanda vyetu, tukiviwezesha, tuna uhakika kabisa bei ya mbolea itashuka, kuliko kutegemea viwanda vya nje ambavyo kama kutakuwa kuna vita wananchi wanapata shida, bei inakuwa gharama kubwa, wananchi wanashindwa kujitegemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba vilevile kuwepo na mpango mkakati wa kulipa madeni ya kampuni hizi za mbolea, karibu shilingi bilioni 398 zinadaiwa. Ninajua wakiwezeshwa, wakilipwa, basi tutapata mbolea kwa wakati. Kumekuwa kuna changamoto kubwa sana, mbolea haipatikani kwa wakati, wakulima wanapata shida sana wakati wa kupanda. Kwa hiyo, ninaomba Serikali ihakikishe kwamba, mbolea inapatikana kwa wakati katika maeneo ya wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaendelea kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa ahsante kwa mchango wako. Kengele ya pili.

MHE. DKT. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninaomba Wizara ya Kilimo wapatiwe pesa kwa wakati, ili miradi iweze kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa ahsante. Nilimtaja Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani na Mheshimiwa Ahmed Shabiby, ajiandae.

MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Awali ya yote, nimshukuru sana Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa kibali hiki cha kuweza kusimama ndani ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaendelea pia kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa namna alivyoweza kufufua ushirika hapa nchini na kuimarisha vyama vya ushirika. Pia, ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na viongozi wote wa Wizara ya Kilimo. Kwa kweli, Mheshimiwa Waziri ni kiongozi wa mfano, amefanya vyema, lakini bado hujasahau maono ya mtangulizi wake. Yeye ni kiongozi wa kipekee sana. Ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri amefanya kazi kubwa. Sisi tumwahidi, Waheshimiwa Wabunge na Wajumbe wa Kamati, tutaendelea kumpa ushirikiano mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Mrajisi wa Vyama vya Ushirika, Dkt. Benson Ndiege na Tume yote ya Ushirika, wamefanya kazi kubwa sana kipindi hiki. Wamefufua vyama, wamepeleka fedha nyingi, lakini pia, wamenunua magari karibu mikoa yote na warajisi wote wana magari, kwa ajili ya kuwafikia wakulima. Kwa kweli mnyonge mnyongeni, lakini haki yake mpeni; ninaendelea kutoa pongezi kubwa sana kwa Benki yetu ya Kilimo *(TADB)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Fedha iliahidi kupeleka fedha zaidi ya shilingi bilioni 100 kila mwaka, kwa ajili ya kuongeza mtaji. Kwa Mwaka 2025 ilipeleka zaidi ya shilingi bilioni 365 moja kwa moja, kwa ajili ya mikopo. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 77.4 fedha hizi zilipelekwa kwenye vyama vya ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakwambia vyama vilivyokuwa vimekufa ikiwemo *KAP*, *CCU*, Mbogwe, pamoja na maeneo ya Simiyu ni vyama vilivyokuwa vimekatiwa tamaa, leo vinafanya kazi vizuri. Vimepeleka ushindani mkubwa, leo bei inabadilika na baadhi ya vyama vinalipa malipo ya pili. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri, aendelee kupeleka fedha kwenye Benki ya Kilimo, itakuwa mkombozi mkuu wa wakulima, itaendelea kupeleka fedha na kukuza maeneo mengine ya viwanda na kuwakopesha wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza sana Watumishi wa Benki hiyo wakiongozwa na Mkurugenzi Mkuu, ndugu yangu Frank Nyabundege, wamefanya kazi kubwa sana, wameleta mapinduzi makubwa mno katika vyama vya ushirika. Ni kweli, maono ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan hawa wanayatekeleza kwa vitendo, ninawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipo vyama vingine vya ushirika vinafanya vizuri sana katika kipindi cha Mheshimiwa Rais. Angalia pia, maeneo ya korosho kuna Chama cha Ushirika kinaitwa *TANECU,* kimejenga kiwanda na kinaendelea kujenga viwanda vingine tisa. Tuna *MAMCU,* leo wana magari makubwa nane, tuna *KNCU* wamejenga *business centre* kubwa. Haya yote ni maono ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ana haki ya kupongezwa mama wa watu, hana maneno, hana makeke, lakini ni Mheshimiwa Rais anayefanya kazi kwa vitendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, amewainua wakulima, maono ya Mwalimu Nyerere aliyoyasema kwamba, wakulima waundiwe benki yao. Leo tuna benki ya ushirika na imepelekewa mtaji zaidi ya shilingi bilioni 58 inaenda kuwahudumia wakulima na imefungua matawi maeneo mbalimbali hapa nchini, ikiwemo Tabora, kwa kutumia wakulima wa tumbaku. Kwa hiyo, ninaendelea kuomba vyama vya ushirika viendelee kuangaliwa kwa macho ya karibu, vinafanya kazi vizuri kwa sababu, ndiyo vipo karibu na watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna changamoto kubwa kwenye suala la mbolea, ninaomba na hili wali-*note* tuendelee kuongeza

na ujenzi wa viwanda hapa nchini. Mbolea tunayoitegemea ni inayotoka kwenye nchi za wenzetu, *material* ya kutengeneza mbolea ni yanayotoka kwenye nchi ambazo leo zinapigana vita; mfano, sasa hivi bei inaweza ikapanda kuliko hata mwaka jana kwa sababu ya vita. Serikali iweke bajeti nzuri ya kujenga viwanda vya mbolea viongezeke, hasa *NPK*, *Urea*, *KANI* na mbolea nyingine ambazo zinapatikana kwa wingi, ambazo wakulima wanazitumia, itatusaidia sana kupunguza gharama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba Mheshimiwa Waziri, tuna changamoto kubwa sana kwenye bei ya tumbaku na yeye mwenyewe ni shahidi. *Matrix three* ilitengenezwa mwaka huu ambayo ni wastani wa dola 1.95 na bei ya mbolea ambayo imeenda kwa wakulima ilitumia *matrix* ya mwaka jana ambayo ilikuwa na dola 2.1, ambapo mfuko mmoja wa *NPK* unapelekwa mpaka kwenye *AMCOS* dola 56.22.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiweka tozo za benki *admin storage* ambazo ziko pale mkulima anaenda kukatwa dola 63.89 wakati bei ni dola 1.95. Ni wakati wakulima hawataweza kulipa madeni yao, wakulima hawataweza kumaliza madeni benki. Ninamwomba Waziri, aliyepeleka mbolea ni *TFC* ni Kampuni ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba Mheshimiwa Waziri, wakae wapitie upya bei za pembejeo, wakae wapitie upya bei ya miji, wakae wapitie upya bei ya magunia na wakae wapitie upya bei za dawa. Mahali ambapo tunaweza kupunguza gharama, wapunguze waweze kuuza, wapate faida, warudi tena shambani. Inawezekana kweli walioweka hizi bei wakapata faida kubwa mwaka huu, lakini wakulima wasiende tena shambani msimu unaokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba Waziri suala la bei ya tumbaku na mbolea waliangalie vizuri. Mwaka jana wakati Bunge halijavunjwa, nilishauri, ikiwezekana tuanzishe Mfuko wa Kinga ya Mazao, utatusaidia sana unapofika mtikisiko wa bei. Tuna mazao ya kimkakati, ninampa mfano tu, korosho tumezalisha tani 618,000 lakini pia, tumbaku tumezalisha tani 220,000. Ukienda kwenye

pamba, zaidi ya tani 290,000 ukiziweka hizi ukaamua kutengeneza mfuko wa bei ya pembejeo, kinga ya mazao, tunaweza tukatoka hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakupa mfano wa mwisho, korosho peke yake sisi tunaogopa kuweka tozo, lakini taasisi za wenzetu, ma-*supplier* wenzetu, wanaweka tozo na wanatengeneza faida, lakini sisi tunaona kwamba, tukiweka tozo zinawaangusha wakulima. Kwenye korosho ukiweka shilingi 50 tu, tunakusanya shilingi bilioni 30 kwa mwaka mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye tumbaku ukiweka shilingi 50 unakusanya shilingi bilioni 33, lakini pia, kwenye pamba ukiweka shilingi 50 unakusanya shilingi bilioni 14, kwa mwaka tunapata shilingi 79,180,000,000 tayari hizi fedha tunazipeleka kwenye Benki ya Ushirika, zinakaa pale kusubiri mtikisiko wa bei zetu, zinakaa pale kusubiri mtikisiko wa biashara yetu ya mazao kwa miaka miwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukisema tutunze, ndani ya miaka mitano tutakuwa na zaidi ya shilingi bilioni 395. Hapa Mheshimiwa Waziri ana uwezo wa kuchukua baadhi ya fedha, anajenga kiwanda cha mbolea, atajenga kwenye Kanda ya Juu Kusini, atajenga Kanda ya Magharibi, atajenga Kanda ya Kati; tutaongeza thamani zao letu la pamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kwenye tumbaku tuna changamoto ya *cotton twine*, tuna *jute twine* ni shida, kuna *hessian cloth* ni shida. Tunazipata wapi leo nchi za wenzetu kuna vita?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungekuwa tumekusanya hizi fedha kwa mwaka mmoja, tuna uwezo wa kujenga kiwanda chetu cha kuongeza thamani, pamba tunayo tayari. Kuna vyama ambavyo vinazalisha na kununua pamba tunapeleka kwenye malighafi yetu, tunaongeza malighafi, tunatengeneza faida. Kwa hiyo, ninaomba Wizara wakae, wataalam wapo wanatosha, tena wamebobea, akina Mweli Katibu Mkuu, ninamwamini sana. Watengeneze utaratibu mzuri tuweze kupata fedha, ili tuweze

kuhakikisha kwamba, tunaongeza thamani mazao yetu, lakini pia, kuna zao Mheshimiwa analisahau sana na leo hapa nimesoma bajeti yake hajaliandika. *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa ahsante. Muda wako umekwisha.

MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakuomba dakika moja tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zao la maembe. Zao la maembe umeliacha, maembe kwa mwaka tunazalisha tani 400,000 mpaka 500,000 na 30% mpaka 40% yanapotea kwa sababu ya kukosa soko. Hebu ninaomba hili zao waliingize kwenye Mfumo wa Ushirika, liwahudumie wakulima wanaolanguliwa kwa bei ndogo, wanakosa faida. Uzalishaji kwa mwaka…

MWENYEKITI: Mheshimiwa ahsante.

MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa ahsante. Nilimtaja Mheshimiwa Ahmed Shabiby.

MHE. AHMED M. SHABIBY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuwa mmoja wa wachangiaji. Kwa vile dakika ni chache nitaongea kidogo tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kusema tu kwamba, moja ya Wizara ambazo zinategemewa kwenye nchi hii ni kilimo. Kilimo ndiyo kila kitu kwa wananchi wa Tanzania, Wafanyabiashara wa Tanzania na kwa Viongozi wa Tanzania. Ndiyo maana hata ukiangalia mzunguko wetu wa pesa, hasa dola, inakuwa *stable* wakati watu wanauza korosho, wanauza pamba, wanauza tumbaku, wanauza mazao, utakuta kila kitu kinakaa vizuri. Kama kilimo kisipokuwa vizuri, basi wajue ni matatizo makubwa sana kwenye nchi. Kwa hiyo, nchi hii inategemea sana wakulima

wadogo na siyo wakulima wakubwa. Wakulima wadogo wanategemewa sana kuliko kitu cha aina yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namna ya uwezeshaji kwa hawa wakulima wetu tunamwomba sana Mheshimiwa Waziri wetu wa sasa hivi ahakikishe kwamba, uwezeshaji kwa wakulima wadogo unakua mkubwa na ahadi kwa wakulima wadogo zinakuwepo. Ninatoa mfano, tumetoka kwenye uchaguzi mwaka jana, sisi Wabunge ambao tulikuwa humu, kwa mfano kama Gairo, kuna mabwawa ambayo niliahidiwa, Bwawa la Kibedya, Bwawa la Gairo, Bwawa la Chanjale, Visima, Kisitwi, Msingisi, Chiwe, *aah no!* Wapi panaitwa hapa, Idibo, Chakwale na sehemu nyingine, lakini hakuna hata kitu kimoja kimetekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuache, labda Waziri tunaweza tukasema ni mpya, lakini Naibu Waziri ameniona sana ofisini kwake, sana tu. Kila siku tukikutana, tukiongea na watu wa maji, utasikia hiyo bado kidogo, bado hakuna pesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaomba, kama ahadi haziwezi kutekelezeka tungekuwa tunakaa kimya maana na sisi kwenye majimbo tunaonekana waongo. Sasa hivi wanasema kwamba, wewe Mbunge kila ukija Bwawa la Malindika, bwawa lenyewe halipo. Kwa hiyo, tunaomba sana, kwa mfano hii nchi sasa hivi vyuo vya kati mpaka vyuo vikuu wanaomaliza ni watu zaidi ya 800,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeenda kuanzisha ule mpango wa *BBT,* lakini nao haujafanya vizuri. Haujafanya vizuri kwa sababu, huwezi kumchukua mtu ukammilikisha ardhi, sijui miaka 66, wakati hata katika ule mpango wa kwanza palikuwa na ekari chache, hata watu 10,000 walikuwa hawafiki wakati vyuoni wanamaliza watu 800,000. Wakimaliza watu 800,000 halafu mpango wote kwa mwaka mzima au kwa miaka miwili ni watu 10,000, kwa hiyo tulikuwa tunaleta nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa hatufanyi vitu vya maana. Tuachane na hivi vitu twende kwenye mashamba darasa, ndiyo maana tunayaita mashamba darasa na yawe kila halmashauri.

Kila halmashauri yawepo haya mashamba darasa, hizo pesa ziwe zinakwennda huko kwa sababu, kila halmashauri kuna vijana, wawe wanawezeshwa huko na wawe wanapewa kama kuna shamba la Halmashauri, basi mtu anapewa analima miaka minne, kuna mtandao kuna nini, ukitoka hapo umeshaelewa umuhimu wa kulima na nini, ondoka aje kijana mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ardhi hii haizaliwi wala haikui, ardhi tuliyonayo ni ileile. Sasa tukianza kuiwekea mipango mibaya tutakwenda kwa watu wachache halafu vijana wengine watakuwa hawajui tena umuhimu wa kilimo. Tuache hizi habari za kuanzishaanzisha, nimeona hapa kuna hii inaitwa *NAESA*. Watanzania sasa tumekuwa kiboko kwa kuanzisha hizi *agency* halafu zinagongana zenyewe kwa zenyewe kazi moja. Tuangalie halmashauri zetu, kwa maana tunaenda tunaanzisha *NAESA* haya, tumeanzisha *TARURA*, tumeanzisha maji, zote tumezitoa halmashauri, sasa halmashauri zina kazi gani? Madarasa pekee yake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tuache hivi vitu, lakini tuongeze nguvu ya usimamizi. Kuna vyama vya ushirika, kuna vitu gani, tuongeze nguvu, ili kilimo kile kiendelee kuwa vizuri. Tusipoangalia kwenye hizi *BBT* tunaanzisha vijiji vya ujamaa vya kisasa. Vijiji vya ujamaa vya zamani vilikuwa nyumba za nyasi, sasa hivi unampa mtu hekari 10 unammilikisha miaka 66, kinachotokea ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku akipata kazi *TRA* na yeye ana elimu ya chuo kikuu ataita pale mjomba, ataita shangazi, ataita nani, watajenga nyumba za bati. Kwa hiyo, watakuja kushangaa wanaanzisha vijiji vya ujamaa vya kisasa badala ya mashamba, huo ndiyo ukweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeongea, ninamshukuru sana Mheshimiwa ni msikivu na tumekubalina kwamba, tutakwenda Gairo akaangalie mabwawa. Nilichimba mabwawa binafsi saba, alikuja Naibu Waziri, wakati ule Mheshimiwa Mavunde, alinisifu sana, hata ukiangalia hapa. Nimetoa mashine za umwagiliaji zaidi ya 400 pale jimboni kwangu, leo hii wanalima, kila siku wanatoa

semi trailer tano, nne za mbogamboga na mazao mengine kwenda Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana tukapewa yale mabwawa, lakini hayo mabwawa mpaka leo hayapo. Tunaomba sana Mheshimiwa Waziri atusaidie, atupatie hayo mabwawa. Ninajua ni msikivu na Naibu Waziri wake anamnong'oneza hapo, amwambie ukweli, ninashukuru sana na ninawapongeza. *(Makofi)*

MHE. ELIBARIKI I. KINGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MHE. AHMED M. SHABIBY: Mheshimiwa Mwenyekiti, enhe! Lete Taarifa hiyo. *(Kicheko)*

MHE. ELIBARIKI I. KINGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa. Hapa, Kingu.

MHE. AHMED M. SHABIBY: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, labda niseme tu.

MHE. ELIBARIKI I. KINGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MHE. AHMED M. SHABIBY: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tulikuwa tunaomba sana hivi vitu vya…

MHE. ELIBARIKI I. KINGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa! *Of course,* ni haki yangu, *yes*.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Shabiby, endelea.

MHE. AHMED M. SHABIBY: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwa sababu, dakika ulizonipa ni chache, ninashukuru na ninaomba Wizara ya Kilimo ituangalie sana watu wa Gairo kwa sababu, hatupati mbegu za ruzuku, hatupati mbolea ya ruzuku. Inakuja kiujanjaujanja kidogo tu, pale tunatumia samadi tu. Kwa hiyo, watuangalie kwenye haya masuala ya mabwawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa, ahsante kwa mchango wako.

Waheshimiwa Wabunge, ninaomba nimtangaze mgeni mmoja wa Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Ndugu Godfrey Chongolo, ambaye ni Mkurugenzi wa Manispaa ya Kinondoni, Ndugu Hanifa Suleiman Hamza, ambaye pia ni mmliki wa Kiwanda cha Mbolea ya *Organic* inayotokana na taka ozo. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa uchangiaji wetu kwa mchana wa leo. Watakaoanza kuchangia jioni ni Mheshimiwa Bahati Keneth Ndingo, Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi, Mheshimiwa Devotha Daniel na orodha itaendelea.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, ninasitisha Shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

(Saa 7.01 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)

(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)

Mwenyekiti (Mhe. Cecilia D. Paresso) Alikalia Kiti

MWENYEKITI: Waheshimiwa, tukae.

Katibu.

NDG. MONICA MWAGA – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

(Majadiliano Yanaendelea)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na majadiliano ya hotuba ya Wizara ya Kilimo, tunaanza na

Mheshimiwa Bahati Keneth Ndingo, ajiandae Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta.

MHE. BAHATI K. NDINGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kupata fursa jioni ya leo kuwa mchangiaji wa kwanza. Nianze kwa kumshukuru sana Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kweli katika Awamu yake ya Sita, wananchi wa Mbarali tumenufaika kwa kupata miradi mingi sana ya kilimo, kwa hiyo tunashukuru sana kwa maono yake mazuri kwenye sekta hii ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri na timu yao, kwa hakika hatuna mashaka na wakulima tunayo matumaini makubwa sana na ninyi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo mambo machache ya maombi, lakini na ushauri. Nafahamu Waziri kesho atafanya hitimisho la hoja yake, atakapokuja nimwombe Wanambarali wana kiu ya kusikia. Wakati Rais amepita Mbarali aliwaahidi wakulima wa Mbarali kwamba ameshaanza mazungumzo ya mwekezaji kuachia shamba moja ili wakulima wadogo wa Mbarali, chini ya uangalizi wa Wizara ya Kilimo wapatiwe eneo lile ili waanze kufanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tulitarajia msimu huu unaokwisha, wakulima wadogo wa Mbarali waanze kufanya kazi kwenye shamba hilo. Sasa tutaomba tufahamu ni lini jambo hili litakamilika ili wakulima wadogo wa Mbarali waanze kunufaika na ahadi hii ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuishauri Wizara, tunafahamu Tume yetu ya Umwagiliaji inafanya miradi kwenye mashamba ya watu, haina mashamba ya Serikali, inaenda kwenye sehemu ya mashamba ya wananchi, ndiko ambako inafanya miradi. Watakubaliana na mimi Wabunge ambao wana miradi hii ya umwagiliaji, kumekuwa kuna ombwe kubwa la watu ambao wana fedha nyingi kwenda kuyanunua maeneo yale na kuwaacha sasa wakulima wadogo wadogo kutokuwa na maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia hata juzi, ninadhani mwezi huu nilimshuhudia Mheshimiwa Waziri akiwa Jimboni, pale kwenye Mradi wa Mbarali, Makambako, wananchi walikuwa hawautaki mradi wa umwagiliaji uende pale wakiogopa kuporwa maeneo yao. Sasa tutajikuta miradi hii mikubwa ambayo Serikali inaweka pesa nyingi itakuja kumilikiwa na watu wachache, lakini wakulima wadogo watashindwa ku-*manage* maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishauri, ninatambua Tume ya Umwagiliaji inayo *policy* ya namna ya kuangalia sehemu yote, miradi hii mikubwa inamopita, basi maeneo yale yanakuwa chini ya uangalizi wa Tume ya Umwagiliaji, vilevile kuwatambua wakulima wadogo wadogo wa maeneo yale, ili tuwalinde hawa wakulima wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano, ukienda pale Madibira lile shamba la hekta 3,253 liligawiwa kwa wakulima wadogo wadogo na Serikali imeshawekeza zaidi ya shilingi 8,000,000,000 pale na tuna miradi mingine ambayo ikikamilika ni zaidi ya shilingi 60,000,000,000 Serikali inaenda kuwekeza, lakini wale wakulima wadogo wadogo wote wameshaondolewa. Tutajikuta tunakwenda mbele na watu wachache na kundi kubwa tunaliacha nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala hili ukiangalia hata watu wa Iringa pale Pawaga, malalamiko ni hayo hayo. Wakulima wetu wadogo lazima walindwe kwa kuwekewa sheria, kwa hiyo Mheshimiwa Waziri pamoja na kwamba pale nilipokuwa Jimboni aliwasaidia wale wananchi kwa kuhakikisha wanapata hati, lakini haitoshi lazima tuhakikishe hizi *policy* zinafanya kazi ili wakulima wadogo waweze kulindwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine, ni maombi machache, tunafahamu changamoto zilizopo kwenye mfumo wetu wa stakabadhi ghalani, ni kweli hakuna jambo lolote zuri ambalo halina changamoto, lakini tusifikirie kuachana na jambo hili, ila tu tuboreshe tuhakikishe changamoto zinafanyiwa kazi. Tunayo miradi 26 ambayo imejumuisha kwenye mabonde yote ya nchi yetu, miradi ile ni miradi mikubwa na ya kimkakati. Niombe

sana Serikali itafute fedha hata nje ya bajeti ili miradi hii mikubwa iweze kukamilika tuwasaidie wakulima wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ninaomba niishauri Serikali, tuwekeze fedha za ruzuku kwenye viwanda vyetu hivi vya ndani ambavyo vinatumia malighafi za ndani kwenye mbolea. Mfano, hawa Minjingu, *INTRACOM* ili tuweze kuwasaidia na tumeona tunapopata madhara makubwa labda kama Taifa tunashindwa kuagiza vitu nje. Kwa hiyo, hawa ambao wameanza kuwekeza tujitahidi kuweka ruzuku ili kuwasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni miradi hii ya *P4R*, tunatambua kwamba miradi hii tayari imeshafanyiwa usanifu na inakwenda kuanza, sasa miradi hii huwa inapishana, Serikali inapotoa pesa. Miradi hii wakati wa mvua na shughuli za kilimo haiwezi kutekelezeka, kwa hiyo tuombe michakato yake ifanyike kwa haraka ili tuweze kuhakikisha mwezi Julai wakati wakulima wameshatoka mashambani, basi waweze kupatiwa nafasi, miradi hiyo itekeleze mpaka mvua zinapokuja msimu ujao tunakuwa tumepiga hatua kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, tunatambua, Wizara hii imebeba msingi mkubwa sana, ajira nyingi sana kwa vijana wetu na kwa Taifa letu. Niombe sana, tunasema tunakwenda kwenye uchumi jumuishi tusiache wakulima wadogo pembeni, tuwalinde wakulima wadogo, maana yake hao ndiyo kichocheo kikubwa cha uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, niombe sana, sheria ziletwe tuwalinde wakulima wadogo, hali ya kwenye miradi huko inayoendelea ya Serikali siyo nzuri, watu wananunua maeneo kwa wingi, unakuta shamba moja wapo watu wawili au watatu na tayari Serikali imewekeza *billions of moneys*. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, tunamwamini sana, kama wanavyomwamini Wanamakambako na wakulima wa Taifa hili tunamwamini sana kaka yangu Chongolo, nimwombe sana, atusaidie sana na hatuna mashaka naye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Tunakushukuru Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, wajiandae Mheshimiwa Yustina Rahhi na Mheshimiwa Devotha Daniel.

MHE. MARGARET S. SITTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwa kunipa nafasi ili nichangie hoja iliyopo mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninamshukuru Mwenyezi Mungu pia ninawashukuru wananchi wa Urambo na familia yangu kwa ushirikiano wanaonipa, lakini kipekee niishukuru Serikali inayoongozwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan na hasa kwa kutilia mkazo suala la kuinua kilimo chetu Tanzania. Suala kubwa ambalo linatusaidia sisi katika Mkoa wa Tabora kwa upande wa uchumi ni zao la tumbaku ikiwemo Wilaya ya Urambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumbaku ndiyo inatusaidia kuendeleza hali yetu ya kiuchumi na tulifurahi sana sisi watu wa Tabora tuliposikia kwamba Serikali inatambua sisi ndiyo tunaozalisha zaidi 70% ya tumbaku nchini, wakaona ni vizuri walete Kiwanda cha Mbolea katika Mkoa wa Tabora. Jambo ambalo tunaishi kwa matumaini makubwa, tunajua tutapata sasa mbolea kwa wakati. Ninamwomba Waziri pamoja na kumpongeza yeye na Naibu Waziri na watendaji wote kwa kazi yao, ninamwomba atakapokuwa anahitimisha hotuba yake atuambie je, kiwanda hiki ambacho kinasubiriwa sana na wananchi wa Mkoa wa Tabora, kitaanza kujengwa lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbolea ni ya muhimu sana, kwa mfano kama sasa hivi tayari watu wameanza kuwa na wasiwasi kama mbolea itafika mwezi Mei, unaokuja mwezi Juni kwa sababu tarehe Mosi Agosti wananchi wanaanza kupanda mbegu, wanapandikiza, tayari wameshaandaa vitalu vyao, tarehe Mosi Agosti wanaanza kuweka mbolea na kupandikiza. Je, mbolea imefika, unawahakikishiaje watu wa Tabora wanaolima tumbaku kwamba mbolea itafika kabla ya mwezi Agosti ili wapande mbegu kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huo huo nichukue nafasi hii kuwashukuru kwa kweli hawa wanaonunua tumbaku, kampuni mbalimbali zinazonunua tumbaku, wapo wanaolipa kwa wakati tunashukuru sana, lakini kwa sababu ya muda siwezi kuwataja ila tunawapongeza, lakini wapo ambao bado wakulima wanawadai. Serikali inatuambia nini kuhusu wakulima waliouza tumbaku yao mpaka sasa hawajalipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikutajie madeni waliyonayo, kwa mfano, wakulima ambao wanadai mpaka sasa ni dola 452,513, ushuru ambao unatokana na mauzo bado tunadai dola 329,218, Halmashauri yenyewe inadai 920,000,823. Serikali inatuambia nini, hawa watu watapataje fedha zao na mtu anapolima anategemea kwamba akipata ndiyo ataweza kusomesha watoto na kufanya shughuli zingine za maendeleo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la umwagiliaji na sisi kama Mkoa wa Tabora na mimi kwa upande wangu wa Urambo, tunaomba suala la umwagiliaji na sisi tupate maji ya kuweza kuanza kusaidia kupanda, kwa mfano tumbaku pale kupanda mapema, tunaomba suala la umwagiliaji na sisi lipewe umuhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo siwezi kuacha kulizungumzia ni suala la mbegu ya mahindi. Mahindi pia ni zao mojawapo kubwa sana tunalolitegemea sisi kwa chakula, lakini pia na kwa mauzo. Wananchi wananiuliza mimi huko Urambo, kwamba, hivi Serikali ilivyo na wataalam wa kilimo waliosoma kwa muda mrefu, hawawezi kuja na utaratibu wa kupata mbegu ambayo siyo lazima wanunue kila mwaka. Kila mwaka mkulima ananunua mbegu mpya, je, Serikali inaweza kutuletea utaratibu mwingine ambao mbegu itakuwa nzuri, lakini ambao siyo lazima anunue kila mwaka? Kwa msingi huo tutashukuru sana pia suala hilo atakapolizungumzia Waziri mwenyewe.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo makubwa ni hayo, kwamba kiwanda kijengwe, lakini pia tujue lini kitafunguliwa

kitaanza kujengwa, pia kama tulivyosema madai ya wakulima waliouza tumbaku yao, nitashukuru sana kupata majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimalizie jambo la mwisho, tunaomba inapoletwa mbolea tuwe tunaambiwa ni mbolea gani ambayo imepewa ruzuku, kwa sababu wakati mwingine kunakuwa na mchanganyiko, hujui ni ipi, aina gani ya mbolea ambayo imekuja labda kwa ajili ya tumbaku au mazao mengine, ipi ina ruzuku na ipi haina ruzuku. Waziri atatusaidia sana kwa sababu wakati mwingine kunakuwa na mchanganyiko ambao mtu anashindwa kujua aina ya mbolea ambayo imepewa ruzuku na ambayo haina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikifika kama ni ya ruzuku, Mheshimiwa tunaomba wawasogezee wakulima ili wapate karibu na maeneo yao, kwa sababu kipindi kilichopita kupata mbolea ya ruzuku ilibidi wengine wasafiri kwenda sehemu ya mbali na wakati mwingine hata kulala ili aweze kupata mbolea ya ruzuku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaendelea kuwapongeza Wizara kwa kazi kubwa wanayofanya, lakini tunaomba majibu ya kiwanda na mengine kama tulivyoomba kwa niaba ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Yustina Rahhi, wajiandae Mheshimiwa Devotha Daniel na Mheshimiwa Dkt. Charles Jacob Sungura.

MHE. YUSTINA A. RAHHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ya bajeti ya Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya yote ninaomba nimshukuru Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa nchi hii kwa jinsi ambavyo moyo wake uko kwenye kilimo na anachangia kilimo kwa jitihada zake zote, ndiyo maana katika zama hizi za Dkt.

Samia Suluhu Hassan mpaka yule mkulima wa chini kabisa ameona mkono wake, aidha kwa kununua pembejeo zenye ruzuku, kwa kuona miradi ya umwagiliaji. Hata sasa hivi kawasaidia wakulima kupunguza gharama za kilimo kwa kuwapelekea trekta 360 na sasa hivi zinapelekwa trekta 500, *power tiller* 200 na kufufua *Ward Resource Centres* karibu 100, hizi ni habari za Dkt. Samia Suluhu Hassan, tunamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru pia kwa kutupa Mtendaji mahiri sana, mtoto wa mkulima, Mbunge wa Makambako, Mheshimiwa Daniel Chongolo, moto alioanza nao na kukipenda kilimo na kukibeba, ninawaomba watendaji wa Wizara ya Kilimo, wampeni ushirikiano, huyo ndiye atakayetupelekea ufanisi katika Agenda ya Kilimo 2030. Ninamshukuru Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutupa kiongozi mahiri sana katika kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa kwanza ninaulekeza katika Jenga Kesho Iliyo Bora - *BBT*. Haya pia ni maono ya Dkt. Samia Suluhu Hassan akiwa na nia njema ili vijana na wanawake waweze kushiriki katika kilimo na kwa azma kubwa ya kupunguza changamoto ya upungufu wa ajira, hizi ajira milioni tatu ambazo tunazitegemea zipatikane ndani ya Wizara ya Kilimo, zingeweza kupatikana ndani ya mpango wa *BBT*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kila jambo likianza linaanza na magumu, lakini sasa tume-*refine BBT,* ndiyo utaratibu pekee utakaoweza kuwachukua wasomi vijana kujiajiri katika mpango huu. *BBT* ilitengewa shilingi 16,000,000,000 mpaka sasa hivi fedha zilizopelekwa ni shilingi 6,000,000,000. Mpango wa *BBT* kwa mfano kwenye shamba la Chinangali, wanatakiwa miundombinu yote iishe ili waweze ku-*phase out,* watoke sasa kwenye shamba hilo waende kwenye shamba lingine la Ndogoye, lakini washuke kwenye Halmashauri. Kutokukamilisha miundombinu wale vijana kule hawawezi kuendelea na mpango peke yao, ambao wanafanya vizuri wana mashamba, wako kwenye ushirika *AMCOS* na wanalima kilimo cha *contract farming,* wako vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishauri Serikali, kwanza mpango huu ushuke Halmashauri, Wakurugenzi wote watafute mashamba, na mashamba haya wayatoe kwa mpango wa kuwakodisha vijana kwa kila mwaka, wanapomaliza waombe tena, kwa sababu ukisema wapate *title deed* kama ilivyo Chinangali pengine hatuna ardhi ya kutosha, lakini *BBT* imeenda mbali, kuna *BBT* ugani ambapo vyuo vya kilimo wanawatoa Maafisa Ugani nao washuke mpaka kwenye Halmashauri, wakafundishe wale kama shamba darasa. *BBT* siyo lazima iende kwenye kilimo tu, wengine wawepo kwenye usindikaji, kwa namna hiyo, tutatoa ajira za kutosha na *BBT* itakuwa iko vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu mwingine niuelekeze kwenye pembejeo za kilimo. Msingi mkubwa wa kuongeza tija na uzalishaji katika kilimo ni kuwa na pembejeo bora kwa maana ya mbegu, mbolea pamoja na viuatilifu. Ninaipongeza *TARI*. *TARI* wamekuwa wakigundua aina mpya ya mbegu kila mara, kwa mfano kama kipindi hiki wametoa mbegu karibu aina 73 ya mbegu za mazao, lakini vilevile kwa mbegu ya asili wameweza kuchambua, kusafisha na kutunza aina 5,325.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tabia zetu za ulaji sasa hivi watu wamerudi kwenye kutaka mbegu ya asili. Ninaiomba Serikali izalishe hii mbegu ya asili kwenye daraja la kuazimia linaloitwa *QDS* na iitungie sheria ipitiwe na *TOSCI* ili mbegu hizi zipatikane kwenye maduka ya wakala, mkulima atachagua kama anataka hizi mbegu za asili azipate akitaka chotara azipate.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaongea kila siku kupambana na *GMO*, tunapozalisha mbegu zetu wenyewe ndiyo usalama uko hapa, lakini kwa mbegu za chotara ni kweli tumeongeza uzalishaji kutoka tani 79,214 mpaka tani 127,650, zaidi ya 70% tunazalisha wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado mbegu ya mahindi bei yake iko juu, kama pakiti ya kilo mbili inauzwa kwa shilingi 14,000 hadi shilingi 15,000 bado ni gharama kubwa kwa wakulima. Niiombe

Serikali iongeze bajeti na kuwasaidia wakulima wa ndani tujitosheleze kwa uzalishaji wa mbegu yetu ya mahindi huku ndani ya nchi. Tuna uwezo, tuna fursa na tuna mazingira ambayo ni *very conducive*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kusema hivyo, pengine wakulima sasa wa-*graduate* kwenye kupewa ruzuku kwenye mbegu ili hizi fedha za ruzuku ziingie kwenye kuzalisha mbegu na mbegu zipatikane kwa gharama ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mbolea, kutokana na mgogoro wa vita ulioko Marekani, Israeli na Iran sasa hivi ni wazi kwamba mbolea zitapanda bei, kwa vyovyote vile. Sasa hata kwa viwanda vinavyozalisha ndani na kuchanganya mbolea bado kuna virutubisho vitatakiwa vitoke nje kwa wenzetu wenye gesi na mafuta. Kwa hiyo Serikali iwe makini, iwasaidie waingizaji wa mbolea sasa hivi. Kama tunavyoweka mikakati kwenye upatikanaji wa mafuta, mbolea zije za kutosha, zipewe ruzuku kabla ya msimu wa mbegu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile niiombe Serikali, wale wasambazaji wa pembejeo walipwe fedha zao ambazo wamekwisha ku-*supply* ruzuku kwa njia ya pembejeo ili wakulima wasipate shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu mwingine ni kwenye umwagiliaji. Tukitaka kuongeza tija kwenye kilimo ni lazima tuachane na kilimo cha kutegemea mvua; na hapa Serikali iweke kipaumbele kwenye miradi ya umwagiliaji na iweke kipaumbele kwa kutoa fedha kwenye miradi ya umwagiliaji. Kwa mfano, kipindi kilichopita Tume ya Umwagiliaji ilikuwa imeidhinishiwa shilingi 382,138,408,000 lakini mpaka Februari walikuwa wamekwishapewa bilioni 150.6 hii ni sawasawa na 39% au 40. Sasa, kweli tutaleta mapinduzi ya kilimo kwa namna hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali, hizi fedha hata kama zinavuka mwaka Tume ya Umwagiliaji ipewe fedha ikamilishe miradi viporo. Ninaishauri wakamilishe miradi viporo kabla hawajaanzisha miradi mipya; na waende kwenye skimu za

kati na miradi midogo ili ile miradi mikubwa iingie kwenye miradi ya Taifa ya kimkakati kwa sababu fedha zote zinaweza kwenda huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumzie kuhusu ushirika. Ushirika umekuwa na historia mbalimbali katika nchi yetu; kuna wakati ushirika umefanikiwa sana. Tukiangalia Vyama vya Ushirika kama vya *KNCU*, ACU na sehemu zingine matokeo yake tunayaona. Ushirika umesaidia kusomesha, kupata makazi bora, na kupeleka pembeo. Hata hivyo kuna sehemu ushirika ulifeli na umefeli kwa sababu ya viongozi waliopewa dhamana katika chama cha ushirika husika, ambao hawakuwa waadilifu na wala hawakuwajibika. Ninaiomba Serikali iulinde ushirika kwa namna yoyote; iweke mfumo wa kidigitali katika mali za wanachama na wanachama walipewe kwa muda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushirika una rasilimali nyingi; tuna benki ya ushirika, tuna majengo tuna magari; sasa kwa nini Serikali isifikirie hata kuifanya hii ikawa kanda maalum kukaa na mfumo wa *PCCB* na Polisi humu ndani ili wananchi warudiwe na kuwa na imani na chama? Hii ni kwa sababu, salamu za wakulima wanasema mtetezi wa mkulima, ni mkulima mwenyewe na mtetezi wa mkulima, ni mkulima mwenyewe ndani ya ushirika. Kwa hiyo, ninaomba Serikali iangalie namna gani ushirika usifeli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wananchi namna pekee ya kupata masoko yaliyo bora ni kupitia mfumo wa stakabadhi ghalani, lakini mfumo huo umekuwa ukipata migogoro mara kwa mara na unapata migogoro kwa sababu elimu haijatosha kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba elimu ipelekwe kwa wakulima kuhusu namna gani mfumo huu unawasaidia kuondokana na wale walanguzi wa katikati ili mkulima akakutane na bei ile ya mwisho ya mazao yake…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa, ahsante.

MHE. YUSTINA A. RAHHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa, ahsante kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Devotha Daniel, wajiandae Mheshimiwa Dkt. Charles Jacob Sungura na Mheshimiwa Cosmas Mtesigwa Bulala.

MHE. DEVOTHA D. MBURARUGABA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi. Nichukue fursa hii kwanza kuwapongeza wafuatao: Ninampongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo anaifanya. Ameonyesha umahiri mkubwa sana, ameonyesha kwamba yeye ni mama ambaye analipeleka Taifa letu mbele. Sisi kama Waheshimiwa Wabunge tunampongeza sana. Nami binafsi nimeiona kazi yake ameonesha kwamba yeye ni kiongozi mchapakazi; tunampongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia nichukue fursa hii kuwashukuru sana wananchi wa Mkoa wa Kagera hususani wanawake, ambao waliweza kuniamini na kunipigia kura za kutosha na kunipa imani yao. Ninawaahidi kuwa nitawafanyia kazi kulingana na uwezo wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichukue fursa hii pia kukishukuru Chama Cha Mapinduzi ambacho kimeweza kuniamini na kupendekeza jina langu mpaka nikawa Mbunge Viti Maalum Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nielekeze mchango wangu kwenye sekta ya kilimo. Tunafahamu kwamba sekta ya kilimo ni sekta kubwa sana, ni sekta ambayo 70% ya Watanzania wanategemea sekta ya kilimo. Tunafahamu kabisa kwamba sekta ya kilimo inachangia 26% ya pato la Taifa letu. Hivyo ninukuu maneno ya Mheshimiwa Rais, alizungumza bayana kabisa kwamba kilimo ni biashara na mkulima ni mwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haya matamshi makubwa ambayo aliyatoa Mheshimiwa Rais inabidi tutambue kwamba *engine* itakayotupeleka kwenye Dira ya *2050* ni sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niipongeze Serikali kwa miradi mikubwa sana ambayo imeifanya kupitia viongozi wetu hawa; Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kazi kubwa ambazo wamezifanya. Tumeshuhudia miradi mingi ya umwagiliaji imeanzishwa, tumeshuhudia takribani bilioni 633.4 zimekwenda kwenye pembejeo. Hili ni jambo kubwa sana. Ninaomba tuwapongeze sana sekta ya kilimo kwa sababu wakulima wengi; tunafahamu huko tunapotoka; 70% ya Watanzania wanategemea kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kushauri yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakwenda kwenye Mkoa wa Kagera. Tunafahamu kabisa Mkoa wa Kagera ni mkoa ambao unazalisha kahawa 50% na kahawa hiyo ni aina ya *robusta* ambayo inapatikana ndani ya Mkoa wa Kagera. Zao hili linachangia pato la Taifa, tunapata fedha kupitia zao hili na inachangia fedha za kigeni ndani ya Tanzania hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze sana Bodi ya Kahawa wakiongozwa na Mkurugenzi wa Kahawa na Mwenyekiti wa Bodi kwa kazi kubwa ambayo wameifanya ndani ya Mkoa wa Kagera. Tumeona wameanzisha utaratibu wa kutoa miche kwa wananchi. Hili jambo ni kubwa sana na nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, kwa sababu wananchi wanao utayari mkubwa sana wanaonyesha jinsi ambavyo wamelipokea jambo hili. Wengi wameandaa mashamba mapya na wanakwenda kuanzisha kilimo ambacho kitaleta tija. Ningependa kushauri yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Kagera tuna wakulima wa kutosha. Wakulima wale wamejitolea wamejizatiti kupata miche ya kutosha. Nimeona wamepambana, kwamba bajeti ya kilimo inaelekeza tutakwenda kupata miche ya kahawa. Kilio changu, ninaomba hawa wakulima wapate miche ya kahawa ya

kutosha. Kwa nini ninasema hayo, Mkoa wa Kagera unategemea zao la kahawa; na tunafahamu kabisa kwamba kahawa ni moja ya zao ambalo linatumika sana duniani. Tukiwa-*support* kwa kuwapatia miche ya kutosha tutakuwa tumeinua uchumi wa Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda pia kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa sababu zao la kahawa lilikuwa lina tozo 45. Hadi sasa tunavyozungumza zao la kahawa lina tozo tano tu. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanya kazi kubwa sana kuhakikisha wakulima wanapunguziwa tozo. Sasa twende tuwapatie miche ya kutosha, tuhakikishe wanapata miche ya kutosha na tunawapa elimu jinsi ya kupanda ile miche na ukaguzi ufanyike; hapa ninamaanisha *accountability*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunavyo vitalu vya kahawa ambavyo tunaotesha ile miche, lakini bila kuwa na *accountability* ya kutosha tutakuwa tunapeleka miche hatima yake, wananchi watabaki wanalalamika hawajapata miche ya kutosha. Ninaamini bodi tuliyonayo ya kahawa ni bodi makini, ikiongozwa na mwenyekiti; na wale wote waliopo kwenye Bodi ya Kahawa wako makini sana. Tumemwona Mheshimiwa Waziri wetu wa Kilimo ni mtu mpambanaji anafanya kazi kubwa sana. Kwa hiyo, ninawaamini. Kilio changu, wananchi wa Mkoa wa Kagera wapate miche ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kwamba wananchi kwenda kwenye mstari, wanapanga kuanzia asubuhi, lakini miche haitoshi, siyo zuri. Tuhakikishe miche hii inatosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ningependa…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa muda wako umekwisha, hii ni kengele ya pili.

MHE. DEVOTHA D. MBURARUGABA: Mheshimiwa Mwenyekiti, *okay*. Ninashukuru sana na ninazidi kumpongeza Mheshimiwa

Waziri wa Kilimo, ninampongeza sana Mheshimiwa Rais achape kazi. Mheshimiwa Waziri wa Kilimo tupo pamoja naye. Ninashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa, ahsante kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Dkt. Charles Jacob Sungura, wajiandae Mheshimiwa Cosmas Mtesigwa Bulala pamoja na Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud.

MHE. DKT. CHARLES J. SUNGURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi jioni hii ili kuchangia katika Wizara hii ya Kilimo. Kwanza nitoe pongezi nyingi kwa Wizara na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo ndugu yangu Mheshimiwa Chongolo kwa wasilisho zuri. Ninaomba nianze kusema kwamba ninaunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipo hapa kwa ajili ya kuwakilisha Jimbo la Handeni. Jimbo la Handeni ni wakulima wakubwa sana wa zao la mahindi, tunalima sana mahindi na tunategemea sana mahindi katika kilimo, lakini pia katika biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wananchi wa Jimbo la Handeni wanalima tani takribani 120,000 mpaka 150,000; na kwa wastani wananchi hawa wanatoa gunia tano mpaka nane kwa hekari moja. Ukiangalia Jimbo la Handeni lina wastani wa hekta 600,000 mpaka 700,000, ambazo ndizo zinazowezekana kufanyika kilimo cha mahindi. Hata hivyo, kwa masikitiko makubwa wananchi hawa wanalima hekta 60,000 mpaka 80,000 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kwa sababu uwekezaji bado ni mdogo katika ulimaji wa mahindi Jimbo la Handeni. Takribani 85% ya vijana ndiyo wanaolima mahindi, lakini wanalima katika mazingira magumu sana. Hawana pembejeo za kutosha, hawana viuatilifu, hawana mbolea na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niiombe Wizara ihakikishe kwamba inaongeza jitihada kubwa sana kwa wananchi hawa ili waweze kulima mahindi kwa tija kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Handeni pia linaweza kustawi korosho, ufuta pamoja na mbaazi. Ninashangaa pia Wizara kwamba bado imeweka jitihada ndogo sana kuhakikisha kwamba mazao haya yanakuwa *improved* katika Jimbo la Handeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana tumepewa takribani miche 17,500 ya korosho; lakini ukifananisha na wenzetu wa Kusini wamepewa miche takribani 4,220,000 ndani ya mwaka mmoja. Kwa hiyo utaona kwamba bado uwekezaji ni mdogo sana katika Jimbo la Handeni na katika Wilaya ya Handeni na Mkoa wa Tanga kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana tumevuna tani 97.5 tu za korosho. Kwa hiyo unaona kwamba bado uwekezaji huu ni mdogo sana; na zao la korosho ni zao muhimu sana kwa wananchi wa Handeni, kwa sababu kutegemea mahindi kama zao la biashara bado haina tija sana kwa wananchi wangu wa Jimbo la Handeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia tabia ya nchi au *ecological characteristics* za Jimbo la Handeni na Mkoa wa Lindi vinafanana. Kwa mfano *PH* Jimbo la Handeni tuna *PH* ya ardhi *4.5* mpaka *6.5*, ni sawasawa na Mikoa ya Kusini. Joto ni *20-30 degree centigrade* ambazo ni sawasawa na Mikoa ya Lindi. *Altitude from sea level* kule tuna 400 hadi 700, ni sawasawa na mikoa inayolima korosho. Ukiangalia udongo navyo vinafanana, kwa hiyo sioni sababu ni kwa nini Wizara haiweki mkazo katika zao la korosho kwenye Jimbo la Handeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana Wizara hii watakapotoka hapa wanapokuja kwenye majumuisho yao waje na mkakati wa namna ya kubadilisha Jimbo la Handeni liweze kulima zao la korosho, zao la ufuta lakini pamoja na mbaazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwananchi wa Jimbo la Handeni akitaka kununua bati 30 ili ajenge kibanda chake inamlazimu lazima aandae shilingi 750,000. Fedha hizi ni lazima auze gunia 15 za mahindi, ni sawasawa na amelima eka tatu ili aweze kununua bati 30 tu za *gauge* 30. Ukimfananisha mwananchi huyu huyu wa Mikoa ya Kusini wanaolima korosho, yeye atahitaji miti 30 tu ya korosho kupata 750,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninadhani unaona ni namna gani zao hili ni muhimu sana kwa Jimbo langu la Handeni. Hii itasaidia sana wananchi wale waweze kubadilika kiuchumi kwa sababu nguvu wanazo, lakini tunahitaji tu kuwa-*boost* kidogo kutoka katika Wizara yake ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie pia upande wa machungwa. Sisi ni wakulima wazuri sana wa machungwa, lakini bado machungwa yale hayana thamani stahiki. Wanatumia sana madalali ambao wanaenda shambani watanunua shilingi nane hadi shilingi 10, lakini chungwa inapaswa kuuzwa shilingi 50 mpaka shilingi 100. Kwa hiyo niiombe Wizara kupitia taasisi ya mazao mchanganyiko *(COPRA)* watuletee *cold rooms* ili wale wananchi waweze kuhifadhi machungwa yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitamani kuona chungwa liuzwe katika msimu mmoja. Ninatamani kuona chungwa liuzwe ndani ya mwaka mzima; Januari, Februari, Machi hadi Disemba wananchi waweze kuuza machungwa yao kulingana na soko linavyoenda. Kwa hiyo niwaombe tafadhali sana Wizara watuletee *cold rooms* katika maeneo yale ya Handeni ili tuweze kuhifadhi machungwa yetu na tuyauze kwa bei nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takribani 40% ya machungwa yote yanaharibika shambani; kwa kweli ni kuwa *unfair* sana kwa wakulima hawa. Kwa hiyo, mwisho kabisa niwasisitize tena, *cold rooms* ni muhimu sana katika Jimbo la Handeni. Ikishindikana *cold rooms,* basi watuletee viwanda vya kusindika machungwa ili tuongeze thamani ya zao hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa, tunakushukuru kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Cosmas Mtesigwa Bulala na Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud ajiandae.

MHE. COSMAS M. BULALA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa fursa hii adhimu ya kuleta mchango wangu kwenye hotuba ya bajeti ya Wizara ya Kilimo iliyoletwa mbele ya Bunge letu Tukufu na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo. Nimpongeze Waziri wa Kilimo kwa bajeti nzuri yenye kuleta matumaini, lakini pia yenye kutoa dira njema kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutupatia uhai na afya njema na kutuwezesha kusimama hapa katika Bunge hili Tukufu siku hii ya leo. Pia nitumie fursa hii kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Kwimba kwa kuniamini na kunichagua kwa kura nyingi sana kuja kuwa mwakilishi wao hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuleta mapinduzi makubwa kwenye kilimo. Hii inaonyesha maana halisi kwamba kilimo ni uti wa mgongo wa Taifa letu na Mheshimiwa Rais Samia amekuwa kinara katika kuliendeleza hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2021 wakati Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan anakuwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Bajeti ya Wizara ya Kilimo ilikuwa shilingi bilioni 294, lakini leo hii miaka mitano baadaye tunazungumzia bajeti ya trilioni 1.2. Hii ni ishara kwamba Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ni daktari bingwa wa matatizo ya wakulima wa nchi hii ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa nijielekeze kushauri mambo machache katika *presentation* ya

Waziri wetu wa Kilimo ambayo ninahisi yataweza kusaidia ukuaji wa sekta yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo ni sayansi na sayansi yoyote huwa inaendeshwa na tafiti. Nitumie fursa hii kumwambia Mheshimiwa Waziri wa Kilimo tuna haja ya kuongeza bajeti yetu kwenye eneo la utafiti. Sisi kama nchi tumejiwekea malengo makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Dira yetu ya Mwaka 2050 tume-*project* kwamba kipato cha mtu mmoja mmoja kiwe dola za kimarekani 7,000. Hili ni lengo kubwa sana. Pia, Wizara ya Kilimo imesema kwamba thamani ya biashara ya kilimo au thamani ya sekta ya kilimo kufikia mwaka 2050 iwe ni shilingi 100,000,000,000. Haya ni malengo makubwa ambayo ni mara tano ya thamani ya sasa. Mheshimiwa Waziri ili tufikie malengo haya tunahitaji kuwekeza katika utafiti na hasa utafiti wa mbegu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nikisema hivi simaanishi kwamba Wizara haijatenga bajeti ya kutosha kwenye utafiti, lakini tukiangalia bajeti ya mwaka jana kwa mfano, pesa iliyowekwa kwenye utafiti ilikuwa ni chini ya asilimia moja. Hii ni kinyume na lile Azimio la Umoja wa Mataifa la Malabo linalosema kwamba ili tuondokane na umaskini tunatakiwa kuweka angalau asilimia moja ya bajeti yetu ya kilimo kwenye utafiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiacha mbegu za mahindi ambazo *ASA* ambayo ni Taasisi yetu ya Mbegu ya Serikali na wazalishaji binafsi wanazalisha kwa wingi, leo hii ukihitaji mbegu za mazao mengine, kwa mfano ukienda pale *TARI* Uyole ukataka mbegu au *TARI* Ilonga ukataka mbegu ya Mbaazi huwezi hata kupata tani 30.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ukienda hata *TARI* ya pale kwetu Ukiriguru ukawaambie wakupatie mbegu mama ya Dengu hawawezi kukupatia hata tani 20. Tulikuwa na progamu pale Kwimba, tumeanzisha programu tunaiita Ekari ya Mbunge ambapo tumegawa mbegu za Dengu tani 700 kwa kaya zaidi ya 20,000 za wananchi wa Jimbo la Kwimba. Tulipata tabu sana

kupata mbegu na matokeo yake tuliamua tu kutafuta mbegu ambazo ni *improved* tukazi-*grade* hatukuzipata kwenye Taasisi ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nitoe wito kwa Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa atuambie mkakati wake ni upi kwenye kuongeza bajeti ya utafiti hasa kwenye eneo hili la mbegu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbegu sio tu suala la kutufanya tupate tija katika uzalishaji, lakini mbegu pia ni suala la usalama wa Taifa. Mtu akitaka kucheza na sisi kwenye mambo ya usalama wa chakula anacheza na sisi kwenye mbegu. Kwa hiyo tuweke jitihada nyingi kuwekeza kwenye eneo la mbegu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri anaweza kuwa ana-*wonder* atapata wapi pesa ya kuendesha na kuongeza bajeti ya utafiti, nitoe ushauri kwa Mheshimiwa Waziri. Kuna mashirika kwenye Wizara ya Kilimo, Shirika kama *CPB (Cereal and Other Produce Board)* inafanya biashara ya mazao yaani kununua na kuuza mazao kwa wakulima. Kuna shirika kama hilo *TFC (Tanzania Fertilizer Company)*, umeweka mtaji wa shilingi bilioni 118 kwenye Kampuni ya Mbolea Tanzania, lakini leo hii ile kampuni inafanya *turnover* ya shilingi 300,000,000,000, *this is a joke!*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi kuwekeza pesa nyingi namna ile kwenye kampuni ya Serikali kwa ajili ya kufanya kazi ambayo inaweza kufanywa na sekta binafsi. Leo hii *TFC* inaenda kushindana na kampuni kama *ITRACOM, ETG* (kampuni binafsi). Kwa nini tusiache hii kazi kwa kampuni binafsi zilizowekeza mitaji yao hapa na *TFC* ifutwe. Tunaomba Waziri alete hoja kwenye Kamati yetu ya Mitaji ya Uwekezaji wa Umma na sisi tutambariki kampuni hii ifutwe, pesa hii iende kuwekezwa kwenye *TARI* tuweze kuboresha utafiti wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia niongelee eneo la umwagiliaji. Nchi yetu tumejaliwa. Eneo linalofaa kwa umwagiliaji tuna hekta milioni 29, lakini mpaka sasa tunachotumia ni chini ya asilimia tano kwenye umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kuendelea ku-*fund* miradi ya umwagiliaji kwa kutumia ukomo wa bajeti ya Wizara ya Kilimo. Ninapendekeza miradi ya umwagiliaji kwanza isiwe *social,* isiwe miradi ya kijamii, iwe ni *business undertaking*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuitafutie ufadhili nje ya bajeti ya ukomo wa bajeti ya Wizara ya Kilimo. Mheshimiwa Waziri ametuletea *presentation* hapa kwenye bajeti yaeo kwamba tuna miradi ya mabonde 26 ya umwagiliaji ambapo tayari Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imeshafanya *feasibility* na wanatafuta fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mradi mkubwa wa umwagiliaji tunaouandaa wa maji ya Ziwa Victoria na maji ya Ziwa Tanganyika. Miradi hii miwili thamani yake ni zaidi ya trilioni sita. Hatuwezi kuendelea kuipatia pesa kupitia ukomo wa bajeti ya Wizara ya Kilimo. Ninamshauri Mheshimiwa Waziri atafute namna bajeti ya umwagiliaji ijitegemee na tutafute fedha za kui-*fund* miradi hii kama tulivyotafuta fedha kwenye ku-*fund* Daraja la Kigongo - Busisi au tulivyofanya Mradi wa Mwalimu Nyerere au tulivyofanya Mradi wa *SGR*. Mheshimiwa Waziri tutafanikiwa sana na tutafikia malengo katika umwagiliaji. *(makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalize kwa kuzungumzia mifumo ya masoko ya mazao ya wakulima wetu. Ninatoka Jimbo la Kwimba. Kwenye Jimbo la Kwimba sisi ni wakulima wa mazao ya mikunde, mpunga, mahindi na alizeti. Wakati tunalima huwa hatuoni taasisi zozote zikija kwenye maeneo yetu. Huwa hatuoni *COPRA*, *TMX, AMCOS,* hatuoni zote…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa ahsante kwa mchango wako.

MHE. COSMAS M. BULALA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niombe kutoa ushauri kwa Mheshimiwa Waziri, tumeanza taasisi yetu nzuri sana ya *COPRA* ili iweze...

MWENYEKITI: Mheshimiwa muda wako umekwisha.

MHE. COSMAS M. BULALA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa ahsante kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud, wajiandae Mheshimiwa Dkt. Yahya Esmail Nawanda, Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, Mheshimiwa Ado Shaibu Ado na Mheshimiwa Livingstone Joseph Lusinde.

MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa nafasi. Kwanza kabisa ninapenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza Wizara ya Kilimo kuanzia Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa kilimo kwa juhudi mbalimbali wanazofanya katika kuhakikisha sekta hizi za kilimo zinafanya kazi kwa manufaa ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoomba kuongezewa bajeti kwenye sekta za uzalishaji ikiwemo Wizara hii ya Kilimo, tumeona mafanikio makubwa yamepatikana katika kuongeza fedha hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii imefanya mambo mengi kupitia bajeti yetu ya kilimo ikiwemo kuimarisha *TOSCI*, kuimarisha ASA na kuimarisha *TARI*. Tuna maabara za kisasa ambazo kwa sasa tutatoa ithibati ya mbegu ambazo tutaweza kupeleka mpaka nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio hayo yameongeza huduma za ugani kuwapa vitendea kazi vilivyo bora na vya kisasa pamoja na kuongezea elimu ya kutosha kukabiliana na changamoto mbalimbali za kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Wizara yetu hii ya Kilimo iendelee kuongezewa bajeti kwa maana ya kwamba yale matarajio ya Mheshimiwa Rais ili yaweze kufikiwa. Tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuliona hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ambazo zimejitokeza kwenye taasisi yetu hii ya *BBT* zitaweza kutatuliwa tu ambapo

bajeti ya kilimo itakuwa ya kutosha na inatoka kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nia ya Mheshimiwa Rais ni kuhakikisha vijana wa nchi hii wanapata ajira na kujiajiri na kupata kipato. Tukiongeza bajeti na fedha zikatoka kwa wakati mambo mbalimbali changamoto ya huduma za ugani zitaweza kutatuliwa na kuwafikia wananchi na wakulima kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea pamoja na hali nzuri ya sasa hivi kwenye kilimo imeonekana kwamba mazao ya kilimo yamezalishwa kwa wingi kwa wakulima wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajielekeza kwenye sehemu hii muhimu sana ambayo ni silaha kubwa kwa mkulima na kwa Taifa mbolea. Lazima tujihakikishie tuna mbolea ya kutosha katika maghala yetu ili changamoto hii ikijitokeza tuweze kukabiliana nayo hata kwa miaka miwili mpaka mitatu kutokana na changamoto za kidunia zilizoko hivi sasa ambazo kila mtu anazitambua ikiwemo kuwekeza viwanda vya ndani vya mbolea vidogo na vya kati kwa wananchi wazalendo wa Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini kuna wawekezaji wazalendo kwenye sekta za saruji na sekta za mabati, isiwezekane kwenye mbolea wakati malighafi zimo ndani ya nchi na tunaweza. Njia tu ya Serikali kuwawezesha hawa namna bora ya kuwapatia mitaji ikiwa kwenye mikopo kwenye benki zetu ili na wao waweze kuwekeza kwenye sekta hii ya mbolea ambazo tuweze kujitosheleza wenyewe ndani ya nchi tuwe na uhakika na usalama wa mbolea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninajielekeza kwenye umwagiliaji. Ninarudia tena kuhakikisha kuishauri Serikali uwekezaji mkubwa wa fedha kwenye sekta hizi za kilimo kutasaidia kilimo cha umwagiliaji. Yale mabwawa makubwa ya kimkakati yatafutiwe fungu maalum, fungu mahususi kwa ajili ya miradi ile mikubwa ya umwagiliaji ili tuweze kukidhi kilimo cha Mtanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea tujitahidi kulipa wakandarasi wa umwagiliaji ili ile miradi iliyosimama iweze kufunguka na tupate tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajielekeza tena kwenye mbegu za asili. Tuna mbegu zetu za asili ambazo zina virutubisho vya kutosha. Sasa hivi kuna watafiti vijana wetu wamegundua mbegu za asili, virutubisho vya asili, mbolea za asili, viuatilifu vya asili. Ni sasa Serikali iwaone hawa vijana kuwawezesha ili waweze kuzalisha kwa wingi ili mkulima aamue anatumia mbegu za aina gani na kilimo cha aina gani kikiwemo kilimo ikolojia, kilimo hai ili kuweka hali ya afya zetu kwa mazao tunayozalisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado hakuna sheria maalumu iliyowekwa kwa ajili ya mbegu hizi za asili ambazo zitatunza rasilimali hii na urithi huu wa Taifa tulioupata enzi na enzi. Tunataka mbegu za asili zipate ithibati ya kutumika rasmi ziingie kwenye mfumo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ifike wakati mkulima na mlaji aamue anakula mazao ya aina gani? Ya kupitia viwanda mambo ya hivi viuatilifu na mbolea za viwandani au mbegu za asili na uzalishaji wake wa asili kuanzia tangu kwenye udongo mpaka kufika kupata mazao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliposema kuongeza bajeti kumesaidia sana sekta hii ya kilimo. Mpaka mwezi Machi Wizara imesomesha shahada ya uzamili 43 na uzamivu 23. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri wale wataalam wetu wabobezi wa utafiti wa fani mbalimbali kwenye kilimo, maslahi yao yaangaliwe vizuri na watakapofika muda wa kustaafu wasiondoke watafutiwe njia ya kubaki ili waendelee kutusaidia. Kwa sababu inaonekana kwamba wanapomaliza muda wao wanabaki, wakibaki wanachukuliwa na nchi jirani wanakwenda kufanya utafiti wanazalisha mbegu na mbegu zile zile tunakuja kuuziwa tena ndani ya nchi. Hii ni rasilimali kubwa. Wataalam wetu wabobezi lazima tuwalinde na tuwatambue. *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Tunakushukuru kwa mchango wako.

MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaendelea kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anavyozijali na kuthamini sekta zote za uzalishaji, anavyowajali wakulima na wananchi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa ahsante kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Dkt. Yahya Esmail Nawanda.

MHE. DKT. YAHYA E. NAWANDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, lakini pia nichukue nafasi hii kumwambia kaka yangu Chongolo sasa ashike peni, nimpe elimu ya korosho kwa dakika saba, halafu niende zangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zao la korosho katika Mkoa wa Lindi na Mtwara zaidi ya 85% inazalishwa na wananchi wa Mkoa wa Lindi na Mtwara. Mikoa ya Mtwara na Lindi ina jumla ya wakulima 462,803 na jumla kuu ya wakulima wote nchi nzima ni 549,936. Hoja ya msingi inakuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mtwara na Lindi ndiyo vinara wa uzalishaji wa korosho nchini. Hoja yangu kubwa hapa leo nitachangia kuhusu bima ya afya. Chongolo kaka yangu katika jambo kubwa ambalo atatusaidia wananchi wa Mtwara na Lindi hususan wanaolima korosho na tukumbuke na zahanati zetu zote tuweke sanamu yake twende na bima ya afya kwa kila mkulima wa korosho na hesabu iko ifuatavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika zao la korosho mjengeko wa tozo kuna jumla ya fedha shilingi 469. Ushuru shilingi 59, uhifadhi wa korosho, magunia na kila kitu. Leo ninataka nijikite hapa ukisema kwa makisio ya mwaka huu 2026/2027, tunategemea

kuzalisha tani 750,000 sawa sawa na kilo milioni 750. Sasa Chongolo kaka yangu katika hizi tozo zote ambazo ni shilingi 469, hapa ninaomba tu tufanye hesabu kidogo, tutoe shilingi tano tano kwa kila mtu hapa na kwa sababu wengine hawa tumekuwa tunawachangia lakini mambo mengine wala hatuyaoni, sasa tukiamua kuchukua hizi fedha tukarudisha kuwapa bima wananchi wote wanaozalisha korosho inawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawezaje? Twende tukisema kwa makisio ya korosho kilo milioni 750 tukisema tutoe tu shilingi 15 kwenye kila kilo moja tutaenda kutengeneza jumla ya bilioni 11.25 hizi bilioni 11.25 tunaweza kuwahudumia wananchi 75,000 lakini kwenye kitita cha afya ya msingi ambacho mwananchi anaenda kulipa shilingi 150,000 hapa ukijumlisha au ukizidisha mara sita jumla ya wananchi 450,000 wanaenda kunufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukisema tunatoa tu shilingi 15 maana yake Lindi yenyewe ina jumla ya *population* ya wananchi 1,192,000. Kwa hiyo unaweza kusema tukiweza kuwapa bima ya afya wananchi 450,000 maana yake nusu ya watu wote wa Lindi wanaenda kupata huduma ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni jambo kubwa sana na hapa nimekupa mfano wa Lindi pekee yake. Kwa hiyo, tukiweka na Mtwara tukisema tuweke shilingi 20 tunaenda kuongeza na kupata fedha bilioni 15 ambayo itasaidia wakulima 100,000 tukizidisha mara sita maana yake ni 600,000. Maana yake wakulima wa Lindi na Mtwara 50% ya wananchi wote wanaenda kupata bima ya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukisema tuweke shilingi 30 tu Chongolo kaka yangu tunaenda kuongeza au tutapata bilioni 22.5, shilingi bilioni 22 ni sawasawa na wakulima 150,000, ukizidisha mara sita unaenda kupata wakulima 900,000. Wakulima 900,000 ukizidisha mara sita watu wote tunaenda kuhakikisha wananchi wa Lindi na Mtwara wanaenda kupata bima ya afya. Ukisema sasa umalize kabisa chukua shilingi 40 na huu katika mjengeko

hatuongezi hata shilingi moja kwa mkulima. Tunachofanya ni kupunguza tozo ambazo tayari tunazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiweka shilingi 40 tunaenda kupata shilingi 30,000,000,000 ambayo jumla ya wananchi 1,200,000 wanaenda kunufaika. Kwa hiyo, hapo hatujamwingilia dada yetu katika zao lake la *COPRA*, dada yetu Irene, sisi tumejikita kwenye korosho peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukienda kwa Irene dada yetu wa *COPRA* anaweza kutupa jumla ya wakulima, tukiweka kwenye hesabu hiyo kwa sababu ya *projection* yake ni kilo 98,000,000 za ufuta, pekee yake tunaenda kusaidia wakulima 58,000 wa Mkoa wa Lindi na Mtwara. Hii ni idadi kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninachomwomba Mheshimiwa Waziri aje na mkakati wa kuhakikisha sasa tuweze kuwasaidia wananchi wa Mkoa wa Lindi na Mtwara, tuwape bima ya afya bure na inawezekana ndiyo ndoto ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Hapa nimempa hesabu na inawezekana. Kwa hiyo Waziru anapokuja kwenye majumuisho aje atuambie sasa tumekubaliana tutakwenda kuendeleza jambo hili zuri la Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa wananchi wa Mkoa wa Lindi na Mtwara. Kwa kufanya hivyo atawasaidia hawa wananchi na hatutamsahau na namhakikishia tutamjengea sanamu katika zahanati zetu zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine na la msingi ambalo pia ningependa kuchangia ni kuhusu suala la korosho. Korosho tunapopeleka ghalani tumekubaliana mikoa yote inayolima korosho; minada inafanyika siku ya Ijumaa. Siku ya Ijumaa ikifanyika minada watu wote hatutaki korosho hela siku hiyo. Ijumaa sisi hatutaki fedha zetu, Jumamosi hatutaki fedha zetu, Jumapili hatutaki fedha zetu lakini Jumatatu na Jumanne tunataka fedha zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna minada ilifanyika ilichukua zaidi ya miezi miwili bila kulipa fedha. Sasa Mheshimiwa Chongolo akija hapa aje na majawabu hayo, majawabu makubwa ya

bima ya afya, lakini pia kero ya wananchi kukaa muda mrefu bila kulipwa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuseme ukweli *COPRA* inafanya kazi mzuri sana kwenye ufuta, kwenye mbaazi na kwenye mazao mengine na kwa sababu dada Irene ana miaka miwili tu, bado ni mchanga, ninafikiri baada ya miaka mitano na yeye atakuwa mbobezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa tunakushukuru kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, Mheshimiwa Ado Shaibu Ado na Mheshimiwa Livingstone Joseph Lusinde wajiandae.

MHE. JAPHET N. HASUNGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kuunga mkono hoja ya Wizara ya Kilimo. Mwaka 2003 Wakuu wa Nchi za Afrika walikutana kule Maputo, Msumbiji na wakapitisha azimio kwamba bajeti ya kilimo ifikie 10% ya bajeti za Taifa na ikawa ni azimio la nchi zote za Afrika, lakini hapo mpaka leo, hakuna nchi iliyowahi kufikisha 10% ya bajeti ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kusema, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, yeye amethubutu na amefanya vizuri. Kwa sababu bajeti sisi sote tunajua, ilikuwa ni chini ya shilingi bilioni 240, yeye ameongeza zaidi ya mara sita, karibu imefika shilingi trilioni 1.1. Kwa hiyo yeye amefanya vizuri na tuna kila sababu ya kumpongeza kwa hatua alizochukua na maono hayo makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze pia, Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote waliopo kwenye Wizara ya Kilimo kwa kazi nzuri waliyoifanya, lakini pia kwa bajeti nzuri waliyotuletea. Ninawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ambayo imefanya kazi ya kuchambua bajeti hii. Wametushauri tupitishe hii bajeti, nami ninaungana nao, tuipitishe hii bajeti ili twende tukatende sasa, tupate manufaa makubwa ya Wizara yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo kimekuwa na majina mengi, toka miaka nenda rudi. Tulianza tukaiita "kilimo ni uti wa mgongo, siasa ni kilimo, kilimo kwanza, programu ya kuendeleza kilimo", kimekuwa na majina mengi. Kwa nini kimekuwa na majina mengi? Kwa sababu ya umuhimu wa kilimo katika Taifa letu. Ndiyo maana tumekuwa na kila aina ya sera ambazo zimekuwa ziki-*promote* kilimo chetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, kwa nini iko hivyo? Iko hivyo kwa sababu, kilimo kinaajiri karibu takribani 55% ya Watanzania ambao wako kwenye kilimo. Wameajiriwa huko, wanakula maisha yao kwenye eneo hilo. Kwa hiyo, kilimo ni muhimu sana, lakini kilimo kinatoa 66% ya malighafi zote zinazotakiwa kwenye viwanda. Kwa hiyo, kilimo ni viwanda. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, la tatu, kilimo ni biashara kwa sababu fedha za kigeni zaidi ya 30%, tunapata kutoka kwenye kilimo. La nne, kilimo ni chakula, zaidi ya 100% tunapata chakula kwenye kilimo. Tanzania tunajitosheleza kwa chakula. Kilimo hiki ndiyo kinatuwezesha sisi kusema leo hapa, kwa sababu tumekula, tumeshiba kwa kazi nzuri iliyofanywa na kilimo, bila kilimo hatuwezi hata kusema. Mwaka huu pia tumeambiwa, kilimo kimechangia 24.6% kwenye pato la Taifa. Kwa hiyo kilimo ni uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kutokana na hiyo, mambo haya ni muhimu sana na kwa sababu kilimo kina umuhimu katika maendeleo ya Taifa letu, tunahitaji mambo kadhaa yafanyiwe kazi na yaendelee kufanyiwa kazi. Ninajua wameshaanza kuyafanyia kazi na wameyafanyia kazi kwa kiwango kikubwa. Hata hivyo, ninataka nikumbushe, ardhi ya kilimo imekuwa ikipungua mwaka hadi mwaka. Sasa hivi ardhi ya kilimo inavamiwa kila mahali, kwa hiyo, kuna haja ya kuja na sheria ya

kuilinda ardhi ya kilimo, ili hili ongezeko la watu lisije likamaliza ardhi, tukashindwa kupata chakula cha kututosheleza na kufanya biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, wakulima hawa wanapambana na changamoto nyingi. Ikiwemo ukame, yakiwemo magonjwa mbalimbali ya mazao yao, mafuriko, wanarudi na kuwa katika hali mbaya. Unakuta mkulima aliwekeza vizuri, lakini kutokana na hivyo, anakuja kurudi nyuma. Hivyo basi, suala la Bima ya Mazao kwa sasa hivi kwa ulimwengu wa leo, ni muhimu sana Wizara ilitilie mkazo, iendelee kutekeleza Bima ya Mazao ili mazao yetu mengi yawe na bima, tuwakinge wakulima wetu ili wasikumbane na haya majanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, wamempongeza Waziri nimesikia amesema wakulima waliosajiliwa sasa hivi ni milioni tano na kitu, lakini ninaamini ni zaidi na amesema anaendelea na usajili. Sasa ninataka kusema, ni vizuri tukaendeleza tukaweka nguvu zaidi kwenye kuwasajili wakulima, ili tuwatambue ili tuweze kuwahudumia. Kwa sababu kama hatuwajui, hatuwezi kuwahudumia ipasavyo, kwa hiyo, tuwasajili wote, tujue wako wangapi, wanatoa nini, wanafanya nini, wanachangia nini. Hiyo itatusaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la nne, iko haja sasa nchi yetu kutoka, kuuza mazao badala ya kuuza kama malighafi sasa, tuanze kuongeza thamani ya hayo mazao. Tujenge viwanda vya kuongeza mazao. Tulikuwa na *ASDP II* ile ambayo mkazo ulikuwa ni kuongeza thamani ya mazao yetu. Ni muhimu sasa hii programu tukaendelea nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, tunayo mazao yetu mengi na Tanzania ilisikika miaka ya nyuma kwamba ina mazao mengi, tulikuwa na mkonge tunaongoza, lakini sasa hivi hakuna zao ambalo Tanzania inaongoza kwa uzalishaji duniani, wala katika Afrika. Sasa ipo haja, kama korosho tunaona inalipa, tuwekeze zaidi kule, lakini kahawa inalipa, tuwekeze zaidi kule ili wananchi wengi wakalime, tukazalishe tuwe ni nchi ya mfano katika mazao.

Tuchague mazao machache, iwe ni mfano na tuweze kuzalisha kwa kiwango kikubwa na kwa tija zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wana-Songwe sisi, tunahitaji ujenzi wa Soko la Kimataifa la Mazao, ili wote wanaohitaji, waje kununua mazao. Sisi ni wakulima, ni wazalishaji wakubwa, watuletee soko pale, mambo yatakwenda vizuri. Tunahitaji kuongeza kilimo cha kahawa, tunataka watuongezee miche ya kahawai li tuongeze uzalishaji wakati huu ambapo bei zimekuwa nzuri. Wakulima wengi wanataka kwenda kulima zaidi, yaani kupanua mashamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sasa mbegu zile, ile miche ya kahawa ipatikane kwa wakati, lakini pia mbegu za mazao ya kilimo zilizo bora zipatikane, zitatusaidia sana katika kuboresha maisha yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa mbolea, upatikanaji wa madawa, upatikanaji wa mbegu kwa wakati, ni muhimu sana. Itatusaidia sana katika kuimarisha kilimo chetu. Bei ya kahawa sasa hivi na mahindi ni nzuri, lakini tunataka Mheshimiwa Waziri atakavyokuja kuhitimisha bei ya mahindi itakuwaje mwaka huu? Uzalishaji kwetu kule mwaka huu ni mkubwa kweli kweli kwenye mahindi. Tunahitaji sasa masoko, lakini pia tunataka kuwekeza zaidi kwenye mbogamboga na matunda, kwa hiyo sasa watutafutie soko ili tuweze kuuza. Tunahitaji mashamba ya umwagiliaji yaweze kutusaidia zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuongeza tija, tunahitaji mbegu zilizo bora; tunahitaji madawa yaliyo mazuri; tunahitaji mbolea zilizo nzuri. Mwaka jana katika maeneo mengi, katika baadhi ya kata, tulipata changamoto ya kupata mbolea na mbegu zisizofaa. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri, akalitazame, wakasimamieni watuletee mbegu nzuri, watuletee mbolea nzuri itatusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuhitimisha, kilimo ni ajira, kilimo ni viwanda, kilimo ni chakula, kilimo ni uchumi, kilimo ni

biashara. Uchumi wetu utapanda, utakua na utakuwa imara kwa kutegemea mchango wa sekta ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mungu akubariki na ninashukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Ado Shaibu Ado, ajiandae Mheshimiwa Livingstone Joseph Lusinde.

MHE. ADO S. ADO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa maoni yangu katika Bajeti hii ya Kilimo iliyowasilishwa na Waziri mwenye dhamana, rafiki yangu sana, Komredi Daniel Chongolo. Katika kuanzia, ninaomba mapema kabisa niwasilishe salamu ambazo wakulima wa Tunduru wamenituma nizilete kwa Waziri, Mheshimiwa Chongolo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, wamenipa ujumbe wa wakulima wa korosho kwamba pembejeo za korosho bado hazijafika Tunduru na upuliziaji katika jimbo letu unaanza mapema mwezi Mei. Kwa hiyo, wamenituma nifikishe ujumbe kwamba pembejeo zifike mapema ili uzalishaji uweze kupanda na tuweze kumudu maisha yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujumbe wa pili, walionituma Wanatunduru, wamenieleza kwamba mfumo wa stakabadhi ghalani licha ya mafanikio yake bado una changamoto kwenye malipo. Wanamwomba sana Mheshimiwa Waziri yale mambo mepesi mepesi, kwa Kiingereza tunaita *low hanging fruits*, tuyafanyie kazi. Kwa mfano mmoja, wakulima wa korosho mpaka sasa wanakumbana na tatizo la kinachoitwa *dormant accounts*. Yaani akaunti zao zikiwekewa fedha kwa sababu hawazitumii mara kwa mara, wakienda kufuata malipo yao wanaambiwa kwamba hawawezi kuyapata kwa sababu akaunti zimelala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwamini komredi Chongolo hili anaweza kulifanyia kazi kwa kuweka tu utaratibu maalum wa kwamba tunazitambua akaunti za wakulima hawa wa korosho na

tunazipa hadhi maalumu kwamba hizi hazikabiliwi na tatizo la kulala. Utapofika wakati fedha zao zimewekwa zitakatwa kama kawaida sababu wakulima hawa maskini wanasafiri kilomita nyingi, unakwenda benki unaambiwa fedha hakuna tatizo *dormant account*, nenda chama kikuu, rudi kwenye chama cha msingi, hili linawasumbua sana wakulima. Haya nikasema niyatangulize kwa sababu nimepewa ujumbe niufikishe, nami ni mjumbe na mjumbe hauwawi. Ahsante sana na ninaamini Waziri ameyachukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina michango mingine miwili katika eneo linalohusu mwelekeo wa kitaifa. Niwe mkweli kwamba leo nimesikitika sana, kwa sababu nilikuwa na matamanio kwamba mwenendo katika sekta ya kilimo uweke mazingira ambayo ndugu yetu, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo tutaweza kumpima, lakini kwa masikitiko makubwa sana hali ninayoiona sioni kama tunaweza kumpima ipasavyo Waziri wa Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayasema haya kwa makusudi ukitazama Kamati yetu ya Bunge imefanya kazi nzuri sana. Utaona kwamba bajeti iliyowasilishwa leo imeporomoka kwa asilimia saba. La pili, utaona utekelezaji wa bajeti kwa Mwaka wa Fedha uliopita 2025/2026, nao mpaka sasa mwezi Machi ni 42% tu ya utekelezaji. Hii maana yake ni nini? Mipango tunayojiwekea hatuitekelezi na hii inatoa picha mbaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, picha inayozaliwa ni kwamba Serikali ya Chama Cha Mapinduzi imeitupa sekta ya kilimo na imemtupa mkulima wa Tanzania. Hiyo ndiyo picha tunayoipata na yeyote anayewatupa wakulima wa Tanzania anacheza na mustakabali na maslahi ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo langu, kama tunakuja bungeni tunapitisha bajeti halafu hatuitekelezi, ni bora tuache kabisa katika msimu huu wa bajeti tusipitishe bajeti ya kilimo mpaka utekelezaji wa bajeti iliyopita ufanyike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kufanya hivyo zoezi la kupitisha bajeti litakuwa ni zoezi la kinadharia. Kwa hiyo, mchango wangu tunaitaka Serikali iwe *serious* katika utekelezaji wa bajeti na hasa katika utekelezaji wa miradi ya umwagiliaji, kwa sababu hatuwezi kuleta mapinduzi ya kilimo bila kuwekeza vya kutosha katika umwagiliaji. Huo ndiyo mchango wangu wa pili.

MHE. MWANTUMU M. ZODO: Mheshimiwa Mwenyekiti ninaomba nimpe Taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa Mheshimiwa. Mheshimiwa Mwantumu Zodo.

TAARIFA

MHE. MWANTUMU M. ZODO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, ninaomba nimpe Taarifa mzungumzaji, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kupitia Wizara yake kwa kuliona hilo, kuwa nchi haiwezi kusonga mbele kwenye kilimo bila miradi ya umwagiliaji, licha ya kuwa amepeleka pesa kwenye miradi, lakini amenunua magari 26 kwa ajili ya kuchimba visima ili ku-*support* miradi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninavyozungumza hapa magari yapo *site*, yameshatoka Mkoa wa Dodoma na sasa hivi yamehamia mkoa mwingine na yatazunguka nchi nzima licha ya kuwa miradi ya umwagiliaji ipo lakini na magari yanaendelea ku-*support*. Ninakushukuru. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ado unaipokea Taarifa hiyo?

MHE. ADO S. ADO: Mheshimiwa Mwenyekiti, siipokei taarifa hiyo. Siipokei ndyio maana nilitanguliza shukurani kwa Kamati yetu ya Viwanda, Biashara na Kilimo. Taarifa kwenye Kamati inaonyesha kwamba miradi zaidi ya 50 ya umwagiliaji ambayo ilipangwa kuanza haikuanza kabisa. Miradi mingine ambayo ilianza inachechemea na haya ninayoyasema yapo jimboni kwangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mradi mkubwa wa umwagiliaji wa skimu ya Nambarapi mpaka sasa unachechemea ilibidi mwezi Januari uwe umekamilika. Kwa hiyo, haya tunayoyazungumza tunayazungumza kwa ajili ya mapenzi kwa Taifa letu kwamba, Serikali iwe *serious* kwenye utekelezaji wa bajeti. Huo ndiyo mchango wangu wa pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wa tatu na wa mwisho, Serikali imefanya vizuri sana kubadilisha sera yake kutoka sera ya zamani ya kuingilia fedha za kwenye Mifuko Maalum ya Uendelezaji wa Mazao, kwenye korosho tuna *export levy*.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Muda wako umekwisha Mheshimiwa. Nilimtaja Mheshimiwa Livingstone Joseph Lusinde, ajiandae Mheshimiwa Jacqueline Chrisant Mzindakaya.

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nitoe mchango wangu kwa Wizara hii ya Kilimo. Wabunge wengi wamempongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kumteua Mheshimiwa Chongolo na Naibu Waziri pamoja na Katibu Mkuu na watendaji wote akiwemo Mtendaji Mkuu wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji, tunawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuna mashaka na Waziri wa Wizara ya Kilimo. Hatuna mashaka naye, kwanza ni kada asiyetiliwa shaka, lakini pili amekuwa Katibu Mkuu wa chama chetu. Katika majimbo mengi ya wabunge mlioko hapa, Mheshimiwa Chongolo amepita. Kwa hiyo, mengi tunayomwambia hapa Mheshimiwa Chongolo anayajua kwa kuyaona kwa macho. Hatuna shaka naye kwamba atakwenda kuyashughulikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika vitu ambavyo mimi ninawakubali sana, wenzetu Waislamu wanasema Mwenyezi Mungu ndiye anayetoa neema ndogo na neema kubwa, lakini leo mdogo wangu hapa anasema ikiwa neema ndogo bora

tuache kabisa isitolewe. Kitu cha ajabu sana kuwahi kukisikia. Anasema kama bajeti yenyewe ni kidogo hivi basi bora tuache kabisa. Ikitokea hivyo basi ni hatari kubwa sana hata kwenye *level* ya familia, kwamba umepeleka leo ugali maharage halafu mkeo anasema leo hatupokei kabisa tunalala na njaa. Hapana! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazo changamoto kwenye kilimo lakini tuna uhakika kwamba utatuzi wake na majawabu yatatoka kwenye Serikali ya Chama Cha Mapinduzi. Tuna uhakika majibu Mheshimiwa Chongolo na mwenzake wanayo, waendelee kutatua changamoto zinazotukabili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wengi wanazungumzia kuhusu miradi ya kilimo. Mimi hapa ni mnufaika wa *BBT*. Hilo shamba linalotajwa Ndogowe lipo kwenye jimbo langu, Jimbo la Mvumi. Ninapenda nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, nimeona sasa hata vijana wengine wameanza kuhamasika kwenye kilimo. Majuzi nilikuwa ninatembelea pale nimekuwa shamba kama eka 500 hivi, analima huyu kijana Msanii anaitwa Masanja Mkandamizaji. Hiyo imeamsha ari ya vijana wengi wa maeneo yale kuanza kuchangamkia kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumwombe tuendelee kutenga heka za kutosha kwa ajili ya wanakijiji chenyewe cha Ndogowe, wanakijiji wenyewe wa Mlazo na Kata nzima ya Ng'hambaku waweze kushiriki na kupata joto la maendeleo kwenye eneo lile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoitaka Wizara ya Fedha ipeleke fedha kwenye Wizara ya Kilimo, tunafahamu kwamba Wizara ya Fedha inapeleka pesa kwenye maeneo mengi ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge. Mvua nyingi tumepata tunamshukuru Mungu lakini barabara nyingi zimeharibika, ni Wizara ya Fedha hiyo inatakiwa kupeleka, lakini tunaomba mgawanyo wa hicho kidogo kinachopatikana walau usaidie kusukuma mbele Wizara ya Kilimo ili kuweza kutekeleza miradi yake mikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana Waheshimiwa Wabunge nami hapa tunashauri kwamba, ile miradi mikubwa ya kimkakati itafutiwe pesa nje ya bajeti ya Serikali. Ziende zitafutwe fedha kama zilizotafutwa za kujenga *SGR,* kama zilizotafutwa za kujenga Bwawa la Mwalimu Nyerere. Zitafutwe fedha kwa mkakati mahususi kwa ajili ya kukamilisha miradi mikubwa ya umwagiliaji ili bajeti iliyopo isukume mabwawa madogo madogo yaliyopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Mkoa wa Dodoma hatuna mto unaotiririsha maji mwaka mzima. Kwa hiyo, sisi tunapozungumzia kilimo cha umwagiliaji kwetu sisi hakitawezekana kama hatuna mabwawa ya kumwagilia maana mito yetu inakauka yote kwa haraka. Kwa hiyo, tunamsihi sana Mheshimiwa Waziri, ajitahidi kadri inavyowezekana tutafute fedha zisukume miradi mikubwa ili hii miradi midogo itengenezwe na bajeti iliyopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ninataka nizungumzie kuhusu Stakabadhi Ghalani. Stakabadhi Ghalani kuna maeneo ambayo wenzetu wameanza muda mrefu na sisi sasa hivi wametugusa. Siyo jambo baya, lakini tunaomba ugusaji wetu uwe tofauti na maeneo mengine. Kwa mfano, kwanza hatujawekeza kiasi kikubwa sana kwa wakulima wa ufuta, kwa wakulima wa mazao yanayoingizwa kwenye ghala. Kuna watu wamewakopesha pesa wakulima ili walime, hasa kwenye ukanda ule wa Tarafa ya Mpwayungu, Tarafa ya Makang'wa na kidogo Tarafa ya Mvumi. Sasa ninashauri nini Mheshimiwa Waziri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri wale waliowekeza hela zao kwa wakulima wanunue wao kama wakulima wanapenda kuwauzia *cash*, halafu wale wakishanunua waweke kwenye ghala. Wakiweka kwenye ghala wakati wa kuja kuuza, wakulima waalikwe ili waone namna wanavyopunjwa ili mwakani wakulima wasikubali tena kumuuzia mtu. Mbona hili jambo ni rahisi sana? Wala hatuna haja ya kugombana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tuwaombe wananchi wawe watulivu, wale wale wanaonunua kama wanayo *cash*

wakanunue, lakini wale wanunuaji waingize kwenye ghala. Wakishaingiza kwenye ghala wakati wa minada, wakulima waalikwe waje waone namna wanavyopunjwa kwa kuwauzia wale. Matokeo yake yataonekana ndani ya mwaka, wala huhitaji kutumia nguvu, utamwona mkulima mwenyewe tu anaingiza kwenye ghala. Kwa hiyo, wakati mwingine tutumie hesabu kidogo tu kumaliza utata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, imezungumzwa hapa kuhusu mbolea. Tumeona *disaster* zilizotokea duniani, mipaka inafungwa, hebu tuimarishe viwanda vyetu vya ndani. Waheshimiwa Wabunge wamesema kwa uchungu sana na hili ninataka niishauri Serikali, viwanda kama *ITRACOM* hiki cha Dodoma, tuviwekee pale nguvu zetu kubwa ili viwanda vizalishe, mbolea yake inunuliwe ili itusaidie. Pale tuna Minjingu, utafiti umeshafanywa. Tatizo letu kubwa ni kwamba hatutaki kuthamini vilivyo vyetu, tuelimishane ndugu zangu, tutumie vitu vya nyumbani kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, imezungumzwa sana hapa na Waheshimiwa Wabunge na ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri, tujitahidi sana. Tunapozungumza habari ya kilimo bora cha biashara tunazungumzia mbegu. Watafiti wetu wa *TARI* na taasisi zingine zote wanajitahidi sana kwenye kugundua mbegu na kuzisimamia lakini tatizo hatuwapi nguvu za kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua kama kuna Wizara ina mipango, ninataka nimwambie *Comrade* Chongolo Wizara yako ina mipango safi kabisa. Ina mipango ya kutosha na kila kitengo kimejipanga vizuri, tuwawezeshe nguvu ili wafanye kazi. Tunapozungumzia mbegu bora kuna watu wengine wajanja nao wanaingiza mbegu feki. Nchi yetu ina wajanja wengi. Hivi vitengo tuviwekee nguvu ili vikusanye mbegu feki zikamatwe na hatua kali zichukuliwe kwa wanaoingiza mbegu feki kwa ajili ya wakulima wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakusihi sana, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji nimeigusa, nimegusa viwanda vya ndani viongezewe

nguvu. Tunataka tumhakikishie Mheshimiwa Waziri asife moyo hili suala la *BBT,* suala la kuinua vijana sasa hivi kuna vijana wasomi wameingizwa kwenye pamba, tumeona namna ambavyo wamelisisimua zao la pamba. Tumewaona wengine wameingia kulima zabibu, wengine wanalima alizeti, wengine wanataka kufungua viwanda vya mafuta ya alizeti. Tuwekeze nguvu za kutosha ili vijana wetu sasa wajikite kwenye kilimo ambacho kitawapa faida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa lililoshiba hata namna yao ya kuwaza ni tofauti. Vijana hawatawaza mambo ya hovyo, watawaza mambo ya maendeleo. Twende tufanye mabadiliko watu wakipende kilimo. Waimbaji wetu, vijana wasanii waimbe kuhusu kilimo, nyimbo za mapenzi zimeshatosha, sasa hivi tunataka tuone uhamasishaji wa kilimo kutoka kwa wasanii wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ninakushukuru Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Jacqueline Mzindakaya, Mheshimiwa Mwantumu Mzamilu Zodo na Mheshimiwa Jacqueline Kaiza Andrew wajiandae.

MHE. JACQUELINE C. MZINDAKAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa fursa hii. Awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, aliyetuwezesha kufika hapa siku ya leo. Kipekee ninamshukuru Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuzidi kuwekeza katika sekta ya kilimo. Pia, kipekee ninaomba nimshukuru Waziri wa Kilimo na Naibu Waziri wa Kilimo kwa kazi kubwa ambayo wanaendelea kuifanya ili kutimiza maono ya Serikali ya Awamu ya Sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoka katika Mkoa wa Rukwa ambao kitovu cha uchumi wake ni kilimo. Mkoa wetu wa Rukwa una mchango katika uzalishaji wa mazao ya chakula kwa kiwango kikubwa na katika takwimu za mwaka jana, Mkoa wa

Rukwa ulikuwa ni mkoa wa pili katika mchango kitaifa katika uzalishaji wa mazao ya chakula ikiwemo mahindi, mpunga, ulezi na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaomba nijikite katika mchango wangu. Kwanza kabisa ninaipongeza Serikali kwa kuendelea kutoa ruzuku katika pembejeo za kilimo. Vilevile, ninaomba pia niipongeze Serikali kwa kuendelea kununua mazao kutoka kwa wakulima kupitia *NFRA*. Ninakwenda kutoa ushauri ama ombi langu hususan katika Mkoa wangu wa Rukwa. Uzalishaji katika Mkoa wetu wa Rukwa ni mkubwa sana hivyo kiwango ambacho Serikali wanachukua mazao kwa wakulima wa Mkoa wa Rukwa bado hakikidhi uhitaji na kupelekea wakulima wengi kubaki na mazao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaishauri Serikali yetu sikivu ili iweze sasa kuongeza wigo wa masoko kwa kutujengea masoko ya mazao katika Mkoa wetu wa Rukwa na Tanzania nzima kwa ujumla wake. Vilevile, tunaomba pia mipaka iendelee kufunguliwa ili wakulima wetu waweze kupata sehemu ya uhakika wa masoko ya kuuza mazao yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi, ninaomba pia niipongeze sana Serikali kwa kuendelea kujali kwa kutoa elimu ya kilimo kupitia Maafisa Ugani ili kuweza kuleta kilimo chenye tija. Kwa mkoa wetu wa Rukwa tuna upungufu wa Maafisa Ugani kwa 42%. Hivyo basi, ninaiomba pia Serikali yetu sikivu iweze kuhakikisha tunapata ongezeko la Maafisa Ugani hao ili waweze kufika maeneo yote na kwenda kutoa elimu ya kilimo ili hatimaye tukawe na kilimo chenye tija kwa kuwapa elimu bora wakulima wetu wa Mkoa wa Rukwa ili na uzalishaji uweze kuongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na hilo, ninaomba pia nichangie kupitia skimu za umwagiliaji. Tunaishukuru Serikali kwa kuelekeza pesa Mkoa wetu wa Rukwa kwa ajili ya kujenga skimu za umwagiliaji. Kuhusu skimu hizo za umwagiliaji, ninashauri kabla ya kuleta skimu mpya za umwagiliaji, tukamalize kwanza skimu ambazo hazijakamilika zikiwemo Skimu za Umwagiliaji za Singiwe,

Sakalilo, Katongolo, Katuka na Ng'ongo. Kwa hiyo, tunaomba kukamilishwa kwa skimu hizo ili wakulima wa Rukwa wapate uhakika wa kuwa na kilimo endelevu na chenye tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia niongeze kwa kusema tunaipongeza pia Serikali kwa kuthamini kupitia ruzuku, lakini ruzuku zinatolewa tu katika pembejeo. Tunaomba ruzuku itolewe pia katika viuatilifu ambavyo ni dawa za wadudu. Mara kadhaa tunaona wakulima wanapata changamoto ya bei ambazo siyo rafiki katika viuatilifu. Kwa hiyo, tunaomba pia Serikali ielekeze kiwango cha ruzuku katika viuatilifu ili wakulima hao wawe na uhakika wa kupata dawa za kukabiliana na wadudu wanaovamia mazao na kupunguza uzalishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho na la muhimu ni Programu ya *BBT* ambayo nimemsikia katika bajeti Mheshimiwa Waziri amezungumza, ambayo inawezesha wanawake na vijana katika kujinyanyua katika kilimo. Mkoa wetu wa Rukwa una maeneo makubwa lakini mpaka hivi leo tunakosa programu hiyo ambayo itakwenda kumnyanyua mwanamke wa Rukwa, itakwenda kumnyanyua kijana wa Rukwa kiuchumi kupitia kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaiomba Serikali yetu kupitia bajeti hii, katika hiyo Programu ya *BBT*, Mkoa wetu wa Rukwa nao uwepo miongoni mwa mikoa ambayo itakapelekewa programu hiyo. Vijana wetu wawezeshwe elimu, wawezeshwe pesa ili waweze kujikita katika kilimo endelevu ambacho kitatunyanyua katika kipato cha mtu mmoja mmoja kwa Wanarukwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo ninaunga mkono hoja kwa asilimia zote. Ninaomba nimalizie kwa falsafa ya Baba yetu wa Taifa aliyesema kilimo ni uti wa mgongo kwa sababu ndiyo msingi wa maendeleo ya uchumi na maendeleo ya jamii ya nchi yetu ya Tanzania. Hivyo basi, tupitishe bajeti hii na tuendelee kujikita katika kunyanyua sekta ya kilimo. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Ninakushukuru Mheshimiwa kwa mchango wako. Sasa ninamwita Mheshimiwa Mwantumu Mzamilu Zodo, Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga na Mheshimiwa Japhael Masanja Lufungija wajiandae.

MHE. MWANTUMU M. ZODO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi jioni hii ya leo. Kwanza kabisa ninaomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama hapa jioni ya leo. Pia, ninaomba nimshukuru Rais wangu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambaye ni Mwenyekiti wetu wa Chama Cha Mapinduzi Taifa kwa kupitisha jina langu na hatimaye kuwa Mbunge. Kwa hiyo, ninaomba nimshukuru sana Dkt. Samia Suluhu Hassan pamoja na Wajumbe wote wa Kamati Kuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukrani hizo sasa, ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa dhamira yake ya dhati ya kutaka kuona kuwa sekta yetu ya kilimo inaendelea kusonga mbele. Dhamira hii ya dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan inajidhihirisha kupitia bajeti za kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa kipindi cha bajeti ya 2021 bajeti yetu ya kilimo ilikuwa ni shilingi bilioni 294, lakini kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025, wakati wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, bajeti hii tumeona imeongezeka kutoka zaidi ya shilingi bilioni 200 mpaka shilingi trilioni 1.2 na ushee. Hii ni wazi kuwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ana dhamira ya dhati ya kutaka kuwakomboa wananchi kwenye kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitampongeza Waziri wetu wa Kilimo, ndugu yangu Mheshimiwa Chongolo. Wote tunamfahamu Mheshimiwa Chongolo ni mchapa kazi na ni mtu rahimu. Tunamfahamu ameongea sana hapa Kibajaji, alikuwa Katibu wetu wa Chama Taifa. Hii miradi hapa tunayoililia na mingine tunayoipigania yeye anaifahamu yote, kwa hiyo nimefurahi sana kuwekwa kwenye Wizara hii kwa sababu atakwenda kuisimamia vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata wakati Waziri Mkuu anahitimisha bajeti yake, Mheshimiwa Chongolo alisimama hapa akaongea. Kati ya mambo aliyoongea jambo mojawapo lililonifurahisha ni lile alilosema kuwa anakwenda kuweka nguvu kwenye uzalishaji wa mbegu na anakwenda kuziongezea zile taasisi bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kuweka nguvu kwenye uzalishaji wa mbegu, hii bajeti yote na hizi jitihada za Mheshimiwa Rais zitakuwa ni kazi bure. Kwa sababu kipindi cha nyuma wakati wa 2021 uzalishaji wa mbegu ulikuwa ni takriban tani 30,167 lakini kipindi cha Mwaka wa Fedha 2025/2026 ambacho na Mheshimiwa Chongolo ndiyo amekuwa Waziri, wameanza kutekeleza hiyo bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi hiki ambacho sisi tumekuwa hapa uzalishaji wa mbegu umeongezeka kutoka tani 30,000 mpaka tani 54,000. Kati ya hizo tani 54,000, tani 47,000 zinazalishwa na sekta binafsi na tani 7,000 zinazalishwa na taasisi yetu ya mbegu ya *ASA*. Tafsiri yake ni nini? Tafsiri yake ni kuwaongezea nguvu hawa wazalishaji binafsi wa mbegu ili tuweze kusogea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kuwapa nguvu hatuwezi kupata uhakika wa mbegu. Ninamwomba kaka yangu, Mheshimiwa Chongolo tunaweka nguvu kwenye uzalishaji. Nilimsikia hapa asubuhi amesema kuhusu miundombinu. Kuna baadhi ya mashamba yana miundombinu, lakini mengi hayana. Twende tukaboreshe miundombinu kwenye mashamba yetu ya mbegu ili yaweze kuzalisha mbegu mwaka mzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusipoboresha miundombinu wakulima watategemea mvua, mashamba ya mbegu yatategemea mvua, mvua isiponyesha mashamba ya mbegu hayatazalisha, wakulima hawatakuwa na mbegu. Ninaomba twende pia tukaweke nguvu kwenye miundombinu, tukaongeze spidi kwenye miundombinu ya haya mashamba. Wakati huo tunapambana na miradi hii ya umwagiliaji kwenye majimbo yetu,

lakini tuyaangalie na mashamba haya ya mbegu kuendelea kuweka miundombinu ili tupate uhakika wa mbegu bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la mbegu ni tatizo kubwa. Nilishuhudia mwaka huu 2026 ambao wakulima ndiyo wanasubiri kuvuna hapa Dodoma, Kata ya Itiso kwa kaka yangu Deo, wakulima walipanda mbegu zao za alizeti, walikuwa wamenunua kwa mdau mmoja Manyara, mbegu zile hazikuota zote. Walirudia kupanda tena mara ya pili. Hata akitaka idadi ya wakulima wale, wenye uwezo walirudia kupanda, ambao hawana uwezo hawakurudia, kwa hiyo wakulima walipata hasara. Kwa hiyo, sina mashaka na Waziri na nilipata nguvu sana baada ya kusikia anakwenda kuweka nguvu kwenye uzalishaji wa mbegu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri akienda kuweka nguvu kwenye eneo hili dhamira ya Mheshimiwa Rais itafikia malengo, lakini bila kuwa na mbegu za uhakika hatutakuwa na mazao ya uhakika na ziada ya chakula. Wakulima wetu wanategemea ziada ya chakula kama kipato chao. Wanalima ili kupata chakula, lakini wanalima ili kufanya biashara wapate pesa. Kwa hiyo, ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kule Mkoani kwetu Tanga tuna zao la mkonge. Ninaipongeza sana Wizara wanafanya vizuri, lakini changamoto ndogo ni wakulima wale wadogo wadogo wanapata tabu na zile korona. Hakuna korona za kutosha za kuchakata mkonge. Wakati mwingine mkonge wao unaharibika unakuta umeshakomaa, yule mnunuaji mkubwa haendi kununua kule, kwa hiyo hiyo ni changamoto kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine nimeona, mara nyingi, mashamba mengi ya mkonge yanaungua…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako.

MHE. MWANTUMU M. ZODO: Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo langu la mwisho. Mheshimiwa Waziri ajaribu kutuangalia kule Tanga kwenye zao letu lile la machungwa. Ajaribu kutuangalia sana, atupelekee kiwanda kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na ninaomba kuunga mkono hoja ya Wizara hii ya Kilimo. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga.

MHE. HAWA S. MWAIFUNGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Kilimo. Kwanza kabisa ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya na uzima nimeweza kusimama hapa kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ninaomba nimshukuru sana na nimpongeze sana Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kututoa kwenye kilimo tulipokuwa mpaka hapa sasa tulipofikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukisema kwamba hakuna kinachofanyika kwa kweli tutakuwa hatutendi haki. Mnyonge mnyongeni haki yake mpeni, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanya vizuri sana kwenye sekta nzima ya kilimo. Miaka 10 iliyopita nilikuwa upande wa pili, nilikuwa sehemu ya kusisitiza kuhakikisha kwamba wananchi wananufaika na kilimo na leo tunavyozungumza hata mimi kwenye Mkoa wangu wa Tabora tunasema *yes* kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kwanza nizungumzie kuhusiana na suala zima la hii miradi mikubwa ya umwagiliaji. Hapa hata watu wakiangalia kwenye taarifa ya Kamati imeeleza vizuri sana na ninaungana na Wanakamati. Ninaungana moja kwa moja na Kamati kuishauri Serikali kuhakikisha kwamba miradi hii mikubwa ya umwagiliaji zaidi ya miradi 26 inatafutiwa fedha maalum na siyo tusubiri bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukisema tutasubiri bajeti kwenye miradi hii hatutamtendea haki Mheshimiwa Rais. Tutapiga *mark time* miaka 20 hapa miradi hii ya mabwawa haijakwisha na kazi kule haitaonekana. Suala la kilimo cha umwagiliaji halina ubishi, suala hili lina tija na tunaamini kwamba tukiwekeza, kwenye suala zima la mabwawa haya, ninaamini kabisa kwamba tutakwenda kubadilika kutoka kwenye kilimo cha kusubiri mvua na kuwa kilimo chenye tija cha umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niishauri Wizara ingalie uwezekano wa kuhakikisha kwamba fedha inatafutwa nje ya hizi fedha za bajeti kwa ajili ya kumalizia miradi hii mikubwa, tuweze kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais ili akiondoka mwaka 2030, aondoke kifua mbele akiwa amehakikisha kwamba Watanzania sasa tuko vizuri kwenye sekta nzima ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuelezea kuhusiana na suala zima la viwanda vya mbolea na hususan ahadi ya Chama Cha Mapinduzi kwa wananchi wa Tabora. Nimekuja na Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, kijitabu hiki unachokiona, kidogo, lakini kimesheheni kwelikweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 5/9/2025 Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, alikuwepo katika Mkoa wa Tabora, Jimbo la Tabora Mjini, alizungumza na akatoa ahadi ya kuhakikisha kwamba, Tabora tutapata kiwanda kikubwa cha mbolea. Ipo kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, haya siyo maneno yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Mheshimiwa Rais kuzungumza alitukabidhi vitabu hivi na alipokuwa akinikabidhi aliniambia, mwanangu huu ndiyo mkataba baina yetu Chama Cha Mapinduzi na wananchi hawa, utakapokwenda kuzungumza nao. Siku 63 sikuwahi kuacha kutembea na kitabu hiki na kuwaambia Watanzania, Wananchi wa Tabora, kata 29, Chama Cha Mapinduzi kitakwenda kufanya nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa leo ninaomba kumwambia ndugu yangu, mimi sina mashaka kabisa na Mheshimiwa

Chongolo, Waziri msikivu, mpole na mwelewa. Ninaamini Mheshimiwa Waziri anaijua Tabora kuliko inavyomfahamu, amepita kwenye changamoto mbalimbali katika Mkoa wa Tabora, anaijua vizuri, anajua jinsi ambavyo tuna eneo kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi watu wa Tabora, ninavyozungumza na Waziri hapa, tuna kilometa za mraba zaidi ya 76,151. Hakuna mkoa wowote ambao unazifikia kilometa hizi za mraba, lakini tumetengewa sisi watu wa Tabora zaidi ya 26.6%, hili eneo linafaa kwa kilimo na bado halijakwisha. Hizi ni zaidi ya kilomita za mraba 20,199 na hili eneo halijakwisha. Ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri, kama maeneo yaliyotengwa yanaonekana kwamba, yana gharama kubwa, Tabora siyo maskini wa maeneo. Twende tukamwoneshe, kama imeshindikana huko, sisi tupo, tutakwenda kumwonesha maeneo. Waje wawekeze kwenye kiwanda cha mbolea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuna maneno mengine ya kuwaambia Wananchi wa Tabora kuhusiana na suala la kiwanda, lazima kiwanda cha mbolea kije Tabora kwa sababu, mama ameahidi na mama akiahidi anatekeleza. Twende tukatafute eneo tujenge kiwanda cha mbolea katika Mkoa wetu wa Tabora. Haijalishi hata kama haitakuwa kwenye Jimbo la Tabora Mjini, lakini kijengwe kwenye Mkoa wetu wa Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na sisi kuomba kiwanda cha mbolea, sisi ndiyo wenye soko. Tabora tunalima tumbaku kwa zaidi ya 70%, kwa mujibu wa takwimu za Wizara ya Kilimo, zaidi ya 70% ya tumbaku ya nchi hii tunalima sisi Mkoa wa Tabora. Tuna majirani zetu, Katavi, Kigoma, Shinyanga na Simiyu, hawa wote wanalima tumbaku. Kiwanda kikijengwa pale Tabora ni *centre* ya mikoa yote hii kupata mbolea kwa urahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haijalishi, malighafi tunayo inasafiri nchi mbalimbali, inafanya kazi na mbolea inakuja hapa. Kwa nini Tabora? Tabora itafika; tujengewe kiwanda, malighafi itatoka Ruvuma, malighafi itatoka Songwe, malighafi itatoka kokote katika nchi hii, ifike Tabora tutengeneze kiwanda. Mwekezaji

anajua hawezi kupata soko kubwa kama lililoko Mkoa wa Tabora, la tumbaku tunayoilima pale Tabora kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo, leo tunacho kiwanda kingine cha mbolea hapa Dodoma, kipo pale Nala. Ninakumbuka mwaka jana Mheshimiwa Rais alikwenda kukizindua kiwanda kile. Kiwanda kile kinazalisha zaidi ya tani milioni moja kwa mwaka, lakini kimeajiri zaidi ya Watanzania 1,000. Ninaiomba sana Wizara iende ikakae chini na hawa wawekezaji, inawezekana wakaweza kutuzalishia zaidi ya hiki ambacho wanakizalisha sasa, ili sisi suala la mbolea ikitokea vita na kukitokea changamoto zozote, sisi kwenye suala la mbolea tunatakiwa tuwe sawasawa kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini bado ninaendelea kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa miradi ya umwagiliaji katika Mkoa wa Tabora.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. HAWA S. MWAIFUNGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya Tabora ya umwagiliaji…

MWENYEKITI: Muda wako umekwisha, Mheshimiwa.

MHE. HAWA S. MWAIFUNGA: …imebaki sita peke yake, ndiyo ambayo fedha zake zimetengwa, ili ziweze kutumwa. Mingine yote angalau imeishia 50%, lakini mingine imekamilika kabisa…

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako.

MHE. HAWA S. MWAIFUNGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, ninaomba kuwatambulisha kwenu wageni waliopo Bungeni jioni hii, ambao ni Viongozi 35 wa Serikali ya Wanafunzi kutoka Chuo cha Maji, Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa tunaendelea. Sasa ninamwita Mheshimiwa Japhael Masanja Lufungija. Ajiandae Mheshimiwa Ghati Zephania Chomete, ajiandae Mheshimiwa Moses Kaegele.

MHE. JAPHAEL M. LUFUNGIJA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa nafasi. Ninatumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kibali cha kuweza kusimama siku ya leo tena Bungeni nikijadili Taarifa ya Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa mapenzi mazuri ya kuwajali Watanzania, hasa kwenye Sekta kubwa ya Kilimo. Muda mwingi Wizara hii bajeti imekuwa ikipanda kila wakati, lakini Waziri wa Kilimo na Naibu Waziri pamoja na Watendaji wote, tumeona kwenye Kitabu cha Bajeti mambo mengi, mambo mazuri yamewekwa, kwa ajili ya Watanzania, kuwawezesha wakulima wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu ninaomba kuuelekeza upande wa zao la tumbaku. Kwa Tabora na Jimbo la Ulyankulu sisi ni wakulima wakubwa wa tumbaku. Ziko changamoto kubwa za upandaji wa mbolea na kushuka kwa madaraja ya uuzaji. Msimu uliopita wa 2024 mbolea ya *NPK* iliuzwa kwa Dola 60.77, lakini kwa msimu huu mbolea inauzwa kwa Dola 63, jambo hili ni ongezeko kubwa linalokatisha tamaa wakulima. Isitoshe, bei ya madaraja ya zao la tumbaku imeshuka mno, Dola 0 ina madaraja 18, lakini Dola 01 madaraja 29 na Dola 02 madaraja 16; Dola 03 yenye faida kubwa kwa mkulima imepewa madaraja mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili linakatisha tamaa kwa wakulima. Tunaiomba Serikali yetu ione namna ya kuweka ruzuku kwenye mbolea ya *NPK* ambayo ndiyo mbolea inayotumika kwa asilimia kubwa kwenye zao la tumbaku, ili kuwa-*favor* wakulima waweze kupandisha uzalishaji. Wakulima hawa wa tumbaku, Serikali ifikirie wako wakulima, Serikali ikubali wa-*graduate*, wako wakulima wanaoweza kulima kwa kujitegemea, ione haja ya kuwaruhusu wakulima wenye mitaji waweze kulima kwa kujitegemea kuliko kuendelea kuwang’ang’aniza wabaki kwenye kukopeshwa. Hilo ni ombi kutoka kwa wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, tumezungumzia *issue* ya kiwanda cha mbolea. Ilani yetu ya Chama Cha Mapinduzi na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, mwenye mapenzi mema, Mkoa wa Tabora na Wanatabora aliwafurahisha kweli wakati wa kampeni yake. Kiwanda hiki kinahitajika kwa wananchi na wakulima wote wa Mkoa wa Tabora. Itambulike kwamba, watumiaji wakubwa wa mbolea ya *NPK* ni wakulima wa tumbaku na sisi Tabora ndiyo tunaozalisha kwa 70% zao la tumbaku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba Serikali, kama ambavyo watangulizi wamesema, Tabora tunayo maeneo mengi ya uwekezaji, tusitafsirike kwamba, eneo la Tabora linahitaji fidia ya hela nyingi, la hasha! Yako maeneo mengi na wananchi wako tayari kupokea kiwanda hiki. Tunamwomba Mheshimiwa Waziri na Watendaji wote waone umuhimu wa kuwekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mabwawa. Kwenye Ilani, katika Jimbo la Ulyankulu, yameelezwa yatajengwa mabwawa matatu; Bwawa la Kona Nne, Bwawa la Mwamnange na Bwawa la Igombe. Ninaiomba Wizara itoe kipaumbele kwa sababu, jimbo hili wako wananchi wakulima wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili, kulingana na muda. Jimbo la Uliyankulu linazalisha pia, mazao ya chakula, zao la karanga, mpunga na mahindi; tutafutiwe masoko, kwa maana ya kujengewa maghala. Leo karanga iliyoko Jimbo la Ulyankulu, kwa eneo la Ulyankulu wanunuzi wanunua kwa shilingi 2,900 kwa kilo, lakini ikitoka inakwenda kuuzwa Kahama, Kahama wanauza shilingi 3,500. Unaweza ukaona namna ambavyo watu wanalangua, wanahama kwenda eneo dogo, wanapata faida kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mteja wetu mkubwa sisi ni watu wa Rwanda. Tuone haja ya kujengewa maghala na kuhakikisha kwamba, uendeshaji wa zao la karanga unafanyika katika maeneo husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, kulingana na muda, ni suala la pembejeo za kilimo upande wa mahindi. Bado gharama

ni kubwa, mkulima anatumia zaidi ya shilingi 370,000 kwa kiwango cha chini, lakini uangalie leo uzalishaji kwa Mkoa wa Tabora, kimsingi eka moja haizidi magunia 12. Leo mahindi yanauzwa, gunia moja la kilo 108 linauzwa, shilingi 42,000, ukichukua shilingi 370,000 ina maana faida yake ni kama shilingi 50,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili bado halijakaa vizuri. Tunawaomba Wizara, watusaidieni kutafuta masoko, ili kumpa tija mkulima huyu. Vitu vingine vinapanda, lakini upande wa wa mazao ya chakula bado bei zake ziko chini, kwa hiyo, tunakuomba sana Mheshimiwa Waziri...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. JAPHAEL M. LUFUNGIJA: ...hilo hatuna mashaka na Waziri. Yeye ni mchapakazi na watendaji wake wote tunawaamini.

MWENYEKITI: Muda wako umekwisha, Mheshimiwa.

MHE. JAPHAEL M. LUFUNGIJA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana na ninaunga mkono hoja.

MWENYEKITI: Ahsante kwa mchango wako. Sasa ninamwita Mheshimiwa Ghati Zephania Chomete.

MHE. GHATI Z. CHOMETE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa nafasi ya kuchangia. Ninaanza kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, nimesimama hapa kwa mara ya kwanza kuchangia, ninaomba kuwashukuru sana Wanawake wa Mkoa wa Mara walionipa nafasi tena ya kuja kuwawakilisha katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninaamini nitafanya kazi kwa weledi mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikisema kilimo ni uti wa mgongo, ninamaanisha. Ninamaanisha kilimo ni uti wa mgongo kwa sababu, kilimo ni chakula, kilimo ni biashara, lakini kilimo ni ajira, hivyo ninaomba Serikali ipeleke fedha zote zilizoombwa na Wizara ya Kilimo, ili ziende zikatekeleze miradi hii ambayo Wizara ya Kilimo imeomba. Hapa ninampongeza sana Waziri wetu wa Kilimo, Mheshimiwa Daniel Chongolo, anafanya kazi kubwa, nzuri sana iliyo na mfano. Tunasema, Mheshimiwa Rais hakukosea kumpa nafasi hiyo kwa sababu, anaitendea haki. Hongera sana kwa Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajielekeza upande wa ushirika. Ninaipongeza sana Serikali yetu kwa namna ilivyowekeza kwa upande wa ushirika. Tumeona namna gani imewekeza kwenye Benki ya Ushirika, zaidi ya shilingi bilioni 50, leo Benki ya Ushirika inafanya kazi. Ombi letu ni kuhakikisha matawi yanaongezeka katika maeneo mengine, ili kufikisha huduma kwa wananchi kwa haraka, ili kusudi ushirika uendelee kuimarika. Ninaomba Serikali ihakikishe inafungua viwanda vile ambavyo ni vya ushirika, ili kuendelea kuongeza chachu ya mazao, ushindani ndani ya ushirika, mazao yetu yaweze kupata soko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, wamefungua Kiwanda cha Mbogwe kinafanya vizuri, Kiwanda cha *KACU* kinafanya vizuri na pale Simiyu kinafanya vizuri, lakini kuna viwanda vingine bado tunatamani viende vikafunguliwe. Kiwanda kama cha *Nyanza Cooperative Union*, Kiwanda cha *Mara Cooperative Union,* Kiwanda cha *SHIRECU Cooperative Union* ni viwanda vilivyokuwa vinafanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Mkoani Mara, Kiwanda cha *Mara Cooperative Union* kilikuwa kinafanya vizuri sana na pamba ile ilikuwa ni pamba safi, pamba iliyokuwa inapendeka Tanzania Bara na Afrika kwa ujumla. Kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Waziri Kiwanda kile cha *Mara Cooperative Union* aende akakifufue, ili kusudi wananchi wa Mkoa wa Mara na wenyewe waweze kupata ajira. Kaka zetu na wananchi wa Mkoa wa Mara kwa ujumla waweze kuongeza pato katika mkoa wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo ninamwomba Mheshimiwa Waziri, upande wa bei ya tumbaku. Bei ya tumbaku imekuwa sasa siyo bora kwa wakulima na hapa ninampongeza sana kaka yetu Stanley, Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Tumbaku, anaendelea kufanya vizuri, changamoto hizi za bei ya tumbaku aziangalie. Wakulima wa Serengeti wamekuwa wanapata changamoto ya bei hizo kwa sababu, kwa sasa wanauza kwa Dola *1.4* mpaka Dola *1.5,* lakini wamezalisha kwa Dola 1.6. Hii siyo sahihi kwa sababu, wamekopa mikopo wanatamani warudishe, hii itaenda kuwaletea hasara kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba; wazo langu hapa na ushauri ni tuangalie namna bora ya kuziangalia pembejeo. Tukae, tuangalie bei za pembejeo, ili kusudi tuweze kuwasaidia hawa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaendelea kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, lakini pia, ninaendelea kumpongeza Mheshimiwa Daniel Chongolo, Waziri wetu, katika hii stakabadhi ghalani. Stakabadhi ghalani ni maono ya Mheshimiwa Rais, ameenda vizuri na sasa wanaendelea kufanya vizuri katika kuwajali wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu hapa ni tupeleke elimu, ili wakulima waweze kujua namna bora ya kutumia mfumo huu wa stakabadhi ghalani kwa sababu, tunaenda kuwaondolea ile adha ya madalali waliokuwa wanawasumbua, ili kusudi wakulima waweze kupata bei nzuri na huu mfumo uendelee kufanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. GHATI Z. CHOMETE: Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa mbolea.

MWENYEKITI: Muda wako umekwisha, Mheshimiwa.

MHE. GHATI Z. CHOMETE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Moses Kaegele, wajiandae Mheshimiwa Alan Thomas Mvano na Mheshimiwa Sara Msafiri Ally.

MHE. MOSES L. KAEGELE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili kuchangia katika Bajeti ya Wizara ya Kilimo. Ninatumia fursa hii, kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kuwepo mahali hapa, lakini pia, ninatumia fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais na Serikali yake yote kwa namna ambavyo amewekeza kwenye kilimo. Ukiangalia bajeti hii, zaidi ya shilingi trilioni 1.2 inaenda kutekeleza ajenda ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa anayoifanya. Ninajua amejikita sana pia, kwenye umwagiliaji na ninajua umwagiliaji unaenda kuwaokoa sana wakulima wadogowadogo pale ambapo miradi hiyo itaenda kutekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajikita sana kwenye kushauri na pia, kuomba. Ninaanza na suala la bei ya mahindi. Mwaka huu wa Fedha *NFRA* walinunua kilo moja kwa shilingi 700 na ukiangalia dunia ilivyo kwa sasa na mambo yanayoendelea duniani, unaona kwamba, ni lazima tu kama si mbolea basi ni mbegu, gharama zitaongezeka. Ukiangalia wakulima wetu, hasa wa Jimbo la Nkasi Kusini, wao wanategemea sana wauze mahindi, ili wakanunue mbolea ili wakanunue mbegu. Hali hii inaonesha nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaonesha kwamba, wanapokwenda kujiandaa na msimu unaofuata ni lazima Serikali, kupitia *NFRA,* waone namna ya kuongeza hata shilingi 150 kilo ifike shilingi 850, ili wakulima hawa waweze kumudu gharama za kilimo na pia, kumudu gharama za maisha. Watu wa Mkoa wa Rukwa na Jimbo la Nkasi Kusini ili ununue nguo au ununue ng'ombe au ukatibiwe ni lazima uuze mahindi. Ndiyo maana ninaiomba sana Serikali, suala la bei ya mahindi waone namna ya

kuongeza hata shilingi 150 kuwasaidia hawa wakulima kuweza kumudu gharama za uzalishaji, lakini pia, gharama za maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni upatikanaji wa mbolea ya ruzuku. Ni kweli sisi wananchi wa Mkoa wa Rukwa na Jimbo la Nkasi Kusini tunatamani kuona kwamba mbolea inapatikana kuanzia mwezi Agosti, Septamba hadi wa Oktoba. Ukiangalia kuna muda mwingine mbolea zimekuwa zikichelewa na hii inakwamisha wananchi wengi kutokuingia kwenye kilimo na kuvuna mavuno mengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia nimesoma mwongozo wa usambazaji wa pembejeo za ruzuku, nimeona pale kuna jambo ambalo kama Wizara wanatakiwa walitazame. Kwanza hawa mawakala wanapofuata mzigo kwa maana ya mbolea kwa makampuni wanaenda kuwauzia wananchi kwa bei nzuri sana, lakini pale ambapo makampuni wanasafirisha zile mbolea kupeleka Mikoani wanawauzia wale mawakala kwa bei ambayo inawalazimisha wao wakauze ile mbolea nje na bei elekezi ya *TFRA*. Ninaishauri Serikali kwanza kuna umuhimu wa Serikali kuangalia namna ya kutoa mwongozo wa bei elekezi kwa makampuni ambayo wanaenda kusambaza mbolea kwa mawakala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo bei elekezi inawasaidia sana mawakala nao wanunue kwa bei nzuri na wao wakawauzie wakulima kwa bei ambayo ni elekezi kutoka *TFRA*. Niombe sana Serikali, wananchi kimsingi wanaponunua kwa bei ambayo siyo elekezi kwanza wanaona mbona tumesikia taarifa ni hii, lakini imekuja taarifa hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye suala la ombi, Mheshimiwa Waziri ninajua kwamba yeye ni mpambanaji, mpiganaji, watu wa Jimbo la Nkasi Kusini wanaomba mambo mawili tu. Kwanza, wanaomba maghala katika Jimbo la Nkasi Kusini, hadi sasa tuna ghala na wanasafirisha mazao yao mbali sana kutafuta soko, lakini la pili, wanaomba visima vinne kwa ajili ya umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo pekee la Nkasi Kusini ndiyo halina miradi ya umwagiliaji, ukiangalia Bonde la Kati, Bonde la Kipande, Bonde la Kizumbi na kadhalika wanahitaji visima virefu ili siku ya siku waweze kuendesha kilimo cha umwagiliaji. Ninawapongeza kwamba sasa wana magari zaidi ya 19 ambayo yanachimba hadi mita 1,800 kwenda chini kwa maana ya visima virefu vya umwagiliaji. Hizi nyenzo ni muhimu sana, zitatusaidia sana sisi wananchi wa Jimbo la Nkasi Kusini kama tutapata hivyo visima tuweze kuzalisha kwa muda wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa nafasi na niseme kwamba, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa ahsante kwa mchango wako. Sasa ninamwita Mheshimiwa Alan Thomas Mvano, atafuatiwa na Mheshimiwa Sara Msafiri Ally na Mheshimiwa Asha Salum Motto ajiandae.

MHE. ALAN T. MVANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu ambaye anaendelea kutujalia afya njema, vilevile niendelee kuwashukuru sana wananchi wa Kakonko kwa kuniamini na kunituma kuwawakilisha katika hili Bunge Tukufu. Ahadi yangu kwao ni kwamba, nitaendelea kufanya kazi hii kwa uaminifu na nitafanya kazi hii kwa maslahi mapana ya Wilaya ya Kakonko na Nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe vilevile pongezi kwa Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya. Katika Wilaya ya Kakonko yapo mambo ambayo tumeyaona yamefanyika kwa kipindi kifupi, ikiwa ni pamoja na kutuletea mbegu za alizeti za ruzuku. Kwa kweli wananchi wa Kakonko wanashukuru sana, tumepokea na kazi inaendelea ndani ya Wilaya ya Kakonko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili tunashukuru pia tumepata Kituo cha Utafiti wa Mazao katika Wilaya ya Kakonko na tumekwishatenga ekari 267 na kazi inaendelea. Jambo la tatu, tunashukuru pia wakulima wetu wa tumbaku wamekaa muda

mrefu bila kulipwa na siku mbili zilizopita wamepokea malipo ya zaidi ya milioni 300. Tunaishukuru sana Serikali hii inaongozwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan, tunaamini na fedha nyingine ambayo haijalipwa, italipwa ili wananchi wetu waendelee kufanya shughuli zao vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kakonko ingependa kuona mambo kadhaa yanafanyika katika mwaka huu wa fedha. Jambo la kwanza ni kukarabati miundombinu ya umwagiliaji na kujenga ile ambayo haijajengwa. Kwanza kabisa tuna maeneo ya Itumbiko, Liwiti, Katengela, Mwiluzi na Bwaru. Maeneo hayo yote yanafaa kwa kilimo cha umwagiliaji, kwa hiyo tunaamini ili tuweze kuboresha uzalishaji katika sekta ya kilimo, basi Wizara ituangalie kwa jicho la pekee maeneo hayo ili miundombinu iweze kutengenezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, tunaomba sana kiwanda cha kuchakata na kuongeza thamani zao la muhogo kama ilivyoahidiwa, basi jambo hili nalo lifanyike ili wananchi waweze kuona faida katika zao hilo. Jambo la tatu, tumetenga ekari zaidi 1,000 kwa ajili ya *block farming* ya zao ya parachichi, tunaiomba Serikali ilione pia eneo hilo ili tuweze kufanikiwa na wananchi wetu waweze kupata manufaa ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la nne, tunaomba pia zana za kisasa za kilimo ziweze kufika katika Wilaya ya Kakonko, kwa sababu bado wapo wananchi wengi ambao wanaendelea kulima kwa kutumia jembe la mkono. Jambo la mwisho katika mambo ambayo tungependa kuona yanafanyika, ni kuendelea kuhakikisha pembejeo zinapatikana kwa wakati ili wakulima wetu waweze kufanya vizuri na kuongeza uzalishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mambo yote hayo nimetoa pongezi kwa Serikali na nimeona mpango mzuri wa Waziri na mpango mzuri wa Rais. Mambo haya yote yakifanyika maana yake ni kwamba, tunakwenda kuona mageuzi katika uzalishaji wa mazao yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa pendekezo langu mimi ninajikita katika eneo la masoko. Pamoja na mambo mengine yote yatakayofanyika tusipoliangalia vizuri eneo la masoko maana yake ni kwamba tunakwenda kuzalisha kitu kikubwa na mwisho wa siku tutakosa pakupeleka. Jambo la kwanza la kuangalia Wizara hii kwa kushirikiana na Wizara nyingine lazima ije na mpango mkakati wa namna ya kuendea masoko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, soko la kwanza la muhimu la kuangalia ni sisi wenyewe Watanzania tupo zaidi ya milioni 70 maana yake ni kwamba tukiwa na mkakati mzuri sisi wenyewe tutakuwa soko la kwanza kwa mazao tunayozalisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili soko la nchi za jirani yapo mambo yanapaswa kufanyika ili tuweze kuyaendea masoko hayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza, tujenge maghala maeneo ya mipakani ili watu wanaotaka kupeleka mazao nje ya nchi yetu waweze kuwa na sehemu ya kuhifadhia mazao yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, Serikali ijikite katika kuhakikisha kilimo kinachofanyika kinakuwa ni kilimo cha mkataba, watu wasilime bila kujua watapeleka wapi mazao yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, lazima Wizara ije na mpango wa kuhakikisha wananchi wetu wanapata elimu ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza wajue wanapolima wanatumia mbolea gani kwa ardhi gani? Vilevile masoko ya mazao yanapatikana wapi? Kwa hiyo ninashauri Wizara ije mpango wa kuandaa *channel* maalum kwa ajili ya *television* zetu kama walivyofanya wenzetu wa utalii Safari *Channel* inafanya vizuri, watu wakiangalia wanaona fursa zilizopo, tuangalie kwenye *channel* zetu na redio zetu, zitoe habari za elimu kwa ajili ya wakulima wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejikita katika eneo hili kwa sababu jukumu la kumi la Wizara ya Kilimo ni kutafuta masoko na kuratibu masoko, lakini eneo la tatu ni masoko ya kimataifa. Hapa ninapendekeza kwamba Wizara ije na mpango mkakati wa kuyaendea masoko ya kimataifa kwa kuwatumia Mabalozi wetu walioko katika nchi za mbali. Moja kati ya eneo la kupima *performance* ya Mabalozi wetu iwe ni pamoja na kuangalia *exports* wanazozifanya kutoka Tanzania kupeleka kwenye nchi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mambo haya yote muda hauwezi kutosha kuelezea haya, ninaomba sana Serikali iangalie eneo hili la masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, pendekezo langu kwa sababu lazima mambo haya yaende pamoja, unaona Wizara ya Uchukuzi inaingia lazima liweke vizuri miundombinu, unaona Wizara ya Viwanda na Biashara inaingia kwa sababu lazima tutafute masoko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapendekeza ikimpendeza Mheshimiwa Rais aunde Wizara maalum ya masoko ili sasa iende kufanya kazi moja kwa moja kwa kushirikiana na Wizara nyingine ili tuweze kuyatafuta masoko ndani, tutafute masoko ndani ya nchi jirani na tutafute masoko katika nchi za mbali

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa mchango huo ninakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa ahsante kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Sara Msafiri Ally, ajiandae Mheshimiwa Asha Salum Motto na Mheshimiwa Kakulu Kakulu ajiandae.

MHE. SARA M. ALLY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kwenye hii bajeti ya Wizara ya Kilimo. Kipekee ninamshukuru sana Waziri na timu yake kwa hotuba nzuri aliyoitoa yenye mipango endelevu ya kuongeza tija kwenye kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda nitoe shukrani zangu sana kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge, ambayo inashughulikia masuala ya kilimo kwa ushauri mzuri sana ambao Mwenyekiti ameutoa kwenye mchango wake binafsi na kwenye hotuba yake hasa kuongeza masoko na kufanya utafiti kwenye mbegu, kwenye mbolea na namna ya viwanda vyetu vitakavyoongeza uzalishaji na kufanya tathmini kwa wale ambao wameshindwa kuendeleza viwanda, tuone namna nzuri ya kuwaondoa na kuweka wawekezaji wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa ziara aliyoifanya ndani ya Jimbo la Mvomero akiambatana na Waziri wa Mipango na Uwekezaji. Walitembelea maeneo ya uwekezaji ya viwanda vya sukari na mashamba ya miwa, walipata fursa ya kuona changamoto za viwanda ambavyo vinazalisha kwa kiwango kikubwa zaidi ya malengo, lakini changamoto ipo kwa wakulima wa miwa, miwa yao haivunwi kwa wakati na hivyo wanapata hasara kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na masuala ya kuingiza sukari na Mheshimiwa Waziri kwa pamoja walisema watalishughulikia hili. Salamu za wananchi wa Mvomero wana imani kubwa na Mheshimiwa Waziri, ninaamini hakutakuwa tena na kuharibika kwa miwa ya wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa ninakushukuru sana Mheshimiwa Waziri na Serikali, Jimbo la Mvomero lina skimu za umwagiliaji 10 na skimu hizi 50% tayari Serikali imefanya usanifu bado fedha, lakini kwa kipekee tunashukuru kwamba zipo skimu ambazo Serikali imeshatoa fedha. Skimu za Lukenge, Mgongola, Misufini, mkandarasi amepatikana. Skimu ya Dakawa tayari hekta 3,000 zinafanya uzalishaji wa 100%, tunashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijikite kwenye changamoto za kusuasua kasi ndogo ya uwekezaji kwenye miundombinu hii hasa kwenye skimu ambazo Serikali imeshatoa fedha. Tunayo Skimu ya Mgongola, skimu hii imeanza ujenzi tangu mwaka 2021, mkandarasi akaleta changamoto zake, mradi ukasimama wa shilingi bilioni 5.6, Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan

alitupa fedha, mkandarasi akalipwa bilioni 1.7, akapotea akaishia mitini, kwa hiyo skimu ile ipo tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishukuru sana Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kipindi cha muda mfupi alichokaa ofisini kwake, ameweza kutoa ushauri wa namna ya kuachana na huyu mkandarasi, mkandarasi huyu sisi ametushinda. Serikali ya Wilaya, Serikali ya Mkoa, Tume ya Umwagiliaji wamehangaika naye imeshindikana fedha zetu amechukua 1.7 bilioni na fedha iliyobaki ni pungufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba ushauri alioutoa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, basi tuiombe Tume ya Umwagiliaji tuna Mkurugenzi Mkuu mchapakazi pale, masuala ya kisheria yamekwisha ili sasa tuachane na mkandarasi, tukamalizie. Nishauri kwa sababu muda umeenda ni zaidi ya miaka mitatu sasa tangu fedha zitolewe na Serikali na mradi umesimama, niiombe Tume ya Umwagiliaji ikafanye mradi ule kwa *force account* ili sasa wananchi wale wa Jimbo la Mvomero hasa eneo la Tulia ambapo kuna mafuriko waweze kunufaika na miradi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao pia mradi mwingine ambao Mheshimiwa Waziri ametuahidi, ni Mradi wa Lukenge ambao Serikali imewekeza 1.4 *billion,* mradi umekamilika kwenye miundombinu bado pampu. Mheshimiwa Waziri na Serikali wametuahidi kwamba tarehe 30 mwezi huu ambao ni keshokutwa watakuwa wametununulia pampu ya shilingi milioni 800 ili wananchi wale wakafanye uzalishaji. Sasa kwa sababu miundombinu imekamilika miaka miwili iliyopita, ilibaki pampu ambayo Mheshimiwa Waziri ametuahidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine niombe ndani ya skimu zetu za Jimbo la Mvomero, tuna hekta 41,883 uwekezaji uliofanywa na Serikali ni 19% tu sawasawa na hekta 8,002. Kama wenzangu walivyoongea na Wabunge na Kamati ya Bunge ilivyoshauri tunahitaji mapinduzi ya kilimo kwenye kilimo cha umwagiliaji kwa sababu kinakopesheka, tuna uhakika wa kuvuna na tuna uhakika wa masoko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba Benki ya Kilimo, Tume ya Umwagiliaji na Serikali wakae waone namna ya kuleta mapinduzi kwenye sekta ya kilimo hasa kwenye kilimo cha umwagiliaji chenye uhakika ili sekta ambayo imeelekeza kwenye Jimbo langu kwenye 19% tu tuweze tukawekeze kwenye 100% ili tuweze kuzalisha kwa tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni mbolea wameongea wenzangu. Tunavyo viwanda vya ndani vya mbolea, Serikali ione namna ya kusaidia viwanda hivi vikopesheke viweze kuzalisha mbolea ya kutosha na ya uhakika ili wakulima wasipate tabu ya mbolea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninashukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa tunakushukuru kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Asha Salum Motto, ajiandae Mheshimiwa Kakulu Buchard Kakulu. *(Makofi)*

MHE. ASHA S. MOTTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hii Bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dira inasema tujilishe na tuwalishe wengine kibiashara. Tunaweza kuona pia hata kwenye vipaumbele vya Wizara hii inasema kuongeza tija na uzalishaji hivi vyote vinaenda sambamba. Kilimo kama walivyokwisha kusema kwamba ni uti wa mgongo, lakini ukiangalia pia kilimo kimesaidia Tanzania kuajiri 70% ya Watanzania, kwa hiyo kilimo ni ajira. Pia kilimo hiki hiki kimeweza kuchangia pato la Taifa zaidi ya 25% kwa hiyo, hata Dira ya Maendeleo ya Taifa inatambua mchango wa kilimo kama ni kichocheo cha uchumi wetu hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila mbegu na siyo tu mbegu bila mbegu bora na bila mbolea hatuwezi tukasema kwamba tuna kilimo chenye tija. Mbegu bora ni msingi wa kilimo chenye tija na mbegu bora huongeza mavuno. Nitumie fursa hii kumpongeza

sana Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya katika kuimarisha hii Wizara ya Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona uzalishaji wa mbegu bora nchini unavyoendelea kufanya kazi vizuri. Ninatokea Mkoa wa Mtwara mpaka sasa ninaishukuru sana Serikali kupitia Bodi ya Korosho imeendelea kuzalisha miche ya korosho na kuisambaza Mkoa wa Mtwara kwa wananchi wote, wakulima wote wa zao hili la korosho, kwa hiyo na sisi ni wanufaika wa mbegu bora na miche bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na usambazaji huo, ninaomba nitumie fursa hii kumwomba Mheshimiwa Waziri, Waziri wangu ni msikivu sana usambazaji wa miche hii bado unasuasua, wananchi wengi bado hawajafikiwa, hawajapa miche hii na maeneo bado yako mengi. Sisi kama Wabunge wa Viti Maalum tumeendelea kusisitiza na kuhamasisha wanawake wajitokeze kwa wingi kwa ajili ya kuhakikisha na wenyewe wanapanda mikorosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapozungumzia mbolea kilimo chochote kama hatuna mbolea toshelevu maana yake ni kwamba hatutakuwa na tija na kama tulivyoona katika vipaumbele vya hapa wanasema kwamba lazima kuongeza tija na uzalishaji na mbolea huongeza tija na uzalishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kutupatia mbolea na viuatilifu. Mheshimiwa Rais ametoa ruzuku ya bilioni 300, hii ilisaidia sana kupunguza gharama za pembejeo, lakini pia itaongeza tija katika kilimo. Mkoa wa Mtwara wakati anaingia Dkt. Samia madarakani korosho tulikuwa tunalima tani 100,000, lakini sasa hivi zimeongezeka mpaka tani 600,000. Sisi kwetu tumeona na tumefaidika na hiyo ruzuku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nishauri, pamoja na kwamba tuna viwanda vya mbolea hapa Tanzania takribani 48, tuna viwanda viwili ambavyo ni vikubwa na vina uwezo wa kuzalisha tani takribani 1,200 na kitu, viwanda hivi kuna *INTRACOM*

na Minjingu lakini tuna viwanda 14 vya *size* ya kati, tuna viwanda pia vidogo vidogo takribani 32, viwanda hivi vina uwezo wa kuzalisha tani 150,000 kama tulivyoona. Uzalishaji huu ni mdogo sana ukilinganisha na uhitaji wetu Nchini Tanzania ambapo sasa hivi tuna uhitaji takribani wa tani 1,500,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia sana takwimu hiyo inatupelekea sisi kwenda kutegemea 80% ya mbolea kutoka nje. Uzalishaji wa viwanda hivi havina tija, ninaomba sasa niishauri Serikali kwanza kabisa ione namna bora ya kuhamasisha viwanda hivi vya ndani kutumia rasilimali zetu tulizonazo hapa nchini, ikiwemo makaa ya mawe, gesi pamoja na mabaki yale ya taka kwa maana tunaweza tukazalisha wenyewe na tukajitegemea wenyewe bila kutegemea nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu, kama sisi tunazalisha 20% tunategemea mbolea inayotoka nje 80%, kwa kweli hatutaweza kufikia tija katika uzalishaji na hatutaweza kupata ajira, wala kutoa ajira kwa vijana wala kwa wanawake. Hatutaweza kufanya *mutation* kwa Taifa letu. Ina maana uchumi tunapoongelea kupandisha trilioni moja 2050, hatutaweza kufikia tija. Ni lazima tuhakikishe kwamba tunahamasisha hivyo viwanda ambavyo vipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba Serikali ina mpango wa kujenga kiwanda kikubwa sana cha uzalishaji wa mbolea cha *Triple Sulphurs Phosphate,* ninashauri pia Serikali kuendelea kuhamasisha wawekezaji kutoka nje kuja kuwekeza kuzalisha mbolea nchini kwa kutumia rasilimali tulizonazo. Kwa mfano, Mkoa wa Mtwara tunaye mwekezaji ambaye anaitwa *Soil Solution* na yeye anakuja kuwekeza mradi takribani *US Dollar* milioni 627 na anatarajia kutoa ajira kwa wananchi takribani 3,000. Hii kwetu ni *advantage;* vijana wengi watapata kazi na vilevile tutaondokana na utegemezi wa mbolea kutoka nje *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia niishauri Serikali. Maafisa kilimo waendelee kutoa elimu kwa vitendo kwa wakulima juu ya namna bora ya kutibu udongo. Maana pia udongo

umekuwa na changamoto, lakini wananchi wengi kule vijijini hawajui hata namna ya kuutibu udongo; na Maafisa Kilimo wengi hawawafikii wakulima kule chini. Kwa hiyo ninawashauri Maafisa Kilimo watoke kwenye viti washuke chini waende wakawape elimu ya kutosha wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa mwenyekiti, kuna namna pia ya kuwapa elimu namna ya kufanya *crop rotation*. Wananchi wengi hawajui nini maana ya *crop rotation*...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Muda wako umekwisha Mheshimiwa.

MHE. ASHA S. MOTTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Kakulu Buchard Kakulu, ajiandae Mheshimiwa Dkt. Emanuel Qambaji Nuwas na mchangiaji wetu wa mwisho atakuwa Mheshimiwa Dr. Lazaro Kiliani Komba.

MHE. KAKULU B. KAKULU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa nafasi ya jioni, ili nami nipate nafasi ya kuchangia kidogo kwenye sekta muhimu ya kilimo ambayo kwa nchi hii ni sekta mahususi na sekta ya kipaumbele sana. Nitakuwa na mambo matatu ya kuchangia leo kwa ufupi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja nitazungumzia kuhusu ushirika kama nyenzo muhimu sana katika mapinduzi ya viwanda vijijini. Pili, nitazungumzia kuhusu umuhimu wa kuanzisha mamlaka mahususi ya usimamizi wa vyama vya ushirika vya akiba na mikopo, nje kabisa ya usimamizi wa ushirika wa jumla. Tatu, nitazungumzia kuhusu mikopo kwa vijana kwenye sekta ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa pongezi kwa Serikali ya Chama Cha Mapinduzi kinachoongoza nchi yetu kwa sasa, kwa kazi nzuri iliyoifanya katika kipindi kifupi kilichopita kwenye sekta

ya kilimo. Yametokea mapinduzi makubwa sana kwenye sekta ya kilimo katika kipindi cha miaka minne, mitano iliyopita. Ruzuku katika mazao mbalimbali ambayo imepelekea kuongezeka kwa tija na uzalishaji mkubwa sana kwenye sekta yetu ya kilimo na kwa hiyo kama nchi kujitosheleza kwa sehemu kubwa katika chakula na katika mazao ya biashara na kuongeza mapato ya Taifa hasa kupitia mauzo nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, yametokea mageuzi makubwa sana hasa katika sekta za kipaumbele za mazao makubwa ya kilimo hasa korosho na sekta ya kahawa katika kipindi cha miaka michache iliyopita. Tunaipongeza Serikali na haya yote pongezi mahususi na za kipekee zimwendee Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dr. Samia Suluhu Hassan na wanaomsaidia kupitia Waziri wetu wa Kilimo, ndugu yetu na kiongozi wetu wa chama mstaafu, Mheshimiwa Dkt. Daniel Chongolo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajielekeza mchango wangu wa kwanza kwa ufupi sana kuzungumzia ushirika. Ukiniuliza ushirika nitakwambia ushirika ndiyo nyenzo namba moja ya kufanya mapinduzi muhimu sana vijijini hasa kupitia sekta ya viwanda. Jaribu kufikiria idadi ya vyama vya ushirika vilivyoko takribani katika kila sekta nchini. Sekta ya kilimo ikiongozwa kwa vyama vingi vya ushirika, sekta ya madini, sekta ya uvuvi, sekta ya mifugo na kila aina ya sekta unayoijua. Hebu jaribu kufikiria kwamba umefanya mageuzi kidogo sana ya kuhamasisha uanzishaji wa viwanda vya kuongeza thamani kidogo kwenye maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kwanza kitakachofanikiwa ni kusaidia kuongeza mazao yetu na kuyaongeza thamani kwenye maeneo ya vijijini. Pili, utasaidia kuchochea ajira katika maeneo ya vijijini na kwa hiyo kusaidia vijana wetu ambao wanakimbilia mijini kubaki mahali walipo. Tatu na muhimu zaidi, itasaidia kufungamanisha sekta nyingine zilizoko vijijini na kwa hiyo kuchochea ajira kwenye sekta nyingine zaidi nje ya ushirika wenyewe na shughuli zinazohusika na ushirika wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasisitiza kwamba, Mheshimiwa Waziri pamoja na kazi nzuri sana anayoifanya nimwombe; tunamfahamu, ni mchapakazi mzuri sana na juzi nilimshuhudia akitangaza ajenda maalum na kampeni maalum ya kuhamasisha uadilifu, uaminifu na uzalendo katika kusimamia na kuendesha vyombo vya ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri, na ninamwamini kwamba ni mtu ambaye ana msimamo, ni mtu mwadilifu. Ni mtu ambaye akiamua kusimamia jambo analisimamia kweli. Kwa hiyo, tunamtarajia kwamba angalau kwenye eneo hilo na maeneo mengine kwenye sekta yake atayasimamia vizuri. Kwa hiyo, la kwanza lilikuwa ni hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, msisitizo ni kwamba, kwa sababu sekta hii ndiyo inayoajiri watu wengi zaidi kuliko sekta yoyote. Kama tukifanya mageuzi hayo katika viwanda vidogo vidogo kwenye sekta ya ushirika itatusaidia kufanya mageuzi makubwa zaidi na katika muda mfupi sana kuliko eneo lingine lolote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili nizungumzie umuhimu wa kuanzisha mamlaka maalum ya kusomea Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo. Kwa umuhimu wake na kwa sababu inahusika na *transaction* za fedha na Mheshimiwa Waziri na Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi, kwamba eneo hili limekuwa kwa kasi kubwa sana na kuna *SACCOS* kubwa zaidi hasa zinazochukua amana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasisitiza kwamba ni muhimu tuanzishe chombo maalum ambacho kitahusika kabisa kusimamia sekta hiyo ya vyama vya ushirika vya fedha, ili tuviondoe katika usimamizi wa jumla wa vyama vya ushirika. Moja, itatuhakikishia usalama wa fedha; Pili, itasaidia kuchochea kukua kwa haraka kwa sekta hiyo; na Tatu itatusaidia kuongeza kasi ya ukuaji wa akiba na mikopo na ku-*mobilize resources* nyingi sana kutoka kwa watu wadogo wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nisisitize jambo moja kuhusu mikopo kwa vijana. Kwa umuhimu wa sekta yetu na kwa

wingi wa vijana walioko maeneo ya vijijini na kwa umuhimu wa sekta yenyewe, ninaamini, pamoja na kwamba ninajua tumeanza, lakini inabidi tuwe na kasi zaidi ya kuongeza ukubwa wa mikopo kwenye sekta hii ili vijana wetu waliosomea kilimo ambao hawajasomea kilimo walio na uwezo wa kufanya ujasiriamali kwenye sekta hii waweze kufanya vizuri zaidi, tuongeze ajira kwenye sekta hiyo ili ituongezee na kuchochea sekta ya biashara kwenye maeneo ya sekta ya kilimo. Vilevile itusaidie kuchochea na kuongeza mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi wetu pamoja na maendeleo ya jumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba zaidi na muhimu, kilimo kama nyenzo muhimu ya kupunguza umaskini, tukiongeza mikopo kwenye eneo hili, hasa kwa vijana, tutachangia pakubwa katika kupambana na tatizo la umaskini kwenye maeneo ya vijijini na kwa hiyo kuisaidia nchi yetu kupiga maendeleo kwa kasi kubwa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ufupi nina hayo kwa leo. Wakati mwingine tutachangia na kushauriana na Mheshimiwa Waziri kuona namna gani tunavyoweza kusaidia sekta yetu kuendelea mbele. Asante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Sasa ninamwita Mheshimiwa Dkt. Emanuel Qambaji Nuwas.

MHE. DKT. EMANUEL Q. NUWAS: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa uhai, hadi kupata nafasi hii ya kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Kilimo. Ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Rais pamoja na Mheshimiwa Waziri wetu wa Kilimo kwa mpango mzuri ambao amewasilisha kwa ajili ya maendeleo ya kilimo hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema kilimo ni mama na baba wa Wizara zote; kwa sababu katika kilimo tuna ajira, tunapata nishati, biashara, afya, maana madawa yote nayo yanatokana na mimea, lakini vilevile katika kilimo tunapata lishe pamoja na

chakula. Kwa maana ya ajira, tunaona zaidi ya 80% ya wananchi wetu wanapata ajira kupitia sekta hii ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kusema mambo mawili; la kwanza, hii Wizara ni Wizara ya kimkakati kama ilivyo Wizara za Uchukuzi na Nishati. Ningeomba Mheshimiwa Waziri ahakikishe anaongea na hawa, kwa sababu tunapojenga *SGR*, tunapoboresha bandari, ni lazima tuhakikishe kwamba bidhaa zitakazopita katika barabara, katika *SGR* na bandarini ziwe ni bidhaa zinazotokana na kilimo chetu. Kwa hiyo hii Wizara ni Wizara muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama walivyosema Waheshimiwa Wabunge, ninapenda kuishauri Serikali kwamba, bajeti ya upande wa umwagiliaji itoke nje ya bajeti ya kawaida kwa sababu ni eneo la kimkakati. Vilevile, eneo la uzalishaji wa mbolea, tunaona uzalishaji upatikanaji wa mbolea ni kiasi cha 83% ambacho si kiwango kinachotakiwa; lakini bado zaidi ya 60% inatoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunajua kwamba kule duniani tuna mgogoro wa kivita kati ya nchi nyingine; hivyo kutakuwa na changamoto ya upatikanaji wa mbolea katika mwaka unaokuja kama ambavyo tunaona kwenye mafuta. Kwa hiyo, tunaiomba Wizara iweze kuweka mpango mkakati wa mapema wa kuhakikisha kwamba mbolea zitaendelea kupatikana katika msimu unaokuja kwa ajili ya kilimo chetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande pia wa uzalishaji wa mbegu, bado pia mbegu zetu haziwi za kutosha. Ningeomba Wizara nayo itenge fedha maalum kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa mbegu. Moja ya eneo ambalo ninapenda kuchangia, amechangia Mheshimiwa Mbunge mmoja; tuna tatizo la uwepo wa mbegu feki katika majira yale ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaumiza sana mkulima pale ambapo ananunua mbegu 15,000 au elfu kumi na ngapi, anapokwenda kupanda *acre* zote zinakuwa haziwezi kuota.

Lazima udhibiti uwepo na namna ya pekee ni kuongeza uzalishaji wetu wa ndani kwa upande wa mbegu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande pia wa mbolea, tunajua kwamba mbolea ambayo tunayo hapa nchini bado katika nyakati za kilimo kuna wafanyabiashara wachache wanatumia zile fursa. Ninaishauri Serikali kwamba, wale wauzaji na wale mawakala wawe wanaweka bei za mbegu na bei za mbolea kwenye milango, ili mkulima anapofika aone kabisa haitaji kuuliza na iwe ya wazi. Hii itajenga uwazi katika kupata mbolea, lakini pia mbegu kwa bei nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichangie kwenye eneo la mazao machache. Zao moja ni dengu ambalo liko kwenye stakabadhi ghalani. Hakika imekuwa changamoto kwa wakulima wengi. Kwanza, hawapati mbegu nzuri, wanatumia zile zile ambazo walipanda mwaka jana; lakini pili, masoko yao si ya hakika kwa sababu maghala yako machache sana na wakulima hutumia umbali mrefu sana kusafirisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba na ninashauri tuweke soko huria, lakini hao wanaonunua miongoni mwa wakulima waishie kwenye sehemu ya stakabadhi ghalani. Tusitengeneze mazingira ya changamoto kwa wakulima wetu ambao wengi ni wadogo wadogo na wengi wanatumia gharama kubwa sana. Ninaomba tutengeneze soko huria kwenye eneo hilo. Wale wanaotaka kuuza kwa mfumo wa uhuru wauze lakini wote waishie kwenye stakabadhi ghalani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuchangia kwenye eneo la zao la vitunguu maji pamoja na karoti ambalo bado ni changamoto, wengi wanauza kwa mfumo wa lumbesa. Hata leo ukienda kwenye soko la mazao haya kwenye mkoa wowote, bado lumbesa ni changamoto. Mheshimiwa Waziri Mkuu ametoa maelekezo, ninaomba Mheshimiwa Waziri wetu alisimamie hili kikamilifu ili wakulima wapate faida ya mazao yao wanayoyapata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zao la mahindi ambalo hakika linalimwa sana katika mkoa wangu na katika jimbo langu ambalo ninaliongoza; mahindi mwaka huu tumepata bahati na tunaona tutapata mazao ya kutosha. Tunamshukuru Mwenyezi Mungu. Tunaomba Serikali itusaidie kupitia *NFRA*, kwanza kuweza kutoa bei nzuri ili kuwasaidia wakulima ambao wamenunua mbegu na pia wamenunua mbolea. Vilevile, kufungua mipaka mapema ili tupate bei nzuri ambayo itatusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo langu la mwisho ni eneo la umwagiliaji. Tunamshukuru Mheshimiwa Rais Samia, tumepata skimu tatu, tumepata mabwawa mawili. Ninaomba Serikali iweze kukamilisha mradi huu. Tumepata pia visima sita katika kata zetu na zitaenda kusaidia kuongeza wigo wa kilimo cha umwagiliaji ambacho ni kilimo cha hakika sana. Nipende kumpongeza Mheshimiwa Rais Samia kwa ajili ya mradi huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la mwisho ni eneo la mradi wa *BBT*. Tunaomba *BBT* ishuke katika halmashauri ambako ndiko vijana wako na ndiko mashamba yaliko. Tushushe chini ili vijana wengi wakajiajiri kule ili waweze kuzalisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nizungumze kwamba, kilimo bila vifaa na teknolojia haiwezekani. Matrekta na *power tiller* tunashukuru tumesikia kwamba yatakuwepo na yatakopeshwa. Masharti yawe nafuu na yaweze kusambazwa hasa katika maeneo ya vijijini ambako ndiko wakulima waliko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaomba kukushukuru sana na kusema ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Sasa ninamwita Mheshimiwa Dkt. Lazaro Kiliani Komba, ndiye atakayekuwa mchangiaji wetu wa mwisho kwa siku ya leo.

MHE. DKT. LAZARO K. KOMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa nafasi, lakini nitumie pia nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia zawadi hii ya uhai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya katika kuimarisha sekta hii ya kilimo. Kazi hii si ndogo na pongezi hizi ninazozitoa nitazitoa kwa takwimu ili tujue kabisa kwamba kazi kubwa anayoifanya Mheshimiwa Rais inaonekana pia katika maisha ya kawaida na vilevile iko vizuri katika takwimu tulizonazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kaka yangu ambaye sisi tunaomfahamu tunamfahamu kwa ufanisi wake mkubwa katika kazi anazozifanya na hajawahi kushindwa mahali popote alipopata kufanya kazi. Hongera sana kwa Mheshimiwa Waziri, wananchi wa jimbo la Peramiho huwa wanaamini sasa shamba limepata mkulima, kwa hiyo mazao lazima yaongezeke kupitia Mheshimiwa Waziri na timu yake yote akisaidiana na Naibu Waziri ndugu yangu Mheshimiwa Silinde.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetoa pongezi hizi nikiwa nina takwimu zinazopelekea tutoe pongezi hizi. Tutakumbuka Mwaka wa Fedha 2021/2022 uzalishaji wa mahindi katika nchi hii ulikuwa ni tani 6,950,000, wakati mahitaji ya chakula ndani ya nchi ilikuwa ni tani milioni 5,900,000, na hivyo tukawa na ziada ya tani 950,000, ziko pembeni. Miaka michache baadaye, ni miaka miwili tu baadaye uzalishaji uliongezeka kwa kiwango kikubwa kutoka tani milioni sita mpaka kufika tani milioni 10,925,000 kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huo huo matumizi yetu pia yalikuwa yameongezeka kwa sababu ya ongezeko pia la idadi ya watu. Tukawa tunahitaji kutumia ndani ya nchi tani 7,300,000. Hivyo kupelekea kuwa na ziada ya chakula kwa takribani tani 3,600,000. Hizi zipo zinahitaji kutoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu hizi hazijaja kwa bahati mbaya. Takwimu hizi zimekuja kutokana na kazi kubwa

inayofanywa na Wizara ya Kilimo kwa maelekezo ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye amepanga kuimarisha na kukuza sekta ya kilimo ambayo kimsingi inaajiri kwa kiwango kikubwa katika nchi hii ukilinganisha na sekta nyingine tulizonazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme jambo moja; ongezeko hili limesababishwa na ongezeko la pembejeo zile za ruzuku; kwa maana ya mbolea, mbegu, pamoja na madawa. Mwaka wa Fedha 2021/2022 tulikuwa tuna uwezo wa kununua mbolea tani 7,241, lakini miaka miwili, mitatu baadaye ongezeko limekuwa kubwa sana. Tunapata sasa mbolea ya ruzuku kwa tani 21,457 kwa mwaka mmoja. Ongezeko hili ukilitazama ni mara tatu ndani ya kipindi cha miaka miwili. Si jambo dogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, maendeleo yoyote yana tabia ya kuzalisha matatizo. Tumeongeza uzalishaji kwa kiwango kikubwa lakini uzalishaji huu umezalisha tatizo la upatikanaji wa masoko. Sisi wakulima wa mahindi wa Jimbo la Peramiho soko letu kubwa lenye uhakika ni *NFRA;* na *NFRA* ukiitazama imekuwa inaongeza kiwango cha kununua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2022 ilikuwa imenunua tani takribani 58,000, lakini hivi tunavyozungumza kwa msimu uliopita *NFRA* wameongeza na wakanunua tani 457,000. Ongezeko ni kubwa, lakini ongezeko hili haliendani na ongezeko la uzalishaji wa mahindi na hivyo kutengeneza uhaba wa soko kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kuishauri Serikali katika mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza, niishauri Serikali, juhudi kubwa inayofanya katika kuhakikisha sekta ya kilimo inaimarika na kuongeza uzalishaji, juhudi ile ile itumike katika kutafuta masoko ya nje kwa sababu ndani tayari pamekwishajaa na hatuwezi kuuziana wenyewe kwa wenyewe wakati wote tunazalisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wa pili kwa Serikali; ukitazama katika takwimu nilizozitoa tuna akiba ya tani 3,600,000. Ukitoa ile inayonunuliwa na *NFRA* ambayo ni tani 445,000 na ile inayouzwa nje ya nchi, kwa maana ya mahindi kutoka nje ya tani 665,000, bado tunabaki ndani ya nchi na akiba ambayo haijakwenda kokote ya tani 2,500,000, ambazo kimsingi hizi ziko katika maeneo mawili. *Either* ziko kwa wananchi na zimeshindwa kufika sokoni au zimeharibika kwa sababu wamekosa maghala ya kuhifadhia mazao haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ushauri wangu wa tatu kwa Serikali, tuiombe sana Serikali. Sisi wananchi wa Jimbo la Peramiho tunazalisha kwa kiwango kikubwa mahindi; na kwa sababu tunashindwa kuyauza yote kwa wakati, yale yanayobaki tunaomba sana tujengewe maghala katika maeneo manne nitakayoyataja. Tunaomba kujengewa ghala katika Kata za Ndongosi, Kata ya Mbinga Mhalule, Kata ya Magagula na Kata ya Kilagano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukifanya hivi tutakuwa tumesaidia sana maeneo mawili. Jambo la kwanza tutaimarisha uzalishaji na jambo la pili tutashawishi vijana ambao wanapaswa kuingia katika sekta hii kama sehemu ya maisha yao kuwa na fursa na kuona kilimo ni sehemu ya biashara na kwamba biashara hii inakwenda kuimarisha maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikaona nitumie nafasi hii kutoa ushauri katika maeneo haya. Nikushukuru sana kwa nafasi. Niendelee pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kazi kubwa wanayoifanya na sisi wananchi wa Jimbo la Peramiho tuna imani sana na Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa shughuli zilizoorodheshwa kwa siku ya leo katika Kikao chetu cha Kumi na

Nane, Mkutano wa Tatu. Nichukue fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote waliopata nafasi ya kuchangia. Kwa hakika mmetoa michango mizuri na yenye tija kwa wananchi na kwa Taifa kwa ujumla. Hongereni sana.

Baada ya kusema haya, ninaomba kuahirisha Bunge hadi kesho tarehe 29 Aprili, 2026, saa 3.00 asubuhi.

(Saa 1.41 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 29 Aprili, 2026 Saa Tatu Asubuhi)

PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA